

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 30 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu! Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Mkutano wetu wa Kumi na Moja kikao cha Kumi na Tisa, katibu.

#### NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU WA MEZANI:

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

#### NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

#### MHE. HUSSEIN M. BASHE – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe maoni ya Kambi ya Upinzani kama ilivyo ada, Katibu tunaendelea.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU WA MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali tunaanza na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa swalii la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali Mbunge wa Manonga. kwa niaba yake Mheshimiwa Mwanne Nchemba.

Na. 154

**Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Simbo, Ziba, Choma cha Nkola na Igurubi kwa Ufadhilli wa Benki ya Dunia**

**MHE. MWANNE J. MCHEMBA (K.n.y. MHE. SEIF K. GULAMALI) aliuliza:-**

Wilaya ya Igunga ilipata ufadhilli wa Benki ya Maendeleo ya Afrika wa ujenzi wa Vituo vya Afya vya Simbo, Ziba, Choma cha Nkola na Igurubi ambapo Kituo cha Afya cha Ziba, Choma cha Nkola na Igurubi vimekamilika na vifaa tayari viro japo majengo na vifaa katika Kituo cha Afya cha Choma cha Nkola na Igurubi bado havijaanza kufanya kazi. Kituo cha afya cha Simbo bado hakijakamilika na vifaa havipo na wafadhili walishakabidhi Halmashauri bila kukamilisha ujenzi huo.

Je, Serikali inachukua hatua gani kujua nini kilicho jificha juu ya mradi huo kukabidhiwa bila kukamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zahanati ya Ziba na vituo vya afya vya Simbo, Choma cha Nkola na Igurubi vilijengwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Zahanati ya Ziba na Kituo cha Afya Choma cha Nkola vimekamilika na vinatoa huduma, Kituo cha Afya Igurubi kimekamilika, lakini bado hakijaanza kutoa huduma kutokana na kukosekana kwa vifaa vya maabara na watalaan wa dawa za usingizi. Jitihada za kupata vifaa na mtaalam huyo ili huduma zianze kutolewa zinaendelea kufanyika ikiwemo Mkoa na Halmashauri kuititia ikama ya watumishi wenye utalaam wa dawa za usngizi ili wa wapange upya kwenye vituo ambavyo havina wataalam.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kituo cha Afya Simbo haukuweza kukamilika kwa sababu za kibajeti na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto iliujuishwa uongozi wa mkoa wa Tabora kuititia barua yenyewe Kumb. Na. BC. 209/426/02D/20 ya tarehe 11 Desemba, 2013 kuhusu kusimamishwa kwa baadhi ya miradi ukiwemo Kituo cha Afya cha Simbo na kuelekeza Halmashauri kutenga fedha kwenye bajeti zao kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.

Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI imechukua hatua na kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kiasi cha shilingi milioni 400 zilizopatikana kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambazo zinatumika kumalizia jengo la upasuaji na nyumba za watumishi katika Kituo cha Afya cha Simbo pamoja na kukiboresha zaidi na kuongeza miundombinu inayotakiwa kwa ajili ya kutoa huduma zote muhimu ikiwepo upasuaji wa dharura.

**SPIKA:** Swali la nyongeza bado Mheshimiwa Mwanne Mchemba amesimama, aaha, ndio mwenye swali *okay ahsante.*

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nipende kushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri pia niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Wizara ya Afya, Wizara ya TAMISEMI kwa fedha walizotupatia shilingi milioni 400 kwa ajili ya kituo cha afya cha Simbo. Kwa kweli tunaendelea vizuri na ujenzi na muda sio mrefu tutakamilisha mradi huo. Niombe sasa Serikali kwenye vituo vya afya vilivyobakia kama hiki cha Choma cha Nkola uwekeze kwa nguvu kubwa sana fedha hizi zipatikane fedha zingine kwa ajili ya kukamilisha mradi huo ambao uko katika hatua za mwisho.

Kwa hiyo, ni lini sasa Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya kukamilisha hiki Kituo cha Afya cha Choma cha Nkola ili kukamilisha ili zifanye kazi pamoja na Kituo cha Afya cha Simbo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gulamali, Mbunge wa Manonga majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Josephat Sinkamba Kandege tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gulamali kama ifuatavyo. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinamaliziwa vile ambavyo vimeshaanzwa na naomba nimuhakikishie kazi nzuri ambayo imeanzwa na Serikali kuhusiana na ujenzi wa hicho Kituo cha Afya cha Choma cha Nkola itakamilika ni suala tu la bajeti kwa sababu kupanga ni kuchagua lakini nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya vinamaliziwa ili viweze kutoa huduma iliyokusudiwa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nilikuona Mwalimu swali la nyongeza.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Kama ilivyo katika Wilaya ya Igunga Wilaya ya Kakonko ilipata ufadhilli wa kujengewa vituo vya baba, mama na mtoto vitano na katika Wilaya zingine ndani ya

Mkoa wa Kigoma, vituo hivyo vimekamilika vizuri kabisa ni ufadhili wa Bruembag wa Marekani, lakini vituo hivyo vina vifaa vyote kasoro ni watumishi kwa hiyo nimuombe Waziri atoe *commitment* vituo hivyo vitapata watumishi lini ili mfadhili tusiweze kumkatisha tamaa katika Wilaya ya Kakonko na Wilaya zingine ndani ya Mkoa wa Kigoma? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Kandege tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, nikiwa ziarani mkoa wa Kigoma nilipita Kakonko na kwa bahati mbaya muda ambao nimepita Mheshimiwa Mbunge mpaka napita kwake ilikuwa hakuna Kituo cha Afya ambacho kilikuwa kiko kwenye utaratibu wa kujengwa lakini nafarijika kwamba mionganoni mwa wilaya ambazo zimepata pesa kwa ajili ya vituo vya afya ni pamoja na Wilaya yake ya Kakonko.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kwa kushirikiana na wananchi pamoja na wafadhili pale ambapo vituo vya afya vinakamilika ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunapeleka wataalam maana nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma ya afya inatolewa Tanzania nzima naomba niwahakikishie.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa maeneo ambayo yanatakiwa kupelekewa watumishi ni pamoja na kwake na bahati nzuri katika watumishi 49,000 ambao tunatarajia kuwaajiri ambao vibali vitatoka *almost* kama 10,000 tutapata kuhusiana na watu wa afya, hatutasahau kwake. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana bado tuko Wizara hiyo hiyo Waheshimiwa Wabunge swali linaulizwa na Mhesimiwa Platei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini.

Na. 155

**Ahadi ya Kujenga Barabara ya Kilometra Tano  
Haydom na Dongobesh**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu, Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilometra tano katika Mji wa Hydom na Dongobesh, kilometra 2.5 kila Mji.

Je, ni lini barabara hizo zitajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano aliahidi kuboresha barabara za Mji Mdogo wa Haydom na Mji Mdogo wa Dongobesh kwa kujenga barabara za miji hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, makisio ya shilingi bilioni 3.2 ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nyepesi kwa urefu wa kilometra nne katika mji mdogo wa Haydom, yaliwasilishwa kwa mtendaji Mkuu wa TARURA kwa barua yenye Kumb. Na. CA 32/267/01/05 ya tarehe 09/03/2018. Makisio haya yamemfikia Mtendaji Mkuu wa TARURA kipindi ambacho tayari bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 ilishaandaliwa na kwa sababu hiyo fedha hizo zitaombwa katika bajeti zijazo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kuitia TARURA imetengewa shilingi milioni 714.9 za matengenezo ya barabara. Aidha,

katika kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, Serikali inaelekeza *TARURA* katika kila Halmashauri kutenga fedha kwenye bajeti zake za kila mwaka ili ahadi hizo kutekelezwa kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nishukuru wametenga shilingi bilioni 3.2 kwa kuwa barabara zilizohidiwa ina jumla ya urefu wa kilometa 7.5 na sasa wametenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa kilometa nne je, lini sasa mnaweza kutenga kwa kilometa 4.3 zilizobakia? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali la msingi niliuliza kwamba lini inakwenda kujengwa, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuthibitisha kwamba ni lini hasa kweli barabara hii itaanza kujengwa? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu mafupi kwa swali hilo na ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa FLatei Massay nichukue fursa hii kwanza kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akipigania maendeleo ya jimbo lake na Wilaya ya Mbulu kwa ujumla wake. Kama ambavyo nimetoa majibu katika jibu langu la msingi nimeelekeza kwamba wakati wanawasilisha bajeti yenye thamani ya shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya hizo kilometa nne tayari mchakato wa bajeti ulikuwa umeshakamilika na hivyo tumewaelekeza kwamba katika bajeti inayokuja wahakikishe *TARURA* wanatenga kiasi cha fedha za kutosha ili kuhakikisha kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais zinatekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni azima ya Serikali na kwa kadri bajeti itakavyokuwa imeruhusu ahadi za Mheshimiwa Rais na kwa sababu ziko katika uratibu maalum tutuahakikisha tunajenga.

Mheshimiwa Spika, kimsingi sio Mbulu peke yake kwa maana ni pamoja na Dongobesh ambayo nayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais nayo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadri bajeti itakavyoruhusu tutahakikisha kwamba na eneo hilo nalo linajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia nilikuona swali fupi la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ahadi za Mheshimiwa Rais ni pamoja na barabara za Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo pamoja na ile barabara ya Kahe mpaka Chekeleni na ya kwenda Kilema hospitali. Sasa kwa kuwa barabara hizi zimeahidiwa nchi nzima, Serikali haioni busara kuandika barabara zote kwa Waheshimiwa Wabunge ili tujue programu ya ujenzi wa barabara hizi zinafanyika kwa awamu kwa kiasi gani? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Suleimani Jafo Majibu majibu tafadhalli.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia kama ifuatavyo; ni kweli kuna ahadi nyingi za ujenzi wa barabara hasa katika halmashauri za miji na halmashauri za Wilaya. Lakini hata hivyo tulivyofanya ni kwamba barabara hizi ziko za maeneo mawili kuna barabara zile za *TANROADS* na zingine ziko chini ya Ofisi ya TAMISEMI kupitia *TARURA*.

Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tayari ahadi zote za Mheshimiwa Rais zimeratibiwa vizuri na lengo letu ni kwamba ndani ya miaka mitano tutakuwa tunatekeleza awamu kwa

awamu. Kwa hiyo, hizi ahadi zote zimeratibiwa vizuri na tutaenda kuzitekeleza Mheshimiwa Mbatia wala usihofu katika eneo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresa nilikuona swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa swali niulize swali la nyongeza.

Mji wa Karatu ni mji wa kitali kwa sababu ndio langa la kuingilia katika Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, na ahadi ya ujenzi wa kiwango cha lami ilishatolewa toka Serikali ya Awamu ya Nne kwamba Mji wa Karatu watajenga takribani kilometra 10 za lami. Je, sasa ni lini kwa kipaumbele cha kuangalia mji ule ni mji wa kitalii mtajenga kilomita hizo?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa nchi Mheshimiwa Suleiman Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimefika pale Karatu nimeangalia mji na bahati nzuri ni maeneo ambavyo nchi yetu tunapata mapato mengi sana kupitia sekta ya utalii. Kama nilivyozungumza nilivyokuwa ninajibu swali la Mheshimiwa Mbatia ni kwamba lengo letu kubwa ni nini baada ya hii miaka mitano tutahakikisha kwamba kila maeneo tuweze kuyafikia, lakini hata hivyo eneo la Karatu kwa sababu ni eneo la kimkakati kama tulivyofanya tumeanza kufanya kule Serengeti tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo na mimi mwenyewe nitachukua dhamana hiyo kusimamia kwa karibu zaidi utekelezaji wa mji wa Karatu uwe katika mazingira mazuri kwa azma kwamba tunaenda kupata mapato ya Serikali kupitia utalii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea bado tuko Wizara hiyo hiyo ya TAMISEMI, Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene Mbunge wa Ileje uliza swali lako tafadhali. Mheshimiwa Halima Bulembo.

Na. 156

**Upatikanaji wa Vifaa Kuwashudumia Watoto Njiti Nchini**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO (K.n.y. MHE. JANET Z. MBENE)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha vifaa muhimu vya kuhudumia watoto njiti vinapatikana kwenye vituo vya afya na Hospitali za Wilaya?

(b) Je, Wilaya ya lleje itapelekewa lini vifaa hivyo?

(c) Je, Serikali haioni ni muda muafaka wa kumwongezea muda wa likizo ya uzazi, wazazi wa watoto njiti kuwa na miezi sita pamoja na malipo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge wa lleje lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya lleje ina jumla ya vituo 33 vya kutolea huduma za afya ambavyo ni pamoja na hospitali mbili moja ya Serikali na moja ya Kanisa, kituo cha afya kimoja cha Serikali na zahanati 30 ambazo 24 ni za Serikali, nne za dini na mbili zahanati za watu binafsi. Huduma za afya za uzazi zinatolewa katika hospitali mbili kito cha afya kimoja na zahanati 28.

Mheshimiwa Spika, hospitali zote mbili zimetenga chumba maalum kwa ajili ya kuwashudumia wakina mama wanaojifungua watoto njiti kwa kutumia joto la mama baada ya kupewa maelekezo kutoka kwa watoa huduma za afya. Kwa watoto njiti wanaoshindwa kupumua wanasaidiwa kwa kutumia mashine ya kupumulia yaani *oxgen concentrator*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya lleje kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imetenga shilingi milioni 12 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya huduma kwa watoto njiti. Aidha, Mkoa wa Songwe umetenga shilingi milioni 22.1 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya utoaji wa mafunzo maalum ya kumsaidia mtoto njiti yaani *kangaroo mother care*.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya hospitali kuna mashine tatu za kusaidia kupumua *oxgen concentrator*, vifaa vya kuwasaidia watoto wachanga kupumua *resuscitation kits* vipo katika ngazi ya hospitali, kituo cha afya na zahanati zote.

Mheshimiwa Spika, suala la kumwongezea muda wa likizo ya uzazi, wazazi na watoto njiti kuwa miezi sita pamoja ya malipo, Serikali inalichukua na kulifanyia kazi kwa mujibu wa mwongozo wa kanuni za utumishi wa umma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Bulembo nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niulize swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania takwimu zinaonesha watoto 9,000 njiti hufa kila mwaka kutokana na kukosa huduma maalum na wakati mwingine hufariki kutokana na umeme kukatika na kukosa majenereta katika hospitali zetu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza vifo hivi vya watoto njiti?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, nilikuona, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, naomba nijilbu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Bulembo kama ifuatavyo; Serikali inatambua kwamba vifo vya akinamama na watoto vimeduwa vingi na mkakati

ambao tunaenda nao ni pamoja na huu ambao tunaendelea kuufanya wa kuboresha vituo vya afya katika huduma za dharura.

Mheshimiwa Spika, vilevile sambamba na hili tunaweka mkakati wa kuhakikisha kwamba huduma za watoto njiti na watoto ambao wamezaliwa zinapatikana katika hospitali zote katika vituo vyote hivi vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za mkoa pamoja na rufaa.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuendelee na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mlata.

Na. 157

### **Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Singida – Kizaga Iramba**

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. ELIBARIKI E. KINGU)** aliuliza:-

Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago hadi Kizaga – Iramba ni kwa uchumi wa Singida hasa kusafirisha mazao na mafuta ya alizeti, lakini pia ni barabara mbadala inapotokea uharibifu wa barabara kuu ya Mwanza, aidha, barabara hiyo ipo katika llani ya Uchaguzi wa CCM na pia Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo wakati wa kampeni.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Elias Kwandikwa tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninapenda kujibu swali la

Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara inayoulizwa na Mheshimiwa Mbunge inajulikana kama barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga yeny urefu wa kilometra 77.4 ambapo kati ya hizo kilometra 5.7 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometra zilizobakia 71.7 ni za changarawe.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kuwa barabara hii ni moja ya ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitao wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwango cha lami kwa kilometra 71.7 zilizobakia katika barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga utafanyika kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara tajwa. Vilevile *TANROADS* Mkoa wa Singida inaendelea kuifanya matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini hii barabara imekuwa ahadi yake ni ya muda mrefu sana kabla Awamu ya Tano haijaanza. Wamekuwa wakisema wanafanya upembuzi kila mwaka, sasa shilingi milioni 200 anazozisema Waziri hapa ni upembuzi gani huo na hii barabara itakamilika lini kwa sababu imebakia miaka miwili tu tuingie tena kwenye uchaguzi mwaka 2020. Tutawaeleza nini wananchi wa maeneo hayo kwa kutokukamilika kwa barabara hii. Anatoa ahadi gani?

Mheshimiwa Spika, lakini barabara hii anayoitaja pia sasa hivi haipitiki kabisa kwa sababu wananchi wa Ndago wanapata matatizo wanazungukia Kizaga kwa sababu ya mvua. Pia barabara ya Mgungila hadi lyumbu haipitiki, wananchi wanaenda kwa trekta. Ninamuomba Waziri anihakikishie hapa, Jumamosi atakwenda kutembelea barabara hizi ndipo aje atoe majibu hapa Bungeni kwamba zitajengwa lini? Ahsante. (*Makofî*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Elias Kwandikwa. Unapoelekea, Ushetu huwezi kupita huko moja kwa moja? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba barabara hii ni muhimu na kwamba kama itatokea shida kati ya Singida na miteremko ya milima kule Sekenke hii barabara inaweza ikatusaidia kuitisha magari yote yanayokwenda upande wa Bara.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia, kwa sababu barabara za mkoa zinazopita katika maeneo ya Mkoa wa Singida amekuwa mahiri sana kwa kuzifuatilia na niseme tu kwamba kweli kumekuwa na ahadi ya muda mrefu kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha. Lakini Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu wewe pamoja na wananchi wote wa Singida na Watanzania kwa ujumla kwamba kuonesha *commitment* ya Serikali ndiyo maana zile sehemu korofi upande wa Serikali zimeendelea kushughulikiwa na ndiyo maana tuna kilometa hizi 5.7, maeneo ambayo yalikuwa yanasumbua yametengezewa. Lakini kutokana na kuwa na mvua nyingi kwamba tunategemea mvua zikipungua maeneo mengi ambayo umeyataja tutaendelea kwenda kuyarekebisha.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba pamoja na kwamba tumetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa eneo hili lenyewe ni eneo ambalo ni fupi. Nikuahidi tu kwamba itakuwa ni sehemu ya kuanza kujenga

hii barabara. Kwa hiyo, pamoja na hiyo, tumetenga pia shilingi milioni 150 eno hilo za Kizaga – Sepuka mpaka Mlandala ni sehemu ambayo ni korofi. Kwa hiyo ukichukua kiasi kile nilichokitaja, shilingi milioni 200 na hii shilingi milioni 150, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kwamba kazi itafanyika vizuri na sisi kwa kweli tunaona uko umuhimu wa hii barabara kuitengeza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tunafahamu kwamba kutoka Singida, kwenda Shelui barabara hiyo imekuwa ni ya miaka mingi na imechakaa na sio muda mrefu miaka ijayo tutaenda kuifanyia matengenezo makubwa. Kwa hiyo, barabara hii tunaitegemea pia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inatupa huduma wakati wa matengenezo makubwa ya barabara hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la kwenda Jumamosi kutembelea maeneo haya, Mheshimiwa Mbunge labda baadaye tuzungumze tu tuone ratiba ambayo nitakuwa nayo kama nafasi itakuwepo ni kwamba tutaenda kuiona hii barabara kwa sababu Singida sio mbali na mimi niseme Singida ni ukweni kwangu kwa hiyo na mimi naona ni muhimu niende nione maeneo haya. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Niliwaona Mheshimiwa, Oliver Semuguruka na Mheshimiwa AishaRose Matembe.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la barabara ya Singida Magharibi linafanana kabisa na tatizo la barabara ya Nyakanazi – Rusaunga – Rusumo. Barabara hii kuna ukarabati unaoendelea haukidhi viwango kutokana na magari mazito yanayopita kuelekea nchi za jirani za Rwanda na Burundi, Congo na Uganda. Je, Serikali haionti umuhimu wa kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sababu ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Serikali inaona umuhimu wa kutengeneza barabara hii ndiyo maana tumeshapata fedha na hatua za manunuzi zinaendelea kufanya ukarabati mkubwa barabara hii ya kutoka Nyakanazi kwenda Rusahunga. Matengenezo haya ni muendelezo wa harakati za Serikali kuiboresha barabara hii ambayo ni kutoka Isaka kwenda hadi Usaunga.

Kwa hiyo, kile kipande cha kutoka Isaka kwenda mpaka Nyakanazi ni ukarabati ulikuwa unaendelea pamoja na changamoto ambazo zilijitokeza kwamba tutaendelea kusimamia vizuri kwa sababu tumekuwa na changamoto ya upitishaji wa magari makubwa na hasa haya magari makubwa yanatumia hizi tairi ambazo wanaita *super single*, zimekuwa na changamoto kubwa ya uharibu wa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa teknolojia ambayo sasa tumeendelea kuifanyia kazi kama Wizara ili kuweza kumudu changamoto hii iliyojitekeza tutafanya matengenezo kwa ubora zaidi kuliko kipindi kilichokuwa kimepita. Kwa hiyo, Mheshimiwa Semuguruka usiwe na wasiwasi na najua tumeongea na wewe juu ya jambo hili nikupongeze sana lakini harakati za manunuzi zinaendelea vizuri, barabara hii itatengenezwa ili tuweze kutatua changamoto ambayo imekuwepo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo liliopo Singida Magharibi linafanana kabisa na tatizo liliopo Singida Kaskazini. Kwa kuwa barabara ya Singida – Ilongero – Mudida - Kungi –

Kidarafa hadi Haydom yenye urefu wa kilometra 93.4 ujenzi wake umekuwa ni wa muda mrefu sasa na ina ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nhe.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuikamilisha barabara hii kwa haraka iwezekanavyo ili kuharakisha shughuli za maendeleo hususani kwa wananchi wa Singida Kaskazini? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa baraba hii kwa sababu inajua kwamba wakazi wengi wa Singida wanapata huduma ya hospitali katika hospitali ya kule kule Haydom na kwa umuhimu wa barabara hiyo pia maeneo haya yana uzalishaji mkubwa sana wa mazao na wananchi wa Singida wanaitegemea sana hii barabara kwa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge hata katika bajeti hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wameipitisha wiki iliyopita tumeongeza kasi kidogo. Tulikuwa tunaendelea kutengeneza kilometra chache za lami lakini safari hii tumeongeza angalau kidogo. Kadri tutakavyopata pesa tutaendelea kuishughulikia barabara hii mpaka tuweze kuunganisha na barabara ambayo kimsingi Wabunge wengi wanaotoka maeneo ya Singida, Simiyu, Shinyanga na maeneo pia ya Manyara wanategemea barabara hii itakayokuwa ikitoka Mbulu kuja Haydom kuja Mkalama, kuvuta Sibiti kwenda ule upande mwagine wa mikoa ya kanda za ziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, barabara hii ni muhimu kwa sababu tutakapoikamilisha barabara hii na viunganishi vyake hivi vitachochea ukuaji mkubwa sana wa maendeleo katika maeneo haya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge

nakupongeza lakini uvute subira. Tutajitahidi kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa kwa kasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Bado tuko Wizara hii hii. Swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini. Hayupo, kwa hiyo, swali lake basi linalala, tunaendelea na maswali mengine. Mheshimiwa Bobali. (*Makofi*)

Na. 158

**Fidia kwa Nyumba Zilizowekwa Alama ya "X" ya Rangi ya Kijani**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA)** aliuliza:-

Serikali imeweka alama ya "X" ya kijani kwenye nyumba ya maeneo ya wananchi ikimaanisha kuwa wanatakiwa kuondoka na hawana ruhusa ya kuendeleza maeneo yao au nyumba zao, hadi leo hii wananchi hao hawajalipwa fidia na wengine nyumba zao zinabomolewa.

(a) Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia?

(b) Kwa kuwa nyumba zao zinabomoka na hawawezi kuhama bila fidia. Je, Serikali inawaambia nini wananchi hao?

(c) Kwa kuwa uwepo wao katika maeneo hayo ulikuwa kisheria, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia viwanja mbadala wananchi hao kwa ajili ya makazi mapya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Jimbo la

Kilwa Kusini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara ya mwaka 1932 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1967 na kufanyiwa tena mabadiliko mwaka 2007 ambapo eneo la hifadhi ya barabara lilibadilika kutoka mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande kwa barabara kuu na barabara za mikoa kuwa mita 30 na hivyo kufanya eneo la hifadhi ya barabara kuwa mita 60 badala ya mita 45 za awali.

Mheshimiwa Spika, kutohakana na mabadiliko hayo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilifanya zoezi la kuainisha maeneo yote yaliyoathirika na Sheria mpya ya Barabara ya mwaka 2007 kwa nchi nzima. Aidha, wananchi wote wenye mali zao katika eneo la kuanzia mita 22.5 hadi 30 kutoka katikati ya barabara kila upande ambao wamewekewa alama ya "X" ya kijani watalipwa fidia kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa pindi utakapofanyika ujenzi au upanuzi wa barabara na mali zao kuathirika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, swali la nyongeza tafadhalii.

**MHE HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mbunge Selemani Bungara alikuwa anazungumzia zaidi barabara yake, vijiji vilivyowekewa alama ya "X" kwenye barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Lindi katika vijiji vya Nangurukuru, Kiwawa, Mavuji na maeneo mengine ya Mbwenkulu pamoja na Kilanjelanje nahii ni barabara ambayo tayari imeshajengwa, ni *trunk road* lakini hii alama ya "X" ya kijani imewekwa kwenyemaeneo ya nyumba za watu. Sasa nataka kujuua mna mpango wa kuipanua hii barabara maana tayari imeshakuwa ni ya lami lakini mmewafuata wananchi huko waliko. Mna mpango wa kuipanua ama mnataka kujenga tena nyingine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; tatizo la alama ya "X" liko pia hata kwenye maeneo ya Jimboni kwangu maeneo ya Milola pamoja na Lutamba ambako kuna barabara ya mkoa inayotoka Lindi Mjini kuelekea Ruangwa. Barabara hii ina muda mrefu haina mpango wa kuendelezwa lakini pia alama za "X" zimekwenda kuwekwa kwenye nyumba za watu ambapo nyumba nyumba zenyewe mnazijua, ni nyumba za miti na nyumba sasa zinabomoka.

**SPIKA:** Sasa swalii!

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Naomba kujua, ikiwa nyumba zitabomoka kwa sababu mmezuia watu wasiendeleze, hawa wananchi mtawalipa fidia kabla ya kuanza kujenga hizo barabara? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bobali anazungumza kwamba kuna wananchi wa vijiji vya Nangurukuru, Mavuji, Kilanjelje ambapo tayari barabara imejengwa na anauliza je, tuna mpango wa kuipanua au kujengwa upya.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kuwa na hifadhi ya barabara ni takwa la kisheria, kwa hiyo, kuwepo na sheria inatupasa tu watu wote tuweze kutengeneza hii sheria lakini kwa sababu maalum, kwa sababu swalii lako la kwanza kwamba hifadhi ya barabara ni muhimu iwepo wa hiyo upanuzi wa barabara unaweza kafanyika wakati wowote lakini niseme tu kwamba kama Serikali lazima mtazamo wetu uwe miaka mingi ijayo. Kama hatuwezi kuipanua sisi lakini yaweza kuwa watoto wetu wakaja wakaipanua barabara hii. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa maeneo haya uliyoyataja waone tu kwamba upanuzi wa barabara sio suala la muda mmoja ni suala la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaweka hifadhi ya barabara kwa sababu maendeleo ya nchi yanakuwa, mahitaji ya barabara yanaweza yakahtajika miaka 100 ijayo. Kwa hiyo, niwaombe tu wananchi maeneo haya ya hifadhi tuendelee kuyatunza, yatatusaidia leo na siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara hii ya kutoka Lindi Mjini kwenda Ruangwa ziko nyumba ambazo kimsingi unasema ziko nyumba ambazo tunaona kwamba sio za kudumu. Kwa hiyo, niseme tu kwamba pale ambapo tutaanza upanuzi wa barabara, watakaokuwa na hizi nyumba zikiwa bado zipo zitatathminiwa kutokana na sheria inavyotaka. Iko Sheria ya Ardhi, iko Sheria ya Umiliki wa Ardhi lakini niseme kwamba fidia inaangalia mambo mengi, inaangalia hizo nyumba zitakazokuwepo, inaangalia rasilimali zingine kama ardhi.

Kwa hiyo, wale ambao bahati mbaya nyumba hizi hazitakuwepo kwa sababu ni *temporary* basi watapata fidia kutokana na rasilimali zingine ambazo zitakuwa kwenye maeneo ikiwepo ardhi, mimea na mazao mengine kama yatakuwepo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaenda na swali la mwisho kwa Wizara hiyo kwa siku ya leo. Litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe Mbunge wa Kavuu.

Na. 159

### **Kukamilika kwa Daraja la Kavuu**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Daraja la Kavuu limekwishakamilika.

Je, ni lini daraja hilo na barabara ya kutoka Majimoto – Inyonga vitaanza kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Mto Kavuu lililopo katika barabara ya Mkoa ya Majimoto – Inyonga ulikamilika mwezi Agosti, 2017 na magari yakaruhusiwa kupita kwenye daraja hilo. Aidha, ukomo wa uzito wa magari yanayoruhusiwa kupita kwenye daraja hilo la chuma (*Mabey Compact Bridge*) ni tani 30.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Majimoto – Inyonga yenye urefu wa kilometra 135 lilipo daraja hilo inapitika vizuri ukiacha kipande cha kilometra nne ambazo kuna maeneo korofi na kupitika kwa taabu wakati wa mvua. Mkandarasi wa kufanya matengenezo anasubiri mvua zikipungua aendelee na kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Katavi itaendelea kuboresha barabara ya Majimoto – Inyonga hususan maeneo korofi ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi milioni 446 zimetengwa kwa ajili ya kufanya matengenezo na kuboresha maeneo korofi katika barabara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kikwembe tafadhali, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba tu nianze kusema kwamba msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Viongozi wote wa Serikali yangu ninawaheshimu, ninawaheshimu sana na ninawapenda, lakini katika swali hili Serikali haijanitendea haki. Hakuna gari linalopita katika hii barabara, mimi nimetoka ziara huko.

Mheshimiwa Spika, hizi pesa zinazosemwa shilingi milioni 446 zilitengwa sio zimetengwa ni mwaka 2017/2018

sasa tuko kwenye bajeti ya 2018/2019. Ninachotaka kusema na ninauliza ni lini barabara hii itaanza kutumika kwa sababu haitumiki zaidi ya magari madogo ya DC na gari la Mkurugenzi ndio yanayoweza kupita tena kwa kuibia, hakuna gari linalopita. Wananchi wangu wanatoka Majimoto wanakuja mpaka Mpanda Mjini wanalala Mpanda Mjini kesho yake ndio wanapanda mabasi kwenda Tabora na sasa hivi njia ya Tabora haipitiki maana yake hata treni mabehewa hawajaongeza. Kwa hiyo, wananchi wangu wanapata shida, ni lini barabara hii ya Majimoto - Inyonga; toka daraja hili limekwisha mwaka juzi na alipita aliyekuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Ngonyani akalikagua na akatoa maelekezo tunasubiri kupatiwa mzani ili barabara ile ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa nashangaa naambiwa barabara inapitika, inapitika wapi mimi mwenyewe Mbunge wa Jimbo sijapita kwenye hii barabara, wananchi wangu hawajapita, inapitika vipi? Basi hizi hela mlizonitengea mwaka huu za *rehabilitation from Inyonga to Majimoto* kilometra 74 mmeweka shilingi milioni 170, naomba zitolewe haraka na barabara hiyo ianze kupitika haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa majibu ya Majimoto - Inyonga hatari kabisa hakuna barabara huko inasemekana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofatilia eneo hili ambalo ni korofi sana kuhusu daraja pia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu kwamba na mimi nitakuwa tayari kwa kweli kwa bahati mbaya katika Mkoa wa Katavi sikupata nafasi ya kutembelea nimetembelea mikoa mingi, lakini Mheshimiwa Mbunge mambo mengine tutajadiliana nitapenda nitembee na wewe tukiwa kule kule. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Wewe Msukuma wewe kiswahili kizuri rekebisha.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, niseme ni kweli kwamba ujenzi wa daraja kama nilivyo sema kwenye jibu la msingi limekamilika hata Mheshimiwa Mbunge amekiri pia katika jibu la msingi nimesema iko kipande cha kilometra nne ambacho kilikuwa bado ni kikorofi. Kwa hiyo, ujenzi wa daraja lazima uwe na mahusiano pia na barabara ambazo ziko karibu na eneo hili. Kwa kutambua hilo katika bajeti hii ambayo tumepitisha kipo kiasi kingine cha jumla ya shilingi milioni 452 kwenye maeneo mbalimbali ambayo yanaunganisha daraja hili ambayo tumetenga kwa ajili ya kufanya maboresho makubwa hili tatizo Mheshimiwa Mbunge analolizungumza tuweze kuliondoa.

Mheshimiwa Spika, zipo shilingi milioni 200 zingine ambazo tumezitenga ili tuweze kufanya usanifu tena na kufanya michoro katika eneo la Kibaoni kuja Majimoto. Kwa hiyo, hii inaonesha tu namna Serikali iko *committed* kuhakikisha kwamba eneo hili linapitika na niseme kwa kweli Jimbo hili ni kubwa maeneo ni makubwa na eneo hili linapata maji mengi sana ambayo yanaelekea mengine katika Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, eneo hili kwa kweli la Kavuu lina shida nydingi ndio maana lina shauku kubwa ya kutembelewa ili tuweze kubadilishana mawazo ili kwa upande wa Serikali tuweze kutatua yaliyopo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nakuomba tu uvute subira na hata baada ya kipindi hiki baadaye tuzungumze zaidi ili tuweze kupanga na kuratibu safari ya kwenda Kavuu, ahsante sana.

**SPIKA:** Hii mambo ya Mawaziri wanatembeatembea na Wabunge huko hairuhisiwi mpaka Spika atoe kibali.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona *gallery* zetu zimejaa kabisa leo tuna wageni wengi kweli ni heshima kubwa sana kwetu na wageni wetu pia mnaona baadhi ya viti viko wazi isiwashangaze sana baadhi ya Wabunge bado wamelala mpaka saa hizi hawajaamka kutokana na maumivu mbalimbali. Unajua jana habari nilizonazo ni kwamba Wabunge ambaao ni wapenzi wa Yanga mpaka sasa hivi

wamelala, hawajaweza kufika Bungeni hapa. Akina Mwigulu, akina Mkuchika nasikia baadhi yao wamelala na viatu vitandani maana yake hawakumbuki hata kuvua viatu. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini baadae watakuja Waheshimiwa kwa hiyo msiwe na wasiwasi, ahsante sana nilikuwa natoa tu taarifa kuhusu mahudhurio ya humu ndani yatarekebika tu wataamka mchana huu, *hangover* bado kubwa kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto swalii la Mheshimiwa Taska Mbogo litaulizwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

Na. 160

### **Kuanza Kazi kwa Chuo cha Afya Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI (K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO)** aliuliza:-

Wilaya ya Mpanda Mkoani Katavi ina Chuo cha Afya tangu mwaka 1975 na baadae chuo hicho kilifungwa kwa sababu ya uchakavu wa majengo. Miaka ya hivi karibuni chuo hicho kilianza kukarabatiwa ili kiweze kutoa mafunzo kwa Maafisa Afya.

Je, lini chuo hicho cha afya kitaanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Afya Mpanda kilikuwa kinatoa mafunzo ya maafisa afya wasaidizi kuanzia mwaka

1975 hadi 1998 ambapo kilisimamishwa kutoa mafunzo hayo, kutokana na mabadiliko ya kimfumo wa mafunzo. Usitishaji huu ulikuwa ni kwa vyuo vyote vilivyokuwa vikitoa mafunzo hayo ambavyo ni Newala na PHCA Iringa. Mwaka 2010 Wizara ilianza ukarabati wa chuo hicho ili kuweza kuanza kutoa mafunzo ya utabibu msaidizi na uugazi na ukunga ngazi ya Astashahada ukarabati ambao kutokana na ufinyu wa bajeti haukukamilika kwa wakati, hadi mwaka 2014 kwa kutumia ufadhili wa fedha kutoka Mfuko wa Dunia Mzunguko wa Tisa (*Global Fund Round 9*) tumeweza kukamilisha ukarabati huo mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, ukarabati huo umekamilika na mazingira ni mazuri sasa kwa kufanya kazi na kwa mafunzo. Lengo la Wizara kwa sasa ni kuanzisha mafunzo ya matabibu wasaidizi, wahudumu wa afya ya jamii na uugazi na ukunga kwa mwaka wa masomo wa 2018/2019 na hasa baada ya kupata watumishi wa kusimamia mafunzo. Hatua za kupata usajili na ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundii (NACTE) kwa mafunzo hayo umekwisha anza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 wizara imepeleka maombi ya ajira mpya kwa sekta nzima ambapo kati ya ajira 52,000 zinatarajiwani kutolewa na Serikali, tunatarajia sekta ya afya itapewa kipaumbele.

Aidha, katika kibali hicho kilichotarajiwani kutolewa na Serikali, vyuo vyaa afya vitapewa kipaumbele katika kupangiwa watumishi na Chuo cha Mpanda kitapewa kipaumbele cha kupangiwa watumishi wanaohitajila ili mafunzo yaweze kuanza rasmii mwaka wa masomo 2018/2019.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi swali la nyongeza tafadhali

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kutokana na kutoanza kazi kwa chuo hicho, miundombinu imeanza kuchakaa na pia kuna masuala ya wizi yanendelea katika chuo hicho, Serikali inasema nini kwa maana ya kunusuru miundombinu ya chuo hicho?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili lengo la chuo hicho ni kuzalisha wauguzi na matabibu na watu hawa ilikuwa wafanye mazoezi kwa vitendo katika Hospitali ya Mpanda, lakini ni hospitali ambayo ina changamoto nyingi kama uhaba wa wodi na vifaa tiba. Serikali inasema nini katika kuisaidia hospitali hiyo ya Mpanda?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Faustine Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, makusudio ya Serikali ni kuanza kutoa mafunzo katika mwaka wa masomo 2018/2019 na tunaamini sasa baada ya kuanza masomo haya hizi changamoto nyingine ndogo ndogo ambazo zimeanza kujitokeza za uchakavu pamoja na wizi zitakuwa zimepungua kwa kiasi kikubwa. Lakini pamoja na hiyo kauli ambayo ametoka kuisema Mheshimiwa Mbunge tutaimarisha ulinzi kuhakikisha kwamba udokozi ambao unafanyika pale hauendelei kutokea.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake la pili ameongelea suala la mazoezi kwa vitendo kwa wale wanafunzi watarajiwa katika chuo kile. Ni kweli na mimi nimepata fursa ya kutembelea Hospitali ya Mpanda ambayo tunaitumia kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ina changamoto nyingi sana lakini kusudio la Serikali pamoja na maboresho haya ambayo tumeyafanya katika chuo chetu hiki. Kusudio la Serikali na katika bajeti ambayo mmetoka kutupitishia Mkoa wa Katavi ni mmoja wa mikoa ambayo tumelenga kujenga hospitali kubwa mpya ya rufaa ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, ninaamini itakapokamilika hospitali hii wanafunzi hawa wataweza kupata fursa nzuri zaidi ya kuweza kupata mafunzo kwa vitendo.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Lubeleje na Waziri Kivuli utapata nafasi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi Wizara ya Afya mna lengo gani kuhusu Maafisa wa Afya? Kufunga vyuo vya Maafisa wa Afya Wasaidizi ambao walikuwa muhimu sana katika zahanati na vituo vya afya na kazi yao kubwa ilikuwa ni kutoa elimu ya afya, kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Kwa nini mlivifunga na mtafungua lini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kutoka kwa Bwana Afya Mheshimiwa Lubeleje.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa maafisa afya vilevile tuna vyuo 74 ambavyo vinatoa mafunzo mbalimbali katika kada hizi za afya. Naomba nikiri ni kwamba na sisi ndani ya Serikali tumekuwa tunafanya mapitio ya mahitaji na umuhimu wa kada mbalimbali katika sekta za afya sio kwamba tumefuta mafunzo katika kada hii ya Maafisa wa Afya ila sasa tumekuwa tunaangalia wapi tuweze kuongeza nguvu na kuwekeza nguvu kubwa zaidi ili katika hivi vyuo vyetu 74 viweze kuwa na tija na kuweza kutoa elimu stahiki kwa walengwa na mahitaji ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo swali la mwisho la nyongeza

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na nipongeze sana timu ya Simba. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na vyuo hivi vya afya kufungwa au kutokukarabatiwa pia vyuo vya maendeleo nchini vina hali mbaya sana na tunajua taaluma hii ni muhimu sana na ingesaidia pia kwenye masuala ya afya kwa ujumla wake. Je, ni lini Serikali itakarabati vyuo hivi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Faustine Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tunatambua ni kweli kada ya maendeleo ya jamii ni kada muhimu sana na ni kada mtambuka katika kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo na Serikali imeliona hilo na bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii tumetembelea baadhi ya vyuo ambavyo vinatoa elimu katika kada hii. Lengo la Serikali katika bajeti hii tumetenga tena fedha kuhakikisha kwamba ukarabati huu unaendelea kufanyika kwa awamu kwa kadri ya fedha tunapozipata.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo linalekezwa Wizara ya Nishati litaalizwa na Mheshimiwa Joseph Leonard Haule Mbunge wa Mikumi.

Na. 161

### **Hitaji la Nishati ya Umeme Jimbo la Mikumi**

**MHE. JOSEPH L. HAULE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Jimbo la Mikumi hasa katika Kata ya Ulaya, Zombo, Tindiga, Mhenda, Kilangali, Vidunda, na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mikumi lina vijiji 57 na kati ya vijiji hivyo 16 vina umeme. Katika utekelezaji wa azma ya Serikali ya kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini ifikapo mwaka 2021 vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme katika Jimbo la Mikumi vitapatiwa umeme kupitia mradi wa REA Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza na wa pili.

Mheshimiwa Spika, vijiji nane nya Ihombwe, Kwalukwambe, Vidunda, Madizini, Zombolumbo, Malui, Udung'hu na Kigunga vimejumuishwa katika mpango wa kupatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu wa Tatu mzunguko wa kwanza. Kazi za kupeleka umeme katika vijiji hivyo zitahusisha ujenzi wa kilometra 26 za njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 33 na kilomita 32 za njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 0.4, ufungaji wa transforma 16 na uunganishaji umeme wateja wa awali 533. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 2.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza katika Mkoa wa Morogoro umekwishaanza na Mkandarasi Kampuni ya *State Grid Electrical and Technical Works Ltd.* anatarajia kukamilisha kazi hizo mwezi Juni, 2019. Vijiji vilivyobaki 33 vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haule nilikuona swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, asante sana, kwanza nionyeshe masikitiko yangu makubwa sana Jimbo la Mikumi ni jimbo la kitalii pia limebarikiwa kuwa na kidatu ambayo inasambaza umeme kwenye maeneo mengine. Jimbo la Mikumi linausikia tu huo umeme kwenye bomba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati alitembelea Jimbo la Mikumi na aliwaahidi wananchi wa Mikumi wa Kata Ulaya, Tindiga, Zombo, Masanze, Muhenda, Malolo, Uleli Ng'ombe, Kisanga, Luhembe, Kilangali, Tambuka Reli na Msimba katika Mji Mdogo wa Mikumi kwamba watapata umeme kwa wakati muafaka. Je, Serikali ni lini itatimiza ahadi yake ambayo iliwaahidi wananchi wa Jimbo la Mikumi?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili Serikali imeingia mkataba na mkandarasi anaitwa *State Grid* na Serikali ilisaini

mkataba kwamba watawalipa wakandarasi asilimia 10 ya ule mkataba ambao walikuwa wamekubaliana lakini mpaka leo *State Grid* hawajalipwa hata shilingi moja kiasi kwamba inasababisha wanafanya kazi kwa kusuasua na hao watu ni muhimu kwetu kwa sababu wanawafuta machozi wananchi wa Mikumi ambao wana kiu kubwa ya kupata umeme. Je, ni lini Serikali itawalipa wakandarasi hawa wa *State Grid* ili waweze kuendelea kufanya kazi yao iliyotukuka kule Mikumi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, maswali yake mawili alijielekeza kwanza kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati aliyoifanya katika Jimbo la Mikumi na ahadi yake ya kuyapatia umeme maeneo ambayo ameyataja ikiwemo maeneo ya Ulaya na kata zingine. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na kutokana na jibu langu la msingi kwamba maeneo yote haya yatapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA Awamu ya Tatu unaoendelea mzunguko wa kwanza na mzunguko wa pili*. Na kama mwenye Mheshimiwa Mbunge alivyouliza swalii la nyongeza amekiri kabisa kuwepo kwa mkandarasi anayeitwa *State* katika Mkoa wa Morogoro ambaye amepewa kazi ya kusambaza miundombinu ya umeme awamu ya kwanza.

Kwa hiyo, nataka nimthibitishie ahadi ya Mheshimiwa Waziri iko pale pale na muda muafaka ni kuanzia sasa mpaka Juni, 2019 awamu ya kwanza ambako vijiji tisa vitapatiwa umeme lakini kwa vile ambavyo vinasalia ni awamu ya pili ambayo mzunguko utaisha Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili nataka niseme mkandarasi *State Grid* ni kweli alikuwa hajalipwa asilimia 10 lakini kwa kweli hii ilikuwa ni kutokana na yeze mwenyewe kuchelewa kuwasilisha *document* mbalimbali ambazo zilitakiwa ili aweze kukidhi vigezo vya kulipwa asilimia 10 ya mkataba. Moja ya kigezo ambacho alishindwa kukitimiza kwa wakati ni uwasilishaji wa *performance bond* katika

Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Lakini nataka nimthibitishie amekamilisha na utaratibu wa malipo unaendelea. Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi huyu anaendelea na kazi na ndio maana katika Wilaya yake ya Kilosa ameshaendelea kuwashaa umeme katika Kijiji cha Mandela.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Waziri maswali ya umeme ni mengi yaani, huku tumchukue Mheshimiwa Devotha Minja, CCM tumchukue Mheshimiwa Omary Mgumba kwa kuanzia.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Katika Kijiji cha Matongolo, Kata ya Dumila, Wilaya ya Kilosa ni miaka mingi nguzo za umeme zimesambazwa chini, nguzo zilizounuliwa kwa kodi ya Watanzania mpaka zimeanza kuoza huku wananchi hao wakiwa hawana umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwa wananchi wa Kijiji cha Matongolo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, kwa kifupi tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri Mheshimiwa Devotha Minja amepata kunieleza hili jambo la kwamba katika Kijiji cha Matongolo, Kata ya Dumila kuna nguzo za umeme zimewekwa muda mrefu lakini mpaka sasa wananchi wa maeneo hayo hawajapatiwa huduma hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhaidi na nilimwahidi Mheshimiwa Devotha Minja kwamba tutafanya ziara katika kijiji hicho ili kujiridhisha nini kilijiri na nani aliyesababisha kuwepo kwa nguzo ambazo muda mrefu zimekaa na zinaweza zikaharibika ikawa hasara, tutachukua hatua kwa ambaye amehusika na masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini nilimthibitishia Wakala wa Nishati Vijiji wanaendelea kufanya sensa ya maeneo ambayo miradi ya awamu ya kwanza au ya pili ya likwama kwa sababu nyine yoyote, ili iweze kuwapatia wakandarasi na kukamilisha maeneo yale. Kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba nguzo zipo lakini tu kilichofanyika nguzo hazikusimamishwa na huduma haikupatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nilithibitishie Bunge lako na maeneo haya yapo, si mengi, lakini katika mikoa mbalimbali na kila ambapo tulipokuwa tukibaini basi tulikuwa tunaelekeza na kazi inafanyika. Kwa hiyo, nikuthibitishie maeneo yote haya tutayafanya kazi, ili ile huduma iliyokusudiwa na Serikali iweze kupatikana. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge wa Longido na Mheshimiwa Mbunge wa Bunda, maswali ya nyongeza, tuanze na Longido.

**MHE. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na kwa kunipa nafasi niulize swalidogo la nyongeza katika sekta hii.

Mheshimiwa spika, kwa kuwa tatizo la Mikumi halina tofauti sana na tatizo la Longido, kwanza nipende kuishukuru Serikali kwa sababu katika Awamu ya Pili kati ya Kata 18 za Wilaya ya Longido 10 zilifikiwa na umeme, kati ya vijiji 49 vya Wilaya ya Longido vijiji 19 vilifikiwa na umeme na kati ya vitongoji 176 vya Wilaya yangu, vitongoji 36 vilifikiwa na umeme kwa ajili hiyo kwanza nitangulize shukrani kwa Serikali kwa kutufanya kazi hiyo nzuri ambayo wananchi wanaifurahia.

Mheshimiwa Spika, swalidogo la REA Awamu ya Tatu ndio inakuja sasa, je, hivi vijiji vyangu 30 ambavyo bado havijafikiwa lini vitaanza kupelekewa umeme, ukizingatia kwamba nina Tarafa moja ya Ketumbeine yenye vijiji zaidi ya 20 na Kata sita kubwa ambazo bado hazijaguswa kabisa na umeme huu? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunapokea shukrani zake na yeye tunampongeza pamoja na ugeni wake, lakini amekuwa akifanya kazi katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme kwa Awamu hii ya III inayoendelea Mkandarasi wa Mkoa wa Arusha ni Kampuni ya *Nipo Group Limited* na kwa kweli, katika moja ya wakandarasi wanaofanya vizuri yeye ni mmojawapo, anaendelea na kazi na hivyo vijiji 30 ambavyo ameviainisha vitapatiwa miundombinu ya umeme katika Awamu hii ya Kwanza ya Awamu ya Tatu, lakini pia vitakamilishwa katika mzunguko wa Awamu ya Pili ambayo inakamilika Juni, 2021. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la mwisho kabisa Mbunge wa Bunda

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Bunda kuna vijiji 21 ambavyo vimepewa nafasi ya kupewa umeme wa *REA* na kwa bahati nzuri Waziri ambaye alikuwa Naibu ambaye ni Waziri kwa sasa hivi Mheshimiwa Kalemani alifika pale na kufanya ufunguzi kwa Mkoa wa Mara, lakini vijiji vya Nyang'aranga, Bigegu, Nyaburundi, Nyabuzume, Marambeka na vijiji vingine viliviyobaki kama wamekata tamaa hivi, ni muda mrefu sana hawajapata umeme na kasi ya kuweka umeme wa *REA* katika Jimbo la Bunda ni ndogo sana, katika vijiji 21 ni vijiji viwili tu vimeanza kuwekewa nguzo.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujiuliza yako malalmiko kwamba, mkandarasi anayefanya kazi Mkoa wa Mara hajalipwa malipo yake. Iko kwamba kuna kasi ndogo ya kuweka umeme katika Mkoa wa Mara na hasa Jimbo la

Bunda. Naomba kujua kwa Waziri ni lini vijiji hivi sasa vitapata umeme?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amethibitisha hapa ndani ya Bunge kwamba kati ya vijiji vyake ambavyo vimeainishwa kupata umeme katika awamu hii kazi imeanza kwenye vijiji viwili, lakini naomba nimthibitishie katika Kijiji cha Nyabehu, *Mugaja Central* na *Mugaja Primary* umeme umeshawashwa. Kwa hiyo, alichokuwa anasisitiza anasema kasi ndogo, lakini nataka nimthibitishie mkandarasi DERM ambaye anafanya katika Mkoa wa Mara kazi anaendelea, lakini changamoto ambayo ameieleza ilikuwa tu ya mradi wa *REA Awamu ya Pili* kwamba ndio alikuwa na madai, lakini tumekaa naye na utaratibu wa malipo unaendelea, lakini yeye kazi za mradi wa Awamu ya III anaendeleanazo.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu mikataba hii ni tofauti naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, utekelezaji wa kazi za *REA Awamu ya* *Tatu hazihusiani* na za *REA Awamu ya Pili*, lakini kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaendelea na uhakiki wa madai ya *REA Awamu ya Pili* na wakandarasi watalipwa na Mkandarasi huyo DERM ataendelea na kazi pamoja na malipo yake kuwa ynaendelea kuandaliwa. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la mwisho kabisa la nyongeza kule mwisho tafadhal!

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, asante, ninaitwa Daniel Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki. Nashukuru kwa nafasi hii niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme la Mikumi ni sawa na tatizo la umeme Manyoni. Katika vijiji vyangu vya Chikombo, Mpola, Nkonko, Iseke, Igwamadete, Sanza, Ikasi, Chisinjisa, Imalampaka na Mazuchii, ilikuwa vipate umeme tangu *REA Awamu ya Pili*, lakini mkandarasi alishindwa kazi

akatimuliwa na Serikali. Je, ni lini sasa Serikali itamleta makandarasi mwingine aweze kukamilisha kazi hii? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kuwapa fursa Wabunge mbalimbali kuulizia masuala ya nishati ndani ya Bunge. Na niwashukuru Wabunge wote waliopata fursa na wanavyoweza kufuatilia masuala ya nishati katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, nipende kuchukua fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kujibu swali la Mheshimiwa Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki kuhusu suala la miradi ya *REA* na vijiji ambavyo ameviaainisha ambavyo vilitakiwa kupata miundombinu ya umeme kwenye mradi wa *REA* Awamu ya Pili. Na kama mwenyewe Mheshimiwa Mbunge alivyosema kweli, kulikuwa na matatizo ya mkandarasi ambaye alikuwa anaitwa *Spencon* na Wizara kuititia Wakala wa Nishati Vijijini ilichukua hatua, mkandarasi yule tulisitisha mkataba wake na taratibu za zabuni zilikamilika na mkandarasi ambaye wa kufanya kazi kwa vijiji ambavyo Mkandarasi wa *Spencon* aliacha na miundombinu na vifaa mbalimbali kazi katika maeneo ya Singida na Mkoa wa Kilimanjaro inaendelea kwa sababu wakandarasi walipatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge mimi na ye ye pamoja na Wabunge wa maeneo ambayo miradi hii ilikwama, pamoja na hata Mheshimiwa Waziri tutafanya ziara katika maeneo hayo kukagua hizo kazi zinavyoendelea, ili zikamilike kwa wakati na lengo tulikuwa tukiwapa miezi sita.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, muda umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona wakati wa maswali ya Wizara ya Nishati Wabunge ambao huwa wanasi mama kutaka kuiliza maswali ya nyongeza ni wengi sana, ni dalili ya kuonyesha kwamba, kuna mahali hapa endi *speed kidogo*. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sisi tungkuomba sana, hebu uwe karibu sana na watu wa Nishati kuhusu miradi ya *REA*. (*Makofi*)

Ukweli ni kwamba, miradi ya *REA* imesimama. Sasa kama imesimama lazima kuna shida mahali fulani, maana wakandarasi wapo, kila kitu, basi kwenye malipo hapo hebu kaeni mlirekebishe hilo vizuri maana hiyo, miradi ndio ukombozi wa Watanzania hasa, na fedha yenye we tume-*ring fence*, sasa tatizo ni nini? Na ipo, kwa hiyo, tunatoa wito mkae m-sort out hicho kitu. (*Makofi*)

Wageni waliopo Jukwa la Spika ni pamoja na mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Mwenyekiti wa Wamiliki wa Vyuo vya Afya Visivyokuwa vya Serikali (*AFECOT*), Ndugu Mahmoud Mringo. Ahsante sana Ndugu Mringo, kumbe wakati tunajibu swali la vyuo vya afya hapa wadau wako hapa hapa, ahsante sana Ndugu Mringo, karibu. (*Makofi*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni Katibu Mkuu Dkt. Leonard Akwilapo. Karibu pale ulipo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Profesa James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu - Elimu Ave Maria Semakafu. Ave-Maria maarufu alikuwepo wakati wa Bunge la Katiba hapa, wameambatana na Wenye viti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo vilivyoko chini ya Wizara hiyo ya Elimu. (*Makofi*)

Pamoja na hao pia, wako wadau au washirika wa maendeleo ambao ni wakutoka Canada, Ndugu Alice Birnbaum, karibu sana. Kutoka Canada pia Zebedayo Kyomo, kutoka *UNICEF* Pantalee Kapich, kutoka *DFID* John Lusingu, yuko wapi John? Hayupo eeh? *SIDA*, Ndugu Helena Reutesward kutoka *SIDA*, *UNESCO* Ndugu Faith Shayo na

wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Ndalichako ambao ni familia yake wakiongozwa na mama yake mzazi, Mama Mary Ndalichako. Karibu sana mama, karibu sana Bungeni kwetu. (*Makof*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 82 wa Mheshimiwa William Olenasha, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na Chuo cha Mipango, vyote vikiwa hapa Dodoma. Wageni hao karibuni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Waziri hukuniambia tu, wanatoka Ngorongoro wote hawa? Wanatoka Ngorongoro, aah! Hebu wale wanaotoka Wilaya ya Ngorongoro simameni, Yesu na Maria, aisee! Hongereni sana. Yaani halafu mtu anasimama Bungeni anasema hakuna maendeleo nchi hii, Jamani, eeh! Zamani kutafuta mmoja tu aliyeko Chuo Kikuu Ngorongoro huwezi kupata, mmoja, leo tazama na hiyo ni vyuo vya hapa Dodoma tu peke yake nchi inakwenda jamani, huo ndio ukweli. (*Makof/Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza kutoka Zanzibar, Mheshimiwa Talib Ali Talib ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini Magharibi. Karibu sana, karibu kada. (*Makof*)

Wageni 94 wa Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Mkoani Dodoma. Karibuni sana, ooh, wengine wako huku, karibuni sana. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaye ni Mwenyekiti wa Wazazi CCM Wilaya ya Mbulu, Ndugu Domiano Dia, karibu sana pale ulipo. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambao ni viongozi waandamizi wa *The Humanity Actions for Childrens' Foundation* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana, wako pale. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha CBEcha Mjini Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka ambao ni Madiwani wa Viti Maalum na makada wa CCM kutoka Mkoa wa Kagera. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani na makada kutoka kule Kagera. (*Makofi*)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wageni 59 ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Halafu kuna wageni saba ambao ni wanafunzi kutoka *Saint John*wakiongozwa na Ndugu Charles Njau, wale wa *St. John* karibuni sana popote pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni 50 ambao ni vijana kutoka Chama cha Skauti Tanzania Mkoani Dodoma wakiongozwa na Salama Katunda, ambaye yeye ni kiongozi wa Skauti Kanda ya Mashariki. Oohh! Skauti, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge huo ndio mwisho wa matangazo yetu. Sasa tuendelee, Katibu!

#### **NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Iko mingapi? Mitatu eeh! Katibu nitajie. Haya tuanzie visiwani Mafia.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa sambamba na Kanuni ya 47(1),(2) mpaka (3); nitaisoma kwa

ufupi tu; "Baada ya muda wa maswali kwisha Mbunge yeoyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zinavyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe, ili Bunge kujadili jambo halisi na la dharura na la muhimu kwa umma."

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu Kisiwani Mafia sasa hivi viboko zaidi ya 40 wamevamia maeneo ya wananchi wanarandaranda kama mbuzi. Shughuli za kijamii na za kiuchumi haziendelei tena.

Mheshimiwa Spika, ningemuomba pia Waziri wa Elimu azifunge shule katika Kata za Ndagoni, Balemi na Kirongwe kwa sababu wanafunzi wako katika hatari ya kuuawa na viboko. Wiki tatu zilizopita Mwenyekiti wa CCM kata ya Ndagoni ameuliwa na kiboko.

Mheshimiwa Spika, tumetoa taarifa kwa maana ya kuandika barua Wizarani, Wizara imepeleka wataalam, wataalam walipofika pale kitu walichokifanya wamepiga picha na wakaitisha mikutano ya wanakijji na kuwatisha kwamba yeoyote atakayechukua hatua za kuwauwa viboko wale atafungwa miaka 30 na jana wataalam wale wamerudi Dar es Salaam bila kuchukua hatua yoyote dhidi ya viboko wale.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba nitoe hoja na ninawaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono. Shughuli za Bunge leo zisimame tujadili jambo hili kwa sababu, kule wananchi hawafanyi shughuli zozote, wanafunzi hawaendi shule na wavuvi hawaendi baharini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Majibu umeyapata, hujaungwa mkono. Tunaendelea na Mheshimiwa Selasini. (*Kicheko*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ni jambo dogo tu, inawezekana wasaidizi wako kuna taarifa hawakupi, hasa zinazohusu ukumbi wetu. Baadhi ya viti katika ukumbi wetu sasa hivi ni hatarishi. Viti kama cha kwangu hiki leo kimenifinya makilio, ni lini viti vyako vitabadiishwa ili Wabunge waweze kufanya kazi zao katika hali ambayo watakuwa katika amani na salama? Ahsante sana. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa hawa watu wa ajabu sana, wanasema ni sehemu gani hasa? (*Kicheko/Makofi*)

*Point noted* Mheshimiwa Selasini, tumeichukua. Tuachie tatarudi na majibu ya uhakika. Asante sana.

Mheshimiwa Lubeleje, ndio wa mwisho.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuuliza jambo moja.

Mheshimiwa Spika, naomba Kauli ya Wizara ya Nishati, mvua kubwa zimenesha, mabwawa yote yamejaa maji, lakini kuna baadhi ya Wilaya umeme unakatika kila wakati kwa siku unaweza kukatika mara tatu, mara nne na jana kulikuwa na tukio kubwa Simba na Yanga, lakini umeme unakatika, Wilaya nydingi tu, hasa Wilaya ya Kongwa, Wilaya ya Mpwapwa, Chamwino pamoja na Gairo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba maelezo Mheshimiwa Waziri wa Nishati atoe kauli kama mabwawa yamejaa, ni sababu zipi ambazo zinafanya umeme ukatike katika Wilaya hizo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hili swalii ni muhimu sana, wananchi kule jimboni kwangu jana hawakuona Simba wakifanya vitu vyao, kabisa kwa sababu ya umeme. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, Wizara ya Nishati, muangalie, siku moja mje mjaribu kutufafanulia kidogo. Kwa kweli umeme unakatikakatika kila wakati kiasi kwamba imekuwa sasa taabu kidogo. Panahitajika baadae mje mtueleze hasa ni nini kinachoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nashukurusa sana. Baada ya hapa namkaribisha Mheshimiwa Chenge aweze kuendelea na shughuli za hapa mezani. (*Makof*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mtoa hoja, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Ndalichako. (*Makof*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu, likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na

kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu. Kwa heshima kubwa kabisa napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wake imara na kwa ujasiri wa pekee alionao katika kusimamia rasilimali za Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika jukumu hili la kusimamia sekta ya elimu, sayansi na teknolojia na ninamhakikishia kuwa nitaendelea kufanya kazi hii kwa moyo wangu wote na kwa uadilifu wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, kwa uongozi wake thabiti na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa usimamizi wake mzuri wa kazi za kila siku za Serikali. Miongozo na maelekezo mbalimbali wanayonipatia imesaidia kuboresha kazi katika Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uongozi wake uliotukuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Juma Nkamia kwa kuendelea kunipa ushirikiano mzuri na kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Spika Bunge la Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Job Ndugai; Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulla Ackson kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa weledi, hekima na busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Wenye viti wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuongoza mijadala ndani ya Bunge letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kuniunga mkono wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Ninawashukuru sana wazazi wangu kwa malezi mazuri ambayo wamenipatia. Kwa namna ya pekee kabisa ninamshukuru sana mama yangu mpendwa ambaye leo hii yupo hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 na maombi ya fedha zitakazoiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yallyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2017/2018. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ulizingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Dira ya Maendeleo ya Taifa pamoja na Sera zinazohusu Sektâ ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,337,348,364,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 663,123,000 zili kuwa ni kwa ajili ya Fungu 18 - Tume ya UNESCO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018 Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi 1,336,685,241,000 kwa ajili ya Fungu 46 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 419,843,419,000 zili kuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 918,841,822,000 zili kuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 1,005,731,159,774.73 ambayo ni sawa na asilimia 75 ya fedha

zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 321,824,364,822 ni kwa Matumizi ya Kawaida ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 77 ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, shilingi 683,906,794,925 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 75 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia Ithibati ya Shule na kutoa vibali vyta kuanzisha na kuendesha shule. Katika mwaka 2017/2018 jumla ya shule 154 zilizokidhi vigezo zimesajiliwa. Aidha, Wizara imetoe vibali vyta kuongeza tahasusi za masomo katika shule 37 na imetoe vibali vyta ujenzi wa shule mpya 112 zilizotimiza vigezo.

Aidha, ili kuhakikisha utoaji wa elimu unazingatia viwango vilivyowekwa, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Udhhibit Ubora na imeandaa Kiunzi cha Udhhibit Ubora kwa Shule pamoja na zana zake na kutoa mafunzo elekezi ya Mfumo kwa Wadhhibit Ubora wezesaji Kitaifa. Aidha, imefungua ofisi tano za Udhhibit Ubora katika Wilaya za Songwe, Kigamboni, Ubungo, Chalinze na Ushetu ili kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Elimu ya Sekondari kimeratibu na kusimamia ushiriki wa wanafunzi wa Kitanzania katika mashindano ya Uandishi wa Insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika mashindano hayo mwanafunzi Michael Msafiri Nyarangu aliyekuwa kidato cha nne mwaka 2017 katika Shule ya Sekondari Kibaha alishika nafasi ya Kwanza.

Aidha, mashindano ya Insha ya SADC wanafunzi wawili wameingia 10 bora na wanafunzi hao ni Neema Steven Mtwanga wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari Lugalo – Iringa na Fadhili Sanga wa Shule ya Sekondari Nasuli iliyopo Wilaya ya Namtumbo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya tathmini ya hali ya miundombinu katika vyuo vyote 55 vyta Maendeleo ya Wananchi na tathmini hiyo imebainisha uwepo wa uchakavu katika miundombinu, vifaa, mitambo na utumishi

wa watumishi katika vyuo hivyo. Aidha, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu wa miundombinu na imepanga kufanya ukarabati wa vyuo 20 vya maendeleo pamoja na kuongeza majengo katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018 Wizara imeratibu *scholarships* 135 za wanafunzi katika Vyuo vya nje ya nchi ambazo 10 za Jumuiya ya Madola zikijumuisha nane za Uingereza na mbili za New Zealand, 12 Urusi na 113 za China. Aidha, Wizara imekamilisha mchakato wa maombi ya *scholarships* za Jumuiya ya Madola kwa mwaka wa masomo 2018/2019 na kupendekeza majina 26 kwa hatua zaidi. Pia imefadhlili wanafunzi raia 10 wa China kusoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imeratibu kusainiwa kwa mkataba wa mahusiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Hungary ili kuwezesha upatikanaji wa fursa 30 za ufadhili kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu na tayari maombi kwa ajili ya mwaka 2018 yameshafanyiwa kazi na majina 30 yamependekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu la kuratibu na kusimamia uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu, Wizara imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya makubaliano na Serikali ya Finland katika mradi wa kuendeleza ubunifu nchini wenye thamani ya Euro 12,773,000, ambazo ni sawa na shilingi billioni 34.7 za Kitanzania. Pia imefanya makubaliano na Serikali ya Finland katika Mradi wa Pili wa Kuendeleza Ubunifu katika nchi za Kusini mwa Afrika ambapo Tanzania inaingia kwa mara ya kwanza. Mradi huo unalenga kuboresha ushirikiano wa kikanda wa ubunifu katika biashara na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha udhibiti na usimamizi wa rasilimali, Wizara imefanya ukaguzi wa mapato,

matumizi na usimamizi wa mali katika vyuo sita vya Ualimu ili kuhakikisha kwamba mapato Serikali yanakusanywa kikamilifu na matumizi yake yanazingatia sheria, kanuni na taratibu. Pia imefanya tathimini ya mali katika Makao Makuu ya Wizara, Vyuo 35 vya Walimu, Ofisi 11 za Udhibiti Ubora wa Shule na Ofisi 160 za Wilaya ili kutambua na kupata thamani halisi ya mali ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imetoe mafunzo ya menejimenti ya viashiria hatarishi yaani *risk management* kwa watumishi 243 walioko Makao Makuu ya Wizara pamoja na Taasisi zake na vihatarishi vinavyoweza kuisababishia Wizara kutofikia malengo yake viliorodheshwa na kuwekewa mikakati ya udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi, Wakala na Vyuo vya Elimu ya Juu viliuyo chini ya Wizara vinawajibika katika kufanikisha utoaji wa elimu bora nchini pamoja na kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu. Utekelezaji wa kazi za Taasisi unaonekana kwenye kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 20 hadi 41 na kwa sababu ya muda nitaeleza baadhi ya taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Taasisi ya Elimu Tanzania; katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Taasisi imeandaa na kuchapa vitabu vya kiada vya masomo saba ya darasa la nne na imeboresha vitabu vyote vya kiada vya darasa la kwanza hadi la tatu na nakala 8,450,000 zimekwisha chapwa na kusambazwa shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kuendesha mitihani katika ngazi elimu ya msingi na sekondari, ualimu na katika mwaka 2017/2018 pamoja na kutekeleza jukumu hilo la uendeshaji wa mitihani, Baraza limenunua mashine ya pili ya kufungia mitihani (*Poly Wrapping Machine*) na mashine ya rangi ya uchapaji wa mitihani (*Full Colour Printing Machine*). Mashine hizi mbili zitasaidia sana katika kuongeza ufanisi katika uchapishaji wa mitihani na kuimarisha usalama wa mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu Tanzania imefanikisha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi zifuatazo:-

Kigongo iliyoko Misungwi, Mugeza ya Ngara, Sima A – Bariadi kwako wewe Mwenyekiti; Ikungi - Singida Vijijini, Mundindi – Ludewa, Shule ya Wasichana ya Rugambwa pamoja na Shule ya Wasichana Jangwani. Pia imekamilisha kukarabati wa shule 10 kongwe kati ya 17 za awamu ya kwanza na tayari shule 10 zimekabidhiwa ambazo ni Shule za Sekondari ya Pugu, Mzumbe, Kilakala, Msalato, Ilboru, Same, Nganza, Mwenge, Tabora Wavulana na Tabora Wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imeendelea na ukarabati wa Shule saba kongwe za sekondari ambazo ni Ruvu, Dodoma, Bihawana, Bwiru Wasichana, Sengerema, Kondoa Wasichana na Korogwe Wasichana. Vilevile imeendelea na ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari na imeratibu ujenzi wa nyumba 40 za walimu ambapo nyumba 15 zimekamilika na pia imeweza ujenzi wa matundu ya vyoo 312 na madarasa 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi imeendelea na kazi ya ujenzi wa Chuo cha Ufundji Stadi cha Wilaya ya Namtumbo ambapo ujenzi unatarajiwaa kukamilika Septemba, 2018. Imejenga jengo la karakana ya umeme wa viwandani katika Chuo cha Ufundji Stadi cha Mkoa Mwanza ambao umefikia asilimia 90 na imeendelea na ujenzi wa Karakana katika Chuo cha Ufundji Stadi cha Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji limetengeneza na kuboresha mifumo ya kielektroniki kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Udhahili na Uhakiki kwa wanafunzi wa Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Afya vya Serikali, Mfumo Uganishi baina ya mifumo ya Baraza na vyuo ambao unarahisisha udahili uhakiki wa wanafunzi, Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Rasilimali katika Vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*ADEM*) umeendelea na jukumu lake la kuimarisha uongozi wa elimu na kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu. Katika mwaka 2018 sambamba na jukumu hilo, Wakala umefanya ukarabati wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanachuo 450 na kumbi mbili za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala pia imeendesha mafunzo kwa Walimu 1,568 wa Vituo vyta Elimu ya Nje ya Mfumo Rasmi (*MEMKWA*) yenye lengo la kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ili kuhakikisha kuwa wanafunzi ambao wanapata elimu nje ya mfumo rasmi wanapata elimu iliyo bora.

Kuhusu Bodii ya Mikopo ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi, raia wa Tanzania wanaosoma katika taasisi za elimu ya juu na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo. Katika mwaka 2017/2018 Bodii imetoe mikopo kwa wanafunzi 122,623 ambapo wanafunzi 33,244 ni wa mwaka wa kwanza na 89,379 ni wanaoendelea na masomo.

Pia Bodii imetoe mikopo na ruzuku kwa jumla ya wanafunzi 351 wanaoendelea na masomo nje ya nchi. Aidha, hadi kufikia Machi, 2018, Bodii ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 132.30 za mikopo illioiva ambayo ni sawa na asilimia 101 ya lengo la mwaka 2017/2018 ambalo ilikuwa ni shilingi bilioni 130. Kwa hiyo, hapa nikiweka msisitizo, tayari mpaka kufika Machi tulikuwa tumeshavuka lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Bodii ya Mikopo imewabaini wadaiwa sugu 147,231 na katii yao wadaiwa 42,213 wameanza kufanya marejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume imeratibu zoezi la udahili kwa jumla ya waombaji 63,737 ambao

wamedahiliwa moja kwa moja katika vyuo ambavyo wameviomba wenyewe. Pia imeandaa maonesho ya 12 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambayo yalitoa fursa kwa vyuo kuonyesha na kutangaza shughuli zao. Pia imefanya ukaguzi wa vyuo kwa lengo la kujiridhisha kama utoaji wa elimu ya juu unazingatia vigezo vya ubora vilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania imeendelea na jukumu lake la kudhibiti mionzi katika vituo vya huduma kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ilipima mionzi kwa wafanyakazi 423 kutoka vituo 68 na kubaini kuwa kiasi cha mionzi kilikua kwa kiwango kinachokubalika kimataifa. Pia imeendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa maabara ya kisasa na imepokea vifaa vya maabaraku toka Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, ambavyo vitasaidla Tume kutimiza kwa ufanisi majukumu yake ya kusimamia udhibiti na matumizi ya usalama katika nchi nii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Juu vimeendelea na kazi yake ya kufundisha, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na jamii kwa ujumla. Maelezo ya kina kwa kila chuo yanapatikana katika Kitabu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 42 mpaka wa 62. Sababu ya muda nitaelezea baadhi ya vyuo. Nitaanza na Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimetekeleza mpango wa Serikali wa kuunganisha mifumo yake ya kieletroniki kama vile *Student Academic Registration Information System* na kuwezesha malipo ya ada kufanyika kieletroniki katika Mfumo wa Malipo ya Serikali, yaani *Government e-Pay Gateway*. Kimeendelea kutoa bila malipo yoyote mafunzo ya TEHAMA kwa wanafunzi wenye ulemavu ambapo wanafunzi wasioona 42 na viziwi 37 walipata mafunzo na lengo ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum nao wanapata hii teknolojia ya habari na mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kimeboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kufanya ukarabati wa nyumba sita za makazi, mabweni 16, majengo sita ya ofisi, majengo mawili ya ofisi na kuwezesha upatikanaji wa ofisi tano za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mwaka 2017/2018 kimeendelea na ukamilishaji wa jengo la maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,600. Ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua washiriki 600 na taasisi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja. Maktaba hii ni ya kipekee kwa ubora na ukubwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dodoma kimefanya utafiti wa nishati mbadala za kupikia katika kaya nchini na utafiti katika Kanda ya Kati ya kutambua Sumu Kuvu (*Aflatoxins*) kwenye vyakula. Pia imefanya tafiti nne zilizolenga kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji katika stadi za kusoma kuandika na kuhesabu. Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia kuboresha ufundishaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Mzumbe kimejenga madarasa na jengo la utawala Kampasi ya Mbeya ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za utawala chuoni na ongezeko la madarasa litatoa fursa ya kuongeza udahili wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kimetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo kimefanya tafiti za genetiki za uzalishaji wa mbegu bora za mazao ambao umewezeza chuo kuzalisha mbegu bora za aina nne za maharage. Mbegu hizo zina uwezo wa kuzaa zaidi na kustahimili ukame na magonjwa na hivyo kuwa na manufaa zaidi kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia chuo kimefanya tafiti kuhusu kuzalisha mbegu bora mbili za mpunga ambazo ni mwangaza na kalalu. Mbegu hizi zimesaidia mkulima kukabiliana na ugonjwa wa mpunga na hivyo kufanya kilimo cha mpunga kuwa na tija zaidi. Kimefanya utafiti wa kutumia menejimenti ya ekolojia kudhibiti panya kwenye mazao ya mahindi na mpunga na kimeanza ujenzi wa jengo la wanafunzi wa Shahada za Uzamivu katika Shule Kuu ya Uchumi, Kilimo na Masomo ya Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kimeendelea na ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo katika Kampasi ya Mloganzila, kimeratibu ufunguzi wa majaribio na ufunguzi laini wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Mloganzila iliyozinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 25 Novemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kimeendelea na ujenzi wa mabweni na majengo mengine ya ufundishaji katika Kampasi ya Mloganzila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimefunga viti visivyohamishika kwenye madarasa matano katika Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 692 kwa wakati na kimeendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuweka wanafunzi 720 kwa wakati mmoja ambavyo vyote kwa pamoja vitaboresha mazingira ya wanafunzi katika kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kimetoa ushauri elekezi katika miradi ifuatayo; ukarabati wa shule za sekondari 17 na Vyuo vya Ualimu 15, ujenzi wa ofisi za Hal mashauri ya Wilaya ya Kiteto na Mafia, ujenzi wa barabara ya lami ya Sumbawanga na ujenzi wa jengo la x-ray katika Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya. Pia kimeendelea na ujenzi wa maktaba ambayo itakuwa na uwezo wa kuweka wanafunzi 2,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundı Arusha kimeanza programu za Stashahada zinazohusu Uhndisi wa masuala ya Mabomba, Mafuta, Gesi na Uzalishaji wa umeme. Programu hizi zitawezesha vijana wetu kushiriki kikamilifu katika fursa ambazo zinapatikana katika maeneo hayo. Pia kimepata vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia iliyonunuliwa kwa mkopo wenyе masharti nafuu kutoka Serikali ya Australia na kimekamilisha ujenzi wa bwawa la kuvuna maji na miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mafunzo la umwagiliaji liliopo Oljoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imeweka vifaa vya TEHAMA katika jengo la kufundishia (*Teaching Tower*) na jengo hilo ambalo ujenzi wake ulikuwa unaendelea limekamilika na tayari limezinduliwa rasmi na limeshaanza kutumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela imefungua vituo vinne vya umahiri vya kimataifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Utafiti na Umahiri cha Ufundishaji Endelevu katika Chakula, Uhifadhi wa Virutubisho na usalama wa chakula, Kituo cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu, Kituo cha TEHAMA cha Afrika Mashariki na Kituo cha Ubunifu wa Teknolojia na Nishati. Vituo hivyo vimeongeza ari ya kufanya utafiti na idadi ya wanafunzi wa masomo ya uzamili na uzamivu. Pia imeanzisha mradi wa utafiti na uzalishaji wa ndizi bora zenyе kuhimili magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie utekelezaji wa miradi ya maendeleo na nitaanza na programu ya lipa kulingana na matokeo (*EP4R*). Programu hii imewezesha ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika Vyuo saba vya Ualimu vya Tandala, Nachingwea, Tarime, Kinampanda, Mandaka, Patandi na Ilonga. Aidha, Chuo cha Ualimu cha Murutunguru kitajengwa upya kwa sababu uchakavu wake ulikuwa ni mkubwa na hakifai kufanya ukarabati. *EP4R* imewezesha pia ujenzi wa mgahawa wenyе uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine

cha Kilimo, lakini imewezesha pia ununuzi wa magari 54 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za udhibiti ubora wa shule, ufuatiliaji na tathmini na imewezesha ujenzi wa miundombinu katika shule 290 iliyojumuisha pamoja na mambo mengine madarasa 1,308, matundu ya vyoo 1,560, mabweni 129, nyumba za walimu nane pamoja na mabwalo saba, majengo ya utawala nane, maabara nne na maktaba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuimarisha Stadi za Mafunzo ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu unafadhiliwa na Mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu (*Global Partnership for Education - GPE Fund*). Katika mwaka 2017/2018 programu hii imewezesha ukamilishaji wa Kiunzi cha Udhibiti Ubora wa Shule na imewezesha ununuzi wa pipipiki 2,894 kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji wa elimu kwenye ngazi ya kata. Pia imewezesha ununuzi wa magari matano kwa ajili ya kuimarisha shughuli za udhibiti ubora wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu unagharamiwa na Serikali ya Canada kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania na unatekelezwa katika Vyuo vya Ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Kitangali na Ndala. Katika mwaka 2017/2018 ujenzi umeendelea katika Chuo cha Ualimu Shinyanga ambapo nyumba za Walimu zimekamilika, lakini pia ujenzi wa mabweni mawili, madarasa, maktaba na ukumbi wa mihadhara unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Chuo cha Ualimu Mpuguso ujenzi unaendelea wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 308, nyumba za kwa ajili ya familia 13, maktaba, maabara, kumbi za mihadhara na ukumbi wa mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Chuo cha Ualimu Kitangali vilevile nyumba za walimu 11 zinajengwa, madarasa 16, maktaba, ukumbi wa mihadhara na mabweni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 308.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Chuo cha Ualimu Ndala nyumba za wakufunzi zenyet uwezo wa kuchukua familia nane na nyumba ya Mkuu wa Chuo zinaendelea na aidha, sehemu ya pili ya ujenzi ambayo itahusisha mabweni, madarasa, ukumbi wa mihadhara umeanza tarehe 24/2/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu unalenga kuimarisha Mafunzo ya Ualimu katika Vyuo 35 vya Ualimu vya Serikali. Katika mwaka 2017/2018, kupitia mradi huu umefanyika ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuimarisha utoaji wa Elimu ya Ualimu. Pia mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Walimu yamefanyika ili mtaala uendane na Elimu ya Msingi ulioboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 120 yaliyojumuisha elimu ya jinsia na elimu jumuishi yametolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ina jukumu la kuratibu na kutoa ushauri kuhusu elimu, sayansi, habari na utamaduni katika muktadha wa Kimataifa. Katika mwaka 2017/2018 Tume imeandaa na kuchapisha na kusambaza jarida la Tanzania na *UNESCO* Toleo la 14 na imeandaa maandiko saba ya miradi kwa ajili ya kuombea ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utekelezaji, sasa naomba nijielekeze kwenye Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 na nitaanza na kipengele cha kuimarisha ujuzi na kuendeleza ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara itatekeleza yafuatayo; kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi kwa kutoa ruzuku kwa ushindani kwa Vyuo vya Ufundis nchini; kuendelea kutoa ruzuku za masomo ya ufundi kupitia *scheme* za vocha za mafunzo kwa vijana wasio na uwezo wa kujiendeleza ambapo jumla ya vijana 7000 watanufaika. Pia itanunua

vifaa ili kuwezesha vyuo vya maendeleo ya wananchi 20 kuweza kutoa mafunzo ya ufundi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa usajili wa shule, Vyuo vya Ualimu na vituo nje ya mfumo rasmi na itafanya ukaguzi wa asasi 11,327 zikiwemo shule za msingi 8,785 na sekondari 2,480 na vyuo vya ualimu 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie usimamizi wa elimu msingi na sekondari. Katika mwaka 2018/2019 eneo hili litaandaa mwongozo wa kitaifa wa uendeshaji wa elimu ya awali unaozingatia viwango vilivyowekwa na itafanya ufuatiliaji wa utoaji wa elimu ya awali, msingi kwa kuzingatia matokeo ya upimaji wa kitaifa wa darasa la pili, darasa la nne pamoja na mitihani ya kumaliza darasa la saba na mtihani wa kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara yangu itaendelea kusimamia masuala mtambuka na itawajengea uwezo walimu wa malezi shulenii na katika Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha huduma ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi. Pia itaendesha mafunzo ya elimu kwa afya na usafi wa mazingira kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika mikoa 10 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa elimu ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum na itatekeleza masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itakamilisha Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi kwa mwaka 2018 hadi 2021 ili kuwawezesha wadau wa elimu kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika kuimarisha elimu jumuishi, lakini pia itafanya ufuatiliaji wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum ili kubaini changamoto wanazozipata na kupatia ufumbuzi wa changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepanga kuratibu ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Mkoa wa Kagera na itaendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafundi ya Ufundı Stadi katika Mkoa wa Njombe ambapo ujenzi huu ulikuwa umekwama kutokana na uwezo mdogo wa mzabuni *Herkin Builders Limited* ambaye hakufanya kazi ambavyo inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara itasimamia kuanza kwa ujenzi wa Vyuo vya VETA vya Mikoa ya Rukwa, Simiyu na Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa sayansi, teknolojia na ubunifu; katika mwaka 2017/2018 Wizara itatambua na kutegemeza teknolojia zinazosalishwa nchini na kuweka mazingira bora ya upatikanaji, uhaulishaji na uhauwilishaji wa teknolojia hizo. Itaandaa mpango kazi wa kusimamia uanzishwaji na uimarishaji wa vituo na kuendeleza teknolojia na ubunifu nchini na itaandaa mkakati wa kukuza ujuzi na utaalam asilia na ubunifu nchini katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika kazi zitakazofanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara yangu. Malengo ya Taasisi kwa mwaka 2018/2019 yanaonekana katika ukurasa wa 86 hadi 123 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaeleza taasisi chache na nitaanza na Taasisi ya Elimu Tanzania. Katika mwaka 2018/2019 taasisi itatekeleza shughuli zifuatazo: itaendelea na uandishi wa vitabu na moduli za mafunzo ya ualimu itaanza kurusha vipindi vya kikaragosi (*cartoons*) kwa lengo la kuwezesha wanafunzi kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na itaandaa vitabu vya hadithi kwa ajili ya shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itaandaa na kutoa mafunzo ya wawezeshaji wa programu za kisomo na kufanya kampeni ya kisomo kwa kanda za kitaaluma. Pia itajenga na kuweka mtandao wa TEHAMA ili kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na

ujifundishaji katika programu zote zinazotolewa na taasisi. Aidha, itaongeza udahili wa wanafunzi wanaosoma elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka wanafunzi 10,420 mpaka wanafunzi 12,000 na itafanya hivyo kwa kufungua vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi za sekondari katika mikoa mipyga ya Songwe, Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itafanya utafiti wa programu nje ya mfumo rasmi ili kubaini hali halisi ya sasa ya stadi za vijana na watu wazima wasiokuwa na stadi za kisomo na kupanga mikakati ya kuwapatia elimu stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundistiadi (*VETA*) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 200,000 mpaka 250,000; itaendelea na ujenzi wa karakana tatu za vyuo katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Manyara, lakini pia itaendelea na ujenzi wa karakana mbili za ufundistiadi za zana za kilimo na ufundistiadi wa uungaji vyuma katika Chuo cha Ufundistiadi Arusha; itaanza ujenzi wa vyuo vya ufundistiadi katika Wilaya ya Chunya, Kilindi, Nyasa na Ukerewe; na itamalizia ujenzi wa madarasa mawili na mabweni katika Chuo cha Ufundistiadi cha Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishwaji na uendeshwaji wa maktaba za shule, vyuo, taasisi na Halmashauri za Miji pamoja na Manispaa na Wilaya hapa nchini. Pia itafanya upanuzi wa Maktaba ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka cha Bagamoyo na Jengo la Maktaba Dodoma. Aidha, itaanza ujenzi wa Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa wananchi katika mikoa hiyo kupata huduma za maktaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imepanga kuunganisha na kuifanya mifumo ya upangaji, ulipaji na urejeshaji mikopo kuijendesha (*Full Automation and Integration of Systems*) na itatoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 427 kwa wanafunzi wapatao 123,285. Itaendelea na utekelezaji wake wa

mkakati wa kukusanya marejesho ya mikopo ilioiva ambapo inatarajia kukusanya jumla ya bilioni 157.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itaendelea kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kurejesha mikopo pamoja na taratibu zinazohusu utoaji na urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania itafanya ukaguzi wa vyuo 20 vya elimu ya juu kwa lengo la kuhakikisha ubora wake unakidhi, lakini pia itafanya uhakiki wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza ili kujiridhisha kama wamekidhi vigezo vya kudahiliwa katika *program* husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itaananza na kuendeleza atamizi za ubunifu katika Halmashauri za Miji ya Mbeya na Dodoma na itawatambua wagunduzi na wabunifu nchini na kuwawezesha kuendeleza ubunifu na ugunduzi wao ambapo miradi 20 ya wabunifu itafadhiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Tume itahamasisha matumizi ya teknolojia mpya kama *Bioteknolojia, Nanoteknolojia, Mekatroniksina Bigdata* ili kuchochea ukuaji wa uchumi na hasa uchumi wa viwanda wa Mheshimiwa Mwijage. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa itaananza na kuendeleza kumbi za ubunifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Tume ya Nguvu za Atomiki itaanaza ujenzi wa maabara awamu ya pili na itaendelea na ukaguzi katika migodi sita inayofanya kazi ili kubaini hali ya viwango vya mionzi na usalama kwa ujumla. Pia itaendelea na ukaguzi wa vituo vipatavyo 150 vyenye vyanzo vya mionzi na kupima kiasi cha mionzi katika sampuli angalau 6,000 za vyakula na mbolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Vyuo vya Elimu ya Juu vitaendelea kutekeleza jukumu lake la kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu. Maelezo ya kina ya vyuo vyote yanapatikana katika ukurasa wa 98 hadi 118 wa Kitabu changu cha hotuba na kwa sababu ya muda nitaelezea baadhi ya vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; katika mwaka 2018/2019 chuo kinatarajia kuongeza idadi ya miradi ya utafiti kutoka 209 hadi kufikia 250 sawa na ongezeko la asilimia 20. Pia inatarajia kuongeza idadi ya machapisho katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa kutoka 250 hadi 390 ambalo ni ongezeko la asilimia 10 na kuongeza idadi ya majarida ya Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka tisa hadi 24 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimepanga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3,250 hadi 3,700 kwa shahada ya kwanza na kuongeza wanafunzi wa Uzamili na Uzamivu kutoka 171 hadi 400, lakini kitatoa elimu na ushauri wa kitaalam kwa washiriki 350 wakiwemo wakulima, Maafisa Ugani pamoja na Watafiti na kitaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na kutekeleza miradi ya tafiti iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, katika mwaka 2018/2019 kitaendelea na mpango wake wa kuboresha huduma kwa wagonjwa na mfumo wa taarifa za wagonjwa; kitakamilisha uandaaji wa mpango wa uzalishaji mali wa Hospitali ya Kufundishia ya Mloganzila; kitakamilisha ujenzi wa kituo mahiri cha magonjwa ya moyo cha awamu ya kwanza katika Kampasi ya Mloganzila na kitaendelea na tafiti za magonjwa ambukizi, magonjwa yasiyoambukizwa na magonjwa yasiyopewa kipaumbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa katika mwaka 2018/2019 kitakamilisha ujenzi wa maabara ya sayansi na *computer*, kitatekeleza miradi 13 ya

utafiti na utoaji ushauri na kitatoa chapisho la tatu la jarida la chuo *Mkwawa Journal for Education and Development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam katika mwaka 2018/2019 kitaendelea na ujenzi wa jengo la makazi ya utafiti pamoja na kuweka mifumo ya kiusalama na miundo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kitaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 2,409 hadi 4,500 na kuanza kutoa mafunzo ya wahandisi barabara katika ngazi ya Stashahada katika Kampasi ya Rukwa. Kitaandaa mfumo wa kuzalisha gesi kwa kutumia samadi kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuwasha taa kwa maeneo ya vijijiini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli za Taasisi, Wizara na Vyuo Vikuu sasa naomba nijielekeze katika miradi ambayo itatekelezwa katika mwaka 2018/2019 na nitaanza na mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 140 kwa ajili ya kufanya shughuli zifuatazo; kujenga madarasa 2,000 na matundu ya vyoo 2,000 katika shule za msingi na sekondari; kujenga mabwalo kwa shule 85 zilizopata hadhi ya kudahili wanafunzi wa kidato cha tano; kununua vifaa vya maabara katika shule 1,800 za wananchi; kukarabati shule kongwe 25 zikijumuisha shule za sekondari, Arusha, Weruweru, Shinyanga, Rungwe, Mawenzi, Bukoba, Mara, Mtwara Wasichana, Lyamungo, Masasi Wasichana, Lindi, Kilosa, Machame Wasichana, Sumbawanga, Tarime, Kibasila, Tunduru, Tumaini, Pamba, Mbeya Kutwa, Moshi Wavulana, Ifunda Wasichana, Iringa Wasichana, Ashira na Mwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itafanya ukarabati na upanuzi wa Vyuo nane vya Ualimu ambavyo ni Bustani, Vikindu, Mtwara Kawaida, Mtwara Ufundii, Singachini, Monduli, Bunda na Katoke. Pia itafanya ununuizi wa magari 20 kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vinne vya Ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu umetengewa jumla ya shilingi bilioni 20,241,960 kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo; kununua vifaa vya kufundishia kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu 35; kununua vifaa kwa ajili ya elimu maalum katika Vyuo vya Patandi, Mtwara Ufundu na Mpwapwa. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na kununua vifaa vya TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu na kuviunganisha na Mkongo na wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itatoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 821. Pia tutaoa mafunzo kazini kwa wakufunzi 1,439 katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na lugha, elimu ya awali, sayansi, hisabati, sayansi ya jamii na elimu ya afya. Pia kupitia mradi huu tutaandaa mfumo wa mawasiliano wa utunzaji wa taarifa za elimu ya ualimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari; kupitia mradi huu Wizara inapanga kujenga shule mpya za sekondari za kisasa kabisa katika mikoa saba ambayo ni Mkoa wa Njombe, Lindi, Singida, Katavi, Geita, Ruvuma na Manyara. Pia katika shule hizo tutajenga nyumba za walimu nane katika kila shule mpya na tutanunua samani na vifaa vya kujifunzia katika shule hizo mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako niweke msisitizo, tunakarabati shule kongwe, lakini haiwezekani shule kongwe zilikuwa ni zile tu tangu tunapata uhuru. Sasa awamu ya tano inatengeneza shule kongwe mpya ambazo tunaanza kuzijenga mwaka wa fedha 2018/2019. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumie mradi wa kukuza ujuzi (*Tanzania Innovation Systems*) au kwa kifupi TANZIS. Kupitia mradi huu Wizara itaibua na kutambua wabunifu 70 mahiri kwa lengo la kusaidia kukuza ujuzi wao

na itaimarisha mazingira ya ubunifu kwa kuwasaidia wabunifu wachanga kupata vifaa na msaada wa kitaalam ili kuendeleza mawazo yao katika mazingira halisi ya kibashara. Vilevile itawapatia nafasi wabunifu kutembelea nchi ya Finland ili kujifunza mambo yatakayoweza kuendeleza ubunifu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nielezee kazi zitakazofanywa na Tume ya Taifa ya *UNESCO* ambayo ni Fungu Namba 18. Tume itaendelea kushirikisha Wizara, taasisi na umma kwa ujumla katika kuboresha masuala ya elimu, sayansi, habari na utamaduni. Pia itaendelea kushiriki katika kupanga na kutekeleza progamu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu na watumishi katika Wizara ya Elimu katika kufanikisha majukumu yetu na kipekee kabisa namshukuru kwa dhati Mheshimiwa William Tate Olenasha, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Nawashukuru Katibu Mkuu Dkt. Leonard Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kazi kubwa wanazozifanya pamoja na ushirikiano mkubwa wanaonipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Bodi, Kamisheni na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara kwa kuendelea kusimamia vyema taasisi zao. Pia nawashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, wamiliki wa shule binafsi, watumishi wote wa Wizara, wanataaluma, wanafunzi na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano mzuri wanaonipa. Maoni na mapendekezo yao yamekuwa chachu ya kuboresha utendaji wa Wizara yangu. Wizara itaendelea kutambua na kuthamini michango ya wadau wote wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi washirika mbalimbali wamechangia kufanikisha mipango ya elimu na kwa sababu ya muda naomba kutambua wachache. Washiriki hao ni

pamoja na Canada, China, Cuba, India, Italia, Hungary, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Uswisi, Marekani, Australia, Ireland, Ufaransa, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Korea ya Kusini, Ubelgiji, Jumuiya ya Afrika na Jumuiya ya Maendeleo ya Ulaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Washirika wa Maendeleo wamechangia ikiwa ni pamoja na *Global Partnership in Education*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *British Council*, *Japan International Cooperation Agency*, *Korea International Cooperation Agency*, *Swedish International Cooperation Agency*, Umoja wa Ulaya, *UNDP*, *UNESCO*, *UNICEF* na wadau wote ambao sikuweza kuwataja kwa sababu ya muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kwenye maombi ya fedha. Ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,406,469,626,000 ili kutekeleza majukumu yake ambapo fedha hizo zimegawanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 476,500,224,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Wizara na shilingi 383,838,645,092 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa taasisi zilizo chini ya Wizara. Shilingi 929,969,402,000 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi 618,969,400,000 ni fedha za ndani na shilingi 311,000,002,000 ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Tume ya *UNESCO* Wizara inaomba jumla ya shilingi 666,855,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kati ya fedha hizo shilingi 334,392,000,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 332,293,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninasimama kwa unyenyekevu na heshima kubwa kabisa kuliomba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili

na kuitisha makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu kwa mafungu yote mawili, yaani Fungu 46 na Fungu 48 yenye jumla ya shilingi 1,407,136,431,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu kabisa naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunisikiliza lakini pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, Kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2017/18. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2018/19.

2. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu. Kwa heshima na taadhima napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuiongoza Nchi yetu vyema na kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Vile vile, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa usimamizi mzuri wa shughuli za kila siku za Serikali na kunipatia Miongozo na Maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi katika hii Wizara. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**3. Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb) na Makamu Mwenyekiti Juma Nkamia (Mb) kwa kuendelea kunipa ushirikiano mzuri na kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**4. Mheshimiwa Spika**, Napenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi, busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyevitii wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza mijadala ndani ya Bunge letu Tukufu.

**5. Mheshimiwa Spika**, Naomba kuchukua fursa hii pia, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kwenye uchaguzi mdogo akiwemo Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Siha), Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia (Kinondoni), Mheshimiwa Damas Daniel Ndumbaro (Songea Mjini), Mheshimiwa Justine Joseph Monko (Singida Kaskazini) na Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Longido).

**6. Mheshimiwa Spika**, Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utelekezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/18 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 na maombi ya Fedha zitakazowezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yaliyopangwa.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA  
2017/18**

7. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2017/18 ulizingatia llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 – 2020/21, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, pamoja na Sera zinazohusu Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Bajeti Iliyoidhinishwa Katika Mwaka 2017/18**

8. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Wizara yangu iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 1,337,348,364,000.00** katika mafungu mawili tofauti, yaani Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia) na Fungu 18 (Tume ya Taifa ya UNESCO) ambalo nitaeleza utekelezaji wake baada ya Fungu 46.

**Bajeti Iliyoidhinishwa ya Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia)**

9. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Bunge lako Tukufu iliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,336,685,241,000.00** kwa Fungu 46 ambapo **Shilingi 419,843,419,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 916,841,822,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

10. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi 1,005,731,159,774.73** sawa na asilimia 75 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na kwa Miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo **Shilingi 321,824,364,822.48** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **77** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, **Shilingi 683,906,794,952.25** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **75** ya Bajeti ya Maendeleo.

11. **Mheshimiwa Spika**, Fedha zilizotumika hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 zilikuwa ni **Shilingi 749,795,644,445.99** sawa na asilimia **75** ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 281,874,146,587.30** zilitumika kwa Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 467,921,497,858.69** zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo.

#### KAZI ZILIZOTEKELEZWA MWAKA 2017/18 KWA FUNGU 46

12. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inatekeleza majukumu yake kuititia Idara, Vitengo na Taasisi kama ilivyofafanuliwa katika majukumu ya Wizara. Naomba nianze kwa kutoa taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/18 kama ifuatavyo:

#### Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu

13. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kusimamia Ithibati ya Shule kwa lengo la kutoa vibali vya kuanzisha na kuendesha shule vikiwemo; ujenzi wa shule, umiliki na umeneja wa shule na usajili wa shule. Jumla ya shule 154 zilizokidhi vigezo zimesajiliwa kati ya shule 171 zilizoomba usajili. Mchanganuo wa shule zilizosajiliwa unajumuisha Shule za Awali na Msingi 123 na Sekondari 31.

Vile vile, Wizara imetoea vibali vya kuongeza Tahasusi za masomo kwa Shule 37 za Sekondari kati ya 50 zilizoomba. Wizara pia imetoea vibali vya ujenzi wa shule mpya 112 zilizotimiza vigezo kati ya maombi 167 yaliyopokelewa. Vibali hivyo vilitolewa kwa shule za Sekondari 19, Awali na Msingi 63, Awali pekee 29 na Chuo cha Ualimu kimoja.

14. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ina jukumu la kusimamia Uthibiti Ubora wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, ili kuhakikisha kuwa viwango vya utoaji wa elimu vilivywewekwa vinazingatiwa na kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu bora. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza yafuatayo:

- (i)     imeandaa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule pamoja na zana za utekelezaji wa Kiunzi. Aidha, imeendesha Mafunzo elekezi ya mfumo mpya wa utekelezaji wa kazi za Uthibiti Ubora wa Shule ambayo yalifanyika kwa Wathibiti Ubora wawezeshaji wa kitaifa 51 watakaoendesha mafunzo elekezi kwa Wathibiti Ubora wa Shule katika ngazi ya Kanda na Wilaya; na
- (ii)    imefungua ofisi mpya 5 za Uthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya za Songwe, Kigamboni, Ubungo, Chalinze na Ushetu kwa lengo la kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya hizo.

#### **Usimamizi wa Elimu ya Sekondari**

**15. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18 kitengo cha Elimu ya Sekondari kimeratibu na kusimamia ushiriki wa wanafunzi wa Kitanzania katika mashindano ya Uandishi wa Insha za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Wanafunzi wa Sekondari kwa lengo la kuwajengea uwezo katika uandishi na ujenzi wa hoja. Katika mashindano ya Afrika Mashariki mwanafunzi *Michael Msafiri Nyaruga* wa Kidato cha Nne (2017) kutoka Shule ya Sekondari Kibaha – Pwani, alishika nafasi ya Kwanza. Aidha, katika mashindano ya insha ya nchi za SADC wanafunzi wawili (2) wameingia katika 10 bora. Wanafunzi hao ni *Neema Steven Mtwanga* (Kidato cha Sita) wa Shule ya Sekondari Lugalo - Iringa na *Fadhila Sanga* (Kidato cha Nne) wa Shule ya Sekondari Nasuli iliyopo Wilaya ya Namtumbo- Ruvuma.

**Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi**

**16. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Wizara imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i)     kukamilisha Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2017-2021 (*Education Sector Development Plan – ESDP*)

pamoja na Mpango wa Utekelezaji (*Operational Plan*) wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu; na

(ii) kukamilisha na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Kanuni za Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu zitakazoimarisha ukusanyaaji wa marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

**Kuendeleza Elimumsingi k w a Kutoa Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu**

**17. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imetoa mafunzo ya matumizi ya TEHAMA kwa jumla ya Wakufunzi 250 na Wathibiti Ubora 25 kwa lengo la kuimarisha ujuzi na maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) imetoa mafunzo ya Elimu ya Awali kwa jumla ya Wakufunzi 38 na Wathibiti Ubora 25 kwa lengo la kuimarisha ujuzi na maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(iii) imedahili jumla ya wanachuo wapya 7,454 wa Mafunzo ya Ualimu wakiwemo 4,368 wa Astashahada (Cheti) na 3,086 wa Stashahada. Hii imefanya jumla ya wanachuo wote waliopo katika Vyuo vya Ualimu kuwa 20,236.

**Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**18. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vimedahili jumla ya wanafunzi 5,050 na kuwapa mafunzo katika fani za Upishi, Kilimo na Ufugaji, Ufundis Umeme wa Majumbani, Ufugaji Samaki na Nyuki, Ususi na Ufumaji, Usindikaji wa Vyakula na Matunda, Ushonaji, Uchomeleajji Vyuma, Umekanika, Kompyuta, Useremala, Uashi, Utengenezaji Mapambo, Ujasiriamali, Uendeshaji Hoteli na Umeme wa Magari.

- 19. Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya tathmini ya hali ya miundombinu katika Vyuo vyote 55 vya Maendeleo ya Wananchi. Tathmini hiyo imebaini uchakavu wa miundombinu, vifaa, mitambo na upungufu wa watumishi katika Vyuo hivyo. Aidha, Wizara inafanya upembuzi yakinifu wa miundombinu ambapo kwa sasa taarifa ya upembuzi inaanndaliwa na itakamilika tarehe 4 Mei, 2018. Baada ya kupata taarifa hiyo Wizara itafanya ukarabati na ujenzi katika vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi katika Awamu ya Kwanza.
- 20. Mheshimiwa Spika**, Kupitia ushirikiano na wadau wa Elimu ambao ni *Karibu Tanzania Organization, Master Card Foundation, Aflatoun* na Ubalozi wa Sweden nchini Tanzania, Wizara imeweza kuandaa programu mbili ambazo ni *Elimu Haina Mwisho na Mpira Fursa*. Programu hizi zimejikita katika kutoa elimu ya stadi za maisha na ujasiriamali kwa wasichana nje ya mfumo rasmi wa elimu na pia kufungua fursa ya ajira kwa mchezo wa mpira wa miguu. Kiasi cha Dola 100,000 zimetengwa kwa kipindi cha miaka minne (4) na tayari kwa mwaka 2017-18 wasichana 569 wamepata mafunzo hayo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, katika Programu ya *Mpira Fursa* ambapo kiasi cha Paundi za Uingereza 550,000 zimetengwa kutumika kwa kipindi cha miaka minne (4), jumla ya wasichana 523 kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii 27 wamepata mafunzo ya kuwawezesha kushiriki katika mchezo wa mpira wa miguu.

### **Kuainisha Mahitaji ya Nchi katika Ujuzi na Kuuendeleza**

- 21. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (*Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ*) imekamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (*Skills Development Fund*) kwalengo la kutoa ruzuku kwa vyuo na taasisi za mafunzo katika ngazi zote pamoja na waajiri wa sekta binafsi ili kufadhili programu za mafunzo zinazozingatia mahitaji ya soko la ajira. Programu hizo zinahusisha sekta sita za kipaumbele zilizoainishwa katika mpango mkakati wa taifa wa

kuendeleza ujuzi (*National Skills Development Strategy*), ambazo ni kilimo, TEHAMA, nishati, ujenzi, uchukuzi na utalii. Katika Awamu ya Kwanza mfuko unatarajijiwa kutoa ruzuku kwa programu za sekta ya Kilimo. Taratibu za kuwapata wanufaika zipo katika hatua za mwisho na sherehe ya kuwatangaza washindi itafanyika kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2018.

### **Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya fundi Stadi**

**22. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeratibu taratibu za kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa miundombinu, majengo, vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi;
- (ii) imeratibu maandalizi ya awali ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Simiyu, Geita na Rukwa; na
- (iii) imeratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara na umeme kwenye eneo kitakapoengwa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera ambapo barabara na nguzo za umeme vimefikishwa hadi eneo la ujenzi wa Chuo.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**23. Mheshimiwa Spika**, Wizara ina jukumu la usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini. Aidha, masuala ya Ithibati na Utibiti wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini yanatekelezwa kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imeratibu Skolashipu 135 za wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Nje ya Nchi zikiwemo 10 za Jumuiya ya Madola (Uingereza 8 na New Zealand 2); Urusi 12 na China 113. Aidha, imekamilisha mchakato wa maombi ya Skolashipu za

Jumuiya ya Madola kwa mwaka wa masomo 2018/19 na kupendekeza waombaji 26 ambao majina yao yamewasilishwa kwenye Baraza la Skolashipu za Jumulya ya Madola kwa hatua zaidi. Vile vile, imekamilisha mchakato wa kupokea maombi na kupendekeza majina 30 kwa ajili ya Skolashipu za Serikali ya Hungary kwa mwaka 2018/19;

(ii) imefadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kutekeleza mkataba wa ushirikiano wa kiutamaduni kati ya Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;

(iii) imeratibu kusainiwa kwa mkataba wa mahusiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Hungary ili kuwezesha upatikanaji wa fursa za masomo 30 (5 Uzamivu, 15 Uzamili na 10 Shahada za Kwanza) kila mwaka kwa kipindi cha miaka Mitatu;

(iv) imefuatilia maendeleo ya udahili na uandikishwaji wa wanafunzi katika taasisi za Elimu ya Juu pamoja na maendeleo ya utoaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(v) imefuatilia zoezi la udahili wa wanafunzi unaofanyika moja kwa moja kwenye Taasisi za Elimu ya Juu; na

(vi) imeratibu uanzishaji na usimamizi wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (*African Center of Excellence (ACE II)*).

Katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kuna Vituo viwili ambavyo ni Kituo cha Umahiri cha Afrika cha Ubunifu wa Mbinu za Kudhibiti Wadudu na Wanyama Waharibifu kwa Kutumia Teknolojia ya *Bio-Sensor (African Center of Excellence for Innovative Rodent Pest Management and Bio - Sensor Technology (IRPM&BTD))* na Kituo cha Kusini mwa Afrika cha Kutafiti Magonjwa yanayoambukiza (*Southern African Centre for Infectious Diseases Surveillance (SACIDS)*). Aidha, katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson

Mandela kuna vituo viwili ambavyo ni Kituo kwa ajili ya Utafiti wa Miundombinu na Nishati Endelevu (*Water Infrastructure and Sustainable Energy Centre for the Futures*) na Kituo cha Ushirikiano cha Utafiti na Maendeleo ya Kilimo na Ufundishaji (*Collaborating Centre for Research, Evidence, Agricultural Advancement and Teaching Excellence and Sustainability (CREATEs)*). Vituo hivyo vimeanzishwa ili kuongeza fursa za masomo katika ngazi ya uzamili na uzamivu; na hivyo kuongeza idadi ya wataalamu wenye umahiri katika kukabiliana na changamoto za kijamii na kiuchumi.

### **Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**24. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jukumu la kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini, Wizara katika mwaka 2017/18 imetekeliza kazi zifuatazo:

(i) imefanya makubaliano na Serikali ya Finland katika mradi wa kuendeleza ubunifu nchini wenyе thamani ya Euro 12,773,000, ambapo Serikali ya Tanzania inachangia Euro 3,823,000 na Serikali ya Finland inachangia Euro 8,950,000. Mradi utatoa msaada wa kitaalamu kwa wabunifu pamoja na nafasi ya kushindania fedha za kuendeleza ubunifu. Mradi huu utachochaea ushirikiano kati ya Wanataluma, Wabunifu na wenyе viwanda; na

(ii) imefanya makubaliano na Serikali ya Finland katika mradi wa Awamu ya Pili wa Kuendeleza Ubunifu katika nchi za Kusini mwa Afrika ambapo Tanzania inashiriki kwa mara ya kwanza. Nchi nyingine ni pamoja na Afrika Kusini, Botswana, Namibia na Zambia. Mradi huu unalenga kuboresha ushirikiano wa kikanda katika ubunifu pamoja na mifumo ya ubunifu ya nchi wanachama ili kuongeza mchango wa ubunifu katika biashara na maendeleo kwa ujumla. Mradi huu wa Awamu ya Pili wa Kuendeleza Ubunifu katika nchi za Kusini mwa Afrika una thamani ya Euro 12,550,000 ambapo wabunifu kutoka nchi wanachama watashindanishwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa taasisi

kibunifu ili ziweze kuwasaidia wabunifu kupata ushauri wa kitaalamu. Vile vile, mradi huu utaimarisha uwezo wa Wajasiriamali kifedha ili waweeze kuingiza bidhaa zao sokoni na kuweka mazingira rafiki kwa shughuli za wabunifu.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu**

**25. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jukumu la kusimamia na kuendeleza Rasilimaliwatu, kwa mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza yafuatayo:

- (i) imefanya uhamisho wa watumishi 43 toka Dar es Salaam kuja Dodoma na kufanya jumla ya watumishi waliohamishiwa Dodoma kuwa 273 kati ya watumishi 328 wanaotakiwa kuhamia Dodoma. Uhamisho huu umelenga kutekeleza Mpango wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Mkoani Dodoma;
- (ii) imetoa mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (*Open Performance Review and Apraisal System – OPRAS*) kwa watumishi wote wa Makao Makuu ya Wizara, Vyuo 35 vya Ualimu, Ofisi 11 za Uthibiti Ubora wa Shule Kanda na Ofisi za Uchapaji (Press A, Press B na Tabora). Lengo la mafunzo ni kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi kwa kuweka malengo ya pamoja baina ya mwajiri na mwajiriwa na kuijipima kwa kipindi cha nusu mwaka na mwaka;
- (iii) imetoa Mafunzo Elekezi (*Induction Course*) kwa watumishi wapya 89 ili kuwajengea ufahamu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maadili ya Kazi katika utumishi wa umma kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi;
- (iv) imeratibu na kuendesha Mafunzo ya Awali ya Mfumo wa Kupokea, Kutunza na Kusambaza Nyaraka za Ofisi (*E-Office*) kwa watumishi 20 wa Masijala na Maafisa 02. Mafunzo yalilenga kuwawezesha watumishi wa Wizara kuanza kutumia mfumo huu ili kuleta ufanisi, kupunguza gharama na kuongeza kasi ya mawasiliano katika ofisi; na

(v) kuratibu uhakiki wa vyeti vyaa elimu na taaluma kwa waombaji wa kazi ya Ualimu kwa ajili ya kujaza nafasi **3,033** za walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Kilimo na Biashara katika shule za Serikali kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa walimu wa masomo hayo.

### **Usimamizi wa Rasilimali za Wizara**

**26. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha udhibiti na usimamizi wa rasilimali za Wizara, katika mwaka 2017/18 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kukagua matumizi ya fedha za Mpango wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (*Literacy and Numeracy Education Support - LANES*) katika mikoa 10 na Halmashauri 20 ili kuona kama fedha zinazotumwa na Wizara zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali;
- (ii) kukagua matumizi ya fedha za Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) katika shule 50 zilizo katika Halmashauri 22 ili kuona kama kazi zilizotekelvezwa zinathamani ya fedha zilizotumika;
- (iii) kukagua mapato, matumizi na usimamizi wa mali katika vuo 6 vya Ualimu ili kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali yanakusanya kikamilifu na matumizi yanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali;
- (iv) kuthaminisha mali za Wizara katika makao makuu ya Wizara, Vuo 35 vya Ualimu, ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za Kanda 11 na Wilaya 160 ili kutambua na kupata thamani halisi ya mali za Wizara;
- (v) kukagua matumizi ya fedha za Mpango wa Lipa kwa Matokeo (EP4R) katika makao makuu ya Wizara na Shule za Sekondari; na
- (vi) kutoa mafunzo ya menejimenti ya viashiria hatarishi (*Risk Management*) kwa watumishi 243 walioko

makao makuu ya Wizara pamoja na taasisi zake. Katika mafunzo hayo vihatarishi vinavyoweza kuisababisha Wizara kutofikia malengo yake viliorodheshwa na kuwekewa mikakati ya udhibiti. Aidha, matokeo ya ukaguzi uliofanywa yameiwezesha Wizara kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani itakayoisaidia kufikia malengo iliyojivekea.

## **SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA KWA MWAKA 2017/18**

**27. Mheshimiwa Spika**, Taasisi, Wakala na Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyo chini ya Wizara, vinawajibika katika kuchangia usimamizi na hatimaye kufanikisha utoaji wa elimu bora nchini. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 shughuli zilizotekelawa ni kama ifuatavyo:

### **Taasisi ya Elimu Tanzania**

**28. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Elimu Tanzania katika kipindi cha mwaka 2017/18, imetekeliza yafuatayo:

(i)      kuandika Vitabu vya Kiada vya masomo 7 ya darasa la IV. Vitabu hivyo ni vya masomo ya Hisabati, Sayansi na Teknolojia, Maarifa ya Jamii, Uraia na Maadili, *English, French* na Kiswahili;

(ii)     kuboresha vitabu vyote vya kiada aina 17 vya Darasa la I – III vilivytakiwa kufanyiwa mapitio. Jumla ya nakala 8,450,000 za vitabu vilivyopitiwa zimechapishwa na kupelekwa shulen;

(iii)    kutathmini miswada ya vitabu vya ziada 108 kutoka kwa makampuni/watu binafsi ambapo miswada 17 ilipitishwa kwa masharti ya kufanyiwa marekebisho madogo; miswada 47 ilipitishwa kwa masharti ya kufanyiwa marekebisho makubwa na miswada 44 ilikataliwa kwa kutokidhi vigezo vya ubora;

- (iv) kuboresha Mihtasari ya masomo ya Kidato cha I-IV na V-VI kwa Mtaala wa mwaka 2005 na 2009 ili kuendana na wakati;
- (v) kutafsiri Moduli za Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Lugha ya Kiswahili na kuhariri Moduli za Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali;
- (vi) kupokea na kufanya tathmini vitabu vya ziada 120 kutoka kwa watu na makampuni binafsi;
- (vii) kufanya utafiti kwa ajili ya kukusanya taarifa, maoni na mapendekezo ya kuboresha Mtaala wa Elimu ya Ualimu Ngazi ya Cheti katika mikoa 10 ya Tanzania Bara, ambayo ni Mbeya, Njombe, Mara, Mtwara, Kagera, Dodoma, Tabora, Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro; na
- (viii) kuhariri na kuboresha zaidi moduli za mafunzo ya uendelezaji walimu kazini ili kuimarisha umahiri wa walimu katika kufundisha na kujifunza.

#### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**

**29. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kipindi cha mwaka 2017/18 imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili wanafunzi 2,873 katika programu za Astashahada, Stashahada na Shahada. Jumla ya wanafunzi wote wanaoendelea na masomo katika programu zinazotolewa kwa njia ya kawaida na Masafa ni 4,175 ambapo wanawake ni 2,116 sawa na 51% na wanaume ni 2,059 sawa na 49% ya wanafunzi wote;
- (ii) imekamilisha ujenzi wa uzio wa kiwanja cha TEWW katika Mkoa wa Rukwa na kuandaa Mchoro wa jengo la ofisi katika mkoa wa Kagera; na
- (iii) kusajili jumla ya vituo 104 vinavyotoa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi ili kuongeza fursa ya elimu ya sekondari kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi.

## **Baraza la Mitihani la Tanzania**

**30. Mheshimiwa Spika,** Baraza lina majukumu ya kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi na Sekondari, Ualimu Ngazi ya Cheti na Stashahada na Mtihani wa Maarifa. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Baraza la Mitihani Tanzania limetekeleza yafuatayo:

- (i) limeendesa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Jumla ya watahiniwa 1,192,655 wa Darasa la Nne walisajiliwa ambapo watahiniwa 1,158,499 sawa na asilimia 97 walipimwa; na jumla ya watahiniwa 521,759 wa Kidato cha Pili walisajiliwa ambapo watahiniwa 486,742 sawa asilimia 93 walifanyiwa upimaji huo;
- (ii) limeendesa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi na Kidato cha Nne mwaka 2017. Jumla ya watahiniwa 916,885 wa Elimu ya Msingi walisajiliwa ambapo watahiniwa 909,950 sawa na asilimia 99 walifanya Mtihani huo; na jumla ya watahiniwa 385,802 wa Kidato cha Nne walisajiliwa kufanya Mtihani ambapo watahiniwa 374,938 sawa na asilimia 97 walifanya Mtihani huo;
- (iii) limesajili jumla ya watahiniwa 76,789 watakaofanya Mtihani wa Kidato cha Sita Mei 2018;
- (iv) limesajili jumla ya Wanachuo 9,895 ambapo kati ya hao 8,848 ni wa ngazi ya Cheti na 1,047 ni wa ngazi ya Stashahada ambao wanatarajia kufanya mitihani Mei, 2018; na
- (v) limenunua mashine ya pili ya kufungia mitihani (*Poly wrapping machine*) na mashine ya rangi ya uchapaji mitihani (*Full Colour Printing Machine*) ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha usalama wa mitihani.

## **Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**31. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imefanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 8 za walimu zinazoweza kuchukua walimu 6 kila moja katika shule za Sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu kufikika kwa ajili ya kuanza ujenzi. Nyumba hizo zitakapokamilika zitakuwa na uwezo wa kuchukua walimu 48 kwa wakati mmoja;
- (ii) imetoa jumla ya shilingi milioni 700 kama mkopo kwa Chuo Kikuu Mzumbe kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara;
- (iii) imefanikisha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum katika shule zifuatazo; Shule ya Msingi Kigongo - Misungwi, Shule ya Msingi Mugeza - Ngara, Shule ya Msingi Sima A - Bariadi; Shule ya Msingi Ikungi - Singida Vijijini; Shule ya Msingi Mundindi - Ludewa na Shule za Sekondari za Wasichana za Rugambwa - Bukoba na Jangwani - Ilala;
- (iv) imekamilisha kukarabati na kukabidhi shule 10 kongwe kati ya 17 za awamu ya kwanza. Shule hizo ni Shule za Sekondari Pugu, Mzumbe, Kilakala, Msalato, Ilboru, Same, Nganza, Mwenge, Tabora Wavulana na Tabora Wasichana;
- (v) imeendelea na ukarabati wa Shule 7 za Sekondari ambazo ni Ruvu, Dodoma, Bihawana, Bwiru Wasichana, Sengerema, Kondoa Wasichana na Korogwe Wasichana;
- (vi) imeendelea na ujenzi wa mabweni katika Shule za Sekondari Mkula - Busega, Kamagi - Sikonge, Ihyonga - Mlele, Lulumba - Iramba, Kibakwe - Mpwapwa, Endasak - Hanang, Kilumba - Nyasa, Kisange - Kasulu, Muyenzi - Ngara, Kibaigwa - Kongwa na Ufana - Babati ambapo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Aidha, Ujenzi wa bweni katika Shule ya Msingi Munguli - Singida upo katika hatua za mwanzo;
- (vii) imeandaa miongozo itakayotumika katika kazi za ufuatiliaji na tathmini ya miradi;

(viii) imeratibu ujenzi wa nyumba 40 za walimu ambapo nyumba 15 zimekamilika; na

(ix) imejenga matundu ya vyoo 312 na madarasa 39 katika shule 26.

### **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETA)**

**32. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Mamlaka imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na kazi ya ujenzi wa chuo cha Ufundsi Stadi cha Wilaya ya Namtumbo ambapo ujenzi unatarajiwaa kukamilika mwezi Septemba, 2018. Ujenzi wa chuo utakapokamilika utaongeza fursa ya mafunzo kwa vijana wapatao 600 katika fani mbalimbali za ufundi stadi;

(ii) imejenga jengo la karakana ya umeme wa viwandani katika Chuo cha Ufundsi Stadi cha Mkao Mwanza ambapo ujenzi umefikia asilimia 90. Ujenzi utakapokamilika utaongeza fursa ya mafunzo kwa vijana katika fani ya umeme wa viwandani. Hatua hii itawezesha upatikanaji wa wataalamu wenye ujuzi na umahiri wanaohitajika katika sekta mbalimbali za kujenga uchumi wa kati kupitia viwanda;

(iii) imekamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika mikoa ya Geita, Simiyu na Rukwa;

(iv) imeendelea na ujenzi wa Karakana ya Teknolojia ya Ushonaji katika Chuo cha Ufundsi Stadi cha Mkao wa Pwani. Ujenzi wa Karakana hiyo umefikia asilimia 80 na unatarajiwaa kukamilika mwezi Juni,

(v) imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu wa Ufundsi Stadi Morogoro na kwa sasa hatua ya majadiliano na mkandarasi inaendelea na mkataba wa ujenzi unatarajiwaa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2018; na

(vi) imepata vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika fani ya umeme katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

### **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

**33. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Baraza limetekeleza yafuatayo:

(i) limekagua Vyuo 36 vya Elimu ya Ufundi sawa na asilimia 72 ya lengo na kuvisajili vyote baada ya kukidhi vigezo vya msingi vya kuanza mafunzo;

(ii) limeshauri na kuviselekeza Vyuo 26 vya Elimu ya Ufundi kuhusu utaratibu wa kufikia hatua ya Ithibati ambapo Vyuo 10 vimepata Ithibati ya Awali na Vyuo 16 vimepata Ithibati kamili;

(iii) limehakiki ubora wa mafunzo kwa Vyuo 460 vya Elimu ya Ufundi. Matokeo ya uhakiki yameonesha mapungufu kadhaa katika uendeshaji ukiwemo uwiano usiordhisha wa Mwalimu kwa Wanafunzi, uwepo wa Walimu wasio na sifa, uhaba wa miundombini, mitaala ambayo haina ithibati. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kusitisha na kupunguza udahili;

(iv) limetengeneza na kuboresha mifumo ya kielektroniki kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Mifumo hii ni pamoja na:

a) Mfumo wa Udhili na Uhakiki kwa wanafunzi wa Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Afya vya Serikali ili kupata takwimu sahihi na kwa wakati na kusaidia kufanya maamuzi sahihi katika mipango ya elimu;

b) Mfumo Unganishi (*Intergrated System*) baina ya mifumo ya Baraza na vyuo (mitihani, udahili na uhakiki wa udahili). Mfumo huu unarahaishisha udahili vyuoni, uhakiki wa wanafunzi waliodahiliwa pia kupata takwimu mbalimbali kama vile matokeo ya mitihani kwa programu

mbalimbali na idadi za wanafunzi wanaosoma Elimu ya Ufundu na takwimu za wahitimu wanaomaliza programu mbalimbali zinazotolewa na vyuo vya ufundu nchini;

- c) Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Rasilimaliwateru katika Vyuo vya Elimu ya Ufundu ambao unahusika katika kusajili na kutoa takwimu kuhusu Rasilimaliwateru vyuoni; na
- d) Mfumo wa Kuchakata Matokeo ya Mitihani na Mfumo wa Kupokea na Kuchakata Maombi ya Hati za Matokeo. Mifumo hii itawezesha kuzalisha hati za matokeo kwa wahitimu wa Vyuo vya Afya, Mifugo na Ualimu.

#### **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**34. Mheshimiwa Spika**, Mojawapo ya jukumu la Wakala ni kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa walimu na viongozi wa elimu, ili kuimarisha uongozi, kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya uongozi na uendeshaji wa elimu. Katika mwaka 2017/18, Wakala umetekeleza yafuatayo:

- (i) umedahili walimu 1,831 (wanaume ni 1,039 (57%) na wanawake ni 792 (43%)) kwenye kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na kozi ya Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule. Aidha, Wakala umedahili Walimu Wakuu 704 wanaume ni 518 (73%) na wanawake ni 186 (17%) kutoka mikoa ya Mbeya, Iringa na Songwe wanaochukua kozi ya Astashahada ya Uongozi, Usimamizi na Utawala katika Elimu;
- (ii) umeendesha mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Shule kwa walimu 49 wa shule zisizo za Serikali zilizo chini ya usimamizi wa Jumuiya za Kiislamu Afrika ili kuimarisha usimamizi wa taaluma. Mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu katika maeneo ya Usimamizi na Utawala wa Shule; Ushauri na Unasihi; Utekelezaji wa Sera za Elimu; Udhibiti wa Majanga shulen; Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi; Ufuatilizaji na Tathmini ya Mipango ya Shule; Usimamizi wa Raslimali za

Shule; Usimamizi na Utunzaji wa Kumbukumbu za Shule pamoja na Usimamizi na Tathmini ya Mtaala;

(iii) umefanya ukarabati wa mabweni 2 yenye uwezo wa kuchukua wanachuo 450 na kumbi 2 za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanachuo 150 kila mmoja;

(iv) umekamilisha michoro kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kampasi za Mbeya na Mwanza ambazo zitakuwa na uwezo wa kudahili wanachuo 700;

(v) umefanya maboresho ya Mtaala wa Stashahada ya Menejimenti na Utawala katika Elimu (DEMA); na

(vi) umeratibu uendeshaji wa mafunzo kwa Walimu 1,568 wa Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi (MEMKWA) yenye lengo la kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

### **Bodi ya Huduma za Maktaba**

**35. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Huduma za Maktaba ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba kwa watu wote nchini; kuanzisha, kuendesha, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi ya Mikoa, Wilaya hadi Vijiji pamoja na kutoa mafunzo na kuendesha Mitihani ya Taaluma na Ukutubi. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Bodi imetekeliza yafuatayo:

(i) imewezesha upatikanaji wa vitabu 25,966, kati ya hivyo Vitabu 316 vilipatikana kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 1975 ambayo inamtaka kila mchapishaji wa vitabu na majarida nchini kuwasilisha katika Bodi nakala 2 ya kila chapisho, vitabu 829 vilinunuliwa na vitabu 24,821 vilipatikana kupitia msaada. Aidha, magazeti 9,829 na majarida 1,458 yalipatikana. Machapishohaya kwa ujumla wake yanaongeza fursa ya wananchi kupata elimu;

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba kwenye jumla ya shule 18 (Shule za

Msingi 2 na Sekondari 16) ili kujenga utamaduni wa kujisomea na kuongeza maarifa; na

(iii) imetoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi 826 katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo kwa mchanganuo ufuatao: Cheti cha Msingi (NTA 4) wanafunzi **212**, Cheti (NTA 5) wanafunzi **287** na Stashahada (NTA 6) wanafunzi.

### **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**36. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo. Katika mwaka 2017/18 Bodi imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi **122,623** ambapo wanafunzi **33,244** ni wa mwaka wa kwanza na **89,379** ni wanaoendelea na masomo;

(ii) imetoa mikopo na ruzuku kwa jumla ya wanafunzi 351 wanaoendelea na masomo nje ya nchi: Urusi **16**, Ujerumanji **22**, Ukraine mmoja, Misri **2**, Msumbiji **117**, Algeria **168**, Cuba **24** na Serbia mmoja;

(iii) imeboresha mifumo ya uchambuzi, upangaji na urejeshwaji wa mikopo kwa kuunganisha mifumo hiyo na mifumo ya malipo ya kibenki na mfumo wa malipo wa Serikali;

(iv) imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 132.30 za mikopo ilioiva sawa na asilimia 101% ya lengo la mwaka 2017/18, ambalo lilikuwa ni Shilingi bilioni 130;

(v) imeshiriki katika maonesho ya 12 ya Vyuo Vikuu na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) ambapo elimu juu ya shughuli za taasisi kwa wateja na wadau mbalimbali ilitolewa kwa wanafunzi na wadau wengine; na

(vi) imewabaini wadaiwa sugu 147,231 na kati yao 42,213 wameanza kufanya marejesho ya fedha za mikopo waliyopatiwa.

### **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**37. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, kuhakiki ubora wa Elimu na kuidhinisha Programu zifundishwazo ili zikidhi mahitaji ya Taifa na soko la ajira. Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Tume imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu zoezi la udahili ambapo jumla ya waombaji **63,737** (wanaume **38,779** na wanawake **24,958**) walidahiliwa katika vyuo mbalimbali. Aidha, Kati ya wadahiliwa hawa **50,292 (78.9%)** wamesajiliwa katika vyuo vya umma (wanaume **30,801** na wanawake **19,491**) na wadahiliwa **13,445 (21.1%)** wamesajiliwa katika Vyuo visivyo vya Serikali (Wanaume **7,978** na Wanawake;

(ii) imepokea maombi ya kutathmini na kuidhinisha programu **124** za masomo kutoka Vyuo Vikuu nchini. Jumla ya programu **21** zimepata idhini na programu za masomo **103** zinafanyiwa kazi na wataalam;

(iii) imepokea maombi ya kutathmini na kutambua tuzo **1,676** za ngazi mbalimbali zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchi za nje. Kati ya tuzo hizo **1,412 (87%)** zilitambuliwa, tuzo **10 (0.59%)** hazikutambuliwa na tuzo **254 (15%)** ziliwasilishwa bila ya kuwa na taarifa zinazojitosheleza, hivyo waombaji wameelekezwa kuzikamilisha ili ziweze kufanyiwa tathmini; na

(iv) imeanza kutumia mfumo maalum wa *University Information Management System (UIMS)* kupokea taarifa mbalimbali ili kurahisisha utoaji wa taarifa za Vyuo Vikuu na kutengeneza kanzidata ikiwemo takwimu za wanafunzi waliodahiliwa, waliohitimu na taarifa za wahadhiri kwa ujumla wao.

**38.** **Mheshimiwa Spika**, ili kurahisisha utoaji wa taarifa za Vyuo Vikuu, Tume iliandaa maonesho ya 12 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika katika viwanja vya Mhazi Mmoja, Dar es Salaam. Lengo la Maonesho hayo ilikuwa ni kutoa fursa kwa Vyuo kuonesha na kutangaza shughuli mbalimbali zinazoendeshwa na Chuo husika na kuwapa wanafunzi fursa ya kupata taarifa mbalimbali za vyuo.

**Tume ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**39.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Hati Idhini, Wizara ina wajibu wa kuimarisha utumiaji wa Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati pamoja na kuendeleza wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Katika mwaka 2017/18 Tume ya Sayansi na Teknolojia, imetekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) imekamilisha vijarida vitatu vya taarifa ya kisera vinavyotoa ushahidi wa kisayansi (*Policy Briefs*) katika maeneo yafuatayo:
  - (a) uzuiaji wa uharibifu wa mazao baada ya mavuno;
  - (b) upunguzaji wa migogoro ya wakulima na wafugaji; na
  - (c) uvunaji wa mazao ya baharini kwa upande wa Zanzibar.
- (ii) imeandaa Kiunzi cha Kutathmini Maombi ya Uendelezaji wa Ubunifu uliotokana na matokeo ya utafiti uliofadhilliwa kwa kushirikiana na Serikali ya Afrika Kusini. Aidha, Kiunzi hiki kitatumika katika kutathmini maombi ya uendelezaji wa ubunifu nchini kwa kupitia fedha za kuendeleza Ubunifu katika Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE);
- (iii) imefadhili miradi ya utafiti 20 inayօendelea ya utafiti inayofadhilliwa kwa kushirikiana na SIDA na imepokea mawazo ya miradi 387 katika maeneo ya viwanda, TEHAMA, kilimo, afya, mazingira na maliasili;

(iv) imeendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanga ambayo ipo kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji. Aidha, Tume imetoa tangazo la kufadhili miradi mipyä ya ukarabati wa miundombinu ya utafiti katika taasisi za utafiti na maendeleo; na

(v) imefadhili watafiti 27, (23 ni wa Shahada ya Uzamili na 4 Shahada ya Uzamivu) ambao wapo katika hatua mbalimbali za kuhitimisha masomo yao.

### **Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania**

**40. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Tume ya Nguvu za Atomiki ya Tanzania imeendelea na jukumu lake la kudhibiti mionzi katika vituo vya huduma kwa kufanya yafuatayo:

(i) imepokea maombi 237 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ambapo maombi yote yalipata vibali baada ya kukidhi matakwa ya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya mwaka 2003. Vigezo vinahusisha chanzo cha mionzi, sifa za kitaaluma za msafirishaji na mtumiaji na mpango wa uhifadhi wa kudumu wa mabaki ya chanzo cha mionzi;

(ii) ilipima kiasi cha mionzi kwa wafanyakazi 423 kutoka katika vituo 68 kwa kutathmini kiasi cha mionzi kwenye vifaa vya kupima mionzi kwa wafanyakazi. Kiwango cha mionzi kwa wafanyakazi kwa kipindi cha miezi mitatu kilikuwa chini ya 5 *microsivart*, kiwango ambacho kinakubalika kimataifa;

(iii) imekagua vituo 23 vinavyotumia mionzi na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama wa watumiaji na mazingira;

(iv) imesajili vituo vipyä 56 vya watumiaji wa vyanzo vya mionzi na kufanya kuwa na jumla ya vituo 806 vinavyotumia mionzi;

(v) imetoa leseni 237 kwa wamiliki wa vyanzo vya mionzi;

(vi) imeendelea na ujenzi wa Maabara ya kisasa Awamu ya Kwanza ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2018; na

(vii) imepokea vifaa vya Maabara kutoka Jumuiya ya Umoja wa Ulaya. Vifaa hivyo vinasaidia kujenga uwezo wa Tume kutimiza majukumu yake katika usimamizi na uthibiti wa matumizi salama ya vyanzo vya mionzi.

**41. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya mionzi vinadhibitiwa na haviathiri mazingira na afya za viumbi hai, Wizara kuititia Tume ya Nguvu za Atomiki:

(i) imekagua vituo vya mionzi katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mtwara pamoja na Mipaka ya Namanga, Tarakea, Sirari, Holili, Horohoro na Tunduma ili kutathmini hali ya vifaa vinavyotumika;

(ii) imefanya tathmini ya mahitaji kwa ajili ya kuboresha ulinzi na usalama wa vyanzo vya mionzi katika Kituo cha Matibabu ya Saratani cha Bugando;

(iii) imekagua na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama kwa watumiaji wa Vituo vitano vya *Ocean Road Cancer Institute* (Dar es Salaam), *Bugando Medical Centre* (Mwanza), *Vector and Vector Borne Diseases Research Institute* (Tanga), *Secondary Standard Dosimetry Laboratory* (Arusha) na *Central Radioactive Waste Management Facility* (Arusha). Vile vile, Wizara kuititia Tume imefungua ofisi zake katika mipaka ya Rusumo, Mtukula, Tarakea, Holili, Horohoro, Bandari ya Tanga na Tunduma kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mionzi ili kuzuia vyakula visiingie nchini kama havifai kwa matumizi ya binadamu;

(iv) imefanya upimaji wa viwango vya mionzi kwa sampuli 2,012 ili kuhakikisha afya za wananchi zinalindwa dhidi ya mionzi. Kati ya sampuli hizi, 1,002 ni za vyakula

vinavyoingia nchini, 602 ni za vyakula vinavyokwenda nje ya nchi, 112 ni za mbolea, 238 ni za vyakula vya wanyama na 58 ni sigara za aina ya Pall Mall (8), Winsten (12) na Marlboro (38);

(v) imetengeneza vifaa 43 vya elektroniki na vifaa 9 vya ukaguzi na uhakiki wa vifaa vya ujenzi wa barabara (*Troxler Gauges*) pamoja na mashine ya uhakiki wa mionzi (*Calibration Irradiation Machine*) katika Maabara ya Uhakiki wa Mionzi ya *Secondary Standard Dosimetry Laboratory (SSDL)*;

(vi) imesimika mifumo na vifaa vya maabara na kutoa mafunzo ya namna ya kuvitumia pamoja na kuvifanya matengenezo kwa lengo la kuboresha maabara ya *X-Ray Florescence (XRF)*, *Gamma* na *Alpha*; na

(vii) imetoa mafunzo ya mifumo ya ubora kwenye maabara za kinyuklia kwa watumishi watatu wa Tume, yaliyoshirikisha washiriki 32 kutoka nchi 26 za Kanda ya Afrika.

### **Vyuo vya Elimu ya Juu**

**42. Mheshimiwa Spika**, Elimu ya Juu ni mojawapo ya nguzo muhimu ya kuwezesha Serikali kufikia malengo yake ya maendeleo kwa kuzalisha rasilimaliwaitu yenye ujuzi stahiki. Hivyo, Wizara imeendelea kuratibu shughuli zake ikiwa ni pamoja kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuinua ubora na kuongeza fursa kwa wanafunzi wengi zaidi kuijunga na Elimu ya Juu. Katika mwaka 2017/18, Vyuo Vikuu vimetekeleza yafuatayo:

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**43. Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu H u r i a kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimetoa mafunzo ya ana kwa ana ya Shahada ya Uzamili katika Programu za *Masters of Community Economic Development (MCED)* na *Masters of Arts in Social*

Work (MASW) kwa kutumia mfumo wa *Blended Learning Mode (Learning Management System and Face to Face)*;

(ii) kimetekeleza mpango wa Serikali wa kuunganisha mifumo yake ya kieletroniki kama vile *Student Academic Registration Information System* na kuwezesha malipo ya ada kufanya moja kwa moja kieletroniki katika mfumo wa Serikali wa *Government e-Pay Gateway* kupitia Wizara ya Fedha na Mipango; na

(iii) kuendelea kutoa bila gharama yoyote mafunzo ya TEHAMA kwa wanafunzi wenye ulemavu, ambapo wanafunzi wasioona 42 na viziwi 37 walipatiwa mafunzo.

### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**44. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kimefanya yafuatayo:

(i) kimetekeleza mradi wa *Council for the Development of Social Science Research in Africa (CODESRIA)* kuhusu mitaala ya Vyuo Vikuu na mahitaji ya soko;

(ii) kimeratibu uwasilishaji wa matokeo ya tafiti kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu 10 na kwa wanafunzi wa Shahada za Uzamili 115;

(iii) kimekamilisha uchapaji wa kitabu cha majumuisho ya warsha za utafiti kuhusu Maendeleo ya Ushirika;

(iv) kimeendelea kuratibu zoezi la kutoa machapisho matatu ambayo ni (*Jounal of Cooperative and Business Studies, Research Report Series Journal na Workshop Proceeding on "The Joint Workshop on Innovation and Enterpreneurship in Cooperative, The Private Sector and Public Services; Lesson From Sweden and Tanzania*); na

(v) kimeboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kufanya ukarabati wa nyumba 6 za makazi, mabweni 16 na majengo 2 ya ofisi na kubadili matumizi ya jengo moja

na kuwezesha kapatikana kwa ofisi 5 za watumishi kuptitia mradi wa *Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support*" (MIVARF).

### **Chuo Kikuu cha Ardhi**

**45. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimetoa huduma za ushauri kwa jamii na kutekeleza miradi mbalimbali ya ushauri wa kitaaluma ikiwa ni pamoja na *Master Plans* za miji ya Geita, Kilwa, Nzega, Urambo, Sikonge na Mafinga;

(ii) kimefanya miradi ya utafiti 69 katи ya miradi 30 iliyotarajiwa kufanyika kwa mwaka 2017/18. Baadhi ya Miradi hiyo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti na uvumbuzi kwa ajili ya kutunza ardhi na usimamizi wa mazingira kwa maendeleo ya nchi na kuwajengea wananchi uwezo wa kupunguza maafa hasa kwa wanajamii wanaoishi maeneo hatarishi Tanzania (*Regional Disaster, Risk and Vulnerability Reduction Capacity Development*);

(iii) kimegharamia mafunzo kwa Watumishi waendeshaji 25 wa Shahada ya Uzamili, 12 wa Shahada ya Kwanza, 20 wa Stashahada. Aidha, kimegharamia mafunzo kwa wanataaluma 56 wa Shahada ya Uzamivu na 22 wa Shahada ya Uzamili; na

(iv) kimefanya ukarabati wa mabweni 5 na kuwezesha wanafunzi 457 kupata malazi katika chuo hicho.

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**46. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/18 Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeongeza idadi ya miradi ya utafiti kutoka 145 hadi 209; machapisho yameongezeka kutoka 337 hadi 354 na majarida kutoka 21 hadi 46. Tafiti hizo,

zililenga kuboresha Teknolojia ya Kuzalisha Togwa ya Ndizi, Kukuza Sekta ya Mafuta na Gesi, Kuboresha na Kuhifadhi Mazingira na Kutengeneza Teknolojia rahisi ya kutenganisha Madini ya Shaba ili kuwawezesha Mafundi Mchundo na Wachimbaji wadogo wadogo kutenganisha shaba kwa ufanisi na tija;

(ii) kinaendelea kukamilisha ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua katika mabweni mapya ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 60. Ujenzi utakapokamilika utasaidia kuondoa maji ya mvua yanayosimama katika eneo hilo; na

(iii) kimeendelea na ukamilishaji wa kazi za nje za ujenzi wa jengo la maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,600, ukumbi wa mkutano wenye uwezo wa kuchukua washiriki 600 na *Confucius Institute* yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja.

### **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**47. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimegharamia masomo kwa jumla ya wafanyakazi 377; katika nyanja za Shahada ya Uzamivu (220), Shahada ya Uzamili (113), Shahada ya Kwanza (20), Stashahada na Astashahada (24);

(ii) kimefanya utafiti wa nishati Mbadala za Kupikia Katika Kaya nchini Tanzania, lengo ni uboreshaji wa makaa ya mawe na mabaki ya kilimo (*bio - briquettes*) kwa ajili ya matumizi ya kupikia kwenye kaya;

(iii) kimefanya utafiti katika Kanda ya Kati wa Kutambua *Sumu Kuvu (Aflatoxins)* katika vyakula vilivyo tayari kupikwa mionganoni mwa kaya na uelewa wa jamii juu ya Sumu Kuvu kwenye vyakula vyaa watoto;

(iv) kimeratibu tafiti 4 zilizolenga kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu chini ya mradi wa LANES katika maeneo yafuatayo:

- (a) Kiunzi cha Upimaji wa Stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu kwa Watoto (*National Framework for the Assessment of Children's Literacy and Numeracy Learning in Tanzania*);
- (b) Mazingira ya nyumbani na darasani yanavyochangia katika kujenga Stadi za Kusoma na Kuhesabu kwa wanafunzi wa Darasa la I & II (*Promoting Reading and Arithmetic Skills Among STD I & II Pupils in Tanzania Primary Schools; The Role of Home and Classroom Environment*);
- (c) Kukuza Ufahamu kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi kwa kupitia Maudhui ya Kielektroniki (*Enhancing Early Grade Primary School,Pupils' Comprehension Through E-Content*); na
- (d) Kukuza Umahiri wa Usomaji wa Watoto kwa kupitia Mkakati wa Kumuendeleza Mwalimu *Improving Pupils' Reading Fluency Ability in Early Grade Through Teacher Development Strategy in Five Selected Districts*).

Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia wadau wote wa elimu kupata ufumbuzi wa changamoto za ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Msingi. Aidha, wadau wa elimu wataelewa umuhimu wa kufundisha na kujifunza kwa kutumia maudhui ya kielektroniki na kuweka mikakati ya jinsi ya kuitumia.

### **Chuo Kikuu cha Mzumbe**

**48. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimehuisha mitaala ya Programu 2 kati ya 11 za Shahada (*MSc Environment Management na MA Development Policy*) ili kuendana na Mwongozo wa Vyuo Vikuu wa mwaka 2006;

(ii) kimejenga madarasa na jengo la utawala Kampasi ya Mbeya ili kuongeza majengo ya ofisi, na hivyo kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za utawala chuoni; na

(iii) kimetekeleza mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango wa kuunganisha mifumo yake ya kieletroniki kama vile *Student Academic Registration Information System* na kuwezesha malipo ya ada kufanyika moja kwa moja kieletroniki kupitia mfumo wa Serikali wa *Government e-Pay Gateway*.

### **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**49. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimefanya utafiti wa Genetiki na Uzalishaji wa mbegu bora za mazao ambao umewezesha chuo kuzalisha mbegu bora nne za maharage kama zifutavyo: SUA -90-1990; Rojo-1997; Mshindi-2006; na Pesa-2006. Sifa za mbegu hizi ni kuzaa zaidi na kustahimili ukame na magonjwa. Aidha, maharage yake huiva kwa haraka yanapopikwa ukililinganisha na mbegu za asili. Mbegu hizi zimeanza kuzalishwa na wakulima katika baadhi ya sehemu za Mikoa ya Morogoro na Kilimanjaro. Pia mbegu hizi bora zimetumiwa na wazalishaji wa mbegu kuzalisha mbegu bora zaidi hapa nchini na katika nchi tunazoshirikiana nazo ambazo ni Marekani na Zambia;

(ii) kimefanya utafiti kuhusu Sayansi na Teknolojia ya Chakula ambapo utafiti huo umegundua matumizi ya unga wa ubuyu kwa matumizi mbalimbali hususan katika kutengeneza "jam" na kujiongezea kipato. Matokeo ya utafiti huu yamepata haki miliki yenye namba TZ/P/10/CC276 kutoka (*Business Registrations and Licensig Agency - BRELA*) ya mwaka 2016;

(iii) kimefanya utafiti kuhusu kuzalisha Mbegu bora mbili za mpunga ambazo ni Mwangaza na Kalalu. Mbegu

hizi zimesaidia wakulima wa zao la mpunga kukabiliana na ugonjwa wa mpunga ujulikanao kama "Rice Mottle Virus" na hivyo kuwa na kilimo cha mpunga chenye tija. Mbegu hizi zinakomaa mapema na hazishambuliwi na wadudu tajwa;

(iv) kimefanya utafiti wa kutumia menejimenti ya ekolojia kudhibiti panya kwenye mazao ya mahindi na mpunga. Mradi huu umebuni teknolojia ya kudhibiti panya waharibifu na hivyo kuongeza uzalishaji na pato la wakulima;

(v) kimefanya utafiti kuhusu magonjwa ambukizi ya binadamu na mifugo. Utafiti huu umeboresha ukusanyaji wa taarifa za magonjwa kwa haraka na utengenezaji wa zana za utambuzi wa magonjwa vijiji hasa ya mlipuko na hivyo kupunguza athari za magonjwa hayo kwa jamii kuititia *African Centre of Excellence for Infectious Diseases*;

(vi) kimeandaa mitaala mipya 10 ya Shahada ya Kwanza na 7 ya Shahada za Uzamili;

(vii) kimenunua jumla ya vitabu 1,018 katika fani 594 kati ya vitabu 1,000 vilivyopangwa kununuliwa; na

(viii) kimeanza ujenzi wa jengo la wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu katika Shule Kuu ya Uchumi Kilimo na Masomo ya Biashara.

### **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**50. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2017/18 chuo kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeendelea na tafiti mbalimbali zikiwemo tafiti za magonjwa yasiyoambukiza, yanayoambukiza na yasiyopewa kipaumbele kama vile Tafiti za Ukimwi (*DNA-prime HIV vaccine, Key population size estimation and intergrated Biobehavioral surveys*), malaria (*Atemethanine resistance studies*), Kichocho (*Female Genital Schistosomiasis and*

*Linkage to HIV) na magojwa yasiyoambukiza (Etiology of esophageal cancer, genetics of cancer, Gene-expert for Diagnosis of Breast Cancer);*

- (ii) kimeendelea kutoa huduma na mafunzo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Mifupa Muhimbili;
- (iii) kimeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na Afya ya Binadamu kwa serikali kama vile Mpango wa kuzuia Malaria, UKIMWI, Chanjo kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama UNAIDS, UNICEF na WHO;
- (iv) kimeboresha jukwaa la kujifunzia kupitia TEHAMA (*E-learning platform*) kwa wanafunzi wa Shahada mbalimbali ikiwemo Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii - *Masters of Public Health* kwa masafa yanatumia jukwaa hill;
- (v) kimeendelea na ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo Kampasi ya Mloganzila;
- (vi) kimekamilisha Mwongozo wa Tiba na Njia Bora za Kujikinga na VVU ili kuwezesha watoa huduma kutoa huduma kwa usahihi na kwa umahiri;
- (vii) kimeratibu ufunguzi wa majoribio (*mock opening*) na ufunguzi laini (*soft opening*) wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Mloganzila ili kuanza kutoa huduma za tiba katika hospitali hiyo; na
- (viii) kimeendelea na ujenzi wa mabweni na majengo mengine ya ufundishaji kwenye Kampasi ya Mloganzila.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**51. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Chuo kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimeendelea na jumla ya miradi 5 ya shughuli za utafiti na kutoa machapisho 6;

- (ii) kimeanzisha programu za Shahada ya Uzamili katika Elimu kwa masomo ya Kemia, Baiolojia na Jiografia;
- (iii) kimeweza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanafunzi na wanajumuiya ya chuo kwa kufanikisha ujenzi wa jengo la huduma za kibenki kwa ushirikiano na Benki ya CRDB;
- (iv) kimewajengea uwezo wafanyakazi 78 katika ngazi mbalimbali ambapo wanataaluma 67 na wafanyakazi waendeshaji 11 wako masomoni; na
- (v) kimeboresha na kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kumalizia ujenzi wa ukumbi wa mihadhara ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1200 kwa wakati mmoja na utakuwa na vyumba 20 vya ofisi za Wallimu na vyumba 2 vya kuhifadhi mitihani.

#### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**52. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi 47 wenyе mahitaji maalum;
- (ii) kimeimarisha miundombinu ya TEHAMA kwa kununua vifaa vya Mfumo wa Mtandao wa Taarifa za Kijiografia ikiwemo ununuzi na uunganishaji wa Kompyuta 20; Aidha kimenunua Kompyuta 10 kwa ajili ya maabara ya wanafunzi na 25 kwa ajili ya wafanyakazi;
- (iii) kimeajiri wafanyakazi 16 kati yao 10 wanataaluma na 6 waendeshaji; na
- (iv) kimeajiri wafanyakazi 16 kati yao 10 wanataaluma na 6 waendeshaji.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**53. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimenunua na kufunga vifaa vyatya kisasa vyatya kufundishia na kufunga viti visivyo hamishika kwenye madarasa 5 katika Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 692 kwa wakati mmoja. Vifaa na viti hivyo vimeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (ii) kimekamilisha ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi katika Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 720 kwa wakati mmoja. Kukamilika kwa Hosteli hii kumeongeza fursa ya wanafunzi kuishi katika mazingira bora na tulivu; na
- (iii) kimepata vitabu 20,000 vipyta kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya maktaba ya Chuo, uwepo wa vitabu hivyo umeboresha huduma za maktaba.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**54. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi mwaka 2017/18, Chuo kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimeandaa mitaala 12 na kuwasilishwa Tume ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya kupatiwa ithibati. Mtaala wa Stashahada ya Uhandisi wa Vifaa Tiba umepata ithibati sambamba na Idara itakayokuwa na dhamana ya kutoa mafunzo hayo;
- (ii) kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 105, Stashahada mmoja, Shahada ya Kwanza 20, Shahada ya Uzamili 52 na Shahada ya Uzamivu 32. Aidha, watumishi 41 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi;
- (iii) kimetoa ushauri elekezi katika miradi ifuatayo:
  - (a) ukarabati wa shule za sekondari 17 na vyuo vyatya ualimu 15 vyatya Serikali;

- (b) ujenzi wa ofisi za Halmashauri za Wilaya za Kiteto na Mafia;
  - (c) kiwanda cha kusaga nafaka cha *East African Starch Ltd* kilichopo Mbeya;
  - (d) barabara ya lami Sumbawanga; na
  - (e) jengo la *X-ray* katika Hospitali ya Kanda ya Rufaa Mbeya.
- (iv) kimeendelea na ujenzi wa maktaba awamu ya kwanza ambao umekamilika kwa asilimia 57. Jengo hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2500 kwa wakati mmoja.

### **Chuo cha Ufundı Arusha**

**55. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Chuo kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimedahili wanafunzi **900** wa mwaka wa kwanza (Astashahada na Stashahada);
- (ii) kimeanzisha programu tatu **(3)** mpya ambazo ni "*Pipe Works, Oil and Gas Engineering*" (Astashahada), "*Electrical and Hydropower Engineering*" (Astashahada) na "*Electrical & Automation Engineering*" (Shahada);
- (iii) kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa jumla ya watumishi 43 na watumishi 11 waligharamiwa mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo haya yataongeza umahiri wa watumishi katika kutoa mafunzo, kufanya tafiti pamoja na ushauri wa kitaalamu ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia;
- (iv) kimepata vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia iliyonunuliwa kwa mkopo nafuu kutoka Serikali ya Austria kwa ajili ya Karakana 2 za Uhndisi Magari na Karakana 1 ya Useremala. Vifaa hivi vitasaidia kuongeza

wataalamu wa ufundi (nguvu kazi) kwenye sekta ya viwanda ili kutekeleza Sera ya nchi kuelekea kwenye Uchumi wa katiba wa viwanda; na

(v) kimekamilisha ujenzi wa bwawa la kuvuna maji ya mvua, mifereji ya umwagiliaji na miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mafunzo ya umwagiliaji Oljoro.

### **Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**56. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 2,089 (wanaume 1,648; wanawake 441) ambapo, Stashahada ya Kawaida ni 1,063; Shahada ya Kwanza ni 998 na Shahada ya Umahiri ni 28. Aidha, imesajili wanafunzi 17 katika Kampasi yake mpya ya Myunga iliyopo Songwe kwa ajili ya kozi mpya ya Ufundi Mchundo katika Teknolojia ya Habari (*Technician Certificate NVA Level 3 Technician Certificate NVA Level 3*);

(ii) imeandaa Mtaala na kuanzisha kozi mpya ya Stashahada ya Kawaida ya Teknolojia ya Bidhaa za Ngozi (*Ordinary Diploma in Leather Products Technology (NTA Level 4-6)*) katika Kampasi ya Mwanza na kuuwasilisha kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) kwa ajili ya kupatiwa ithibati. Vilevile imeandaa mtaala wa kuanzisha kozi mpya ya Shahada ya Umahiri katika Uhandisi wa Nishati Endelevu (*Masters of Engineering in Sustainable Energy*) na kupata ithibati ya NACTE. Masomo yataanza mwaka wa masomo wa 2018/19;

(iii) imenunua magari 2 (Basi aina ya Isuzu yenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 60 na *Toyota Hilux Double Cabin*) kwa ajili ya kuwezesha mafunzo viwandani;

(iv) imegharamia chakula kwa wanafunzi 683 na mafunzo kwa vitendo (*Industrial Practical Training*) kwa wanafunzi 550 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT); na

(v) imeweka vifaa vya TEHAMA katika jengo la kufundishia (*Teaching Tower*) na samani katika baadhi ya vyumba.

### **Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha**

**57. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili wanafunzi 187 na kufikisha jumla ya wanafunzi 400 kutoka 213 ikiwa ni ongezeko la asilimia 88. Ongezeko hili limetokana na msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na Vituo Mahiri katika kufadhili wanafunzi;

(ii) imeandaa program 2 za uzamili na uzamili ambazo ni PhD in *Innovation and Management* na MBA in *Intellectual Property Right* na kuwasilishwa TCU kwa ajili ya kupewa ithibati. Aidha, imeandaa mitaala 10 katika Shule ya Sayansi ya Viumbe Hai na Uhandisi Biolojia (*Life Sciences and Bio- Engineering*) na Sayansi ya Hisabati na Ukokotoaji;

(iii) imefungua vituo vinne vya Umahiri vya kimataifa vinavyofadhiliwa na wafadhili mbalimbali. Vituo hivi ni:

(a) kituo cha Utafiti na Umahiri katika Ufundishaji Endelevu katika Chakula na Uhifadhi wa Virutubisho na usalama wa chakula - *Centre for Research, Agricultural advancement, Teaching Excellence and sustainability in food and nutritional security* kinachofadhiliwa na Benki ya Dunia;

(b) kituo cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu - *Water Infrusrtucture and Sustainable Energy* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia;

(c) kituo cha TEHAMA Afrika Mashariki - *Centre of ICT in East Africa* kwa ufadhili wa DAAD Ujerumani; na

(d) kituo cha Ubunifu wa Teknolojia na Nishati (*Innovative Technology and Energy*) chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea.

(iv) inatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya majitaka ya machinjio ya Mwanza kwa kujenga mfumo wa kisasa wa kusafisha majitaka yatokanayo na machinjio kuu na kuzalisha gesi kwa matumizi ya machinjioni. Mradi huu uko katika hatua za majoribio ya mwisho; na

(v) imeanzisha mradi wa utafiti wa uzalishaji wa ndizi bora na zenyе kuhimili magonjwa ambapo imeanzisha vituo vyा mafunzo Tarakea na Lyamungo kwa ajili ya kutoa mbegu bora za migomba ya aina mbalimbali.

#### **UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18**

**Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu - EP4R)**

**58. Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga katika kuimarisha Sekta ya Elimu kwa kuzingatia ubora na usimamizi wa rasilimali fedha na manunuzi ya umma kwa ajili ya mipango ya elimu. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara kuititia mradi wa Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) imetekeliza shughuli zifuatazo:

(i) imeandaa michoro ya majengo, makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi 50 za Uthibiti Ubora wa Shule. Kazi inayoendelea ni kuchambua gharama za ujenzi kutoka kwa wakandarasi. Kazi ya ujenzi itaanza mwezi Juni, 2018;

(ii) imewezesha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Vyuo 7 vya Ualimu Awamu ya Pili ambapo ukarabati upo katika hatua mbalimbali. Vyuo hivyo ni Tandala, Nachingwea, Tarime, Kinampanda, Mandaka, Patandi na Ilionga Aidha, Chuo cha Murutunguru kimeanza kujengwa

upya kufuatia taarifa ya Wahandisi kubaini kuwa chuo hicho kimechakaa na hakifai kufanyiwa ukarabati;

(iii) imegharamia ujenzi wa mgahawa wenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja katika Bweni la Nicholous Kuhanga Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambapo ujenzi umefikia asilimia 70 ya ukamilishaji;

(iv) imenunua magari 54 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora wa shule na ufuutiliaji na tathmini;

(v) imewezesha kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa utakaokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa mkupuo;

(vi) imewezesha ujenzi wa maabara katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa – MUCE kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa walimu wa masomo ya Sayansi katika shule za sekondari;

(vii) imesimamia na kutekeleza vipaumbele na viashiria vya Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (*Education Program for Results - EP4R*) na kuwezesha Serikali kupata Dola za Kimarekani milioni 49.7 sawa na **Shilingi 109,340,000,000.00**; na

(viii) imewezesha ujenzi wa miundombinu katika Shule 290 (Msingi 180 na Sekondari 110) ikiwemo madarasa 1,308, matundu ya vyoo 1,560, mabweni 129, nyumba za walimu 8 (*2 in one*), mabwalo 7, majengo ya utawala 10, maabara 4 na maktaba 1.

#### **Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya KKK**

59. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wenyewe umri wa miaka 5-13 walio ndani na nje ya mfumo rasmi. Mpango huu unafadhiliwa na

mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu (*Global Partnership for Education-GPE Fund*). Katika mwaka 2017/18 Wizara kuititia mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya KKK (*GPE-LANES*) imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

- (i) ukamilishaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule ambacho kimepitishwa na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na kitawezesha kufanya shughuli za uthibiti wa ubora wa shule kwa ufanisi zaidi;
- (ii) ununuzi wa pipipiki 2,894 ambazo zitasambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali katika mikoa 19 ifikapo mwezi Juni, 2018;
- (iii) imenunua magari 5 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Uthibiti Ubora wa shule; na
- (iv) kuandaa maudhui ya kieletroniki na kuweka mikakati ya kutumia maudhui hayo katika ufundishaji na ujifunzaji wa KKK. Rasimu ya awali imekamilika na iko katika kufanyiwa majaribio.

#### **Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**60. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umejikita katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vya Ualimu pamoja na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Katika mwaka 2017/18, Wizara kuititia mradi huu imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

- (i) umegharamia ununuzi wa vitabu 1,948 vya fani za umeme, madini, ujenzi na umwagiliaji katika;
- (ii) umegharamia usanifu wa jengo la ghorofa tatu la maabara, madarasa na ofisi za wakufunzi katika Chuo cha Ufundi Arusha. Mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo amekabidhiwa eneo la ujenzi tarehe 19 Machi 2018 na kazi ya ujenzi inaendelea; na

(iii) umegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi saba wa Chuo cha Ufundı Arusha na watumishi watano wa Vyuo vya Ufundı Stadi.

### **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu**

**61. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Canada. Mradi unalenga kuboresha miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzi katika vyuo vinne vya ualimu. Katika mwaka 2017/18 Wizara kuititia mradi huu imetekeleza shughuli zifuatazo katika Vyuo vya Ualimu vya Ndala, Shinyanga, Kitangali na Mpuguso:

(i) imekamilisha ujenzi wa jengo la nyumba za walimu la ghorofa 2 kwa ajili ya familia 4 ambalo tayari limekabidhiwa katika Chuo cha Ualimu Shinyanga. Aidha, imeendelea na ujenzi wa majengo 2 ya bweni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 152 kila moja na ujenzi wa uzio kwa ujumla umekamilika kwa asilimia 90. Aidha, Ujenzi wa majengo 2 ya madarasa yenye vyumba 8, ujenzi wa maktaba na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara vimefikia asilimia 60;

(ii) imeendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu Mpuguso yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 308, nyumba za walimu majengo 3 ya ghorofa na nyumba 1 ya kawaida kwa ajili ya familia 13 vyote kwa ujumla vimekamilika kwa asilimia 85. Ujenzi wa maktaba, maabara, ukumbi wa mihadhara, ukumbi wa mkutano na ujenzi wa vyoo ambavyo kwa ujumla vimekamilika kwa asilimia 62;

(iii) imeendelea na ujenzi wa nyumba 11 za Wakufunzi katika Chuo cha Ualimu Kitangali ikiwemo nyumba ya Mkuu wa Chuo ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 68. Aidha, ujenzi wa madarasa vyumba 16, maktaba, ukumbi wa mihadhara kwa wanafunzi 240, na majengo mawili ya mabweni yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 308 umefikia asilimia 60; na

(iv) imendelea na ujenzi wa nyumba 5 za wakufunzi (kiwemo nyumba ya Mkuu wa Chuo) katika Chuo cha Ualimu Ndala; majengo 2 ya ghorofa kwa ajili ya wakufunzi yenye uwezo wa kuchukua familia 8; vyote kwa ujumla vimekamilika kwa asilimia 70. Aidha, katika sehemu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Ualimu Ndala, Mkandarasi Skywards Construction company alikabidhiwa eneo la ujenzi tarehe 27.11.2017. Ujenzi katika sehemu hii unahusisha: mabweni 2 ya ghorofa, madarasa ghorofa 2, jengo la mihadhara, maktaba na maabara. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 24.02.2018 na inatarajiwa kukamilika kwa kipindi cha miezi 18 tangu kuanza kwa kazi. Kwa sasa ujenzi upo hatua ya msingi kwa majengo yote.

#### **Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu**

**62. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unalenga kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu katika Vyuo 35 vya Ualimu vya Serikali. Katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia mradi huu imetekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Vyuo 35 vya Ualimu ili kuweka mazingira rafiki ya utoaji elimu ya Ualimu;
- (ii) imeanza Mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Ualimu ili kuwa na mtaala unaokidhi mahitaji ya sasa na unaoendana na mtaala wa elimu msingi ulioboreshwa;
- (iii) imetangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa na Kemikali za Maabara za Sayansi kwa Masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia kwa ajili ya vyuo vya ualimu kuwezesha ujifunzaji wa masomo hayo kwa vitendo;
- (iv) imetangaza zabuni ya Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji;

(v) imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 120 yaliyojumuisha elimu ya jinsia na elimu jumuishi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika Vyuo vya Ualimu; na

(vi) imempata mkandarasi na mshauri elekezi wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ili kuongeza uwezo wa kudahili na pia kuweka mazingira mazuri ya ujifunzaji kwa kuwa majengo yaliyopo hayafai kwa ukarabati. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei 2018.

### **TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**63. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza mafanikio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) kwa mwaka 2017/18 naomba sasa nitoe utekelezaji wa Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18).

**64. Mheshimiwa Spika,** Tume hii ina jukumu la kuratibu na kutoa ushauri kuhusu Elimu, Sayansi, Habari na Utamaduni katika muktadha wa kimataifa. Aidha, Tume inashiriki katika kutengeneza viwango vya ubora vinavyotakiwa katika Nyanja ya Elimu, Sayansi na Utamaduni kwa kutoa maoni moja kwa moja au kwa kushirikisha wadau kutoa maoni katika maandalizi ya nyaraka mbalimbali kama vile mikataba na makubaliano ya kimataifa.

**65. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Tume ilikadiria kukusanya maduhuli yenyeye thamani ya **Shilingi 40,000,000.00**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Tume imekusanya jumla ya **Shilingi 57,529,487.17** sawa na asilimia **144** ya lengo.

**66. Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2017/18 yalikuwa ni **Shilingi 663,123,000.00** (Mishahara **Shilingi 330,830,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 332,293,000**). Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2018 Tume imepokea jumla ya **Shilingi 500,972,100** sawa na asilimia **76** ya makadirio. Kati ya fedha hizo

Mishahara ni **Shilingi 246,668,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 254,304,100.00**.

**67.** **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2018 Tume imetumia jumla ya **Shilingi 425,223,615.00** sawa na asilimia **85** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 246,668,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 178,555,615.00**.

**68.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Tume imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imeratibu udhamini kwa ufadhili wa UNESCO wa mafunzo kwa watanzania 8; nchini Korea 3, Ireland 1, Israel 1 na China 3;
- (ii) imeandaa, kuchapisha na kusambaza jarida la "Tanzania na UNESCO" Toleo la 14 ambapo nakala 700 zimesambazwa kwa wadau mbalimbali;
- (iii) imeandaa maandiko 7 ya Miradi ya kuboresha Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Mawasiliano na Habari pamoja na Utamaduni na Urihi wa Dunia kwa ajili ya ufadhili kutoka UNESCO na Wadau wengine;
- (iv) imetoa mafunzo ya namna ya kutambua, kuhakiki ubora wa taarifa kwa wanafunzi wa Sekondari za Jangwani, Azania, Tambaza na Zanaki;
- (v) imekagua na kufanya tathmini katika Hifadhi ya Milima ya Udzungwa ili kuona kama kuna uwezekano wa kuwa na maeneo Tengefu ya Ndege;
- (vi) imekagua Mradi wa "*Heritage Archive of Tanzania*";
- (vii) imetoa mafunzo kwa wanachuo na vijana mbalimbali kuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia yaliyofanyika Zanzibar;

(viii) imekusanya data ili kusaidia katika program ya *Preservation of Digital Heritage (Collection of Arabic Manuscripts and Books)*;

(ix) imeratibu Ushiriki wa nchi yetu pamoja na ripoti za Mtandao wa Kishule wa UNESCO-ASP Net, nchini Kenya; na

(x) imeshiriki katika mikutano mikuu iliyofanyika nchini Ghana, Ufaransa na Ujeruman kuhusu maeneo Tengefu (*Biosphere Reserves*) ilijojadili juu ya Kupunguza Umaskini Kupitia Maendeleo Endelevu.

**69. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza kwa kirefu utekelezaji wa mafungu yote mawili yaani Fungu 46 na Fungu 18 naomba sasa nielezee Mpango na Bajeti ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2018/19.

### **C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA 2018/19**

**70. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19, Wizara yangu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

#### **Kuendeleza Elimu ya Msingi kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu**

**71. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Vyuo vya Elimu ya Ualimu vitadahili jumla ya wanachuo **8,152** wa Mafunzo ya Ualimu wakiwemo **2,470** wa ngazi ya Astashahada na **5,682** wa ngazi ya Stashahada ya masomo ya Sayansi (2,863), Elimu Maalum (395), Elimu ya Ufundı (116), Elimu ya Awali (1,563), Masomo ya Fani (124), Michezo (315), Elimu ya Msingi (762) na Stashahada ya Sayansi Jamii (2,014).

**72. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo, Wizara itatoa mafunzo kwa Wanachuo **20,535** wa Vyuo vya Ualimu wa mwaka wa Kwanza hadi wa Tatu ili kuoanisha nadharia na vitendo. Aidha, itatoa mafunzo kabilishi kwa Wanafunzi wasichana 200 wa Kidato cha Sita wa masomo ya Sayansi na Hisabati wenye sifa pungufu (*Principal Pass* moja na *Subsidiary* moja) kwenye masomo

ya kufundishia ili wapate sifa stahiki za kusomea Stashahada ya Ualimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

**Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo Katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**73. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kuvii marisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kutoa mafunzo bora kwa kufanya yafuatayo:

- (i) kujenga mazingira bora ya kutolea mafunzo kwa kujenga na kukarabati Miundombinu katika Vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi;
- (ii) kuwajengea uwezo Wakufunzi na Watumishi wengine 250 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili waweze kutoa elimu bora ya nadharia na vitendo kwa wanafunzi;
- (iii) kuratibu zoezi la tathmini ya kubaini mahitaji ya sasa ili hatimaye kuandaa mitaala ya kozi fupi zitakazopewa ithibati na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu pamoja na kozi zitakazo lenga kuleta chachu ya maendeleo ya wananchi katika eneo husika; na
- (iv) kugharamia chakula kwa wanafunzi 5,050 katika Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi.

**Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundu**

**74. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kusimamia Sera, Sheria na Miongozo katika Sekta ya Elimu ili kuhakikisha kuwa elimu katika ngazi zote inatolewa kwa ubora unaokusudiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) itapitia Sera ya Elimu na Mafunzo kwa Lengo la kuhakikisha kuwa inaendana na hali halisi ya sasa;

- (ii) itapitia Miongozo na Nyaraka mbalimbali zinazohusu utoaji wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari nchini ili ziendane na mahitaji ya sasa; na
- (iii) itaandaa miongozo na nyaraka kadri mahitaji yatakavyo jitokeza.

#### **Kuainisha Mahitaji ya Nchi Katika Ujuzi na Kuuendeleza**

**75. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19, Wizara kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kazi kwa ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi itatekeleza yafuatayo:

- (i) kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za kazi kwa kutoa ruzuku kwa ushindani kwa Vyuo vya Ufundii nchini;
- (ii) kuendelea kutoa ruzuku za Masomo ya Ufundii kupitia Skimu za Vocha za Mafunzo (*Trainee Voucher Scheme*) kwa vijana wasio na uwezo wa kuijendeleza ambapo jumla ya vijana 7000 watanufaika;
- (iii) kuviwezesha Vyuo 20 vya Maendeleo Wananchi kutoa mafunzo ya ufundi kwa kuvikarabati na kuvinunulia vifaa;
- (iv) kuzijengea uwezo taasisi za VETA, NACTE na TCU ili kusimamia Ubora wa Elimu ya Ufundii na Stadi za Kazi; na
- (v) kuimarisha Vyuo vya VETA na Elimu ya Ufundii kwa kuvinunulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya Uanagenzi (*Apprenticeship*).

#### **Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**76. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kusimamia Ithibati ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu na Kusimamia Ubora wa Elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) kuanzisha mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vituo Nje ya Mfumo Rasmi;
- (ii) kufanya ufuatiliaji wa Shule, Vyuo vya Ualimu na vituo Nje ya Mfumo Rasmi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kuangalia kama vinakidhi vigezo;
- (iii) kukagua jumla ya asasi **11,327** zikiwemo shule za Msingi **8,785** za Sekondari **2,480** na Vyuo vya Ualimu **62**;
- (iv) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Miongozo na Nyaraka kuhusu uboreshaji wa Elimusingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu;
- (v) itafanya tafiti mbalimbali za kielimu kwa lengo la kubaini changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji ili ziweze kupatiwa ufumbuzi; na
- (vi) itakarabati Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule 40 za Wilaya za zamani kwa gharama ya **Shilingi Billioni 1.5**.

#### **Usimamizi wa Elimu ya Msingi na Sekondari**

**77.** **Mheshimiwa Spika**, Katika kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari, katika mwaka 2018/19 Wizara itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaandaa Mwongozo wa Kitaifa wa uendeshaji wa Elimu ya Awali unaozingatia viwango. Lengo la Mwongozo huo ni kufafanua viwango vya Elimu ya Awali kwani kwa sasa kuna mifumo mingi ambayo inahitaji uratibu wa karibu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi hao kusoma katika mazingira tulivu na salama yenye kusaidia kuinua ubora wa elimu na mafunzo;
- (ii) itagharamia chakula kwa wanachuo 20,236 na Mafunzo kwa Vitendo (*BlockTeaching Practice - BTP*) kwa wanachuo 12,782 katika Vyuo vya Serikali 35 vya Ualimu;

(iii) itafanya ufuatilaji wa utoaji wa Elimu ya Awali na Msingi kwa kuzingatia matokeo ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Pili na la Nne pamoja na Mtihani wa kuhitimu Darasa la Saba;

(iv) itafanya ufuatilaji wa uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza katika shule tatu za Msingi kwa kila kanda 11; na

(v) itafanya ufuatilaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera zinazohusu Elimu ya Sekondari ili kuinua ubora wa Elimu itolewayo.

#### **Usimamizi wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

**78. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itafanya yafuatayo:

(i) kutekeleza mpango wa Mtaala wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo wa Elimu (*Intergated Program for Out of School Adolescent-IPOSA*) wenye Stadi za Kisomo (KKK), Ufundii Stadi wa Awali (*Pre-Vocational*), Stadi za Maisha (*Life Skills*) na Ujasiriamali (*Enterprenuership*) kuititia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

#### **Usimamizi wa Masuala Mtambuka katika Elimu**

**79. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kusimamia Masuala Mtambuka kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kuwajengea uwezo walimu wa malezi Shulenii na katika Vyuo vya Ualimu ili kuimarishe stadi za utoaji wa Huduma ya Ushauri na Unasihi kwa wanafunzi, kwa lengo la kukabiliana na changamoto wanazopata;

(ii) kusambaza mwongozo wa utoaji Huduma ya Ushauri na Unasihi shulenii na katika Vyuo vya Ualimu ili kuimarishe huduma hiyo; na

(iii) kuendesha mafunzo ya Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika mikoa kumi ya Tanzania Bara.

**Usimamizi wa Elimu Maalum**

**80. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa Elimu ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania, Wizara kwa mwaka 2018/19 itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2018-2021 ili kuwawezesha wadau wa elimu kushiriki kwa ufanisi katika utekelezaji wake;

(ii) itafanya ufuutiliaji wa utoaji wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ili kuhakikisha kuwa wanafaidika na fursa za Elimu nchini; na

(iii) itaandaa mkakati maalumu wa kutoa Elimu maalumu utakaowezesha kupunguza changamoto za ufundishaji, ujifunzaji na utahini ambazo zinawakabili walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**81. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/2019 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) kuratibu ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera kitakachojengwa kwa ruzuku kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;

(ii) kuendelea na ujenzi wa chuo cha Mkoa cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Njombe na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Mikoa ya Rukwa, Simiyu na Geita; na

(iii) kugharamia chakula na mafunzo kwa vitendo (*Industrial Practical Training*) kwa wanafunzi 903 wa Chuo cha Ufundi Arusha.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**82. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Wizara imepanga kufanya yafuatayo:

- (i) kuratibu Skolashipu za Wanafunzi wa Vyuo Vikuu zinazotolewa na nchi rafiki za Jumuiya ya Madola (Uingereza na New Zealand) pamoja na nchi nyingine zikiwemo China, Hungary, Russia, Algeria na Misri;
- (ii) kufadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (iii) kufutilia maendeleo ya udahili na uandikishwaji wa Wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu na maendeleo ya utoaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;
- (iv) kufutilia utendaji wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (*African Centre of Excellence – [ACE II]*) ambavyo viko katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela; na
- (v) kuendeleza ufadhili wa masomo ya wanataaluma kutoka katika Vyuo Vikuu vya Umma katika Shahada za Uzamili na Uzamivu katika nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

### **Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**83. Mheshimiwa Spika**, Katika kutambua, kujenga, kukuza na kuendeleza ubunifu kwa Watanzania katika nyanja ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kati. Katika mwaka 2018/19 Wizara itafanya yafuatayo:

- (i) itatambua na kutegemeza teknolojia zinazozalishwa nchini na kuweka mazingira bora ya upatikanaji, uhaulishaji na uhawilishaji wa teknolojia hizo;

- (ii) itaandaa mpango kazi wa kusimamia uanzishwaji na uimarishaji wa vituo vyta kuendeleza teknolojia na ubunifu nchini;
- (iii) itaandaa programu za kujenga uelewa kwa wananchi katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kujenga uchumi wa viwanda;
- (iv) itasimamia na kuendeleza mchango wa teknolojia ya nyuklia katika maendeleo ya Taifa; na
- (v) itaandaa mkakati wa kukuza ujuzi na utaalamu asilia wa wabunifu nchini katika ngazi zote ili kuibua vipaji vyao.

#### **Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu**

**84. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Wizara itatekeleza yafuatayo:

- (i) kuanza Ujenzi wa Ofisi ya Wizara Dodoma kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya watumishi ya kufanya kazi;
- (ii) kuandaa Mpango wa Wizara wa Kurithishana Madaraka (*Succession Plan*) kwa lengo la kuandaa watumishi kwa ajili ya kushika madaraka;
- (iii) kutoa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (*Open Performance Review and Apraisal System – OPRAS*) kwa watumishi wa ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi;
- (iv) kuendeleza matumizi ya Mfumo wa mawasiliano wa kupokea, kutunza na kusambaza nyaraka za ofisi (*E-Office*) kwa kuwapa mafunzo watumishi wa masjala ili kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yao; na

(v) kuhakiki vyeti vya elimu na taaluma kwawaombaji wa kazi ya ualimu katika shule za Serikali kulingana na vibali vitakavyotolewa kwa lengo la kuhakikisha kuwa watakaoajiriwa wanakidhi vigezo vya Muundo wa Utumishi wa Kada za Walimu.

### **Usimamizi wa Rasilimali za Wizara**

**85. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kukagua Mapato na Matumizi ya Wizara na taasisi zifuatazo; Vyuo vya Ualimu 15, Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za Kanda 11, Vituo vya Elimu vya Uchapaji 2 (*PRESS A* na *Kisomo Mwanza*);
- (ii) kukagua menejimenti ya rasilimaliwateru na malipo ya mishahara kwa watumishi wa Wizara;
- (iii) kukagua taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba yote ya Wizara;
- (iv) kukagua miradi yote ya maendeleo inayotekelze wa Wizara;
- (v) kukagua fedha zinazopelekwa katika Taasisi 6 za Wizara (*HESLB, NECTA, NACTE, TEA, ADEM* na *TIE*);
- (vi) kukagua mifumo ya utawala bora na uendeshaji wa Wizara; na
- (vii) kukagua utunzaji wa mali za Wizara (*Asset Management*).

### **URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**86. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Taasisi na Wakala tunazozisimamia. Shughuli zilizopangwa kufanyika mwaka 2018/19 katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:

## Taasisi ya Elimu Tanzania

**87. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Taasisi litatekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kuboresha mtaala wa Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne na mtaala wa Elimu ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada;
- (ii) kuendelea na uandishi wa vitabu vya kiada kwa Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita na Moduli/Vibutu vya Elimu ya Ualimu pamoja na kuandaa maudhui ya kielektroniki kwa Darasa la Kwanza na la Pili;
- (iii) kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa Elimumsingi kwa kutumia mtaala ulioboreshwa;
- (iv) kurusha hewani vipindi vya Vikaragosi (*Cartoons*) kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na la Pili, kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu( KKK);
- (v) kuandika vitabu vya hadithi vya shule za msingi; kufanya uhakiki na tathmini ya vitabu vya ziada na maudhui ya kielektroniki; na
- (vi) kuandika na kuchapa Mitaala, Mihtasari na Moduli za Mafunzo kwa ngazi ya Cheti na Stashahada ya Ualimu.

## Baraza la Mitihani la Tanzania

**88. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Baraza litatekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,609,247 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2018;
- (ii) kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 965,255 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Septemba, 2018;

- (iii) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 547,846 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2018;
- (iv) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 440,382 pamoja na mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,500 wanaotarajiwa kufanya Mitihani hiyo mwezi Novemba, 2018;
- (v) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 80,628 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2019;
- (vi) kuendesha Mtihani wa Cheti na Stashahada ya Ualimu kwa watahiniwa 12,500 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2019;
- (vii) kuendesha upimaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 10,250 wa Darasa la Pili;
- (viii) kutoa na kusambaza vyeti kwa wahitimu wa Darasa la Saba;
- (ix) kuandaa Miundo ya Mitihani (*Examination Format*) ya Kidato cha Pili, Kidato cha Nne, na Kidato cha Sita kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa elimu; na
- (x) kuchapa na kusambaza vitabu vya tathmini ya Upimaji na mitihani ya kitaifa katika ngazi zote za Elimu ya Msingi na Sekondari.

#### **Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**89. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2018/19 Mamlaka imetenga kiasi cha **Shilingi 9,750,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatizo:

- (i) kuwezesha ujenzi wa nyumba 15 za walimu katika shule za sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi;

- (ii) kuwezesha ujenzi wa madarasa 300 kwenye shule za msingi 60 zenyenye uhitaji mkubwa;
- (iii) kuwezesha ujenzi wa mabweni 10 ya wasichana kwenye Shule za Sekondari zilizo kwenye maeneo magumu kufikika; na
- (iv) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**90. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Taasisi imetenga jumla ya **Shilingi 2,852,474,000** kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo;

- (i) kuandaa na kutoa mafunzo ya wawezeshaji wa programu za kisomo na kufanya kampeni ya kisomo kwa kanda za kitaaluma kujenga na kuweka mtandao wa TEHAMA ili kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji wa programu za elimu na mafunzo za TEWW;
- (ii) kuongeza wanafunzi wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka 10,420 mpaka 12,000 kwa kufungua vituo kwenye mikoa mipyä mitano ya Songwe, Geita, Katavi, Njombe na Simiyu;
- (iii) kuimarisha uwezo wa Maktaba ya TEWW kwa kuweka mifumo ya TEHAMA itakayotumika katika ufundishaji na ujifunzaji na kuongeza eneo la kujisomea;
- (iv) kufanya utafiti katika programu ya elimu nje ya mfumo rasmi ili kubainisha hali ya sasa ya vijana na watu wazima wasio na stadi za kisomo na kupata taarifa mahususi za kupanga mikakati ya kuwapatia elimu stahiki; na
- (v) kukarabati na kufanya upanuzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Kampasi ya Morogoro.

## Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufund Stadi

**91. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018/19 Mamlaka imetenga **Shilingi 39,491,923,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu katika vyuo vya Ufund Stadi nchini kutoka 200,000 mpaka 250,000;
- (ii) kuanza ujenzi wa Chuo cha Ufund Stadi cha Kagera;
- (iii) kujenga karakana 3 katika vyuo vya mafunzo ya Ufund Stadi katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Manyara;
- (iv) kuendelea na ujenzi wa karakana 2 za ufund wa zana za kilimo na ufund wa uungaji vyuma katika chuo cha Ufund Stadi Arusha;
- (v) kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufund Stadi katika Wilaya za Chunya, Kilindi, Nyasa na Ukerewe;
- (vi) kumalizia ujenzi wa madarasa 2 na mabweni 2 katika chuo cha Ufund Stadi cha Wilaya ya Makete;
- (vii) kuweka vifaa vya mafunzo katika karakana ya Kisasa ya Useremala katika Chuo cha VETA Dodoma;
- (viii) kuwajengea uwezo walimu wa ufund stadi ili kuboresha ujuzi wao uendane na mabadiliko ya kiteknolojia;
- (ix) kuimarisha ubora wa ukaguzi "quality audit" katika vyuo vya mafunzo ya ufund stadi vilivyo sajiliwa na VETA katika Kanda mbili;
- (x) kutoa ithibati na usajili wa kudumu kwa Vyuo vya Ufund Stadi vitakavyokidhi vigezo vilivyowekwa;
- (xi) kutoa mafunzo ya Ualimu wa Ufund Stadi Morogoro kwa walimu 700 katika ngazi ya cheti na stashahada; na

(xii) kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETMIS) ili kudhibiti taarifa za mafunzo na watumishi.

### **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundsi**

**92. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2018/19 Baraza litaendelea kuboresha Elimu na Mafunzo ya Ufundsi nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kukagua na kusajili Vyuo vya Ufundsi vitakavyokidhi sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundsi, pamoja na kukagua na kutoa miongozo itakayoviwezesha vyuo kupata ithibati kamili endapo vitakidhi vigezo vilivyowekwa;

(ii) kufuatilia na kutathimini vyuo 400 vya Elimu ya Ufundsi ili kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yana ubora na yanakidhi soko la ajira; na

(iii) kuratibu uandaaji wa Mitaala 45, kuhuisha Mitaala 6 na Kukuza Mitaala 10 ya Kitaifa inayozingatia umahiri katika vyuo vya Elimu na Ufundsi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

### **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu**

**93. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Wakala unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kudahili walimu 2,300 watakaosoma Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) na Stashahada ya Ukaguzi wa Shule;

(ii) kudahili Walimu Wakuu 486 kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Songwe na Njombe watakaosoma Astashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Shule za Msingi ili kuwajengea uwezo wa kusimamia Shule zao; na

(iii) kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa wajumbe 2,115 wa Bodi za Shule za Sekondari kuhusu Nyaraka na Miongozo mbalimbali ya

Elimu; Uongozi na Utawala wa Shule; Muundo na Majukumu ya Bodi za Shule; Usimamizi wa Fedha na Manunuzi; pamoja na Uaandaaji wa Mpango wa Maendeleo ya Shule.

### **Bodi ya Huduma za Maktaba**

**94. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Bodi itatekeleza yafuatayo:

- (i) kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;
- (ii) kutoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka katika ngazi ya Cheti cha Msingi (NTA 4) wanafunzi 350, Cheti (NTA 5) wanafunzi 320 na Stashahada (NTA 6) wanafunzi 340; na
- (iii) upanuzi wa Maktaba ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi yaraka cha Bagamoyo na jengo la Maktaba ya Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa Wananchi wa Mikoa hiyo kupata huduma za Maktaba. Kiasi cha **Shilingi 2,500,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

### **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**95. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Bodi imepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) kuunganisha na kufanya mifumo ya upangaji, ulipaji na urejeshaji mikopo kuijiendesha (*Full automation and integration of systems*);
- (ii) kutoa mikopo ya **Shilingi billioni 427** kwa wanafunzi wapatao **123,285**, katika yao wakiwemo wanafunzi wa mwaka wa kwanza **40,544** na wanafunzi wanaoendelea na masomo wapatao **82,741**;
- (iii) kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa ukusanyaji wa mikopo iliyoiva na kukusanya **Sh. 157,700,000,000.00** kwa mwaka;

(iv) kuendelea kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kurejesha mikopo kutoka kwa wanufaika, pamoja na kuujulisha umma kuhusiana na mwongozo wa utoaji mikopo kwa kuzingatia mahitaji ya kitaifa, sifa za waombaji na tarehe ya kuanza kupokea maombi ya mikopo; na

(v) kutoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye vigezo vya kupata mikopo na ruzuku hizo.

### **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**96. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Tume itafanya yafuatayo:

(i) kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa Kupitia Mifumo na Miongozo mbalimbali inayotumika kusimamia Uthibiti na Ithibati ya Elimu ya Juu nchini;

(ii) kukagua Vyuo 20 vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuhakiki ubora wake;

(iii) kufanya tathmini kwa programu 100 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini na kuzisajili zitakazokidhi vigezo;

(iv) kufanya tathmini na kutambua Tuzo 2,500 za ngazi za Shahada zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyopo nchi za nje;

(v) kuboresha Mfumo wa kutumia TEHAMA katika utoaji na ukusanyaji taarifa kutoka vyuo vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji;

(vi) kushiriki katika kongamano na mikutano ihusuyo uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini;

(vii) kuratibu Maonyesho ya 13 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu vyuo na programu mbalimbali zitolewazo; na

(viii) kuhakiki wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliodahiliwa katika vyuo vya Elimu ya Juu ili kujiridhisha kama wamekidhi vigezo vya kudahiliwa katika programu husika.

### **Vyuo vya Elimu ya Juu**

#### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**97. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kitakeleza yafuatayo:

(i) kudahili jumla ya wanafunzi 17,220 wa fani mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao; wanafunzi 4,000 watadahiliwa katika fani ya Cheti, wanafunzi 3,000 Stashahada, wanafunzi 8,000 Shahada ya Kwanza, wanafunzi 2,100 Shahada ya Uzamili na 120 Shahada ya Uzamivu; na

(ii) kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika nyanja za mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano.

#### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**98. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kitakeleza yafuatayo:

(i) kusajili wanafunzi 4,386 wakiwemo wanafunzi 716 wa Astashahada, 1,074 wa Stashahada, 2,390 wa Shahada, 40 wa Stashahada ya Uzamili, 133 wa Shahada ya Umahiri na 33 Shahada ya Uzamivu;

(ii) kujenga maktaba yenyewe uwezo wa kuchukua watumiaji 2,500 kwa wakati mmoja, ujenzi huu umetengewa **Shilingi 2,000,000,000**; na

(iii) kuanzisha Stashahada 2, Shahada za Kwanza 2 na Shahada za Uzamili 2 kwa lengo la kupanua wigo wa programu za mafunzo ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kukidhi mahitaji ya sasa.

### **Chuo Kikuu cha Ardhi**

**99. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo Kikuu cha Ardhi kitaktekeleza yafuatayo:

(i) kufanya miradi ya tafiti 30 hususan katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo. Aidha, Chuo kitatoa huduma za ushauri kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi kwa Wilaya 5 na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa maafisa watendaji wa halmashauri pamoja na wananchi;

(ii) kuendelea kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ardhi (*Lands Building*) na kuliunganisha na mfumo wa maji; na ujenzi wa Maabara (*Multi-Purpose Laboratory*) na kukarabati karakana, nyumba za watumishi na madarasa. **Shilingi Billioni 2.5** zimetengewa kwa ajili ya shughuli hii;

(iii) kudahili wanafunzi 4,700;

(iv) kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 53; wanataaluma wakiwemo 28 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na 25 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili;

(v) kumalizia kupitia na kuboresha mitaala 84 ya Chuo na kuiwasilisha Tume ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya kuidhinishwa;

(vi) kufanya miradi ya utafiti 30 katika maeneo ya usimamizi wa Ardhi na mazingira, makazi na majengo;

(vii) kuandaa machapisho 154 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi, na majengo; na

(viii) kutoa huduma za jamii juu ya matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi kwa Wilaya tano (5) kwa maafisa watendaji wa Halmashauri pamoja na wananchi;

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**100. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018/19 Chuo kitatkeleza yafuatayo:

(i) kuongeza idadi ya miradi ya utafiti yenye ufadhili wa washirika wa maendeleo kutoka 209 hadi 250 (ongezeko la asilimia 20);

(ii) kuandaa "Juma la Utafiti" na kuonyesha matokeo ya tafiti za Chuo kupitia majarida, magazeti, runinga na redio; kitatoa mafunzo maalum ya utafiti na uchapishaji kwa wanataluma 80 na wanafunzi 80 wa shahada za uzamili; na kitapanua wigo wa kutangaza huduma za ushauri kwa njia mbalimbali zikiwemo kushiriki maonesho ya kitaifa na kimataifa na kutumia runinga, magazeti, machapisho na vipeperushi;

(iii) kuongeza idadi ya machapisho katika majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka 354 kwa sasa hadi 390 (ongezeko la asilimia 10);

(iv) kuongeza idadi ya majarida ya kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka 9 kwa sasa hadi 24 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao;

(v) kununua vitabu, samani na mashubaka kwa ajili ya Maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(vi) kuongeza vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(vii) kufanya upanuzi wa Hosteli za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo zimetengwa **Shilingi Billioni 2.**

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**101. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kudahili wanafunzi 12,269 wa Shahada ya Kwanza 10,487 wa Stashahada 1,581 na wa Astashahada 201; na

(ii) kitafanya tafiti kumi (10) katika Nyanja mbalimbali na kitatoa huduma za ushauri kwa watakaohitaji. Vilevile, Chuo kinategemea kuwa na mahusiano (collaborations) na taasisi mbili (2) mpya za kimataifa.

**Chuo Kikuu cha Mzumbe**

**102. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kufanya tafiti katika maeneo 21. Aidha, kitatoa mafunzo na kutekeleza kazi za ushauri wa kitaalamu katika maeneo 37 ya Menejimenti, Uongozi na Sayansi ya Jamii;

(ii) kudahili wanafunzi wapya 4,712 (Cheti 173, Astashahada 418, Shahada ya kwanza 3,202, Shahada ya Umahiri 909 na Shahada ya Uzamivu 10);

(iii) kuendeleza ujenzi na uwekaji samani katika jengo la madarasa na utawala, Kampasi ya Mbeya ambapo jumla ya **Shilingi 2,500,000,000.00** zimetengwa kwa mwaka 2018/19;

(iv) kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya eneo la Iwambi, Kampasi ya Mbeya;

(v) kuboresha huduma na miundombinu ya TEHAMA;

(vi) kufadhili wanataaluma 8 kusoma masomo ya Shahada ya Umahiri na 10 kusoma masomo ya Shahada ya Uzamivu.

### **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**103. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo;

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa Kwanza wakiwemo wanafunzi wa Shahada za Kwanza kutoka 3,250 hadi 3,700 Shahada za juu (Uzamili na Uzamivu) kutoka 171 hadi kufika 400. Ongezeko hili ni kutohana na kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ambapo jumla ya **Shilingi 8,000,000,000.00** zimetengwa kwa mwaka 2018/19;

(ii) kuendesha programu 80 za utoaji wa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa washiriki 350 wakiwemo wakulima, maafisa ugani na watafiti;

(iii) kuongeza ushirikiano na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi;

(iv) kuvijenyea uwezo wa kifedha na kitaalamu vitengo vya uzalishaji ili viweze kuongeza mapato ya ndani ya Chuo kwa asilimia kumi (10%); na

(v) kufanya tafiti mbalimbali zaidi ya 150 kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, Chuo kitatoa huduma ya elimu na ushauri kwa wakulima 2,500 kwa kutumiambini mbalimbali kama semina, kozi fupi, warsha, runinga na redio kwa lengo la kupunguza umasikini kwa wananchi. Chuo kitaendelea kujenga na kukarabati Miundombinu ya Chuo na kutekeleza miradi ya tafiti.

### **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**104. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo;

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa shahada ya kwanza na ya uzamili kwa asilimia 50;

- (ii) kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kujifunzia kutoka asilimia 10 hadi kufikia asilimia 20;
- (iii) kutengeneza vigezo vya kupima uadilifu kwa wanafunzi (*Professionalism Assessment Tool*);
- (iv) kufundisha walimu vinara (*Health Professional Educators*) kwa kila skuli;
- (v) kutengeneza mpango wa kuboresha huduma kwa wagonjwa (*Patient Centered Service Strategy*) na kuboresha mfumowa huduma na taarifa kwa wagonjwa (*Health Information Management System*);
- (vi) kukamilisha uandaaji wa mpango wa uzalishaji mali wa hospitali ya kufundishia na taaluma – Mloganzila;
- (vii) kuongeza uwiano wa wanafunzi wa kike kufikia asilimia 40;
- (viii) kukamilisha ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo awamu ya I (*Cardiovascular Centre of Excellence*) katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili Kampasi ya Mloganzila kwa tengeo la **Shilingi 1,800,000,000**;
- (ix) kutoa mafunzo kwa makundi tafiti katika skuli (*Research Clusters*);
- (x) kuanzisha tafiti mpya 2 na kutoa ushauri wa taaluma tiba 5 kwa kila skuli;
- (xi) kufanya mkutano wa kitaaluma wa sita (*6<sup>th</sup> MUHAS Scientific Conference*) ili kutoa taarifa za tafiti; na
- (xii) kuendelea kufanya tafiti za magonjwa ambukizi (*HIV Vaccine Trial, Intergrated Biobehavioral Surveys For Key Population, Prep for HIV, Malaria Na Tuberculosis*), magonjwa yasiyoambukiza (*Non-Communicable Diseases*), magonjwa yasiyopewa kipaumbele na (*Neglected Tropical Diseases*) na mfumo wa afya (*Health System Research*).

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**105. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitaktekeleza yafuatayo:

- (i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4,066 hadi 5,338 na kuboresha maktaba moja ya Chuo;
- (ii) kutoa mafunzo ya kina katika programu za elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali, ngazi ya kati mpaka ngazi ya juu ya kada ya ualimu;
- (iii) kurekebisha na kuboresha mitaala katika programu za elimu na kutekeleza utafiti na uzinduzi wa programu ya elimu ya mazoezi na sayansi ya michezo;
- (iv) kukamilisha ujenzi wa maabara ya sayansi na kompyuta, kwa tengeo la shilingi billioni 2;
- (v) kusomesha watumishi 90 katika mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya Kwanza, Umahiri na Uzamivu;
- (vi) kutekeleza miradi 13 ya utafiti (*Research Projects*) na utoaji ushauri (*Consultancy*) ambapo miradi 7 ni endelevu na miradi 6 itakuwa mipya; na
- (vii) kuchapisha machapisho 50 kwenye majarida mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na kutoa chapisho la tatu la jarida la Chuo liitwalo *Mkwawa Journal of Education and Development (MJED)*.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

**106. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitaktekeleza yafuatayo;

- (i) kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 2,100 kati ya hao 700 wanatarajiwa kuwa wa fani ya Sayansi;

(ii) kuandaa mitaala 4 mipyä ya Shahada za Awali na Umahiri; na

(iii) ujenzi wa Jengo la Makazi ya Wanataaluma Watafiti pamoja na kujenga madarasa na kuweka mifumo ya kiusalamä na miundombinu ya TEHAMA chuoni kazi hii imewekewa tengeo la **Shilingi billioni 2.**

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**107. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuboresha elimu na utendaji kazi kwa watumishi kwa kuendesha mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 12 wa taaluma na wafanyakazi 6 wa utawala na mafunzo ya muda mfupi kwa wahadhiri 12 na wafanyakazi wa utawala 10;

(ii) kuanza ujenzi wa jengo la maktaba Kampasi ya Kivukoni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ambapo **Shilingi millioni 500** zimetengwa; na

(iii) kujenga Bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar ambapo kiasi cha **Shilingi millioni 500** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**108. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Chuo kitatekeleza yafuatayo;

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 4,209 kwa mwaka wa masomo 2017/2018 hadi kufikia wanafunzi 4,500 kwa mwaka wa masomo 2018/2019;

(ii) kuanza kutoa mafunzo ya uhandisi katika ngazi ya stashahada katika Kampasi ya Rukwa kwa mwaka wa masomo 2018/2019. Mafunzo yataanza kutolewa katika fani ya Uhandisi Barabara;

- (iii) kuendelea na kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 ili kukidhi mahitaji ya huduma bora za maktaba kwa wanafunzi na wahadhiiri, ambapo **Shilingi billioni 2** zimetengwa kutekeleza kazi hii;
- (iv) kuendelea kuongeza matumizi ya nishati mbadala ili kuwa na vyanzo endelevu vya nishati kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chuo;
- (v) kufanya tathmini ya mali za wananchi katika eneo ambalo limeainishwa kuongezwa katika Kampasi ya Rukwa ili lifikie ukubwa wa hekta 500. Kiasi cha **Shilingi 20,000,000** kutoka mapato ya ndani kimetengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli hiyo;
- (vi) kuanzisha bustani ya mimea kwa matumizi ya kitaaluma na kuleta ustawi wa mazingira ya Chuo. Kiasi cha **Shilingi 114,079,093** kutoka mapato ya ndani ambapo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 50,000,000** ni msaada kutoka *Tanzania Forest Fund*;
- (vii) kujenga jengo lenye vyumba viwili vya madarasa vitakavyokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 kwa pamoja kwa kutumia fedha zinazotokana na mapato ya Chuo ya ndani ambapo kiasi cha **Shilingi 270,000,000** zimetengwa;
- (viii) kugharamia chakula kwa wanafunzi 338 na mafunzo kwa vitendo (*Industrial Practical Training*) kwa wanafunzi 268 wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya;
- (ix) kufanya tafiti zinazolenga kuongeza ubunifu na kuendelea kutoa ushauri elekezi katika nyanja za sayansi na teknolojia ili kuchochaea ukuaji wa uchumi wa viwanda na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo katika jamii;
- (x) kuunda gari dogo kwa ajili ya kubebea mizigo midogo midogo kwa lengo la kurahisisha kazi za uvunaji kwa wakulima wa viazi. Mfano wa Gari umeundwa na unaendelea kuboreshwa ili kukidhi maoni ya wadau

mbalimbali. Faida ya gari hilo litasaidia huduma za usafirishaji wa mizigo ambayo haiendi umbali mrefu. Kiasi cha **Shilingi 5,527,000** kutoka mapato ya ndani kimetengwa kwa kazi hiyo;

(xi) kuandaa mfumo wa kuzalisha gesi kwa kutumia samadi kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuwasha taa katika maeneo ya vijjini. Mfumo wa uzalishaji wa gesi kwa ajili ya kupikia kutokana na samadi uliundwa na kujaribiwa katika maeneo ya Mbozi. Mfumo huu unasaidia kupunguza uharibifu wa misitu na kupunguza gharama za maisha kwa wananchi wenye mifugo ambao wanaweza kupata njia mbadala ya nishati kwa kutumia samadi; na

(xii) kuunda mashine kwa ajili ya kupukuchua mazao mbalimbali. Mashine hii itasaidia kupunguza upotevu wa chakula wakati wa kupukuchua na pia kupunguza muda wa kupukuchua mazao na hivyo kumpa mkulima muda mwingu katika shughuli nyingine za kiuchumi. Kiasi cha **Shilingi 3,000,000** kimetengwa.

### **Chuo cha Ufundı Arusha**

**109. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kufanya utafiti wa matumizi bora ya maji katika kilimo cha mpunga kwa kushirikiana na *Japan International Research Centre for Agricultural Sciences (JIRCAS)*;

(ii) kufanya utafiti wa mradi wa umeme Wilayani Mbulu chini ya ufadhili wa Wakala wa Umeme Vijjini (REA) ambapo umeme utakaozalishwa utahudumia vijiji viwili vy'a Kwermus na Amoa;

(iii) kufanya utafiti wa majoribio ya mitambo midogo iliyoundwa ya kuzalisha umeme utokanao na nishati ya Maji katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa;

(iv) kuendelea na utafiti kuhusu uundai wa helikopta;

(v) kuanza ujenzi wa mitambo ya kuzalisha meme utokanao na nishati ya maji katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa kwa kushirikiana na mwekezaji mwenza;

(vi) kukamilisha ukarabati na ufungaji vifaa katika karakana 5 za Chuo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo karakana zitakazopata vifaa ni pamoja na karakana 2 za uhandisi mitambo, karakana moja ya useremala na karakana 2 za uhandisi magari kwa tengeo la **Shilingi 100,000,000** fedha za ndani;

(vii) kujenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 250 kwa pamoja kwa tengeo la **Shilingi 250,000,000** fedha za ndani;

(viii) kujenga na kukarabati miundombinu ya madarasa, maabara na karakana katika vituo vya mafunzo vya Kikuletwa na Oljoro kwa tengeo la **Shilingi 1,945,319,000.00**;

(ix) kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa wanafunzi wapatao 500 kwa utaratibu wa Skimu za Vocha za Mafunzo kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na

(x) kukamilisha ufungaji wa mtandao wa intaneti (*Local Area Network*) katika majengo yote ya Chuo kutoka kwenye Mkongo wa Taifa ili kuboresha utoaji wa mafunzo kupitia TEHAMA ambapo kiasi cha **Shilingi 600,000,000** hela za ndani zimetengwa.

**110. Mheshimiwa Spika**, vile vile Chuo cha Ufundis Arusha kitatoa ushauri wa kitaalamu kuhusu:

(i) tathmini ya uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara, ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi; na

(ii) ufungaji wa *Solar PV* kupitia mradi wa *Sustainable Solar Market Packages (SSMP)*.

## Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam

**111. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili wanafunzi wapya 1,700 na kuendelea kuhudumia wanafunzi 2,900; wanaoendelea hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 4,600;
- (ii) kukamilisha upanuzi wa jengo la Maktaba kwa kutumia mapato ya ndani ambapo **Shilingi 400,000,000.00** zimetengwa;
- (iii) kuweka samani za ndani na miundombinu na vifaa vyta TEHAMA katika jengo jipya ambapo zimetengwa **Shilingi 1,000,000,000** fedha za ndani;
- (iv) kuanzisha kozi mpya za Shahada ya Uhandisi katika Madini na Shahada ya Umahiri katika Uhandisi wa Nishati Endelevu;
- (v) kuendelea kuhudumia wafanyakazi 36 walioko masomoni;
- (vi) kupeleka wanafunzi 550 mafunzo ya vitendo viwandani;
- (vii) kuanzisha kozi ya Stashahada ya utengenezaji viatu na kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya kitaalam katika teknolojia ya ngozi katika Kampasi ya Mwanza; na
- (viii) kuendelea na utoaji wa mafunzo ya u f u n d i mchundo na kuanza maandalizi ya kutoa mafunzo ya muda mrefu katika Kampasi ya Myunga.

## Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha

**112. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Taasisi itatekeleza yafuatayo:

- (i) kudahili wanafunzi 215; Shahada ya uzamili 175 na Uzamivu 40;
- (ii) kuhamasisha upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya kitafiti kwa kuandika maandiko yapatayo 48;
- (iii) kuongeza idadi na mahusiano mazuri na wadau wetu wa kimataifa kutoka 24 hadi 30, wadau wa kanda ya afrika mashariki kutoka 29 hadi 35 na wadau wa ndani ya nchi kutoka 17 hadi 25;
- (iv) kuanza ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja ambapo **Shilingi 1,000,000,000** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/19; na
- (v) kukamilisha tafiti 12 zinazoendelea.

**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia**

**113. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Chuo kitaktekeleza yafuatayo:

- (i) kupima ardhi na kufuatilia upatikanaji wa H a t i Miliki za ardhi ya Chuo kwa Kampasi za Butiama, Ranya na Serengeti;
- (ii) kuanzisha programu 5 na kununua vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
- (iii) kuandaa mitaala 10 kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza, kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa na TCU;
- (iv) kuimarisha shughuli za mafunzo na huduma za ugani kwa jamii za wakulima, wafugaji, wavuvi, na wachimbaji madini wadogowadogo walioko jirani na Chuo; na

(v) kuandaa michoro na mpango wa matumizi ya Ardhi kwa ajili ya Chuo kwa tengeo la **Shilingi 1,000,000,000**.

### Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH

**114. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Tume imetenga jumla ya **Shilingi 9,680,000,000** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kuanzisha na kuendeleza Atamizi za Ubunifu katika Halmashauri za Mji wa Mbeya na Dodoma zinazolenga kukuza ubunifu kwa jumla ya vijana 50;
- (ii) kuwatambua wagunduzi na wabunifu nchini na kuwawezesha kuendeleza ubunifu na ugunduzi wao kupitia mfuko wa MTUSATE. Tume itafadhili miradi 20 kwa kutumia Mwongozo ulioandalishi ambao unaweza kupatikana Tume ya Sayansi na Teknolojia;
- (iii) kuhamasisha matumizi ya teknolojia mpya kama *Bioteknolojia, Nanoteknolojia, Mekatroniki* na *Bigdata* ili kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kuandaa na kufanya majukwaa ya majadiliano pamoja na kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari;
- (iv) kuandaa vipindi na makala 42 zinazohusiana na masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU) na kuzisambaza katika Radio na Televisheni ili kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika kuboresha shughuli za kiuchumi na kijamii; na
- (v) kuanzisha na kuendeleza kumbi za Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuchochea uanzishwaji wa kampuni za kiteknolojia ili kukuza ubunifu na kuongeza ajira kwa vijana.

### Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania

**115. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Tume itatekeleza yafuatayo:

- (i) kuanza ujenzi wa maabara ya Tume awamu ya pili ambayo itaboresha utoaji huduma, kuongeza mapato na ufanisi katika utendaji wa kazi za Tume ambapo kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** imetengwa;
- (ii) kupokea na kutathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004;
- (iii) kuendelea na ukaguzi wa migodi 6 (*Geita Gold Mine - Geita, Bulyanhulu Gold Mine - Kahama, North Mara Gold Mine - Tarime, Buzwagi Gold Mine - Kahama, Williamson Gold Mine - Shinyinga, Stami Gold Tulawaka -Biharamulo*) inayofanya kazi ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo;
- (iv) kuendelea kukagua vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 150 ili kubaini hali ya usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla;
- (v) kuendelea na usajili wa vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 1,045;
- (vi) Kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi kwa Wafanyakazi 1,600;
- (vii) kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo vinne na kuyahifadhi katika jengo maalumu (*Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF*) liliopo Arusha;
- (viii) kupima kiasi cha mionzi katika sampuli angalau 6,000 za vyakula na mbolea;
- (ix) kuimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 24 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyngine;
- (x) kuendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (*Radionuclide Monitoring Station-TZP- RN64*)

kilichopo katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons*;

(xi) kuendelea kuratibu miradi mipya sita (6) ya kitaifa na miradi 30 ya kikanda ambayo itagharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*International Atomic Energy Agency- IAEA*);

(xii) kufanya kagazi kwenye vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyoayonishwa (*Non-Ionizing Radiation*)mfano minara ya simu, redio, runinga, na vifaa vingine vyta mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika; na

(xiii) kufungua ofisi za Tume katika kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Mkoa wa Mbeya na Kanda ya ziwa Mkoa wa Mwanza. Vigezo vinavyotumika kuchagua kanda ni uwepo wa vyanzo vyta mionzi.

#### **MALENGO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2018/19**

##### **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu)**

**116. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R) kwa mwaka 2018/19 imetenga kiasi cha **Shilingi 140,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kutoa motisha kwa Halmashauri zote kutokana na utekelezaji wa vigezo vyta EP4R, Ufuatiliaji na Tathmini ya Uendeshaji wa Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu;

(ii) kutoa Motisha kwa shule za Msingi na Sekondari zilizofanya vizuri na zilizoongeza kiwango cha ufaulu katika Mitihani ya Taifa ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne 2018;

- (iii) kujenga madarasa 2,000 na matundu ya vyoo 2,000 kwa Shule za Msingi na Sekondari;
- (iv) kujenga mabwalo kwa shule 85 zilizopanuliwa kwa ajili ya kudahili wanafunzi wa Kidato cha Tano;
- (v) kununua vifaa vya Maabara awamu ya pili kwa shule 1,800 za Sekondari za Wananchi;
- (vi) kukarabati Shule Kongwe 25 za Sekondari ambazo ni; Arusha, Weruweru, Shinyanga, Rungwe, Mawenzi, Bukoba, Mara, Mtwara Wasichana, Lyamungo, Masasi Wasichana, Lindi, Kilosa, Machame Wasichana, Sumbawanga, Tarime, Kibasila, Tunduru, Tumaini, Pamba, Mbeya Kutwa, Moshi Wavulana, Ifunda Wasichana, Iringa Wasichana, Ashira, na Mwanza Sekondari;
- (vii) kukarabati na kupanua Vyuo 8 vya Ualimu ambavyo ni Bustani, Vikindu, Mtwara Kawaida, Mtwara Ufundu, Singachini, Monduli, Bunda na Katoke; na
- (viii) kununua magari 20 kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu.

**Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK**

**117. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (*Literacy and Numeracy Education Support-LANES*) kwa tengeo la **Shilingi 4,000,000,000** kwa kufanya yafuatayo:

- (i) kufanya tathmini ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikakati ya Sekta ya Elimu;
- (ii) kufanya tathmini ya mwisho ya utekelezaji wa shughuli za Programu ya LANES pamoja na Sekta ya Elimu (*Joint Education Sector Review - JESR*);

(iii) kuwezesha kitengo cha Tathmini na Ufutiliaji cha Wizara ili kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za programu ya LANES; na

(iv) kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum.

**Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundu, Mafunzo ya Ufundu Stadi na Elimu ya Ualimu**

**118. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itatekeleza yafuatayo: -

(i) kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundu Stadi cha Mkoa wa Njombe na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundu Stadi vya Mikoa ya Simiyu, Geita na Rukwa ambapo kiasi cha **Shilingi 24,500,000,000** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo;

(ii) kuanza ujenzi katika Vyuo vya Ualimu 6 vya Dakawa, Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Butimba ambapo **Shilingi 5,450,000,000** zimetengwa kwa ujenzi huo; na

(iii) kuanza ujenzi wa Chuo cha Ufundu Stadi cha Mkoa wa Kagera chini ya ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.99 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo.

**Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu**

**119. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vinne vya Ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali kwa tengeo la **Shilingi 12,370,0451,500**.

**Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu**

**120. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu imetenga jumla ya **Shilingi 20,241,960,000** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kununua vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia kwa vyuo 35 vya Ualimu na vifaa vya Elimu Maalum kwa Vyuo 35 vya Patandi, Mtwara Ufundsi na Mpwapwa;
- (ii) kuimarisha Mifumo ya TEHAMA, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa Vyuo vya Ualimu na Kuvunganisha katika Mkongo wa Taifa;
- (iii) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga na kukarabati maktaba za Vyuo 8 vya Ualimu ambavyo ni Bustani, Vikindu, Mtwara Kawaida, Mtwara Ufundsi, Murutunguru, Monduli na Bunda;
- (iv) kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 821;
- (v) kutoa mafunzo Kazini kwa wakufunzi 323 wa masomo ya Lugha, 162 wa Elimu ya Awali, 279 wa Sayansi, 132 wa Hisabati, 381 wa Sayansi ya Jamii na 162 wa Elimu ya Afya;
- (vi) kuandaa mfumo wa mawasiliano na utunzaji taarifa za Elimu ya Ualimu (Kanzidata);
- (vii) kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Hisabati ya Korogwe *Maths Project* na kutoa mafunzo kwa Walimu 200 wa somo la Hisabati wa shule za Msingi na Sekondari;
- (viii) kuandaa Mkakati wa Jinsia na kutoa Elimu ya Jinsia kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- (ix) kuwezesha uendeshaji wa shughuli za mradi na kufanya ufuatilaji na tathmini;
- (x) kutoa ufadhili kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu 500 wa fani za Sayansi, Kilimo na Ufundsi kusomea *Postgraduate Diploma* ya Ualimu ili waweze kuwa Walimu wa Sayansi wa Shule za Sekondari; na
- (xi) kutoa ufadhili kwa Wakufunzi wa Chuo cha Ualimu Patandi kuijendeleza katika ngazi ya Shahada ya Pili kwenye Elimu Maalum.

**Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni:**

**121. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara imetenga jumla ya **Shilingi 17,033,235,000** kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

- (i) kujenga miundombinu ya Maji na Vyoo katika Shule za msingi 500;
- (ii) kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa pamoja wa miundombinu ya vyoo na maji kwa kuzingatia mwongozo wa SWASH kwa kushirikiana na Wizara zinazotekeleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira ili kubaini mafanikio, changamoto katika kutekeleza Kampeni hii na kutoa ushauri stahiki; na
- (iii) kutoa Elimu kuhusu utumiaji wa mwongozo wa SWASH kwa Wathibiti Ubora wa Shule na Waratibu wa SWASH wa Halmashauri na Mikoa ili waweze kukusanya takwimu za SWASH na kutoa taarifa kwa kutumia mfumo kila robo ya mwaka.

**Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (*Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP*):**

**122. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itatekeleza yafuatayo:

- (i) kujenga shule mpya za Mikoa katika Mikoa 7 ambapo jumla ya **Shilingi 21,000,000,000** zimetengwa;
- (ii) kujenga nyumba za walimu 8 kwa kila shule katika shule mpya 7 za Mikoa ya Geita, Njombe, Lindi, Singida, Katavi, Ruvuma na Manyara ambapo jumla ya **Shilingi 2,800,000,000.00** zimetengwa; na
- (iii) kununua samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule mpya 7 ambapo jumla ya **Shilingi 700,000,000.00** zimetengwa.

**Mradi wa TANZIS (*Tanzania Innovation Systems*):**

**123. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19, Wizara itaanza kutekeleza yafuatayo kwa teneo la **Shilingi 6,589,351,000:-**

- (i) kuibua na kutambua wabunifu 70 mahiri Tanzania, kutoka makundi saba (Vyuo Vikuu, Ufundu Stadi, Ufundu wa Katu, Atamizi na Kumbi za Ubunifu, Taasisi za Utafiti, Viwanda na Shule za Sekondari) ambayo kila kundi moja litatoa wabunifu 10 kwa lengo la kusaidia kukuza ujuzi utakaowezesha kujenga Tanzania ya Viwanda;
- (ii) kuimarisha mazingira ya ubunifu kwa kuwasaidia wabunifu wachanga kupata vifaa na msaada wa kitaalam ili kuyaendeleza mawazo yao katika mazingira halisi ya kibliashara na kuonekana katika jamii;
- (iii) kuwaunganisha wabunifu wenye taaluma mbalimbali na kuwapa mtaji ili waweze kutatua changamoto mbalimbali hasa katika maeneo ya viwanda vilivyopo nchini ili vifanye kazi kwa ufanisi;
- (iv) kuwapatia nafasi wabunifu wachanga, wataalamu vyuoni, wataalamu katika sekta ya umma na sekta binafsi, kutembelea nchi ya Finland ili kujifunza mawazo mapya yatakayowezesha kuendeleza ubunifu wao; na
- (v) kuhamasisha umma kuhusu mradi pamoja na kuwajengea uwezo waendelezaji wa ubunifu ili kuwa na uelewa wa pamoja.

**TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**124. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2018/19 Tume itatekeleza yafuatayo:

- (i) kushirikisha Wizara, Taasisi za Umma, Taasisi binafsi pamoja na wadau mbalimbali katika kuchangia kuboresha maswala ya Elimu, Sayansi, Habari na Utamaduni; na

(ii) kuendelea kushiriki katika kazi za UNESCO haswa katika kupanga na kutekeleza program mbalimbali za UNESCO.

#### D. SHUKRANI

**125. Mheshimiwa Spika,** Napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa William Tate Olenasha (Mb) Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu,Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao wa karibu katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara yetu.

Napenda pia kuwashukuru, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara, Wanataaluma, Wanafunzi na Wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninatambua na kuthamini sana mchango wenu mzuri katika kuhakikisha kuwa sekta ya elimu nchini inaendelea kuimarika.

**126. Mheshimiwa Spika,** Washirika mbalimbali wa Maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru na kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Canada, China, Cuba, India, Italy, Hungary, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Sweden, Uingereza, Ujeruman, Korea Kusini, Uturuki na Ubelgiji. Aidha natoa shukrani za dhati kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

**127. Mheshimiwa Spika,** Napenda kuyashukuru baadhi ya mashirika yaliyochangia katika kufanikisha Programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia: Aga Khan Education

Service, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Commonwealth Secretariat, DAAD, DfID, Global Partnership for Education, Inter University Council of East Africa (IUCEA), Japan International Cooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organisation (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Human Development Innovation Fund (HDIF), Swedish International Development Agency (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), UNESCO, UNICEF, USAID na WaterAid.

#### **E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19**

**128. Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,406,469,626,000.00** ili kutekeleza majukumu yake.

**129. Mheshimiwa Spika**, Katika maombi haya:

(i) **Shilingi 476,500,224,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 406,267,946,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 70,232,278,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) **Shilingi 383,838,645,092.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 331,948,039,001.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 51,890,606,091.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(iii) **Shilingi 929,969,402,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo a m b a p o **Shilingi 618,969,400,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 311,000,002,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**130. Mheshimiwa Spika**, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba jumla ya **Shilingi 666,855,000.00** ikiwa

yote ni matumizi ya kawaida (**Mishahara** ni 334,562,000.00 na Matumizi mengineyo ni **Shilingi** 332,293,000.00).

**131.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya bajeti ya mafungu yote mawili (Fungu 46 na Fungu 18) yenyeye jumla ya **Shilingi** 1,407,136,481,000.00.

**132.** **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe pamoja na kwa waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza.

#### **KUTOA HOJA**

**133.** **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako. Tunaendelea. Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mheshimiwa Hussein Bashe. (*Makofii*)

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kusoma Taarifa ya Kamati, naomba kufanya marekebisho kidogo ukurasa wa 25 wa taarifa mliyopewa, kielelezo namba nane kinachohusu mchanganuo wa ufaulu wa asilimia baina ya Shule za Serikali na zile zisizo za Serikali kwa mwaka 2016/2017, sehemu ya matokeo ya mwaka 2016 namba mbili 2 Shule za Serikali kwenye shule 50 Bara isomeke asilimia sita badala ya asilimia nne iliyoandikwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii ya awali kabisa kuipongeza Serikali katika juhudini wanazochukua kwa niaba ya Kamati katika kurekebisha miundombinu ya elimu katika shule zetu za sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, katika Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1)(a) inaeleza jukumu la Kamati la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kupokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Bajeti ya Wizara, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha wa 2017/2018. Ukaguzi huu ulifanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Lengo kuu la ziara ni kujiridhisha na ufanisi wa Serikali katika kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 289.341sawa na asilimia 77 ya kiasi kilichopangwa kukusanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Fungu 18 (Tume ya UNESCO) Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi

40,000,000. Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Tume ilikuwa imekusanya shilingi 57.5 sawa na asilimia 144 ya lengo. Kamati inapongeza jitihada hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 881.668 sawa na asilimia 65 ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya shughuli zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya fedha hizo, shilingi 287 sawa na asilimia 68 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 594 sawa na asilimia 65 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 18 - Tume ya UNESCO, kiasi cha shilingi 663 kilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo) ya taasisi hii. Hadi kufikia Februari, 2018 kiasi cha shilingi 44.9 sawa na asilimia 67 ya makadirio kilipokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi iliyo chini ya Wizara inazozisimamia ilio katika Mkoa wa Iringa na Mbeya. Miradi hii ni pamoja na mradi wa upanuzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa uliotengewa kiasi cha shilingi bilioni moja sawa pamoja na upanuzi na ukarabati wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ambayo ilitengewa shilingi billioni tatu ambazo zote hazikutolewa. Maeleo ya kina kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali halisi ambayo Kamati iliona wakati wa ukaguzi wa miradi, inatoa ushauri kwamba Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na taarifa ya Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) ulioagizwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu katika Chuo Kikuu cha Elimu Mkwawa ifike mbele ya Kamati kwa ajili ya taarifa na hatua zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali itekeleze maoni ya Kamati yaliyotolewa katika mwaka 2016/2017 ikiwemo kutoa tuzo ya udhamini (*Magufuli*

*Scholarship Award) na uainishaji wa vyuo vikuu (University classification) kulingana na ubora wake.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Fungu 46, inakadiria kukusanya shilingi bilioni 460 sawa na ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Fungu 46, inakadiria kukusanya shilingi milioni 460 sawa na ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 18 (Tume ya UNESCO), Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya shilingi 70,000,000 sawa na ongezeko la asilimia nne la makadirio ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara kupitia Fungu 46 inakadiria kutumia kiasi cha shilingi trilioni 1.4 sawa na ongezeko la asilimia 4.5, kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, kwa upande wa Fungu 18 - Tume ya UNESCO, Wizara inategemea kutumia kiasi cha shilingi milioni 66 sawa na ongezeko la asilimia 0.55 la kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa tatu sasa, Kamati imekuwa ikiongelea kwa kina kuhusu hali ya elimu nchini. Lengo kuu la kufanya hivi ni kutaka sisi wote kama Watanzania tuone mwelekeo wa elimu yetu ili kuweza kuishauri ipasavyo. Sehemu hii imekuwa ikieleza kwa kina kuhusu tafiti mbalimbali zinazofanywa na wadau wa maendeleo katika masuala ya elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu bado inakumbana na changamoto nyingi. Tafiti zinaonesha kuwa bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuweza kutatua changamoto zilizopo kwenye Sekta ya Elimu nchini na kuweza kufikia malengo ya maendeleo endelevu (*Sustainable Development Goals*)

hususan lengo namba nne linalohusu Elimu Bora (*Quality Education*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa matokeo ya programu ya viashiria vya Utoaji Huduma (*Service Delivery Indication*) iliyo chini ya Benki ya Kimataifa ya Ujenzi na Maendeleo/Benki ya Dunia, Tanzania imeongeza uwekezaji wake katika sekta ya elimu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Nchi ilipata mafanikio katika uwekezaji huu kwani kiwango cha kumaliza shule ya msingi kiliongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2012. Kamati inapongeza jitihada hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matokeo hayo, matokeo ya mwaka 2014 ya Benki ya Dunia yanaonesha kuwa asilimia 23 ya walimu (asilimia 20 vijijini na asilimia 36 mijini) hawakuwepo shulenii.

Aidha, tafiti imeonesha pia kuwa asilimia 53 ya walimu walikuwa hawaingii madarasani pamoja na kuwepo katika maeneo yao ya kazi. Maana yake ni kwamba wanafunzi walikuwa wanafundishwa kwa wastani wa masaa mawili na dakika nne ikilinganishwa na wastani wa masaa matano na dakika 12 yanayotakiwa kwa siku. Kwa ujumla ni kuwa wanafunzi wanafundishwa kwa asilimia 40 tu na hivyo kuacha asilimia 60 ya mitaala ikiwa haijaguswa.

Mheshimiwa Spika, tafiti inaendelea mbele zaidi na kuonesha kuwa kwenye shule zenye uwiano mkubwa wa walimu kwa wanafunzi, wanafunzi walikuwa na madarasa machache na hii inaonekana zaidi kwenye shule za sekondari ambapo siyo rahisi kwa mwalimu kufundisha masomo nje ya masomo aliyosomea. Kwa wastani wanafunzi walifundishwa vipindi viwili na nusu tu siku ambayo utafiti ulikuwa unafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonesha pia kuwa wakati mwalimu mmoja tu kati ya watano ndiye anayemudu mtaala wa kufundisha, uwezo wa walimu wa kufundisha somo ni jambo muhimu na linahitaji kushughulikiwa.

Mwanazuoni Thomas Jefferson aliwahi kusema; "*If children are untaught, their ignorance and vices will in future life cost us much dearer in their consequences than it would have done in their correction by a good education.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa stadi za kufundishia ni suala linaloathiri sekta ya elimu, kwani ni mwalimu mmoja tu kati ya 1000 anayepata zaidi ya 80% zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ushahidi wa kutosha kwamba maarifa ya walimu na uwezo wao wa kuhamisha kwenda kwa wanafunzi (kwa maana ya stadi za ufundishaji) ni kichocheo cha matokeo ya kujifunza kwa wanafunzi. Kamati inaona ni muda muafaka wa kuwekeza katika ubora wa elimu na siyo bora elimu kwa kuwepo na walimu bora, mitaala bora na mazingira bora ya kufundishia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaenda mbele zaidi na kuonesha kuwa kuna upungufu mkubwa katika upatikanaji wa vifaa katika ngazi ya shule, kwani asilimia 41 tu ya shule ndizo zilizo na miundombinu inayokidhi kiwango cha chini cha mahitaji. Ni asilimia 47 tu ya shule ndizo zina vyoo vinavyokidhi viwango; ni asilimia 61 pekee zina vifaa vya kufundishia vinavyokidhi kiwango cha chini cha mahitaji na ndani ya darasa ni mwanafunzi mmoja kati ya wanne ana kitabu cha kiada cha hesabu au klingereza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na tafiti hiyo, Kamati pia imechambua tafiti iliyofanywa na Taasisi ya HakiElimu ambayo inaonesha kuwa bado kuna changamoto zinazoathiri ubora wa elimu nchini. Changamoto hizo ni pamoa na walimu wengi hawana taaluma muhimu na stadi za ujuzi wa kufundishia, kwani ni asilimia 15 tu ndio wanaelewa na kuiweza mitaala wanayofundisha. Asilimia 37.8 tu ya walimu ndio wana hamasa ya kufundisha shule za Serikali. Kamati inaona hii inachangiwa na changamoto walizonazo walimu kama kutolipwa stahiki, mafao na madeni yao kwa wakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa wanafunzi katika mitihani ya mwisho ni mbaya. Kwa mfano, katika matokeo ya mwaka 2017, wastani wa asilimia 60 ya wanafunzi wamepata madaraja ya mwisho kwa maana ya *division four* na *division zero*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani yao ya sekondari wanaenda kusoma Udaktari na Uhandisi ilhali wale wanaopata daraja la nne ndio wanaoenda kusoma ualimu. Wakati huo wanachuo wanaofanya vizuri kwa maana ya daraja la kwanza (*first class*) ndio wanabaki Chuo Kikuu kufundisha. Tafsiri yake ni kuwa tunajenga nyumba nzuri kwenye misingi mibovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia hali ya ufaulu wa kidato cha nne kwa kipindi cha mlaka sita na kuona daraja la nne na la mwisho ndiyo linachukua asilimia kubwa kama ilivyosemwa na tafiti ya HakiElimu. Mwaka 2011 wanafunzi waliopata daraja la kwanza mpaka la tatu ni asilimia 10 ya wanafunzi wote waliothiniwa kidato cha nne. Mwaka 2012 ni asilimia 9.5; mwaka 2013 ni asilimia 21; mwaka 2014 ni asilimia 30.8; mwaka 2015 ni asilimia 25 na mwaka 2016 ni asilimia 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya walimu katika shule za msingi imepungua kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi walimu 179,291 mwaka 2017. Upungufu huu wa walimu umesababisha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kuwa 1:159 mwaka 2017 kutoka uwiano wa 1:135 mwaka 2016. Kiuhalsia uwiano unaopaswa kuwa ni 1:25, kwa maana kwamba mwalimu anafundisha madarasa matano na robo kwa wakati mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016, katika shule za sekondari kulikuwa na uhaba mkubwa wa walimu wa Hesabu 7,291; Baiololiajia 5,181; Kemia 5,373 na Fizikia upungufu wa walimu 6,873 kwa mujibu wa Ripoti za *BEST*, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban walimu 30,232 wapo juu ya umri wa miaka 51 na inakadiriwa kati ya mwaka 2018 na 2019 walimu wa shule za msingi wapatao 7,743 wanatarajiwani kustaafuli kutokana na taarifa za *BEST*. Tafsiri ni kuwa upungufu wa walimu katika shule za msingi utaongezeka na hivyo uwiano wa walimu kwa wanafunzi utaathirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 93 ya bajeti ya elimu inayoenda katika Serikali za Mitaa inatumika katika matumizi ya kawaida (posho na mishahara) na asilimia saba tu ndiyo inaenda kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inasikitika sana katika jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuendelea kuwekeza katika elimu ikiwemo kutoa elimu bure, hata hivyo, Kamati imebaini ufaulu wa shule za Serikali unaendelea kushuka. Kamati imepitilia taarifa ya ufaulu baina ya shule za Serikali na shule za binafsi kwa mwaka 2016 na 2017. Hali inaonesha kuwa ufaulu kwa shule za Serikali unazidi kushuka mwaka hadi mwaka kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitilia ripoti ya tafiti iliyofanywa na Taasisi ya TWaweza Kupitia Programu ya Uwezo. Tafiti hiyo ambayo imetolewa mwaka 2017 ilihusisha jumla ya watoto 197,451 kutoka shule za msingi 4,750. Taarifa hiyo inaonesha kuwa wanafunzi mmoja kati ya wanafunzi 10 wa darasa la tatu ndiyo aliweza kusoma *storyya* kiingereza wakati wanafunzi wa darasa la saba ni wanafunzi watano tu kati ya 10 ndio walioweza kusoma *storyhiyo* ya kiingereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi sita kati ya 10 wa darasa la tatu ndio walioweza kusoma vizuri *storyya* kiswahili. Aidha, kwa watoto wa darasa la saba ni wanafunzi tisa kati ya 10 ndio walioweza kusoma vizuri *story* ya aina hiyo. Kwa upande wa hesabu, wanafunzi watatu kati ya 10 wa darasa la tatu waliweza kufanya vizuri majoribio na wale wa darasa

la Saba ni wanafunzi tisa kati ya 10 ndio walioweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti hii inaonesha kuwa, kuna maendeleo mazuri ya ufaulu wa somo la kiswahili kwa watoto wa darasa la tatu, kwani umefaulu umeongezeka kutoka asilimia 29 hadi kufika asilimia 59 mwaka 2015. Kamati inapongeza jitihada hizi na inaamini kuwa jitihada hizi zitaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilihitimisha kupitia Taarifa ya UNESCO *Institute for Statistics "Reducing global poverty through universal primary and secondary education"* ya mwaka 2017 ambayo inaonesha kuwa umaskini unachangia sana ukosefu wa elimu kwani nchi zenyе kipato cha chini ambazo zinajumuisha Afghanistan, Burkina Faso, Ethiopia, Mali, Msumbiji, Niger na Tanzania zinazochangia asilimia kubwa ya watoto ulimwenguni wenye umri wa kwenda shule lakini hawaendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya asilimia 24 ya watoto wote duniani wenye umri wa kwenda shule na hawajaenda, asilimia 13 wanatoka katika nchi masikini, Tanzania ikiwemo. Watoto wanaomaliza shule ni wachache ikilinganishwa na walivyoandikishwa. Watoto walioandikishwa mwaka 2013 ni asilimia 62 na kati ya hao asilimia 27 tu ndio waliweza kumaliza elimu ya msingi kati ya mwaka 2008 mpaka 2014. Aidha, wanafunzi hawa hata wakimaliza shule bado wanakuwa hawana ujuzi unaotakiwa kutokana elimu wanayopata kuwa ya kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumeona sekta ya elimu inakumbana na changamoto nydingi sana na kuna haja kubwa ya kuangalia sekta ya elimu kwa jicho la pekee na kuchukua hatua ya haraka na makusudi ili kuweza kulinusuru Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi huo wa kina kuhusu Bajeti ya Wizara pamoja na hali ya elimu nchini, naomba pamoja na maoni haya, Serikali izingatie

maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa pamoja na Bunge lako tukufu kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini fedha hizi zimekuwa hazitolewi zote na kwa wakati. Tumeona katika vyuo ambavyo Kamati ilivitembelea vilivyotengewa jumla ya shilingi bilioni mbili kwa pamoja, lakini hakuna fedha yoyote iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa miradi hiyo inahusisha ujenzi wa vyumba vyta mihadhara na maktaba ambazo ni nyenzo muhimu sana kwa wanafunzi. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kabla ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwisha fedha zote za miradi zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu zinatolewa ili Wizara iweze kutekeleza miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiliongelea suala la mahusiano baina ya Wizara hii na TAMISEMI kutohana na kutokuwa na mipaka sahihi ya majukumu. Kamati inafahamu kuwa mwezi Aprili, 2016 Serikali ilitoa hati idhini ambayo ilieleleza majukumu ya Wizara hii ambapo Kamati imebaini kuwa Wizara kwa sasa ina jukumu la kushughulikia masuala ya sera, lakini pia mafunzo ya walimu. Hata hivyo, Kamati inapata shida kwa kuwa utekelezaji wa masuala yote ya walimu yakiwemo maslahi yao yapo chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, lakini Kamati inatambua masuala ya walimu pia yanahusisha Wizara ya Utumishi na Fedha na hivyo kufanya suala la uwajibikaji kuwa na ukakasi kidogo. Kamati inashauri kuwepo na uratibu mzuri wa masuala haya ya walimu ili kuweza kuondoa changamoto wanazokumbana nazo walimu kwa kuwajibika na kushughulikiwa masuala yao na mamlaka zaidi ya moja kwa namna yenye kuleta mchanganyiko zaidi kuliko kurahisisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu ni nyenzo muhimu sana katika sekta ya elimu nchini. Hata hivyo, walimu waliopo hawatoshelezzi mahitaji, hali inayosababisha kuzorota kwa elimu yetu. Kamati ina taarifa kuwa mahitaji ya walimu kwa shule za msingi ni 273,000 lakini walimu waliopo ni 175,000 na hivyo kuwa na upungufu wa 35. Aidha, kwa upande wa shule za sekondari, kuna upungufu wa asilimia 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa suala la ajira ya walimu lipo chini ya TAMISEMI, lakini pale kiwango cha elimu kinaposhuka, ni Wizara hii ndio inayoulizwa na hata kusemwa vibaya. Serikali haina budi kuchukua hatua za makusudi kuongeza ajira za walimu ili kulinusuru Taifa, kwani walimu wengi wapo mitaani hawana ajira. Kama Taifa yatupasa tukumbuke usemi wa mwanazuoni Benjamin Franklin aliwhahi kusema: *"An investment in knowledge always pays the best interest."* Hivyo, hatuna budi kama Taifa kuwekeza kwenye elimu kuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua na kuelewa tatizo lililopo la ukosefu wa walimu hasa katika shule za msingi hapa nchini. Hata hivyo, Kamati inaona kitendo cha kuwachukua walimu wa shule za sekondari kwenda kufundisha shule za msingi siyo sawa kwa kuwa kila ngazi ya ualimu ina miongozo na mafunzo yake mahsus. Siyo hivyo tu, kitendo cha kumchukua mwalimu wa sekondari kwenda kufundisha Shule ya msingi kimepokelewa kwa hisia tofauti mionganoni mwa jamii na walimu wenyewe ikiwemo kuhisi kuadhibiwa, hivyo kushusha morali ya kufanya kazi. Kamati inaitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa jicho la kipekee na kufanya maamuzi yaliyo sahihi kwa mustakabali mzuri wa elimu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Teachers Professional Board*; Kamati inaamini kuwa elimu ni haki ya kila mtu na elimu hiyo ni lazima iendane na ubora wake. Tunapoongelea elimu ni muhimu kabisa kuongelea ubora wa walimu kwa kuwa wao ndio wanafundisha watoto wetu. Kwa kuzingatia umuhimu huu, mwanazuoni wa Kituruki Bwana Mustafa aliwhahi kusema: *"A good teacher is like a candle, it consumes*

*itself to light the way to others.*" Walimu wasio na ubora ni dhahiri watazalisha wataalam wasio na ubora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna misemo mbalimbali kuhusu umuhimu wa walimu wenye weledi. Mwanasiasa wa siku nyingi wa Marekani Bob Talbert amewahi kusema: "*Good teachers are costly, but bad teachers cost more.*" (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na walimu wazuri na wenye uwezo wa kutoa elimu yenye ubora unaotakiwa, Serikali haina budi kuunda Bodi ya Taaluma ya Ualimu. Bodi hii kama zilivyo bodi nyingine kama ile ya Wakandarasi itakuwa na jukumu la kufuatilia ubora wa elimu inayotolewa na walimu hawa kwa watoto wetu. Ni kwa msingi huo Kamati inashauri Serikali kuunda Bodi hii mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufahamu ubora wa elimu inayotolewa, suala la ukaguzi ni la msingi sana. Kamati imebaini kuwa kwa muda mrefu sasa Idara ya Ukaguzi katika elimu imekuwa haifanyi kazi yake ipasavyo kutokana na kutotengewa fedha za kutosha. Mwaka 2018/2019 Idara hii imetengewa fedha za ujenzi wa ofisi mpya 50 na ukarabati wa shule 40 za Wilaya. Kamati inaona ujenzi na ukarabati ni jambo jema, lakini suala la ukaguzi siyo la kukaa ofisini tu, ukaguzi maana yake ni kwenda katika mawanda husika (*field visits*) ambapo Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa Idara ya Ukaguzi ili iweze kutekeleza jukumu lake ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili wa watoto wa kike vyuoni; katika ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo hususan katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya pamoja na kile cha Elimu Mkawawa, Kamati ilibaini kuwa watoto wa kike wanaosoma katika vyuo hivyo ni wachache sana ukilinganisha na watoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, wanafunzi wa kike wanaosoma Stashahada ni 344 kati ya wanafunzi 1,759. Aidha, shahada

ya kwanza wanafunzi wa kike ni 365 kati ya 2,459. Hivyo basi, kwa ujumla wanafunzi wa kike wanaosoma katika chuo hicho ni 709 kati ya 4000 sawa na asilimia 17 tu. Kamati inaona ipo haja kama nchi ya kuweka mkakati utakaotilia mkazo na kuwezesha watoto wa kike kusoma masomo ya sayansi katika ngazi ya chini ili kuweza kujiunga na vyuo vikuu vyenye masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya mwaka 2016, Kamati ilieleza kwa kina suala la mfumo wa elimu na ilitolea mfano wa aliyekuwa Rais wa Marekani, Ndugu Ronald Reagan mwaka 1983 alivyofanya maamuzi ya kuunda Tume Maalum ya kuchunguza changamoto ya elimu na Tume hiyo ilikuja na ripoti ilioyujulikana kama *A Nation at Risk; The Imperative for Educational Reform* ambayo ilikuwa ndiyo historia ya mafanikio ya mfumo wa elimu Marekani. Kamati illtoa mfano wa mambo mazuri ambayo iliamini kama Serikali yetu ina nia ya kuboresha mfumo wa elimu nchini, ni vyema ikajifunza kutoka hapo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa pendeleko hilo la Kamati halijawahi kufanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa vipindi tofauti amekuwa akiongelea suala la mfumo wa elimu nchini. Novemba, 2017, alisema; "Tanzania haijaweka msukumo katika kutafakari upya mfumo wa elimu. Kwa hali ilivyo tunahitaji kufanya mapinduzi kwenye elimu."

Aidha, tarehe 18, Machi, 2018 kwa mara nyingine, akizungumza katika hafla ya kumuaga Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Profesa Idris Kikula, Mheshimiwa Mkapa alisema; "Ninaamini kabisa kwamba tuna *crisis*. Ninasoma katika magazeti, ninaletewa *presentation* kutoka sekta binafsi, walimu, *private university*. Napata pia minong'ono kutoka kwa vyuo vya umma kwamba kuna *crisis* katika elimu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Mkapa alisema; "hata ukisoma katika orodha ya shule zetu za sekondari kwenye

ufaulu wao katika 10 za kwanza, ukiangalia unaweza kuwa na uhakika kuwa nane siyo za Serikali, ni za watu binafsi na wakati huo Serikali ndiyo mhimili mkuu wa elimu." Sasa hapo lazima tujiulize, kuna kasoro gani? Kamati inaona dhahiri kuwa kuna ulazima kabisa wa Serikali kuangalia upya mfumo wa elimu nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mfumo huu ni lazima uangalie elimu kuanzia ngazi ya chekechea hadi Chuo Kikuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wanafunzi wawewe kusoma vizuri na kuelewa, uwepo wa vitabu ni jambo la msingi sana. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa vitabu katika shule nyingi hapa nchini. Kwa mfano, vitabu viliyyotoka ni vya darasa la kwanza hadi la tatu tu. Vitabu vya darasa la nne havijatoka na ndiyo wanatakiwa wafanye Mtihani wa Taifa. Tunatambua changamoto ya ubaha wa walimu, lakini mwanafunzi akiwa na kitabu angalau anaweza kujisomea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapata mashaka pia kuhusu umakini wa uandishi wa vitabu hivyo kwa kuwa *Educational Material Approval Committee* ambayo ndiyo ilikuwa na jukumu la kuhariri vitabu imefutwa na mpaka sasa bado hakuna Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kuhariri vitabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali yafuatayo; ivipite vitabu hivyo ili kuhakikisha kuwa havina upungufu kama uliojitokeza katika vitabu vya mwaka 2017. Kamati inatambua kuwa katika mwaka huu wa fedha, Wizara kuitia Mradi Namba 4320 unaohusu Kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania kiasi cha shilingi bilioni 40 kimetengwa kwa ajili ya kuandika na kuchapa mitaala, mihutasari, moduli za mafunzo na kuchapisha vitabu vya shule. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatolewa zote na kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza shughuli iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Bodi ya Mikopo katika kutoa mikopo kwa

wanafunzi wa elimu ya juu. Hata hivyo, Kamati inafahamu changamoto zilizopo katika utoaji wa mikopo ikiwemo baadhi ya wanafunzi kukosa mikopo kwa sababu mbalimbali. Kamati inashauri Serikali kuanzia sasa, ukiacha vigezo vingine, kigezo cha ufaulu kipewe kipaumbele cha kwanza kwa maana mtu aliyefaulu vizuri (*best student*) ndiye apewe kipaumbele cha kwanza kabla ya kuangalia vigezo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuipatia Bodi ya Mikopo fungu lake (*separate vote*) na ijulikane ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na siyo miradi ya maendeleo kama ilivyo sasa, hali inayofanya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii ionekane kubwa kwa kuwa asilimia 48 ni fedha za Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kuwa watoto wote wana haki sawa kupata elimu. Jim Jeffords, Seneta wa Marekani mwaka 1989, aliwahi kusema; “*we have responsibility to ensure that every individual has the opportunity to receive a high quality education from prekindergarten to elementary and secondary, to special education, to technical and higher education and beyond.*” Mtoto mwenye ulemavu ana haki kabisa ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 cha Sheria ya Watu wenye Ulemavu kinaeleza namna watoto wenye ulemavu walivyo na haki sawa ya kuandikishwa shule pamoja na kupata huduma maalum za kujifunzia kutoka kwa mwalimu mwenye sifa stahiki. Aidha, kifungu cha 29 cha Sheria hiyo kinaeleza uzingatiaji wa mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria kueleza haki za watu wenye ulemavu, lakini Kamati imebaini kuwa watoto wenye ulemavu wanakabiliiwa na changamoto nydingi zinazoathiri upatikanaji wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Sheria ya Watoto wenye Ulemavu kutaka watoto wenye ulemavu kutambuliwa

na kusajiliwa, lakini suala hili limekuwa halifanyiki. Watoto hawa wamekuwa wakifichwa kutokana na imani potofu na hivyo kuathiri upatikanaji wa elimu kwao.

Aidha, miundombinu imekuwa siyo rafiki hasa kwa wanafunzi wanaosoma katika shule jumuifu. Kutokana changamoto hizi zote Kamati inashauri; jamii ielimishwe juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wenye ulemavu; Serikali ihakikishe kuwa miundombinu mashulenii inakuwa rafiki kwa watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kama zilivyo nchi nyingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara, bado inakumbana na changamoto ya ukosefu wa Wahadhiri katika Vyuo Vikuu hasa wale wenye Shahada ya Uzamivu (*Ph.D*). Wahadhiri hawa wamekuwa wakihama kutoka katika utumishi wa ualimu na kwenda kutekeleza majukumu mengine hapa nchini ambalo ni jambo jema sana ikwemo teuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inapata wahadhiri wengine wenye Shahada ya Uzamivu kwa kutenga fedha za kuwapeleka kusoma ili waweze kurudi kuwatengeneza wasomi wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Nguvu za Atomiki ni muhimu sana hapa nchini kutokana na majukumu makubwa iliyonayo. Tume hii ndiyo yenye wajibu wa kusimamia matumizi salama ya mionzi, teknolojia ya nyuklia. Kamati imebaini kuwa Tume hii haijulikani kwenye jamii hususan majukumu yake na hivyo ni vyema ikaanza kujitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali haina budi kuiwezesha Tume hii ili iweze kufanya tafiti za kutosha katika Sekta za Kilimo, Afya, Uvuvi, Mifugo, Viwanda, Maji na Nishati kwa lengo la kujiletea maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na *NECTA*. Hata hivyo, hivi karibuni kumekuwepo na usumbufu kwa wanafunzi, hasa wale

wanaosoma kwenye shule zenyе mitaala ambayo siyo ya *NECTA* kuzuiliwa kufanya mitihani ya kidato cha pili kutokana na kutofanya mitihani ya darasa la saba katika mitaala ya *NECTA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inalshauri Serikali kupitia *NECTA*, iorodheshe shule ambazo inaona hazina mitaala ya *NECTA* wala *Cambridge* ili wazazi na wanafunzi waweze kufahamu na kufanya maamuzi stahiki kwa sasa na kuepuka usumbufu huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na sekta binafsi katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kuboresha elimu nchini. Sekta binafsi imechangia kuanzisha shule nydingi na zenyе kuzalisha wataalam wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa shule hizi zinakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo kodi na tozo mbalimbali, zikiwemo ada za mitihani ya kltaifa na gharama za udhibiti ubora kwa mwaka, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Kodi ya Ardhi, Majengo na Ongezeko la Thamani ambazo pamoja na baadhi kuwa na msamaha pale unapoombwa, lakini utaratibu wake siyo rafiki kutokana na kuwepo kwa urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, Kamati imebaini baadhi ya kodi ni kubwa na zinapunguza nguvu na uwezo wa wamiliki wa shule kuendelea na kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuziangalia upya kodi na tozo hizi ikiwa pamoja na kuweka uwiano wa katika kuchangia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kati ya shule za umma na shule binafsi kuwa ni asilimia 0.5 ya pato la mfanyakazi. Kuondoa urasimu katika upatikanaji wa misamaha ya kodi na tozo ili kuwezesha sekta binafsi kupitia msukumo zaidi wa kuwekeza na hivyo kuendelea kuzalisha wataalam wengi na wazuri. Serikali Wizara ya Elimu iweke utaratibu angalau mara mbili kwa mwaka kukutana na wamiliki wa shule za binafsi ili kutatua changamoto zinazoikabili sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru, Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi mzuri, Wajumbe wa Kamati, Waziri wa Elimu Profesa Joyce Ndalichako, Naibu wake William Tate Olenasha, Katibu Mkuu Dkt. Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu, Dkt. Profesa James Mdoe, Dkt. Maria Semakafu pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Pia namshukuru Katibu wa Bunge Mheshimiwa Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson Bisile, Msaidizi wa Kamati yetu Ndugu Modesta Kipiko pamoja na Watumishi wote wa Bunge. Pia wadau wote wa elimu wakiwemo HakiElimu, TWAVEZA, *Policy Forum*, SIKIKA, TAPIE, ADD International/na SHIVYAWATA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitlimisha kwa kuliomba Bunge lako tukufu likubali na kuridhia kuidhinisha makadilio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia - Fungu 46 shilingi 1,406,469,626,000 na Fungu 18 Tume ya UNESCO shilingi 666,855,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA  
MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU  
YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA  
MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI  
YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA 2018/2019  
– KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Nakushukuru kwa kunipa fursa ili kwa kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (6) (5) (c) ilio chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, katika Nyongeza hiyo ya Nane, Kanuni ya 7 (1) (a) inaeleza jukumu la Kamati la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.


**Mheshimiwa Spika**, Kabla ya kupokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Bajeti ya Wizara hii Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo illyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Ukaguzi huu ulifanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Lengo kuu la ziara ni kujiridhisha na ufanisi wa Serikali katika kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

## **2.0 UCHAMBUZI WA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

### **2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Wizara kupitia **Fungu 46** ilikadiria kukusanya Maduhuli ya shilingi **371,604,542,307.46**. Kati ya fedha hizo shilingi **14,258,669,000/=** sawa na asilimia **3.84** zilikadiriwa kukusanya kutoka kwenye Idara za Wizara na kiasi cha shilingi **357,345,873,307.46** sawa na asilimia **96.16** kilikadiriwa kukusanya kutoka katika Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi **287,341,763,666.68** sawa na asilimia **77** ya kiasi kilichopangwa kukusanya. Kati ya kiasi hicho, kilichokusanya, shilingi **8,816,828,827/=** sawa na **asilimia 3.1** ni kutoka katika Idara za Wizara na kiasi cha shilingi **278,524,934,839.68** sawa na asilimia **96.9** kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara. (**Rejea Kielelezo Na.1**)

### Kielelezo Na. 1



**Chanzo: Usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara ya Mwaka 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kuitia **Fungu 18** (Tume ya UNESCO) Wizara ilikadiria kukusanya Maduhuli ya shilingi **40,000,000/=**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Tume ilikuwa imekusanya shilingi **57,529,487.17** sawa na **asilimia 144** ya lengo. **Kamati inapongeza jitihada hizi.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kuitia **Fungu 46**, Bodi ya Huduma za Maktaba pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu zimeongoza kwa ukusanyaji mzuri ambao umezidi **asilimia 100** ya Lengo. **Kamati inapongeza Taasisi hizo kwa ukusanyaji mzuri na inatoa rai kwa Taasisi nyingine kuhakikisha zinafikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli ikiwemo Mamlaka ya Elimu Tanzania ambayo makusanyo yake ni asilimia 15 tu ya lengo.**


#### 2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 (**Fungu 46**) iliidhinishiwa jumla ya shilingi **1,342,117,887,100/=**. Kati ya fedha hizo shilingi **425,276,065,100.01** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na shilingi **916,841,822,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **881,668,618,434/=** sawa na **asilimia 65** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kati ya fedha hizo, shilingi **287,093,933,397/=** sawa na **asilimia 68** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **594,574,685,037.25** sawa na **asilimia 65** kwaajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. (**Rejea Kielelezo Na. 2**)

#### Kielelezo Na. 2




**Chanzo:** usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 18** (Tume ya UNESCO), Kiasi cha shilingi **663,123,000/=** kilitengwa kwaajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi mengineyo) ya Taasisi hii. Hadi kufikia Mwezi Februari 2018 kiasi cha shilingi **443,923,100/=** sawa na **asilimia 67** ya makadirio kilipokelewa (**Rejea Kielelezo Na. 3**)

Kielelezo Na. 3

UPATIKANAJI WA FEDHA KWA FUNGU 46 KWA  
MWAKA WA FEDHA 2017/2018

MIRADI YA  
MAENDELEO  
  
MATUMIZI YA  
KAWAIDA



	MATUMIZI YA KAWAIDA	MIRADI YA MAENDELEO
■ KILICHOPOKELEWA	287,093,933,397	594,574,685,037.25
■ KILICHOIDHINISHWA	425,276,065,100.01	916,841,822,000

Chanzo. Usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa **asilimia 35** ya Bajeti iliyo tengwa kwa **Fungu 46** na **asilimia 33** ya **Fungu 18** ambazo bado hazijapokelewa na Wizara zitatolewa kabla ya Mwaka huu wa fedha kuisha kwani shughuli zilizotengewa fedha hizo bado zipo na ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii ya kitanzania.

**2.3 Maelezo na Matokeo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 14 Machi hadi 21 Machi Kamati ilifanya Ziara ya Ukaguzi wa Miradi iliyo chini ya Wizara inazozisimamia iliyo katika Mkoa wa Iringa na Mbeya. Baadhi ya miradi hiyo ni;

**a) Mradi wa Upanuzi wa Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa (Mradi Namba 4313)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni moja (1,000,000,000/=)** kwa ajili ya upanuzi wa chuo hususan ujenzi wa jengo la Mihadhara. Mradi huu ambao uliana miaka 10 iliyopita (mwaka 2008) ulikuwa wa gharama wa kiasi cha **shilingi Bilioni 3.6**. Hata hivyo katika Taarifa iliyowasilishwa na Mkuu wa Chuo ilionesa Mradi umekuwa ukiendelea kutekelezwa kupitia fedha za Mradi wa Elimu kwa Matokeo Makubwa (*Education Program For Results - EP4R*).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishtushwa na masuala mbalimbali yaliyoelezwa kwenye Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati yakiwemo;

i) Kiasi cha fedha kilichotumika mpaka 2018 ambacho kinafikia **Bilioni 8.4** na bado kuna deni la Mkandarasi shilingi **Milioni 991** na hivyo kama fedha hizi zitalipwa Mradi utakuwa umegharimu kiasi cha shilingi **Bilioni 9.3** ambayo ni takribani mara 2 na nusu ya gharama za awali za mradi ambayo ilikuwa ni shilingi **Bilioni 3.6**; na

ii) Kusitishwa kwa Mkataba wa Mkandarasi wa kwanza MNM ambaye alikuwa amefanya kazi kwa **asilimia 73** na kulipwa fedha kiasi cha shilingi **Bilioni 2.4** sawa na **asilimia 66** ya gharama ya mradi na kuingia Mkataba wa Mkandarasi mwagine CATIC kwaajili ya kumalizia **asilimia 27** kwa gharama ya **shilingi Bilioni 4.9** ambayo ni mara mbili ya gharama iliyolipwa kwa mkandarasi wa kwanza aliyetekeliza kazi kwa **asilimia 73** ya kazi nzima.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliomba kupewa Taarifa ya mchanganuo wa fedha ambao Chuo kimekuwa kinapokea kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu pamoja na kiasi ambacho Wakandarasi wamekuwa wakilipwa. Hata hivyo, Chuo kilishindwa kutoa taarifa sahihi hali ilio lazimu Waziri wa Elimu kuagiza ufanyike Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) ili kuweza kubaini ukweli juu ya Mradi huo.

**b) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Namba ya Mradi 6333)**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 20 Machi, 2017 Kamati ilitembelea Mradi wa upanuzi wa chuo (Ujenzi wa Maktaba) kwa ajili ya kupata sehemu ya wanafunzi kufanya rejea zao ambapo kiasi cha **shilingi Bilioni 3.0** kilitengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kwaajili ya kutekeleza Mradi huu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara, mradi huu uliana katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na ulikadiriwa kuwa na gharama ya shilingi **Bilion 5.5** na ujenzi wake uligawanywa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilikadiriwa kugharimu shilingi **Bilioni 3.35** na awamu ya pili ilikadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi **Bilioni 2.16**.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu kwa awamu ya kwanza ultekelezwa kwa **asilimia 30** ambapo uligharimu kiasi cha shilingi **Bilioni 1.02** sawa na **asilimia 34** ya fedha yote ya mradi kwa awamu ya kwanza uliofanywa na mkandarasi aliyefahamika kama SHIBAT Enterprises Limited ambaye alisimamishwa na Bodi ya Wakandarasi kufanya shughuli za ukandarasi nchini ambayo ilipelekeza pia kushindwa kuendelea na ujenzi wa mradi huu. Chuo ilibidi kuingia na mkataba mpya na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) mwaka 2017 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huu hali iliyopelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi kwa kiasi cha **shilingi Milioni 582** sawa na ongezeko la **asilimia 17** la gharama ya mradi kwa awamu ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka Kamati inatembelea mradi huo, hakuna kiasi chochote cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa maktaba ya hiyo.

**2.4 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia hali halisi ambayo Kamati iliona wakati wa Ukaguzi wa Miradi; inatoa ushauri kwamba:-

a) Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizotengwa kiasi cha shilingi **Bilioni 2** kwaajili ya utekelezaji wa Miradi hii miwili kabla ya

Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuisha ili Vyuo hivi viweze kukamilisha Miradi yake iliyoanza kuitekeleza na kuhakikisha Wanafunzi wanakuwa na mazingira mazuri ya kujisomea; b) Sambamba na Miradi hii, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha zote za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizazra hii zinatolewa kabla ya Mwaka huu wa Fedha kuisha; na

c) Taarifa ya Ukaguzi maalum (*Special Audit*) ulioagizwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu itakapokamiliika ifike mbele ya Kamati kwa ajili ya Taarifa na hatua zaidi.

## **2.5 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu Bajeti ya Wizara hii. Katika kupitia Taarifa ya utekelezaji, Kamati imebaini kuwa yapo baadhi ya maoni yametekelvezwa vizuri kama vile Ujenzi wa Miundombinu. Aidha, baadhi ya maeneo yanaendelea kutekelezwa na yale ambayo Kamati inaona bado hayajatekelezwa ipasavyo itaendelea kuyasisitiza ikiwemo suala la kuwa na tuzo ya Udhamini (*Scholarship Award*) hasa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya kidato cha sita ambayo Kamati ilipendekeza iitwe **Maguful Scholarship Award** na Uainishaji wa Vyuo Vikuu (*University Classification*) kulingana na ubora wake kutokana na kuendelea kuibuka kwa vyuo vingi hapa nchini.

### ***SEHEMU YA PILI***

---

## **3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**


**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yameandalila kwa kuzingatia mipango mbalimbali ikiwemo Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 -2020/2021) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu.

Mpango huu unaeleza kwa kina Shughuli zitakazotekelezwa kama ilivyoainishwa na Waziri mwenye dhamana.

### 3.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara kupitia **Fungu 46**, inakadiria kukusanya shilingi **460,011,442,840.89** sawa na ongezeko la **asilimia 19.2** la kiasi cha shilingi **371,604,542,307.46** kilichokadiriwa kukusanya katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kati ya kiasi hicho kinachokadiriwa, shilingi **16,916,628,402.59** zinatarajiwa kutokana na makusanyo ya Idara na shilingi **443,094,841,438.30** zitatokana na makusanyo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara. (Rejea Kielelezo Na. 4)

Kielelezo Na. 4




Chanzo: Usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara (2018/2019)

**Mheshimiwa Spika**, kupitia **Fungu 18 (Tume ya UNESCO)**, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya shilingi

70,000,000/= sawa na ongezeko la **asilimia 4.9** la kiasi cha shilingi **40,000,000/=** kilichokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. (Rejea Kielelezo Na. 5)

### Kielelezo Na. 5



Chanzo: Usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara (2018/2019)

Mheshimiwa Spika, *Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza Makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa mafungu yake mawili (46 na 18) na inatoa rai kuwa Wizara ihakikishe fedha hizi zote zinakusanywa kabla ya Mwaka wa Fedha kuisha.*

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara kuitia **Fungu 46** inakadiria kutumia kiasi cha shilingi **Trilioni 1.4 (1,406,469,626,000/=)** sawa na ongezeko la **asilimia 4.5** la kiasi cha shilingi **Trilioni 1.3 (1,342,117,887,100/=)** kilichokadiriwa na kuidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Aidha kwa upande wa **Fungu 18** (Tume ya UNESCO), Wizara

inategemea kutumia kiasi cha shilingi **666,855,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 0.5** la kiasi cha shilingi **663,123,000/=** kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 (**Rejea kielelezo Na. 6**).

### **Kielelezo Na. 6**

#### **Chanzo: Usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuungeza Bajeti ya Mafungu haya ya Wizara (Fungu 46 na 18) na imani kuwa kabla ya Mwaka 2030 tutafikia lengo la Azimio la Muscat la Mwaka 2014 linalotaka nchi wanachama kuhakikisha ifikapo 2030 kuwa zimefikia uwezo wa kutenga kati ya asilimia 4 - 6 ya Pato la Taifa kwenye Elimu au angalau asilimia 15 -20 ya Bajeti ya Serikali katika Elimu.**

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa kwa **Fungu 46**, shilingi **406,267,946,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi **70,323,278,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi **929,969,402,000/=** kinaombwa kwa Mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika, Fungu 18** (Tume ya UNESCO), Wizara inaomba **shilingi 334,562,000/=** kwa ajili ya kulipa Mishahara ya Watumishi na shilingi **332,293,000/=** kwa ajili ya Matumizi mengineyo ya Tume.

#### **4.0 HALI YA ELIMU NCHINI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa tatu sasa, Kamati imekuwa ikiongelea kwa kina kuhusu hali ya elimu nchini. Lengo kuu la kufanya hivi ni kutaka sisi wote kama Watanzania tuone muelekeo wa Elimu yetu ili kuweza kushauri ipasavyo. Sehemu hii imekuwa ikieleza kwa kina kuhusu tafiti mbalimbali zinazofanywa na Wadau wa Maendeleo katika masuala ya Elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Elimu yetu bado inakumbana na changamoto nydingi. Tafiti i zinaonesha kuwa bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuweza kutatua changamoto zilizopo kwenye Sekta ya Elimu nchini na kuweza kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals*) hususan **lengo Namba 4 linalohusu ELIMU BORA (Quality Education).**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa matokeo ya programu ya viashiria vya Utoaji Huduma (*Service Delivery Indicators*) ilio chini ya Benki ya Kimataifa ya Ujenzi na Maendeleo/Benki ya Dunia, Tanzania imeongeza uwekezaji wake katika Sekta ya Elimu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Nchi ilipata mafanikio katika uwekezaji huu kwani kiwango cha kumaliza shule ya msingi kiliongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 2000 hadi kufikia zaidi ya asilimia 80 mwaka 2012, **Kamati inapongeza jitihada hizi.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na matokeo hayo, Matokeo ya mwaka 2014 ya Benki ya Dunia yanaonesha kuwa **asilimia 23** ya walimu (**asilimia 20 vijijini na asilimia 36 mijini**) hawakuwepo shulen. Aidha, tafiti imeonyesha pia kuwa **asilimia 53** ya walimu walikuwa hawaingii madarasani pamoja na kuwepo katika maeneo yao ya kazi (shulen). Maana yake ni kwamba wanafunzi walikuwa wanafundisha

kwa wastani wa **masaa 2 na dakika 4** ikilinganishwa na wastani wa **masaa 5 na dakika 12** yanayotakiwa kwa siku. Kwa ujumla ni kuwa wanafunzi wanafundishwa kwa **asilimia 40 tu** na hivyo kuacha **asilimia 60** ya mitaala ikiwa haijaguswa.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti inaenda mbele zaidi na kuonesha kuwa, kwenye shule zenye uwiano mkubwa wa mwalimu kwa wanafunzi, wanafunzi walikuwa na madarasa machache na hii inaonekana zaidi kwenye shule za Sekondari ambapo siyo rahisi kwa Mwalimu kufundisha masomo nje ya masomo aliyosomea. Kwa wastani wanafunzi walifundishwa **vipindi 2 na nusu** tu siku ambayo utafiti ulikuwa unafanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Tafiti zinaonesha pia kuwa, wakati mwalimu mmoja tu kati ya watano ndiye anayemudu mitaala wa kufundisha, uwezo wa walimu wa kufundisha somo ni jambo muhimu na linahitaji kushughulikiwa. Mwanazuoni Thomas Jefferson aliwahi kusema "*If children are untaught, their ignorance and vices will in future life cost us much dearer in their consequences than it would have done in their correction by a good education.*"

**Mheshimiwa Spika**, Ukoefu wa stadi za ufundishaji ni suala linaathiri Sekta ya Elimu, kwani ni mwalimu 1 tu katika 1000 aliyepata alama zaidi ya 80% zinazohitajika. Kuna ushahidi wa kutosha kwamba maarifa ya walimu na uwezo wao wa kuhamisha kwenda kwa wanafunzi (kwa maana ya stadi za ufundishaji) ni kichocheo cha matokeo ya kujifunza ya mwanafunzi. *Kamati inaona ni muda muafaka wa kuwekeza katika ubora wa elimu na si bora elimu kwa kuwepo na walimu bora, mitaala bora na mazingira bora ya kufundishia.*

**Mheshimiwa Spika**, Tafiti zinaenda mbele zaidi na kuonesha kuwa kuna upungufu mkubwa katika upatikanaji wa vifaa katika ngazi ya shule kwani:-

a) **Asilimia 41** tu ya shule ndizo zilizo na miundombini inayokidhi kiwango cha chini cha mahitaji;

- b) Asilimia 47** tu ya shule ndizo zina vyoo vinavyokidhi viwango;
- c) Asilimia 61** pekee zina vifaa vyaa kufundishia vinavyokidhi kiwango cha chini cha mahitaji;na
- d) Ndani ya darasa ni **mwanafunzi mmoja kati ya wanne (25%)** ana kitabu cha kiada cha hesabu au Kiingereza.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na tafiti hiyo, Kamati pia imechambua Tafiti iliyofanya na Taasisi ya Haki Elimu ambayo inaonyesha kuwa bado kuna changamoto zinazoathiri ubora wa Elimu nchini. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- a) Walimu wengi hawana taaluma muhimu na stadi za ujuzi wa kufundisha kwani ni **asilimia 15** tu ndiyo wanalelewa na kuiweza Mitaala wanayofundisha;
- b) Asilimia **37.8** tu ya Walimu ndiyo wana hamasa ya kufundisha shule za Serikali (HakiElimu, 2016), **Kamati inaona hii inachangiwa na changamoto walizonazo walimu kama kutolipwa stahiki, mafao na madeni yao kwa wakati;**
- c) Ufanisi wa Wanafunzi katika Mitihani ya Mwisho ni mbaya. Kwa mfano, katika Matokeo ya Mwaka 2017, wastani wa **asilimia 60** ya Wanafunzi wamepata madaraja ya mwisho (daraja la 4 na daraja 0); *Kamati inatambua kuwa Wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani yao ya Sekondari wanaenda kusoma Udaktari, na Uhandisi ili hali wale wanaopata daraja la 4 ndiyo wanaenda kusoma Ualimu. Wakati huo wanachuo wanaofanya vizuri kwa maana ya daraja la 1 (1<sup>st</sup> class) ndiyo wanabaki Chuo Kikuu kufundisha. Tasfiri yake ni kuwa tunajenga nyumba nzuri kwenye msingi mbovu.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia hali ya ufaulu wa kidato cha nne kwa kipindi cha miaka sita (**Rejea Kielelezo Na. 7**) na kuona daraja la 4 na la mwisho ndiyo linachukua asilimia kubwa kama ilivyosemwa na tafiti ya HakiElimu.

**Kielelezo Na. 7: Hali ya Ufaulu wa Mtihani wa Taifa Kidato cha nne kwa Miaka sita Nchini kwa Asilimia**

*Chanzo: Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia*

- d) Idadi ya Walimu katika shule za Msingi imepungua kutoka **Walimu 191,772** mwaka 2016 hadi Walimu **179,291** mwaka 2017. Upungufu huu wa Walimu umesababisha uwiano wa Mwalimu kwa Mwanafunzi kuwa **1:159** mwaka 2017 kutoka uwiano wa **1:135** mwaka 2016 na wakati kiuhalisia uwiano unapaswa kuwa **1:25**. (Best, 2016 & 2017) **kwa maana kwamba mwalimu anafundisha madarasa matano na robo kwa wakati mmoja;**
- e) Mwaka 2016, katika shule za Sekondari kulikuwa na uhaba mkubwa wa Walimu wa **Hesabu 7,291, Baiolojia 5,181, Kemia 5,373** na **Fizikia upungufu wa Walimu 6,873** (BEST, 2016);
- f) Takribani Walimu **30,232** wapo juu ya **miaka 51** na inakadiriwa kati ya Mwaka 2018 na 2019 Walimu wa Shule za Msingi wapatao **7,743** wanatarajiwa kustaafu. (*Best Regional Data 2017*). **Tafsiri ni kuwa upungufu wa walimu katika shule za msingi utaongezeka na hivyo uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi utaathirika zaidi;**
- g) **Asilimia 93** ya Bajeti ya Elimu inayoenda katika Serikali za Mitaa inatumika katika Matumizi ya kawaida (posho na mishahara) na **asilimia 7 tu** ndiyo inaenda kwenye Miradi ya Maendeleo. **Kamati inasikitika sana.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kuendelea kuwekeza katika elimu ikiwemo kutoa elimu bure hata hivyo Kamati imebaini ufaulu wa shule za Serikali unaendelea kushuka. Kamati imepitia Taarifa ya ufaulu baina ya shule za Serikali na shule za Binafsi kwa Mwaka 2016 na 2017. Hali inaonesha kuwa ufaulu kwa shule za Serikali unazidi kushuka mwaka hadi mwaka kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 8.

**Kielelezo Na. 8 : Mchanganuo wa Ufaulu kwa asilimia baina ya Shule za Serikali na zisizo za Serikali kwa Mwaka 2016 na 2017**

Matokeo ya 2016				
Na.	Aina ya Umiliki wa Shule	Shule 10 Bora	Shule 50 Bora	Bora 100
1	Shule zisizo za Serikali	90%	94%	89%
2	Shule za Serikali	10%	4%	11%
Mwaka 2017				
1	Shule zisizo za Serikali	100%	99%	94%
2	Shule za Serikali	0%	1%	6%

**Mheshimiwa Spika, Kamati pia** imepitia ripoti ya tafiti iliyofanywa na Taasisi ya Twaweza kupitia program ya Uwezo. Tafiti hiyo ambayo imetolewa mwaka 2017 ilihusisha jumla ya **watoto 197,451** kutoka **shule za msingi 4,750**. Taarifa hiyo imeonesha kuwa uwezo wa wanafunzi katika kufanya majaribio inatofautiana kati ya Mkoa na Mkoa na Kati ya Wilaya na Wilaya na kwamba kwa maeneo ya vijijini uwezo wa wanafunzi ni mdogo Zaidi ikilinganishwa na Mjini. Kamati imebaini masuala muhimu yafuatayo:-

- a) **Mwanafunzi 1 kati ya 10 (13%)** wa darasa la tatu ndiyo aliweza kusoma stori ya Kingereza wakati wanafunzi wa darasa la saba ni **wanafunzi 5 kati ya 10 (48%)** ndiyo waliweza kusoma stori hiyo ya Kingereza;

- b) **Wanafunzi 6 kati ya 10 (56%)** wa darasa la 3 ndiyo waliweza kusoma vizuri stori ya Kiswahili. Aidha, kwa watoto wa darasa la 7 ni **9 kati ya 10 (89%)** ndiyo waliweza kusoma vizuri stori hiyo;na
- c) Kwa upande wa hesabu, **wanafunzi 3 kati ya 10 (35%)** wa darasa la 3 waliweza kufanya vizuri majoribio na wale wa darasa la 7 ni **9 kati ya 10 (78%)** ndiyo waliweza kufanya vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, Tafiti pia inaonesha kuwa, kuna maendeleo mazuri ya ufaulu wa somo la Kiswahili kwa watoto wa darasa la 3 kwani umefaulu umeongezeka kutoka asilimia 29 mwaka 2011 hadi asilimia 59 mwaka 2015. *Kamati inapongeza jithhada hizi na inaamini kuwa jithhada hizi zitaendelea.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihitimisha kwa kupitia Taarifa ya UNESCO Institute for Statistics (UIS) "**Reducing global poverty through universal primary and secondary education**" ya mwaka 2017 ambayo inaonesha kuwa;

- a) Umaskini unachangia sana ukosefu wa elimu kwani nchi zenyе kipato cha chini ambazo zinajumuisha Afghanistan, Burkina Faso, Ethiopia, Mali, Msumbiji, Niger na Tanzania zinachangia asilimia kubwa ya watoto ulimwenguni wenye umri wa kwenda shule lakini hawaendi. Kati ya **asilimia 24** ya watoto wote duniani wenye umri wa kwenda shule na hawajaenda, **asilimia 13** wanatoka katika nchi maskini Tanzania ikiwemo; na
- b) Watoto wanaomaliza shule ni wachache ikilinganishwa na walivyoandikishwa. Watoto walioandikishwa shule mwaka 2015 ni **asilimia 62** na kati ya hao **asilimia 27 tu** ndiyo waliweza kumaliza elimu ya msingi kati ya mwaka 2008-2014. Aidha, wanafunzi hawa hata wakimaliza shule bado wanakuwa hawana ujuzi unaotakiwa kutokana elimu wanayopata kuwa ya kiwango cha chini.

**Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo tumeona Sekta ya Elimu

inakumbana na changamoto nyingi sana na kuna haja kubwa ya kuangalia suala la elimu kwa jicho la pekee na kuchukua hatua ya haraka na makusudi ili kuweza kulinusuru Taifa.

### ***SEHEMU YA TATU***

---

#### **5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi huo wa kina kuhusu Bajeti ya Wizara pamoja na Hali ya Elimu nchini, naomba pamoja na maoni haya, Serikali izingatie maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2016 na 2017;

#### **5.1 Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa pamoja na Bunge lako Tukufu kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, lakini fedha hizi zimekuwa hazitolewi zote na kwa wakati. Tumeona katika Vyuo ambavyo Kamati imevitembelea viliwyotengewa jumla ya shilingi **Bilioni 2** kwa pamoja lakini hakuna fedha yoyote iliyotolewa. Ikumbukwe kuwa Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa Vyumba vya Mihadhara na Maktaba ambazo ni nyenzo muhimu sana kwa wanafunzi. **Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kabla ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuisha Fedha zote za Miradi zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zinatolewe ili Wizara iweze kutekeleza Miradi iliyopangwa.**

#### **5.2 Mahusiano ya Wizara na TAMISEMI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiliongelea suala la mahusiano baina ya Wizara hii na TAMISEMI kutohana na kutokuwa na mipaka sahihi ya majukumu. Kamati inafahamu kuwa Mwezi April, 2016 Serikali ilitoa Hati Idhini ambayo ilieleleza Majukumu ya Wizara hii ambapo Kamati imebaini kuwa Wizara kwa sasa ina jukumu la kushughulikia Masuala ya Sera lakini pia mafunzo ya Walimu. Hata hivyo, Kamati inapata shida kwa kuwa

utekelezaji wa masuala yote ya Walimu yakiwemo Maslahi yao yapo chini ya TAMISEMI. Si hivyo tu, lakini Kamati inatambua masuala ya walimu pia yanahuishisha Wizara ya Utumishi na Fedha na hivyo kufanya suala la uwajibikaji kuwa na ukakasi kidogo. *Kamati inashauri kuwepo na uratibu mzuri wa masuala haya ya Walimu ili kuweza kuondoa changamoto wanazokumbana nazo walimu kwa kuwajibika na kushughulikiwa masuala yao na mamlaka zaidi ya moja kwa namna yenyе kuleta mchanganyiko zaidi kuliko kurahisisha.*

### **5.3        Uhaba wa Walimu Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Walimu ni nyenzo muhimu sana katika Sekta ya Elimu nchini. Hata hivyo, Walimu waliopo hawatoshelezi mahitaji hali inayopelekea kuzorota kwa elimu yetu. Kamati ina taarifa kuwa mahitaji ya Walimu kwa Shule za Msingi ni **273,454** lakini walimu waliopo ni **175,946** na hivyo kuwa na upungufu wa walimu **97,508** sawa na **asilimia 35.6**.

Aidha, kwa upande wa Shule za Sekondari na hususan wa Masomo ya Sayansi, mahitaji halisi ni walimu **35,136** lakini waliopo ni **19,285** na hivyo kuwa na upungufu wa walimu **15,851** sawa na asilimia **45.1**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa suala la Ajira ya Walimu lipo chini ya TAMISEMI, lakini pale kiwango cha Elimu kinaposhuka ni Wizara hii ndiyo inayoulizwa na hata kusemwa vibaya. Serikali haina budi kuchukua hatua za Maksudi kuongeza ajira za Walimu ili kulinusuru Taifa kwani Walimu wengi wapo mtaani hawana ajira. Kama Taifa yatupasa tukumbuke usemi wa mwanazuoni Benjamin Franklin aliwhahi kusema "*An investment in knowledge always pays the best interest.*" Hivyo hatuna budi kama Taifa kuwekeza kwenye Elimu kwa kuwa na Walimu wa kutosha.

### **5.4        Walimu wa Sekondari kufundisha shule za Msingi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kuelewa tatizo lililopo la ukosefu wa Walimu hasa katika shule za Msingi hapa nchini. Hata hivyo, Kamati inaona kitendo cha kuwachukua

Walimu wa Shule za Sekondari kwenda kufundisha Shule za Msingi siyo sawa kwa kuwa kila ngazi ya ualimu ina miongozo na mafunzo yake mahsus. Si hivyo tu, kitendo cha kumchukua Mwalimu wa Sekondari kwenda kufundisha shule ya Msingi kimepokelewa kwa hisia tofauti mionganoni mwa jamii na walimu wenyewe ikiwemo kuhisi kuadhibiwa hivyo kushusha morali ya kufanya kazi. *Kamati inaitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa jicho la kipekee na kufanya maamuzi yaliyo sahihi kwa mustakabali mzuri wa Elimu yetu nchini.*

### **5.5 Bodi ya Taaluma ya Ualimu (*Teachers Professionals Board*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaanini kuwa Elimu ni haki ya kila mtu na Elimu hiyo ni lazima iendane na ubora wake. Tunapoongelea Elimu ni muhimu kabisa kuongelea ubora wa Walimu kwa kuwa wao ndiyo wanafundisha watoto wetu kwa kuzingatia umuhimu huu, mwanazuoni wa Kituruki Bw. Mustafa Kemal Ataturk aliwahi kusema kuwa "*A good teacher is like a candle, it consumes itself to light the way to others*". Walimu wasio na ubora ni dhahiri watazalisha wataalam wasio na ubora. Kuna misemo mbalimbali kuhusu umuhimu wa walimu wenyewe weledi. Mwanasiasa wa siku nydingi wa Marekani Bob Talbert amewahi kusema "*Good teachers are costly, but bad teachers cost more.*"

Ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na Walimu wazuri na wenyewe uwezo wa kutoa elimu yenye ubora unaotakiwa, Serikali haina budi kuunda Bodi ya Taaluma ya Ualimu. Bodi hii kama zilivyo bodi nyingine kama ile ya Wakandarasi itakuwa na jukumu la kufuatilia ubora wa elimu inayotolewa na walimu hawa kwa watoto wetu. *Ni kwa msingi huo Kamati inashauri Serikali kuunda Bodi hii mapema iwezekanavyo.*

### **5.6 Ukaguzi wa Shule**

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuweza kufahamu ubora wa elimu unaotolewa suala la Ukaguzi ni la msingi sana. Kamati imebaini kuwa kwa muda mrefu sasa Idara ya Ukaguzi katika Wizara ya Elimu imekuwa haifanyi kazi yake ipasavyo

kutokana na kutotengewa fedha za kutosha. Katika Mwaka huu wa Fedha 2018/2019 Idara hii imetengewa fedha za ujenzi wa Ofisi mpya 50 na ukarabati wa shule 40 za Wilaya. *Kamati inaona ujenzi na ukarabati ni jambo jema lakin suala la ukaguzi siyo la kukaa Ofisini tu, Ukaguzi maana yake ni kwenda katika mawanda husika (field visits) ambapo Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa Idara ya Ukaguzi ili iweze kutekeleza jukumu lake ipasavyo.*

#### **5.7 Usajili wa Watoto wa Kike Vyuo Vikuu**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hususan katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya pamoja na kile cha Elimu Mkwawa, Kamati ilibaini kuwa watoto wa kike wanaosoma katika vyuo hivyo ni wachache sana ukilinganisha na watoto wa kiume. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, katika Mwaka wa Masomo 2017/2018, Wanafunzi wa Kike wanaosoma Stashahada ni **344** kati ya Wanafunzi **1759**, Aidha, kwa shahada ya kwanza wanafunzi wa kike ni **365** kati ya **2459**. Hivyo basi, kwa ujumla wanafunzi wa kike wanaosoma katika chuo hiko ni **709** kati ya **4218** sawa na asilimia **17** tu.

*Kamati inaona ipo haja kama nchi ya kuweka mkakati utakaotilia mkazo na kuwezesha watoto wa kike kusoma masomo ya Sayansi katika ngazi ya chini ili kuweza kuijunga na vyuo vikuu vyenye masomo ya Sayansi.*

#### **5.8 Mfumo wa Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii Mwezi Mei, Mwaka 2016, Kamati ilieleza kwa kina suala la Mfumo wa Elimu na ilitolea mfano wa aliyekuwa Rais wa Marekani Ronald Regans Mwaka 1983 alivyofanya maamuzi ya kuunda Tume Maalum ya kuchunguza changamoto ya Mfumo wa Elimu nchini Marekani na namna bora ya kuenenda ambapo Tume hiyo ilikuja na ripoti iliyojulikana "**A Nation at Risk**" *The Imperative for Educational Reform*" ambayo ilikuwa ndiyo

historia ya mafanikio ya mfumo wa Elimu Marekani. Kamati ilitoa mfano wa mambo mazuri ambayo iliamini kama kweli Serikali yetu ina nia ya kuboresha mfumo wa Elimu nchini ni vyema ikajifunza kutoka hapo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa pendeleko hilo la Kamati halijaweza kufanyiwa kazi na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, tumeona Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Benjamin William Mkapa kwa vipindi tofauti amekuwa akiongelea suala la Mfumo wa Elimu nchini. Novemba 2017 alisema kuwa “**Tanzania hajaweka msukumo katika kutafakari upya mfumo wa elimu, kwa hali ilivyo, tunahitaji kufanya mapinduzi kwenye elimu.**” Aidha, tarehe 18 Machi, 2018 kwa mara nyingine, akizungumza katika hafla ya kumuaga Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Idris Kikula, Mheshimiwa Mkapa alisema kuna janga katika elimu. “**Ninaamini kabisa kwamba tuna *crisis* (janga), ninasoma katika magazeti, ninaletewa *presentation* (mawasilisho) kutoka sekta binafsi, walimu, *private university* (vyuo binafsi). Napata pia minong’ono kutoka kwa vyuo vya umma kwamba kuna (*crisis*) katika elimu,**”

Mheshimiwa Spika, Mzee Mkapa pia alisema “Hata ukisoma katika orodha ya shule zetu za sekondari kwenye ufaulu wao katika 10 za kwanza ukiangalia unaweza kuwa na uhakika kuwa nane si za Serikali ni za watu binafsi na wakati huo Serikali ndio mhimili mkuu wa elimu, sasa hapo lazima tujiulize kuna kasoro gani?”

*Kamati inaona dhahiri kuwa kuna ulazima kabisa wa Serikali kuangalia upya mfumo wa Elimu nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mfumo huu ni lazima uangalie elimu kuanzia ngazi ya chekechea hadi Chuo Kikuu.*

## 5.9      **Ukosefu wa Vitabu Shulenii**

**Mheshimiwa Spika**, ili wanafunzi waweze kusoma vizuri na kuelewa, uwepo wa vitabu ni jambo la msingi sana. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa vitabu katika shule nyingi hapa nchini. Kwa mfano vitabu

viliviyotoka ni vya darasa la kwanza hadi la tatu tu. Vitabu vya darasa la nne havijatoka na ndiyo wanatakiwa wafanye mtihani wa Taifa. Tunatambua changamoto ya uhaba wa walimu, lakini mwanafunzi akiwa na kitabu angalau anaweza kujisomea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapata mashaka pia kuhusu umakini wa uandishi wa vitabu hivyo kwa kuwa EMAC (*Educational Material Approval Committee*) ambayo ndiyo ilikuwa na jukumu la kuhariri vitabu imefutwa na mpaka sasa bado hakuna Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kuhariri vitabu hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

- a) Ivipite vitabu hivyo ili kuhakikisha kuwa havina mapungufu kama yaliyojitekeza katika vitabu vya mwaka jana; na
- b) Kamati inatambua kuwa katika Mwaka huu wa Fedha 2018/2019, Wizara kupitia **Mradi Na. 4320** unaohusu Kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania kiasi cha **shilingi Bilioni 40** kimetengwa kwa ajili ya kuandika na kuchapa Mitaala, Mihtasari, Moduli za Mafunzo na kuchapisha vitabu vya shule za msingi na Sekondari. *Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatolewa zote na kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza shughuli iliyopangwa ikiwa ni pamoja na kuzalisha vitabu na kuvisambaza shulenii.*

## 5.10 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Bodi ya Mikopo katika kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Hata hivyo, Kamati inafahamu changamoto zilizopo katika utoaji wa Mikopo ikiwemo baadhi ya Wanafunzi kukosa mikopo kwasababu mbalimbali. *Kamati inashauri Serikali kuanzia sasa ukiacha vigezo vingine, kigezo cha ufaulu kipewe kipaumbele kwa kwanza kwa maana mtu aliye faulu vizuri (Best Student) ndiye apewe kipaumbele cha kwanza kabla ya kuangalia vigezo vingine.*

**Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Serikali kuipa Bodi ya Mikopo Fungu lake (separate vote) na ijulikane ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na siyo Miradi ya Maendeleo kama ilivyo sasa hali inayofanya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii ioneckane kubwa kwa kuwa asilimia 48 ni fedha za Bodi ya Mikopo.**

### **5.11 Watoto wenyе Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, tufahamu kuwa watoto wote wana haki sawa ya kupata elimu. Jim Jeffords alikuwa Seneta wa Marekani mnamo mwaka 1989 aliwahi kusema "*We have responsibility to ensure that every individual has the opportunity to receive a high quality education from prekindergarten to elementary and secondary, to special education, to technical and higher education and beyond*". Mtoto mwenye ulemavu ana haki kabisa ya kupata elimu.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 cha Sheria ya Watu wenyе Ulemavu** kinaeleza namna watoto wenyе ulemavu walivyo na haki sawa ya kuandikishwa shule pamoja na kupata huduma maalum za kujifunzia kutoka kwa mwalimu mwenye sifa stahiki. Aidha, **Kifungu cha 29** cha Sheria hiyo kinaeleza uzingatiaji wa Mahitaji ya Maalum ya watu wenyе ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Sheria kueleza haki za watu wenyе ulemavu lakini Kamati imebaini kuwa watoto wenyе ulemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi zinazoathiri upatikanaji wa elimu kwao. Licha ya Sheria ya Watoto wenyе Ulemavu kutaka watoto wenyе Ulemavu kutambuliwa na kusajiliwa lakini suala hilli limekuwa halifanyiki. Watoto hawa wamekuwa wakifichwa kutokana na imani potofu na hivyo kuathiri upatikanaji wa elimu kwao. Aidha, miundombinu imekuwa siyo rafiki hasa kwa wanafunzi wanaosoma katika shule Jumuifu. Kutokana changamoto hizi zote Kamati inashauri:-

- a) *Jamii lelimishwe juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wenyе ulemavu ili kuacha kuwaficha kutokana na Imani potofu; na*

*b) Serikali ihakikishe kuwa miundombinu mashulenii inakuwa rafiki kwa watoto wenyewe ulemavu kama vile madarasa, vyoo na njia za kupita.*

#### **5.12 Wahadhiri wa Vyuo Vikuu**

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu kama zilivyo nchi nyiningine za Kusini mwa Jangwa la Sahara bado inakumbana na changamoto ya ukosefu wa wahadhiri katika vyuo vikuu hususan wale wenyewe Shahada ya Uzamivu (PhD). Wahadhiri hao wamekuwa wakihama kutoka katika utumishi wa ualimu na kwenda kutekeleza majukumu mengine hapa nchini ambalo ni jambo jema sana ikwemo teuzi mbalimbali. *Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inapata wahadhiri wengine wenyewe shahada ya Uzamivu kwa kutenga fedha za kuwapeleka kusoma ili waweze kurudi kuwatengeneza wasomi wengine ambao wataendelea kulliletea Taifa letu Maendeleo.*

#### **5.13 Vyuo vya Ufundı - VETA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri miaka miwili iliyopita kuhusu umuhimu wa Vyuo vya Ufundı. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuamua kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundı 28 nchini. Vyuo hivi vitasaidia kuzalisha wataalam wa fani mbalimbali ambao ni chachu katika Maendeleo ya Viwanda. *Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundı (VETA) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 zinatolewa zote na kwa wakati ili tuweze kufikia azma.*

#### **5.14 Tume ya Nguvu za Atomiki**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Nguvu za Atomiki ni muhimu hapa nchini kutohana na majukumu makubwa iliyonayo. Tume hii ndiyo yenye wajibu wa kusimamia matumizi salama ya mionzi, teknolojia ya nyuklia, kubuni na kuendeleza tafiti pamoja na kuratibu miradi mbalimbali ya Kitaifa na Kikanda. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Tume hii haijulikani kwenye Jamii hususan majukumu yake na hivyo ni vyema ikaanza kujitangaza.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, kwa kuwa nchi yetu sasa inaelekea kwenye Uchumi wa kati wa Viwanda, *Serikali haina budi kuiwezesha Tume hii ili iweze kufanya tafiti za kutosha katika Sekta za Kilimo, Afya, Uvuvi, Mifugo, Viwanda, Maji na Nishati kwa lengo la kujiletea Maendeleo Endelevu.*

### 5.13 Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Taasisi hii. Hata hivyo, hivi karibuni kumekuwepo na usumbu kwa wanafunzi hususan wale wanaosoma kwenye shule zenyenye Mitaala ambayo siyo ya NECTA kuzuiliwa kufanya Mithani ya Kidato cha Pili kutokana na kutofanya Mithani ya Darasa la Saba katika Mitaala ya NECTA. Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya shule ambazo zinatambuliwa kwa kuwa na Mfumo wa Cambridge lakini nyingine hazitambuliwi. Ili kuepuka usumbu huko mbele *Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia NECTA iorodheshe shule ambazo inaona hazina Mitaala ya NECTA wala Cambridge ili Wazazi na Wanafunzi waweze kufahamu na kufanya maamuzi stahiki kwa sasa na kuepuka usumbu huko mbele.*

### 5.15 Shule za Binafsi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na Sekta Binafsi katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kuboresha Elimu nchini. Sekta Binafsi imechangia kuanzisha shule nyingi na zenyenye kuzalisha wataalam wazuri. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Shule hizi zinakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo kodi na tozo mbalimbali zikiwemo Ada za Mitihani ya Taifa na Gharama za Uthibiti ubora kwa mwaka, Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi, Kodi ya Ardhi, Majengo na Ongezeko la Thamani ambazo pamoja na baadhi ya kuwa na msamaha pale unapoombwa lakini utaratibu wake siyo rafiki kutokana na kuwepo kwa urasimu. Si hivyo tu, Kamati imebaini baadhi ya kodi ni kubwa na zinapunguza nguvu na uwezo wa wamiliki wa shule kuendeleza na kuboresha miundombinu ya shule. **Kamati inashauri:-**

- a) Serikali kuziangalia upya Kodi na Tozo hizi ikiwa na pamoja na kuweka uwiano wa kuchangia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katì ya Shule za Umma na Shule Binafsi kuwa ni asilimia 0.5 ya pato la Mfanyakazi;
- b) Kuondoa urasimu katika upatikanaji wa misamaha ya kodi na tozo ili kuwezesha Sekta Binafsi kupata msukumo zaidi wa kuwekeza na hivyo kuendelea kuzalisha wataalam wengi na wazuri zaidi.
- c) Serikali (*Wizara ye Elimu*) iweke utaratibu angalau mara mbili kwa mwaka kukutana na Wamiliki wa shule za Binafsi ili kutatua changamoto zinazokabili Sekta ya Elimu nchini.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kuchambua vyema Bajeti ya Wizara hii. Wajumbe wamekuwa wakifanya kazi bila kuchoka na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb	Mjumbe
2.	Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb	Mjumbe
3.	Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb	Mjumbe
4.	Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
5.	Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb	Mjumbe
6.	Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
7.	Mhe. Peter Ambroce Lijualikali, Mb	Mjumbe
8.	Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb	Mjumbe
9.	Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb	Mjumbe
10.	Mhe. Deogratius Francis Ngala wa	Mjumbe
11.	Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
12.	Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb	Mjumbe
13.	Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
14.	Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
15.	Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe

16.	Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb	Mjumbe
17.	Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
18.	Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
19.	Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
20.	Mhe. Mch. Dkt. Getrude Rwakatare, Mb	Mjumbe
21.	Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
22.	Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb	Mjumbe
23.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
24.	Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
25.	Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kukushuru kwa mara nyingine wewe Binafsi kwa kuliongoza vyema Bunge letu. Aidha, nampongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi mzuri.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Prof. Joyce Ndalichako (Mb)-Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Ole Tata Nasha (Mb) - Naibu Waziri, Dkt. Leonard Akwilapo - Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe- Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Ave Maria Semakafu Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipa Kamati katika utendaji kazi wa shughuli zake kila siku ikiwemo wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano mzuri ambao amekuwa akiipa Kamati yetu. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndg. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuipa ushauri wa Kitaalam na kuhakikisha Taarifa hii inakuwa hivi ilivyo. Namshukuru pia Msaidizi wa Kamati yetu Ndg. Modester Kipiko pamoja na Watumishi wote wa Bunge kwa utendaji kazi wake mzuri unaosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini siyo kwa umuhimu,

napenda kuwashukuru wadau wote wa elimu kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kuhakikisha Sekta ya Elimu inakuwa na maendeleo. Wadau hao wamekuwa wakifanya kazi na Kamati kwa karibu sana wakiwamo HakiElimu, Twaweza, Policy Forum, Sikika, TenMet, TAPIE, ADD International na SHIVYAWATA.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuhitimisha kwa kuliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuridhia kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) shilingi **1,406,469,626,000/=** na **Fungu 18**, Tume ya UNESCO shilingi **666,855,000/=**.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono Hoja.

Peter J. Serukamba, Mb.

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA  
MAENDELEO YA JAMII**

30 APRILI, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe kwa taarifa ya Kamati. Tunawashukuru sana Kamati. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, muanze sasa kuchangia, lakini kabla hamjaanza niseme suala la muda. Kwa upande wa wachangiaji Wabunge wa Chama cha Mapinduzi watakaobahatika watakuwa na dakika kumi kila mmoja. Kwa upande wa Kambi ya Chama cha CHADEMA humu Bungeni tunao saba, lakini ni mmoja tu atakuwa na dakika kumi wengine ni dakika tano tano.

Kwa upande wa kambi ya CUF wote ni dakika tano tano, kwa maelezo hayo naanza, mtapata wote kama nafasi itakuwepo tano tano zitawatosha wote ni dakika kumi ambazo ndiyo zina shida tutajaribu, tunaanza Mheshimiwa Profesa Maghembe, atafuatatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Innocent Bashungwa wajiandae.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza hii niweze kuchangia katika hoja hii iliyoko mezani ya Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya elimu imekuwa inapitia mabadiliko makubwa sana katika kipindi cha miaka kumi mpaka 15 sasa. Kwa hiyo, ningependa kwa dhati kabisa nimpongeze Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya uamuzi ambao ni wa kijasiri wa kutoa elimu bure ya msingi. Huu ni uamuzi mkubwa sana kwa sababu katika hatua tuliyonayo sasa ya elimu Rais amekubali tupanue *access* na kwa kuanza ameondoa *fees* katika elimu ya msingi ambayo ni kuanzia darasa la kwanza mpaka *form four*. Kwa hiyo, pamoja na kupanua *access* kwa watoto wengi kupata elimu hii amepanua pia elimu ya msingi kutoka darasa la saba mpaka *form four*. (*Makofii*)

Napenda pia kwa nguvu hizo nipongeze viongozi wa Wizara ya Elimu na hasa binti yangu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndlichako kwa kazi nzuri sana anayoiifanya katika Wizara ya Elimu. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Joyce, *this is very good. (Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda ningetoea mfano huu wa *access* kwa sababu mwaka 2003 wakati mimi ni kipindi changu cha kwanza cha Bungeni hapa vijana waliomaliza *O-Level (form four)* walikuwa 46,000; mwaka jana vijana hao waliomaliza *O-Level* walikuwa wanakaribia 400,000; kwa hiyo, utaona *access* imepanuka kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza elimu hatua ya kwanza kabisa ni kupanua *access*, lakini sasa kilichoko mbele yetu baada ya kupanua *access* lazima sasa tujenge ubora katika elimu yetu, kwa sababu mahali tulipofika sasa tumefika mahali ambapo watoto wanafika darasa la saba wanaweza wasijue kusoma na kuandika. Watoto wanafika *form four* hawawezi kuandika barua, hivi sasa *graduate lawyer* hawezi kuandika *judgment* ya kiingereza. Kwa hiyo, hatua tuliyonayo sasa lazima tuweke

mkakati wa kuboresha elimu yetu ili viwango vilingane na hii *access* ambayo imepanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *level* ya elimu ya msingi ukiangalia matokeo ya mitihani utakuta kwamba kwa miaka yote wala siyo miaka mitano wala siyo miaka sita, watoto wa darasa la saba wanaofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi wanaofaulu mtihani wa hesabu hawazidi asilimia 17 kila mwaka ni hivyo na wanafunzi wanaofaulu mtihani wa Kiingereza katika ngazi hiyo ya msingi hawazidi asilimia 21. Kwa hiyo, kama watoto hawajui hesabu, kama watoto hawajui kiingereza ambacho sasa hatua inayofuata ndicho kinakuwa lugha ya kufundishia haiwezekani watoto hao waweze kupata elimu bora.

Kwa hiyo, jambo la kwanza ambalo tunatakiwa tufanye lazima tuangalie vitabu vinavyotumika, lazima tuwafundishe walimu wetu, tuwe na uhakika kwamba kweli Walimu hawa wanafundisha wana stadi za kufundisha watoto katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano katika mwaka 2007 Wizara ya Elimu ilitoa mtihani wa hesabu wa darasa la saba wa mwaka 1994 ikawapa walimu wa Mkoa mmoja sitautaja ambao wanafundisha hesabu. Watoto wa Mkoa ule walifaulu kwa asilimia 17, lakini walimu waliokuwa wanafundisha hesabu wali-pass kwa asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi utaona kwamba tatizo siyo watoto peke yao na walimu hawana zile *study* zinazohitajika. Wizara sasa imefika wakati ichukue hatua katika kiingereza itengeneze vitabu vya kufundishia watoto. Sisi ambao tulifundishwa mwanzoni na vitabu vile vya kiada vinavyoitwa *New Oxford English Course for Schools*, tulijua kiingereza vizuri sana katika ngazi ile. Mimi sioni sababu gani vitabu vile visihaririwe upya na kuletwa vikafika *level* hii ya leo vikatumika kufundishia watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti umefanywa katika Wilaya ya Moshi Vijijiini na umeonesha kwamba matokeo

mazuri yanaweza kupatikana. Hivyo hivyo ni muhimu sana tuandike vitabu vipyta ya hesabu ya kufundishia watoto, haikubaliki kwamba asilimia 17 tu ya watoto ndio wanaoweza kufaulu hesabu. Tuandike vitabu vipyta, tunayo ile Taasisi inaitwa *Institute of Education* itumike na wataalam tulionao kwenye Vyuo Vikuu watumike kutengeneza vitabu hivi ili viweze kufundisha watoto wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya sekondari tumepanua sana na katika kupanua kuna vitu ambavyo tulifanya lakini bado. Katika ngazi hii wananchi walifanya juhudhi kubwa sana ya kujenga zile shule za sekondari za kata. Walijenga kwa mikono yao wao wenyewe na walipata mafanikio makubwa. Ni muhimu tunavyoongea upanuzi wa elimu ya sekondari tuwapongeze sana wananchi wa Tanzania kwa kiu waliyokuvanayo na nguvu walizotumia kujenga shule za sekondari. Lakini bado ujenzi wa shule za sekondari haujakkamili, bado ujenzi wa shule za kata haujamalizika na hatua iliyofikiwa siyo hatua ya wanavijiji tena, hatua iliyofikiwa ni ya Serikali sasa kwa makusudi kabisa ichukue hatua ijenje maabara zote ambazo zimebaki katika shule za sekondari za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu katika shule zangu 25, wananchi....

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Profesa, hebu subiri kidogo, taarifa Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Profesa katika mchango wake ameongelea mambo mawili ambayo amekuwa akiyashangaa.

Jambo la kwanza ni suala la watoto wetu kutokujua kusoma na kuandika, lakini naomba tu nimpe taarifa ni kwa sababu tumekuwa tukisema kwamba wabadilishe utaratibu wa *multiple choice* kwa mtihani wa darasa la saba, lakini

Serikali imekuwa haisikii. Taarifa nyingine ni kuhusu vitabu vya darasa la nne walimu wetu sasa hawafundishi darasa la nne kwa hakuna vitabu na tumebadilisha kwamba mwisho wao watoto wetu hawa ambao wako darasa la nne...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge usichangie. Endelea Profesa.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia.

Katika ngazi hizi za msingi maana yake, elimu ya msingi na elimu ya sekondari liko jambo lingine kuacha maabara ambalo ni muhimu sana na jambo hili ni Idara ya Ukaguzi wa Shule. Idara ya Ukaguzi wa Shule imekufa, hakuna ukaguzi maana yake kuna Wakaguzi lakini hawana bajeti, kuna ukaguzi lakini hawawezi kwenda shulenii kukagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu elimu ni kama bidhaa nyingine, sema hii ni bidhaa ya thamani kubwa kupita zote, wakati umefika sasa tungeunda *commission* wale walimu wote walioko kule kwenye ukaguzi wangekuwa kwenye Tume ya Ubora wa Elimu. Tungeunda *Education Quality Control Commission* ambayo itakuwa chombo huru chenye uwezo wa kuandikisha shule, chenye uwezo wa kukagua ufundishaji, chenye uwezo wa kuwasimamia walimu wanaofundisha na kama hawafanyi vizuri kuwateremsha cheo, wale wanaofanya vizuri kuwapandisha vyeo na shule zile ambazo zinafanya hovyo kabisa kuzifuta ili kuhakikisha kwamba elimu inapanda kutoka hapo ilipo inakwenda mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu ya juu tumefanya maendeleo makubwa sana katika kupanua upatikanaji wa elimu ya juu. Sasa hivi tunavyo vyuo vikuu karibu 63, lakini hivyo vyuo vikuu sijui nisemeje maana yake viko *very heterogeneous*. Viko vyuo ambavyo ni vyuo vikuu kweli kweli, lakini viko vyuo vikuu ambavyo ungekuwa unahusishwa navyo ungesema jamani siyo mimi, mimi sitaki kukaa huko. Kwa maana hii vyuo vikuu ni lazima vikaguliwe

*very rigorously na hii commission yetu ya Vyuo Vikuu Tanzania.....*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa kwa kwa mchango wako.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono lakini inaelekea yule dada alininyima dakika zangu sikupewa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hapana. Ahsante sana Profesa, Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Dkt. Deodorus Kamala ajandae.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nimpongeze kwa hotuba yake nzuri ambayo imeitoa leo, nilikuwa na karatasi karibia nane za kuchangia, lakini nimejikuta kila akitoa hotuba nachana moja baada ya nyingine na sasa nimebakiwa na kipande nusu ambayo nitaitoa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa programu yake ya elimu bure, katika hili Mheshimiwa Rais ametusaidia hasa ambao tunatoka majimbo ya vijijini ambayo asilimia kubwa wazazi ni wakulima. Kuna changamoto chache fedha hii imekuwa ni kidogo sasa hivi utakuta katika shule zetu za kule vijijini walimu yale mazoezi ya kila Jumamosi wanaandika ubaoni. Kwa hiyo, naomba waongeze pesa ili walimu waweze kwenda kisasa na kuwapunguzia mzigo wa kuandika ubaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine sasa hivi Serikali ambacho inatakiwa tu kuifanya ni kuwafanya walimu waifurahie ile kazi kama kazi zingine wasiichukulie kama tunavyowachukulia, wawajengee nyumba, wawapandishe madaraja kwa muda, maana yake

kumekuwa na changamoto kuna walimu wanafundisha hadi miaka 12 hawajapanda daraja hata moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hili linahusu upande wa TAMISEMI kidogo, lakini naomba mshirikiane na Wizara. Hawa Walimu ambao wametolewa sekondari kupelekwa shule za msingi kuna sintofahamu, kuna walimu ambao wana diploma wameachwa sekondari, wamechukua walimu wenye *degree* wamewapeleka shule za msingi hili ni tatizo kwa sababu mliwaachia Walimu Wakuu na Maafisa Elimu walismamie wenyewe matokeo yake wamefanya ndivyo sivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ukaguzi ameliongelea Mheshimiwa Maghembe; Wakaguzi wengi hawa hata vyombo vya usafiri. Sasa kwa ambao tunatoka majimbo ya vijijini inawawia vigumu kwenda kukagua hizo shule matokeo yake wamekuwa wakikagua makaratasni na ndio maana ufaulu unashuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea suala la vitabu wiki iliyopita kwa kweli hili ni tatizo, tuna shule zaidi ya 170,000 vitabu vya darasa la nne ambao wanatakiwa wafanye mtihani mwezi wa Novemba mpaka leo hii havijatoka. Hebu niambie, kuvisambaza hivi vitabu Serikali yetu ninavyoifahamu na ukosefu wa magari katika Wilaya zetu huko kwenye sekta ya elimu vinaweza vikachukua zaidi ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, wanafunzi wa darasa la nne mwaka huu ninauhakika watafanya mitihani wakiwa hawajapata vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kukariri madarasa, hii iko kwenye *secondary schools*. Wizara tulitoa maoni, Kamati wametoa maoni na Wabunge tunaomba kusitizia, endapo tutaruhusu wanafunzi waende ili mradi waende baada ya miaka mitano tutazalisha kizazi cha wanafunzi ambao hamna kitu. Kwa sababu huwezi ukampeleka mwanafunzi kidato cha pili kama hakuelewa kidato cha kwanza na hawezi akafanya chochote kidato cha pili kama hajafanya kidato cha kwanza.

Kwa hiyo, mngeliachia kwa shule za *private* wao wana utaratibu mzuri wafanye kwa ajili kuzalisha matokeo mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nichangie kwenye upande wa *Loans Board*. Niipongeze Serikali kwa kuongeza fedha za *loans board*, lakini limetokea tatizo sasa hivi hakuna kigezo maalum cha kusababisha wanafunzi wapate mikopo. Kwa mfano, mwenyewe nina ushahidi, kuna Taasisi moja ya Solida Made ambayo ilikuwa inasomesha wanafunzi, inawasaidia kutoka shule za sekondari mpaka Chuko Kikuu. Mwaka huu walikuwa na wanafunzi zaidi ya 400, walikubali kuwalipia ada za Chuo Kikuu wale wanafunzi ambao hawana uwezo, ambao waliwasaidia tangu shule za msingi, lakini walivyofika Chuo Kikuu Serikali ikagoma kuwapa mkopo ikasema hawana utaratibu huo. Zile taasisi walichotaka ni Serikali lwagharamikle fedha za chakula, lakini ada watawalipia wenyewe, Serikali ikakataa. Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu anaweza akanitolea ushahidi nilifika ofisini kwake, Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo nilifika ofisini kwake, lakini wamekataa kuwapa wanafunzi hawa mikopo. Taasisi imetusaidia kuwalipia ada, lakini ninyi mmekataa kutoa fedha za chakula, kwa hiyo hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine niliongea wiki iliyopita Waziri alisema hakunielewa vizuri na Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi. Kumekuwa na tatizo ya Vyuo Vikuu, wanafunzi wetu wa kike wanapata shida mno. Katika vyuo vyetu vikuu kuna walimu ambao wanajulikana kabisa kuwa hawa Walimu ni madume ya mbegu, wanafelisha wanafunzi wa kike, wanataka wawape rushwa za mapenzi ndiyo wawafaulishe. Mheshimiwa Waziri nitashirikiana na wewe kama utanipa ushirikiano, nitakuletea majina ya walimu wa Vyuo Vikuu vyote Tanzania ambao ni madume ya mbegu kazi yao ni kufelisha wanafunzi na kutaka rushwa za ngono. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara chini kitengo chake cha P4R kwa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule za sekondari. Kwanza niwapongeze katika kujenga

shule mpya na nyumba za Walimu. Mimi mwenyewe binafsi nimepata shilingi milioni zaidi ya 500 kwa ajili ya kukarabati shule yangu moja ila ninachoomba hii fedha ya P4R iende moja kwa moja kwenye Halmashauri lakini wasitumie Wakandarasi, kwa sababu tumeshuhudia wakitumia Wakandarasi fedha inakwenda nyingi lakini inafanya kazi kidogo lakini mkitumia *Force Account* ile fedha kidogo inafanyakazi kubwa. Naomba mtoe maelekezo hii fedha mtumie *force account*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kushuka kwa ufaulu. Muda wangu bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia zaidi ya asilimia 60 wanapata *division four* na *division zero*, naomba mtumie nguvu kubwa katika kuwekeza katika vyuo vya ufundi hii mlaka minne ambayo mwanafunzi anasoma kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne tungewekeza kwenye ufundi angeweza ku-*achieve* kitu kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nataka niiase Serikali yangu. Serikali yangu tumeichukulia shule za *private* kama adui, yaani tunavyoichukulia CHADEMA na CCM na ndio Serikali na shule za *private*. Imekuwa kumiliki shule ya *private* ni sawa na kupita na mihadarati katika kituo cha Polisi.

Naomba niwatoe hofu Serikali, mitaala mnatunga ninyi, mitihani mnatunga ninyi, tarehe ya kufanya mitihani mnaweka ninyi, kusimamia mnasimamia ninyi, mitihani mnasahihisha ninyi, matokeo mnatangaza ninyi, hofu yenu ni nini na shule za *private*? Fanyeni vizuri hizi shule za *private* zitakufa zenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulinda muda, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie maoni ya Kamati, hotuba yake ni nzuri sana, tangu nimfahamu Waziri hotuba hii ni ya kwanza, *good!* Endelea hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Ndugu Mlinga kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Balozi Diodorus Kamala na Mheshimiwa Abdallah Bulembo wajiaandae.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii muhimu ya sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya hususani katika sekta hii ya elimu. Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020 tuliahidi kutekeleza elimu bila malipo na tumeona tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeaingia madarakani Serikali inafanyakazi nzuri katika ahadi hii ikiwemo ruzuku ya kusaidia elimu bila malipo imetoka bilioni 19 hivi sasa imefikia bilioni 23, kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali. (*Makofii*)

Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako kwa hotuba nzuri na pia niwapongeze Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Wajumbe wote kwa taarifa nzuri ya Kamati na ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa kaka yangu Naibu Waziri Olenasha kazi nzuri mnayoifanya mkiweka taarifa nzuri ya Kamati na michango ya Wabunge nina imani kabisa tutaleta maboresho makubwa katika sekta ya elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, mimi nina mambo kama manne na muda ukiruhusu basi nitazungumzia mambo matano:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na suala la maslahi ya walimu nchini. Hapa Bungeni toka nimekuwa Mbunge tunakwenda mwaka wa tatu, katika kipindi cha maswali na majibu katika bajeti zilizopita tumezungumzia sana juu ya kero zilizopo kwenye maslahi ya walimu nchini, tumeona *speed* ya kutatua kero hizi haiendei katika *speed* ambayo

inaridhisha. Moja ya changamoto ya *speed* ndogo katika kutatua kero za walimu nchini ni tatizo la muundo wa kitaasisi. Kuna mambo mengine ukiyafuatilia unaambiwa hili suala liko chini ya Afisa Utumishi wa Wilaya, ukitoka kwa Afisa Utumishi wa Wilaya wanasema hili liko Wizara ya Utumishi, ukienda Utumishi wanasema hili liko Wizara ya Afya. Niishauri Serikali, sina shida na *structure* ilivyo ya kitaasisi, lakini Serikali mtambue kwamba lazima muwe *coordinated* vizuri katika kuhakikisha mnatatua changamoto za sekta ya elimu nchini kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kuna walimu Karagwe na nchini toka mwaka 2012 mpaka hivi sasa hawajapandishwa madaraja, kuna walimu nchini ikiwemo Karagwe walimu waliopandishwa madaraja toka mwaka 2012 mpaka hivi sasa mishahara yao haijarekebishwa *ku-reflect* daraja walilopandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu ambao waliondolewa madaraja lakini mpaka hivi sasa wako kwenye daraja hilo hilo, hawajui kama watakanne kwenye daraja hilo mpaka wanastaafu; kuna walimu ambao Serikali iliwhamisha kutoka shule za sekondari kwenye shule za msingi lakini mpaka hivi sasa hawajapata stahiki zao. Kule Karagwe Serikali imetoa shilingi milioni 50 lakini mahitaji halisi ni zaidi ya shilingi milioni 400, wakati Mheshimiwa Waziri ana-wind up nitake kusikia kutoka TAMISEMI na Wizara ya Utumishi na kwa sababu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ndalichako ndiye una dhamana ya kusimamia sera ya elimu nchini tunaomba tusikie majibu ya Serikali mmeji-*coordinate* vipi kuhakikisha mnatatua kero za walimu nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuzungumzia ni uwekezaji katika sekta ya elimu. Wawekezaji katika sekta ya elimu ni wabia wa Serikali na ni wasaidizi wa Serikali katika kutoa huduma ya elimu nchini. Kwa hiyo, Serikali mnatakiwa muwaangalie hawa kama *partners*, Serikali mnatakiwa mtambue kwamba uwekezaji katika elimu *is social investment siyo business as usual*. Kwa

hiyo kwa kutambua hilo, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imezungumzia vizuri changamoto hii. Nipende kuomba Mheshimiwa Waziri hii *perception* iliyopo kwamba kuna *tag of warkati* ya Serikali na sekta binafsi naomba katika *winding up* yako uwahakikishie wawekezaji katika sekta ya elimu na Watanzania kwamba Serikali na hawa wawekezaji mko pamoja na wote ni *partner* katika kutoa elimu nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *tax payments* na *non-tax payments* katika sekta ya elimu ambazo wote tukitambua kwamba elimu ni *social investment* lazima mziondoe kwa sababu hii ni *social investment siyo business as usual*. Kwa mfano...

## TAARIFA

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Innocent, msomi wakati anachangia alikuwa anaongelea suala la Serikali kuipongeza kuhisiana na suala la elimu bure, sasa ninataka nimuongezee kwamba Serikali imekuwa ikijikita kwenye *quantity* na siyo *quality*. Kwa hiyo, naye ajikite kwenye kuishauri Serikali iangalie *quality of education not quantity of the students who are finishing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa hiyo nilitaka nimpatie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashungwa

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimwa Mwenyekiti, taarifa ya ndugu yangu Mwambe siipokei kwa sababu Roma haikujengwa siku moja. Kama nilivyosema kwenye utangulizi wangu toka Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani tumeona jitihada nzuri zikienda kwenye kuboresha sekta ya elimu na ndiyo maana nimesema kupitia Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Wabunge Serikali ichukue ushauri huu ili tuzidi kuboresha sekta ya elimu nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *point* yangu ya tatu na jambo hili nimelisikia hata kwenye taarifa ya Kamati na mdogo wangu Mlinga amelizungumza, zuio la Serikali la wanafunzi wetu kukaririshwa mimi sijaelewa mantiki yake labda Mheshimiwa Waziri wakati una-*wind up* nisikie *rationale* ya kuzuia wanafunzi wasikaririshwe ni nini, kwa sababu ukiangalia takwimu katika ufaulu zina-*alarm* sana, ukiangalia *division zero* na *four* asilimia isiyopungua 60 hawaendi *form five* na vyuo vikuu kwa sababu wanapata *division zero* na *four* kwa vile kujifunza ni *building blocks* na kuna baadhi ya *syllabus* usipozielewa *syllabus* zinazofuata hutazielewa vizuri. Ukizuia wanafunzi wasikariri ili waweze kujenga maarifa na weledi mzuri kabla hawajapanda darasa lingine pia ndivyo unazidi kuchangia katika kufeli kwa wanafunzi kupata *division zero* na *four*.

Kwa hiyo, ushauri wangu Serikali mkae na wadau wa elimu muangalie jinsi ya kuliweka hili vizuri kwa sababu inabidi tuhakikishe watoto wetu tunawaandaa kufaulu lakini kuwa tayari kwa ajili ya soko la ajira pale wanapohitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, hii asilimia 60 au zaidi ambayo inaishia *form four* kwa kupata *division zero* na *division four* niishauri Serikali kuwa na mkakati maalum wa *Vocational Training Institutions* ziweze ku-*absorb* vijana wetu hawa *as many as possible* kwa sababu tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, tunahitaji *skill set* siyo mpaka mtu awe na *degree*, anaweza akawa ana *certificate* ya ushonaji, anaweza akawa na *certificate* ya kutengeneza *grill* lakini tunawaangaliaje na tuna mkakati gani ndani ya sekta ya elimu kama Waziri mwenye sera na una-*coordinate* vipi na Wizara nyininge kuhakikisha kuna mkakati mahsusni ndani ya Serikali wa kuhakikisha wanafunzi wetu hawa wanaopata *division zero* na *four* wanakwenda kwenye *Vocational Training Institutions* na pale wanapomaliza tunahakikisha tunawapa mikopo ya bei nafuu ili na wenywewe waweze kuanza maisha na kupunguza tatizo la ajira nchini na kama mnavyofahamu vijana hawa tusipokuwa na mkakati mahsusni ndipo utakuta hata uhalifu nchini unaongezeka. Kwa hiyo, nipende kuiomba Serikali, pamoja na hili suala la zuio la kukaririsha

mliangalie vizuri. Pia muangalie hawa ambao wanaishia *form four* tuna mkakati gani kuhakikisha wanaenda kwenye *short courses*, wanapata *certificate* na wakishapata hizo *skills* tunawasaidiae kupata mikopo ya bei nafuu ili waweze kujikimu na maisha. (*Makofii*)

Jambo la nne sasa niende Jimboni kwangu Karagwe. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana nilivyokuja kwako nilikwambia kwamba Karagwe wakati naingia kama Mbunge tulikuwa hatuna hata *A-Level*/moja, ulinisaidia sasa hivi tumejenga mabweni mawili pale Bugene Sekondari, *A-Level* imeanza, sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri jiografia ya Karagwe ilivyo nimeshakuomba kwamba tusaidie tupate *A-Level* tatu, Nyabihonza Sekondari imezungukwa na Kata Nane ambazo hazina *A-Level*/kuna mrundikano mkubwa sana wa wanafunzi sasa hivi Bugene Sekondari kwa sababu kwanza miundombinu bado ni michache lakini Wilaya yangu nina wananchi zaidi ya 360,000 na asilimia kubwa ya Taifa hili ni vijana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba Bugene sekondari tusaidie ikamilike iwe *full-fledged A-Level* lakini wakati unafanya hivyo pia nisaidie Nyabihonza Sekondari, Nyakasimbi Sekondari na Kitundu Sekondari na zenyewe zikamilike ili ziweze kusaidia na Wilaya ya kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Wilaya ya Kyerwa, Wilaya ya Ngara tuwe tuna *A-Level* ambazo zitakuwa zinasaidia hii elimu bila malipo ambayo Serikali imeanzisha, wale watoto wakienda sekondari tuwe tuna *A-Level* ndani ya Mkoa ambazo zitasaidia kuandaa Taifa la kesho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* ya mwisho ni Sheria ya Elimu Namba 25...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, nilikuruhusu umalize. Tunaendelea na Mheshimiwa Kamala, Mheshimiwa Bulembo atafuatia.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba hii muhimu iliyopo hapa mbele yetu. Nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Profesa kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kusimamia sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo masuala machache ambayo ningependa kuchangia na nitajaribu kwenda kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo ningependa kuchangia ni kwamba sote tunaelewa Wizara ya Elimu ndiyo inayotoa sera na miongozo ya kusimamia elimu, lakini pia Serikali inazo shule ambazo nyingi zinasimamiwa na TAMISEMI, kwa hiyo Serikali inatoa sera lakini vilevile inamilliki shule. Huwezi ukawa wewe ndiyo unamilliki shule na wewe mwenyewe ndiyo unatoa sera na unajisimamia. Nadhani wakati umefika wa kuwa na chombo ambacho ni *independent* cha kusimamia elimu na chombo hicho sasa tukiunde, kitaundwa kwa sheria (*Tanzania Education Regulatory Authority*) kisimamie shule za Serikali lakini pia kisimamie shule za binafsi na kifanye hivyo kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawezekana na tukifanya hivyo tutaweza kupiga hatua kwa sababu haliingili akilini unakuta Afisa Elimu anasimamia shule binafsi ina upungufu wa choo kimoja au vyoo viwili inafungwa halafu unakuta shule ya Serikali haina choo lakini inaendelea, hii inakuwa siyo sawa. Jambo hili inabidi tuliangalie, labda niseme tu mimi similiki shule lakini siku zijazo ninaweza nikamiliki shule pia, kwa hiyo sina maslahi yoyote katika hili bali nazungumza kwa maslahi mapana ya maendeleo ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ningependa kuzungumzia changamoto. Ziko changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya shule binafsi na nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hussein Bashe kwa taarifa nzuri

aliyowasilisha kwa niaba ya Kamati yake. Mheshimiwa Hussein Bashe kati ya jambo ambalo na mimi najivunia kwa sababu nilikufundisha siasa na naona unajifunza vizuri uendelee hivyo na kwa taarifa uliyowasilisha hapa imebainisha mambo mazito ambayo yatasaidia sekta ya elimu, kwa hiyo unapofundisha wanafunzi wako na wakafanyakazi nzuri wapongeze. Mheshimiwa Bashe nakupongeza kwa kuwasilisha vizuri mawazo ya wenzako kwenye Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ziko nyingi, changamoto hizi lazima tuziangalie na tuzifanyie kazi. Moja, ukiangalia shule binafsi tuna zaidi ya shule 4,000 sasa na shule za Serikali zipo lakini ukiangalia matokeo ya mwaka jana 2017 shule 100 zilizofanya vizuri kulingana na matokeo yaliyotolewa na Wizara ya Elimu, Serikali ilikuwa na shule nne na shule binafsi ni 96 ukiona hivyo maana yake lazima tuangalie Serikali tuna kazi ya kufanya lakini pia lazima tuendelee kuziunga mkono shule hizi binafsi kwa sababu zinapofanya vizuri ndipo tunajivunia kwamba sasa shule 100 bora, kwamba shule 100 bora hizi, 96 ni binafsi na nne tu ndiyo za Serikali sasa ikishakuwa hivyo ni vizuri kuziwezesha hizi shule na kushughulikia changamoto zinazowakabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto zinawakabili ni utitiri wa fedha ambazo wanalipishwa. Kwa mfano, ukihitaji walimu kutoka ndani ya Afrika Mashariki kama ni shule binafsi unaambiwa lazima uende Idara ya *Labour* kule ulipe dola 500 kwa kila mwalimu pia ulipe dola 550 Idara ya Uhamiaji kwa kila mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kati ya jambo ambalo nikiri nadhani na wewe baadae utakiri kati ya jambo ulipokuwa Waziri na mimi nilikuwa Naibu wako tulipokuwa tuna-*negotiate common market* kati ya jambo ambalo nadhani tulikosea ni pale tuliporuhusu kwamba sasa hizi ada zitaendelea kuwepo na tulisema kwamba ziwe kidogo a *token*, isiwe chanzo cha mapato, lakini kama unavyofahamu siku hizi mawazo yetu tulifikiri hii haitakuwa chanzo cha

mapato watu wamegeuza imekuwa chanzo cha mapato sasa matokeo yake tunaziadhibu shule binafsi bila sababu ni jambo ambalo nadhani liangaliwe kwa sababu linaongeza gharama nyingi bila sababu za msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nadhani tuliteleza ukikosea lazima ukubali makosa tulizungumza wakati ule kwamba tunahitaji tu walimu wa *degree* peke yao kutoka nje ya Tanzania, tulifikiri tunao walimu wa kutosha ndani ya nchi, lakini ukweli umeonesha kwamba hata ndani ya nchi hatuna walimu wa kutosha ndiyo maana tuna upungufu wa walimu, pia ukianagalia kwa umakini ni kwamba kwa upande wa walimu wa kufundisha hizi za *english medium* tuna upungufu wa walimu wa sayansi 26,000 na kila mwaka tuna uwezo wa kutoa walimu 2000 sasa tunapozua kwamba walimu wasitoke nje ya Afrika Mashariki tunajadhibu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto ambayo ziko na kodi nyingi zimeorodheshwa hili ni jambo la kuangalia kinachotakiwa ni dhamira ya kujua kwamba shule binafsi hizi siyo binafsi, kwangu mimi naweza nikasema hakuna shule binafsi ni kwamba unakuwa na shule mbalimbali nyingine kwa sababu una uwezo unaziendesha mwenyewe ambazo hauna uwezo unakariobisha *private sector* inafanya kazi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kule kwetu Misensi tuna *Minziro High School*/tunajenga kule, Bwabuki tunajenga *high school/pale* na Bunazi tumeanzisha *high school/inafanya* vizuri, nichukue nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Waziri tunapoendelea kujenga shule hizi *high school* ambazo ni muhimu sana basi niombe Wizara yako itusaidie wananchi wa Miseneye ili tuweze kuenda kwa kasi ambayo inatarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi pia kuzipongeza shule binafsi zilizo katika Wilaya ya Misensi, niipongeze Kadea Sekondari ambayo ina *headmaster* huyu anatoka Uganda, lakini shule hii inafanya vizuri sana karibu

kuliko shule zote na kitu kikubwa alichonacho huyu *headmaster* anasisitiza *discipline*. Nadhani *discipline* ni jambo muhimu sana ukiangalia Kadea Sekondari kitu peke inachozishinda shule zote zilizotuzunguka pale ni *discipline*, wakifanya mitihani wanafanya vizuri kuliko shule zote, lakini kuna shule nydingine pale Kanyigo inaitwa *Kanyigo Islamic Seminary* na hii inafanya vizuri sana ukiangalia sifa yao kubwa waliyonayo ni *discipline*, ukienda kule Tweyambe wanafanya vizuri sana ni *private* hizi sifa kubwa waliyonayo ni *discipline*. Kwa hiyo, Profesa nadhani eneo hili la kusisitiza umuhimu wa *discipline* mliangalie jinsi gani na shule zetu za Serikali zinaweza zikatoa kipaumbele kwanye masuala ya *discipline* ili tuweze kuendelea kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi. Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae. Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi ya leo na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama katika Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema Wabunge wengine na mimi niungane nao kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa kazi nzuri anayofanya na alianza kufanya hata kabla hajawa Waziri, alikuwa mtumishi mwema kule alikokuwa *NACTE* na naamini anaendeleza utumishi huo, mimi sina la kukwambia zaidi ya kukuombea kwa Mwenyezi Mungu na kuwaombea watumishi wengine wa Wizara hii kwa Mwenyezi Mungu ili kazi yao iendelee kuwa njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kupongeza Serikali kwa programu ya lipa kulingana na matokeo (*EP4R*), kwa programu hii wamefanya kazi kubwa

ya ukarabati wa shule kongwe nchini. Katika mkoa wangu wa Dodoma wamekarabati shule ya sekondari Mpwapwa, shule ya sekondari Dodoma, shule ya sekondari Bihawana na Shule ya sekondari ya Msalato pia. Wanafanya kazi nzuri, shule hizi zilikwishachakaa na siku moja tuliiingia katika vyoo vinavyotumika katika shule hizi nilishangaa uwepo wa Mungu kwa wanafunzi, kwa sababu nilishangaa watoto hawapati *fungus*, shule ilikuwa yanatisha hasa vyoo na mabweni.

Kwa hiyo niombe sana Serikali waendelee na programu hii na Mheshimiwa Waziri nikuombe Dodoma sasa ni Makao Makuu na hatuna majengo shule ya mfano na hasa ya wasichana katika Mkoa wa Dodoma, kama kuna uwezekeno programu hii itusaidie kujenga shule kubwa ya kitaifa, shule ya wasichana ambapo wasichana watajengewa mabweni, walimu watakuwa wa kutosha na iwe shule ya sayansi, tunawataka wasichana ambao watasoma sayansi kusaidia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru pia kwamba tumeona Waraka Na. 2 wa mwaka 2016 unayozungumzia kiwango cha ufaulu kwamba mwanafunzi wa *form two* akipata "D" mbili anaruhusiwa kuendelea na elimu, anaruhusiwa kusonga mbele darasa lingine, lakini hao wanafunzi wanaoruhusiwa kwa "D" mbili kwenda *form three* au kidato cha tatu ndiyo hao tunaowategemea kwenda vyuo vikuu, tunawaruhusu kwa ufaulu mdogo mno.

Mheshimiwa Waziri wewe ni Profesa, unajua ulivyo-*fight* kupata uprofesa wako, hukwenda na "D" mbili kidato cha tatu, kuna haja ya kubadilisha ufaulu kwa watoto wa sekondari tunawandaa wanafunzi kuwa maprofesa, tunataka watoto wetu wawe maprofesa kama wewe, tunataka wawe madaktari ufaulu wa chini wa "D" mbili haufai na umepitwa na wakati Mheshimiwa Waziri, niombe Serikali sasa na ukimwambia mtoto "D" mbili anakwenda kidato cha tatu hajishughulishi na kusoma na hata walimu hawaongezi bidii katika kufundisha kwa sababu anajua mtoto akipata "D" mbili anaingia kidato kingine. Kwa hiyo, niombe sasa kuwepo na ushindani ili wanafunzi

wajishughulisse na walimu wajishughulisse kuwaandaa watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne hawapati nafasi ya kuingia kidato cha tano na wale wanaomaliza kidato cha sita wanashindwa kupata nafasi ya kuendelea na vyuo vikuu. Wanafunzi hawa wanarudi mitaani, lakini wanaporudi mitaani hawana kazi za kufanya, tunasema Serikali iwake asilimia tano ya mapato ya Halmashauri zetu ili wajjandae kuwa wajasiriamali, hawana elimu ya ujasiriamali pamoja na elimu wanayopata kwa muda mfupi kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii lakini haiwasaidii sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiimarisha *VETA*, ikaimarisha JKT na ikapeleka vifaa kwa ajili ya kujifunzia, watoto wetu wanaomaliza kidato cha nne wakaenda *VETA* wale wanaomaliza kidato cha sita wakashindwa kuendelea na masomo wakaenda *VETA* wakitoka kule watakuwa na stadi ya kuwatoshya kujitegemea na hata Serikali unapotoa mkopo kwa ajili ya ujasiliamali wanapopewa mikopo ya kutoka Halmashauri zetu watakuwa na uwezo wa kujitegemea. Tunapowapa mikopo na elimu hiyo wanayotoka nayo ya nadharia sidhani kama elimu hiyo inawasaidia na matokeo yake asilimia 40 tu ya mikopo ya vijana inarudishwa asilimia 60 wanashindwa kurudisha kwa sababu hawana elimu ujasiliamali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tafiti zinazofanywa na vyuo vikuu na hasa Chuo Kikuu cha Kilimo (*SUA*). Tunategemea *SUA* iwasaidie wakulima wetu tafiti wanazozifanya za mazao, tabianchi, itusaidie katika kukuza kilimo, lakini tafiti hizi haziwafikii wakulima. Tafiti hizi zinaishia kwenye makaratasi na sana wanafaidi aidha wanaokaa Morogoro na wale ambao wanajuhudi za kufuatilia tafiti hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SUA* imeanzishwa kutusaidia ninaomba sasa tafiti za mazao zinazofanywa na *SUA* ziwafikie wakulima na ziwasaidie wakulima, mbegu wanazozifanyia tafiti zifike kwa wakulima wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida sana na walimu, nyumba za walimu, upungufu wa walimu wa sayansi, hili limezungumzwa na litaendelea kuzungumzwa na Wabunge, Serikali ione namna sasa, elimu bure wanafunzi wengi wanasma, lakini madarasa ni yale yale, madawati ni yale, walimu wameongezeka kidogo, lakini wa sayansi hatuna hilo Serikali ione namna ya kutusaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumzia pia ubunifu kwamba wanawajenga wanafunzi, wanawajenga watu katika ubunifu, lakini tusipoanza katika elimu ya sekondari hatutapata wabunifu wazuri hata katika mambo ya uchoraji, *engineering* na michezo kama hatutawajenga wanafunzi vizuri hatutawapata.

Pia kuhusu elimu ya TEHAMA, katika shule za sekondari hakuna elimu ya TEHAMA kama ipo ni shule za *private*, lakini shule za Serikali kama wanafundishwa ni nadharia, basi tuone namna wanapotoka sekondari wanaokwenda vyuo vikuu wanatamani kuwa wasomee masomo ya TEHAMA lakini anapoanza kule kwanza lugha yenyewe ya kubabaisha ya kiingereza, lakini la pili hajawahi kuiona hiyo *computer* alipokuwa shule ya msingi wanayoiona *computer* ni wale ambao wanasma shule za *private*. Serikali ijenge uwezo kwa Walimu na kujenga miundombinu katika shule zetu za sekondari za Serikali kwamba TEHAMA wanaianza sekondari na anaanza akiwa na vifaa vya kutosha kusomea, miundombinu ianzie sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, tunaendelea Mheshimiwa Ester Mahawe atafuatiwa na Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Bilago na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwemba ajiandae kama tutakuwa na muda.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nianze kwa

kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu iliyoko mbele yetu, pia naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie alipoishia dada yangu Mheshimiwa Bura kwa suala zima la TEHAMA katika shule zetu hasa za Serikali, siyo tu kwamba mtoto anaiona *computer* akiwa labda *secondary, I mean O-Level* pia hatuna mtaala wa TEHAMA katika kidato cha tano na cha sita, kwa hiyo kuna *connection* inakosekana hapo katikati kutoka kidato cha nne mpaka Chuo Kikuu, ninaiomba Wizara ya Elimu ione namna gani wataandaa mtaala wa TEHAMA wa kidato cha tano na cha sita ili watoto hawa waweze kupata muendelezo mzuri wa masomo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Rais Dkt. John Pombe Magufuli, nimpongeze pia Waziri wa Elimu, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya tunafahamu kwamba changamoto ni kubwa, Tanzania ni kubwa na mahitaji ni makubwa hilo tunalitambua, tuseme tu kwa yale ambayo tayari yamekwishakufanyika kwa kweli binafsi kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu niendelee kuwapongeza, pongezi kubwa sana zimuendee Profesa Ndlichako najua anajitahidi sana na timu yake lakini yale ambayo bado hamjaweza kuyafanya ndio haya ambayo tutayasema na tunaendelea kuwaombea Mungu awasadie ili muweze kuyafanikisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la ufaulu wa wanafunzi kuanzia kwenye *level ya primary* kwenda sekondari. Ni kweli kwamba wanaomaliza shule ni wengi, lakini wanaofaulu kwa ufaulu unaotakiwa ni wachache, elimu ni uwekezaji tuwekeze sana kwenye elimu ili kwamba nchi yetu iweze kupona. Elimu ni uhai, elimu ni maisha nilikuwa nafikiri kwamba hata bajeti ya mwaka huu itakapoletwa kusomwa hapa badala ya kuwa na *priority* lukuki hebu tuanze na *priority* namba moja mwaka huu iwe elimu halafu tuone kama hatutaoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila elimu bora nchi hii haiwezei kukombolewa, naomba niseme machache kuitia Wizara hii hasa Mkoa wa Manyara, wanafunzi wa shule wanaosoma katika shule za Wilaya ya Simanjiro na Wilaya ya Kiteto wanasoma umbali mrefu sana hizo ni Wilaya ambazo ni za kifugaji, watoto wanatembea mwendo mrefu kwa mfano pale Orkesment ile shule ndiyo inayotegemewa na Kata nyingi Kata za Kitwahi na vijiji vyake mtoto anatembea kilometra 20 mpaka 30 kwa siku, mtoto huyu akifika shulenii ni lazima atakuwa amechoka na hawezi kumsikiliza mwalimu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba ile shule ina hosteli waongezewe miundombinu ya hosteli ili wale watoto wa kifugaji waweze kupata mahali pa kuweza kutulia na kusoma. Vivyo hivyo katika Kata za Ndodo na Kata zingine za Wilaya ya Kiteto. Wilaya hizi zimekuwa za mwisho muda mrefu katika Mkoa wa Manyara kwa sababu ya miundombinu yake ya umbali wa kutoka watu wanakoishi na shule ziliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie ufaulu wa Kidato cha Nne kwa miaka mitatu minne mfululizo, wanafunzi ambao wamekuwa wakifaalu kwa *division one* mpaka *three* ni wachache mno. Kwa miaka mitatu 2015 - 2016 - 2017 ni wanafunzi 95,000 tu kati ya wanafunzi zaidi ya laki moja wanaomaliza kidato hicho, ifike mahali tukae kama nchi tujadili mustakabali wa elimu nchi hii, vinginevyo kila siku tutakuja na huu wimbo na bahati mbaya sana ni hii tunatumia Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, Sera ni ya mwaka 2014 hivi vitu havi-*match* ndiyo maana mambo mengi yanashindwa kwenda. Sheria iletwe, ibadilishwe, iendane na wakati tulionao sasa vinginevyo huu wimbo bora elimu na siyo elimu bora hautokaa uishe kwenye nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Profesa Ndalichako atakapokuja hapa aseme ni namna gani sasa tutaondoa hizi *zero* nyingi na *four* nyingi kwenye matokeo haya ya kidato cha nne niliwahi kuzungumza hapa kwamba hivi tunachokifanya ni kuhakikisha mwanafunzi amemaliza

shule ama ameelimika? Kwa hiyo, niwaombe sana watu wa Wizara ya Elimu mtakapokuja hapa hebu mje na mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwa vile sasa hatuna ajira za kutosha niliwahi kushauri hata kwenye Kamati nilikokuwepo mwanzo ya TAMISEMI kwamba na niliwahi kuomba Wizara ya elimu pia tuweke mtaala wa ujasiriamali (*entrepreneurship*) kwenye elimu kwa sababu ni kweli hatuna ajira za kutosha ili wanafunzi wetu watoke wakiwa na *skills*, wale watakaokuwa wameshindwa kuendelea na masomo waweze kujajiri ili kupunguza changamoto ya ajira. Siyo hivyo tu, ninajua kwamba Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikipambana sana na suala zima la rushwa, Biblia inasema: "Mfundishe mtoto katika njia impasayo naye hataiacha hata atakapokuwa mzee." (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba mara nyingi ikiwezekena hata suala la rushwa na ubaya wake liwekwe kwenye mtaala ili watoto wafundishwe kuanzia *kindergarten* ubaya wa rushwa watakapokuja kuwa watu wazima kama sisi wanafahamu madhara ya rushwa, sasa hivi tunaongea na samaki mkavu ambaye ameshakuwa mkubwa unam kunja anavunjika, kwa hiyo, haisaidii, vile vitu ambavyo vinahitaji *moral discipline* viwekwe kwenye mitaala yetu ili kuweza kusaidia kuwajenga Watanzania ambao watakuwa wazalendo na nchi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Chuo cha Ualimu Mamira kilichopo Mkoani Manyara. Chuo kile ni chuo cha *Grade A*, wameomba kuanzisha diploma pale kwa maana ya waweze kuwekeza kwenye Walimu wa wa sayansi tu, ombi lao nina hakika lipo kwenye meza ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, wameomba walimu kama watano wa sayansi ili waweze kuwafundishwa walimu wa diploma wa sayansi ili kuweza uondokana na upungufu wa walimu wa sayansi tulionao, ninaomba ombi hilo kama inawezekana lishughulikiwe haraka ili mwaka huu waweze kusajili walimu wa *level* ya diploma na tuweze kuendelea kupunguza huo upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wa sayansi ni kilio nchi nzima; naomba kushauri kwamba badala ya ku-split hizi *effort* ndogo ambazo zinafanywa na Serikali, kwa vile shule ziko nyingi hususani shule za kata za Serikali kama inawezekana shule chache ziwe *identified* kama ni ni kila Wilaya tuwe na shule mbili sinazo-deal na sayansi, maabara zake ziboreshwé na walimu wa sayansi wapelekwe kwenye shule hizo badala ya kuhakikisha kila shule inafundisha sayansi wakati walimu wa sayansi hatuna. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu wa zaidi ya walimu 26,000 wa sayansi, walimu hawa wanastaifu, wanabadilisha taaluma, wengine wanafariki, kwa hiyo itatuchukua zaidi ya miaka 15 mpaka kuhakikisha tunapata walimu, juhudzi za makusudi zinahitajika kuhakikisha kwamba kupanga ni kuchagua, kwa hiyo, tuchague kwamba shule kadhaa zifundishe sayansi na shule zingine ziendelee na masomo mengine ili kuweza ku-utilize walimu tulionao badala ya kuzalisha zero za sayansi kila mwaka, ifike mahali sasa tufikiri nje ya boksi. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee kwa haraka shule ya watoto walemaru ya Katesh A iliyopo Wilayani Hanang', shule ile ina watoto walemaru wapatao zaidi ya 150 na ni shule ya mchanganyiko kuna watoto wasio walemaru pia. Shule ile ni kama imesahaulika sana, pale kuna watoto wenye *albinism* wanapata shida, hawapati yale mafuta kwa ajili ya ngozi zao, miundombinu ya ile shule ni kama imesahaulika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia namna gani wale wanafunzi wa ulemavu tofauti kwenye shule ya Katesh A pale Hanang' waweze kupatiwa msaada ili na wao waweze ku-enjoy masomo yao kama watoto wengine wasio na ulemavu. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme suala la ukaguzi. Ni kweli kwenye kudhibiti ubora tunaona wapo Wadhibiti Ubora wengi lakini zaidi wamekuwa wakidhibiti

ubora kwenye *private schools* wanasahau kudhibiti ubora kwenye shule za Serikali. Ukiona shule hizo wanazosema ni za *private* zinafanya vizuri ni kwa sababu wao wamejikita zaidi kwenye kudhibiti upande wa pili badala ya shule ya Serikali ambazo pia ndiyo nyingi. *Automatically* mtu mwenye shule binafsi yeche mwenyewe ni mdhibiti namba moja, maana hakuna anayetaka ku-*invest* kwa hasara.

Kwa hiyo, wao wange-*focus* zaidi hata kwenye shule za Serikali maana watoto wetu wengi wako kule na mengi hayafanyiki kule. Ninawaomba sana watu wa ukaguzi wapatiwe vifaa kama walivyosema wenzangu kama ni bodaboda hizo ama pikipiki kwa ajili ya ukaguzi ili waweze kuzifikia hizo shule, shule ni nyingi na miundombinu ni...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mwalimu Kasuku Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la *Teachers Professional Board* (Bodi ya Kitaaluma ya Walimu). Bodi hii iliwhi kuandaliwa Muswada na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwenye utawala wa Awamu ya Nne na kuiwasilisha Serikalini ili iweze kufanyiwa mchakato wa kuunda chombo hiki. Mpaka sasa chombo hiki hakijaundwa pamoja na malengo yake mazuri kabisa, kusimamia taaluma ya walimu nchi hii pamoja na nidhamu ya walimu wa nchi hii. Kwa mfano, lengo lilivyokuwa zuri la *Teacher's Professional Board* ikitokea mwalimu wa nchi hii amefanya makosa akafukuzwa kazi anaendelea kwenda kufundisha shule za *private and nobody will ask him or her!* Lakini lengo la hii *Teacher's Professional Board* ilikuwa inaandaa leseni pamoja na vyeti vyaya ualimu unapewa leseni ya kufundishia. Uki-mess up wanakunyang'anya leseni, hautafundisha shule yoyote katika nchi hii. Kwa hiyo, nimuombe Waziri hiki chombo kiundwe kama zilivyo Bodi za Taaluma zingine kiweze kulisiaidia Taifa hilika katika upande wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la ufaulu wa wanafunzi katika Taifa hili. Kidato cha nne, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamati nilitarajia Wabunge wote wawe wamesononeka sana juu ya hali hii na ingekuwa inaruhusiwa kusimama Bungeni kama kwenye msiba kwamba tusimame kidogo kumuombea marehemu nalo tungesimama kwa suala hili kuiombea elimu nchini, lakini watu waliposoma ni *data* tu, wanaziona *data* tu, sawa tu walifaulu hawa sawa tu! Hapana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo hapa, shule binafsi mwaka 2016 shule 10 bora zilikuwemo asilimia 10 za Serikali. Katika shule 50 kulikuwa na asilimia sita za Serikali; shule 100 asilimia 11. Mwaka jana katika shule bora 10 zilikuwemo za Serikali asilimia sifuri. Katika shule 50 asilimia moja katika shule 50 ni za Serikali, shule 100 zilikuwemo asilimia sita. Maana yake elimu ya Taifa hili imebewwa na shule binafsi. Shule za Serikali hakuna chochote. Tungeondoa *private* hapa tungekuwa na wanafunzi sita mwaka jana bora ndani ya wanafunzi mia moja! Halafu tunashindwa kuisaidia Serikali na kuvisimamia iboreshe elimu. Hili halikubaliki! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungewauliza watu wa shule binafsi wanafanyaje? Hii kitu Waziri mngeenda tu mkanong'ona nao, ninyi mnafanyaje mnapata *performance* nzuri kama hii, sisi huku tumekwama, hebu mtusaidie. Siri yao wamesema hivi, kuna motisha ya kutosha kwa walimu, Serikalini hakuna motisha. Shule za Serikali walimu hawana motisha yoyote, hata madai yao wanayodai hawalipwi kwa wakati, madaraja hayapandi hata wanaopandishwa hawarekebishiwi, wanaorekebishiwa hawalipwi *arrears*, mnatarajia nini? Shule binafsi wanao walimu wa kutosha, sisi kila siku hatuna walimu na tume pigia kelele ndani ya ukumbi huu, walimu hawatoshi shulenii, tunaliona jambo la kawaida! Hivi hiki kitu tunakwenda wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetua walimu wa sekondari tumepeleka *primary*, tumeenda kuongeza *frustrations* kwa walimu. Haki Elimu walituambia asilimia 37 ndiyo wamebaki na *morale* ya kufundisha, hawa 60 na

kidogo hawana *morale* kabisa! Ualimu siyo kitu cha kusema lazima utafundisha tu, haiwezekani! *Morale* kwanza, itoke moyoni na kutoka moyoni lazima huo moyo uwe umetengenezwa ukubali kufundisha kwa bidii na nguvu zako zote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, shule binafsi wana kitu wanaita mfumo imara shirikishi wa udhibiti elimu, mfumo wao imara una mkakati wa kukaririsha wanafunzi wanaofanya vibaya ili wasiendelee na makapi.

Sasa nataka Waziri utakapokuja hapa utuambie ni kwa nini unazuia shule *private* zisikaririsha? Kwa sababu mimi ni mzazi nimeamua kumpeleka mtoto wangu *private*, hata angekaririshwa mara mia naendelea kulipa karo, Serikali inawahusu nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niacheni na mtoto wangu nikomae naye mpaka nitakapojiridhisha kwamba viwango vyake vya elimu vimeduwa vizuri na hili mwisho wake ndilo linalosababisha, tumejuliza kwa nini Serikali ina ugomvi na *private*, ni vivu tu! Wana *performance* nzuri, kwa hiyo, ni kama inaidhalilisha Serikali. Kwa hiyo, lazima vivu uwepo ili na wao ufaulu ushuke wote mfanane, muende mnafanana fanana. Matoko yake sasa ufaulu ukiharibika kwenye shule za *private* tunaanza kupeleka watoto Uganda na Kenya wakati hii biashara ilikuwa imekwisha. Ziko shule hapa zinafanya kama Uganda kama Kenya na zaidi ya hapo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu vivu uishe, Serikali iachane na vivu, shule za *private* ziachwe *zi-perform*, wakaririshe, mwanafunzi atoke ni *the best student*. Sisi tunataka wote waende. Subirini muziki utakaokuja wa hii elimu bure! Matoko ya elimu bure yatakuwa zaidi ya haya tutashangaana wote. Tumeweka elimu bure miundombinu imebaki ile ile, hatujajiandaa vizuri, maana *batchya* kwanza nadhani mwaka kesho au kama mwaka huu ya kidato cha nne yenye elimu bure, tutashangaana hapa. Kwa hiyo, tusijifiche kwenye kichaka cha elimu bure tukidhani iko

bomba. Tuangalie elimu bure inafanana na miundombinu tuliyonayo? Inafanana na tunachoweza kubeba kwenye elimu bure? Inaweza kutusaidia zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la walimu wa sayansi, nimepata taarifa walimu waliosoma masomo ya *art* wamepelekwa Chuo cha Kleruu kwenda kujifunza *methodology* ya kufundisha shule za ufundi!

### **MBUNGE FULANI:** Eti?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie hii, walimu waliosoma masomo ya *arts* baada ya kuona wamezidi kule sekondari wamewachukua wakaenda kusoma *methodology* ya kufundisha *practical* shule za ufundi. Wamekwenda lyunga Sekondari, wame-improve failure kwenye *BTP* wameshindwa! Sasa niambeni hivi mimi nimesoma *history, geographhy* labda *HGL, HGK*, mimi na *methododgy*ya sayansi wapi na wapi? Nikajifunze namna ya kufundisha kutengeneza gari, namna ya ku-operate viwanda, eeh, hii kiboko! (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri nyininge masomo ya lugha, kiswahili na kiingereza Tanzania yanaanza kufundishwa darasa la tatu. Hawa shule za *private* wanaanza chekechea kule na wakitoka chekechea hawa walioanza la tatu wanakwenda kukutana kwenye mtihani wa darasa la nne, wale walioanza... (*Makofii/Kicheko*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako Mwalimu muda wetu ndiyo huo. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu amesema nakuja kupongeza ni kweli napongeza na ninaanza kupongeza kwa kusema kwamba naishukuru Serikali yangu kwa namna ya pekee ambavyo imeweza kuanzisha mpango wa elimu bure ambayo imeweza kusaidia watoto wengi kuingia shulen. Kwa mfano,....

**MBUNGE FULANI:** (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

**MHE. DKT. PUDENCIA W. KIKWEMBE:** Tafadhalii naomba usinisemeshe nina majibu, nitakujibu jibu moja uende ukalale. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema naipongeza Serikali kwa sababu hata wazazi wamejitokeza na wameweza kuchangia na kuongeza madarasa, naongelea katika Jimbo langu la Kavuu ambalo Mheshimiwa Ndalichako nilikwishakuja nikakuambia tayari nina maboma 69 katika kuongezea katika idadi ya wanafunzi walioingia, kwa hiyo naomba unisaidie tu shilingi milioni 48 kwa ajili ya kuezeka maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuishukuru Serikali yangu, tayari katika Jimbo langu la Kavuu nimeweza kutatua tatizo la madawati, nilikuwa na upungufu wa madawati 1,000 na nimeyatatua na sasa hivi nayagawa shulen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja katika Vyuo vya Maendelo ya Wananchi. Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi vinatuchanganya na kozi ambazo zimekuwa zikitolewa na VETA, niombe sana hili liangaliwe na wakati mwingine tunashindwa kuelewa ama viko chini ya Wizara ya Afya kwenye Maendeleo ya Wananchi ama viko Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, chuo kilichopo Mkoa wa Katavi cha Maendeleo ya Wananchi, Chuo cha Msanginya bado hakijaanza kufanya lolote na miundombinu yake siyo. Naomba ukiangalie kwa hali ya kipekee ili tuweze

kupeleka watoto wetu pale hasa wa kike ambao hawafiki *form four* waweze kujifunza maarifa mbalimbali ambayo yanaweza kuwasaidia kutatua matatizo yao katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba niongelee kuhusu malipo na madai mbalimbali ya walimu. Kimekuwa ni kilio cha muda mrefu. Mimi ni mwalimu, nimeanza kufundisha Chuo cha Ualimu Sumbawanga kama *first appointment* yangu pale, ninafahamu matatizo ya walimu. Nimefundisha *Mpanda Girls* ambapo niliomba ni shule iliyo kuwa na *form one* mpaka *form four* na ilijengwa kwa msaada wa *DANIDA*. Kwa hiyo ninaomba kwa sababu sasa hivi mmeiweka kama *form five* na *form six* naomba ianze *form one boarding* mpaka *form six* ili na sisi Mkoa wa Katavi watoto wetu wapate nafasi ya kuweza kusoma katika ile shule ambayo ni moja ya shule kongwe ambazo zillijengwa kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike pale *Mpanda Girls*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee sua la TEHAMA, suala hili naomba uliangalie vizuri. Katika shule zangu za msingi, nimefanya ziara katika shule zangu za msingi Jimbo zima, TEHAMA shulen iwanasoma kwa nadharia. Kwa hiyo ninaomba *computer*, Serikali ifanye utaratibu wa kupeleka madarasa ya *computer* pamoja na *computer* kwa ajili ya walimu wa shule za msingi na wanafunzi wa shule ya msingi angalau kila shule moja iwe na darasa moja na upendeleo uanze na Jimbo la Kavuu ili tuweze kufanya maendeleo kwa sababu ni Jimbo ambalo liko vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee hili suala la kuhamisha walimu kuwatoa sekondari kuwapeleka shule za msingi. Kwa kweli halijapokelewa vizuri, kwa mwalimu linaonekana kama ni adhabu, basi naomba wapelekwe *special course* kwa ajili ya kufundisha shule za msingi kwa sababu wao walifundishwa *methodology* shulen iwanasoma kwa ajili ya kufundisha shule za sekondari.

Kwa hiyo, tunaomba sasa kama mnawapeleka kule,

muwapeleke na *special course* kwa ajili ya kujielekeza katika masomo ya shule za msingi bila kuathiri madaraja yao pamoja na vyeo vyao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee suala la asilimia mbili ambayo walimu wamekuwa wakikatwa kwenye mshahara. Tunaelewa kuna kipindi Bunge liliopita tuliongea hapa tukasema kuwe na mikataba, wanaopenda wasaini wakatwe na wasiopenda wasikatwe. Tunajua ni jambo la kisheria lakini sheria inaweza ikaletwa hapa na pia ikafanyiwa kazi ili tuone walimu tunawasaaidiaje. Tunawakata asilimia mbili katika mshahara wao kila mwezi na Chama cha Walimu, Chama cha Walimu kina ghorofa pale ni mtaji lakini walimu bado wanashindwa kukopeshwa kwa ajili ya maendeleo ya maisha yao. Wanashindwa kukopa katika mshahara ambao wanakatwa waweze kujenga maisha yao yawe vizuri hasa kwenye nyumba zao wanazotakiwa kuishi. Kwa hiyo, niombe sana hili mlififikirie na mliangaie. Walimu wengi wamekuwa wakilalamika kuhusu hii asilimia mbili ambayo na mimi nilikwishakatwa na ninaidai kwa sababu siko huko tena, kwa hiyo napenda irudishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee usawa wa elimu. Tunajua elimu ni haki ya kila mwanafunzi. Naongelea shule za *private* na shule za Serikali. Kwa kuwa matokeo ya ufaulu yanaonesha bado ni tatizo na shule nyingi za Serikali ziko vijijini, mwanafunzi wa kijijini anatembea umbali mrefu. Kuna sababu nyingi zinazoweza kusababisha mwanafunzi wa Serikali asifanye vizuri hasa aliyeo kijijini. Ninaomba muangalie namna mtakavyokuwa mnaandaa mitihani sasa kwa ajili ya watoto hawa wanaoenda na magari, wanaokula shulen na wale wanaotembea kwa miguu ili usaili wao uwe tofauti, usiwe unaofanana kwa sababu wako katika mazingira tofauti ili tuweze kuona tatizo liko wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee shule yangu Maalum ya Majimoto. Nina shule pale ya Majimoto Mheshimiwa Profesa Ndlichako. Ninaomba kama utaweza kutuma wasaidizi wako wakafika katika ile shule, Halmashauri

yangu imejitahidi imejenga miundombinu mizuri, tuna mabweni lakini bado tuna mambo machache ambayo tunahitaji Serikali Kuu itusaidie na tunaomba shule hiyo sasa irudi Serikali Kuu itoke Halmashauri ili iweze kuwasaidia watoto wote wenye mahitaji maalum. Ni shule nzuri tumejitahidi kuitengeneza pale, naomba Profesa kwa jicho la pekee utume watalaan yako ije iangalie ile shule tuweze kuona tunaweza kuifanyaje ili iweze kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum hasa wale wenye ulemavu na wengineo ni shule ambayo tayari tuna mabweni matatu tumekwishajenga, tuna madarasa manne na tuna vyoo ambavyo tumetengeneza miundombinu kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, nakuomba sana shule yangu hii kama kawaida yangu nitakuletea *special request* na mahitaji yake ili muweze kuona mnatusaidiaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru Serikali yangu na naipongeza kwa namna pekee ambavyo imekuwa ikifanya kazi chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Napenda niwashukuru Wizara ya Elimu, Mawaziri wote wa Serikali hii kwa sababu wamekuwa ni wasikivu. Ndugu yangu Joyce Ndalichako ni msikivu sana, ni mwalimu wangu wa *statistics* wakati nikiwa chuo kwa sababu mimi nilisoma elimu ya MEMKWA mpaka nimepata Udaktari na hivi naenda kupata Uprofesa. Solazima nijipongeze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba sana Mheshimiwa suala la elimu tuliwekee mkazo ili na sisi kule watoto wetu kule vijiini wawe maprofesa, wawe wahandisi, tunajua tunaenda kwenye mfumo wa viwanda lazima turekebishe mfumo wetu wa elimu. Lazima tuone kwenye sayansi na teknolojia kuanzia kwenye vyuo vya ufundi, kwenye *VETA* ambao wakati mwingine tunaweza tukawa tunawadharau lakini hawa ndio watu wazuri ambao wanaweza wakatufanya miradi yetu mizuri sana katika uchumi unaokuja na viwanda ambavyo tunatarajia kufunguliwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana Mheshimiwa Joyce Ndalichako, suala la elimu sawa naomba

muangalie na mitaala pamoja na mitihani mtakayoweza kuwa mnaitunga kwa *differences* ya mazingira kati ya wanafunzi hasa wa vijiji ni wale wanaokwenda na mabasi ya Martin Luther, Ignatius na kadhalika.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kabisa kwa namna ya pekee uweze kuliweka hili suala ili uweze kuona ni namna gani ambavyo tunaweza kuwasaidia watoto wetu hasa ambao wanaweza...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa niipokee ama?

**MBUNGE FULANI:** Kwani ameshatoa?

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Naomba niendelee kwa sababu ananipotezea muda.

Kwa hiyo, naomba kabisa suala hili Serikali mlitilie mkazo. Ni mawazo yangu binafsi ambayo baada ya kutembelea hali halisi na kuiona shulenii ni mawazo yangu binafsi ninayowasilisha Bungeni kama Mbunge kuishauri Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, sikutaka kuchukua taarifa kwa sababu ya muda. Kwa jioni nitaanza na hawa watatu lakini kabla ya kuwataja nina tangazo.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa William Ngeleja ana tangazo hapa la michezo ningependa nilitangaze. Matokeo ya michezo iliyochewa siku ya Jumamosi tarehe 28 Aprili kwenye viwanja wa Jamhuri Mjini Dodoma. Matokeo hayo ni kama ifuatavyo. Kwa upande wa soka, *Bunge Sports Club (Ndugai Boys)* ilipata magoli manne dhidi ya wachezaji wenzao *NMB* ambao walipata goli moja. Hivyo *Ndugai Boys* ndio walitunukiwa nishani na kikombe cha ushindi. Hongereni sana.

Sasa wafungaji wa magoli kwa upande wa *Ndugai Boys* walikuwa Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Omary Mgumba. Kwa upande wa *netball*, *Bunge Queensna Dodoma Veterans* wote walienda sare magoli 11 kwa 11.

Kwa upande wa *basketball* kwa wanaume, *NMB* walifanikiwa kuishinda *Bunge Sports Club* na kutwaa nishani na kikombe cha ushindi. Mgeni Rasmi wa michezo hiyo alikuwa Kapteni wa Jeshi Mstaafu Mheshimiwa *Comrade George Huruma Mkuchika*, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, michezo hiyo ilitanguliwa na mbio za mwendo wa pole yaani *jogging* ambazo zilianza saa 12 asubuhi na zillihudhuriwa na mamia ya Wabunge na wananchi kwa Dodoma kwa ujumla na zilliongozwa na Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

Pamoja na Mgeni Rasmi, Wabunge wafuatao walitia fora katika mbio hizo; Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Seneta Richard Ndassa, Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Daimu Mpakate, Meneja wa timu yetu Chifu John Kadutu na Mheshimiwa Amina Mollel. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, *Bunge Sports Club* inamshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kushiriki nao kwenye mchapalo ulioandaliwa na Benki ya *NMB* baada ya michezo hiyo. Pia wanasema shukrani pekee ziwaendee wadhamini wa michezo hiyo Benki ya *NMB*.

Aidha, wanaungana na Mheshimiwa Spika na Watanzania kwa ujumla kuipongeza *Simba Sports Club* kwa kuwacharaza Yanga. Waheshimiwa Wabunge, ningelijua hili tangazo lina maneno hayo ya mwisho nisingelisoma lakini ndiyo nimesoma. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale Waheshimiwa tutakaoanza nao mchana, ninao hawa watatu wa kwanza dakika kumi kila mmoja kwa hiyo nusu saa itakuwa imeondoka hapo; Mheshimiwa Rashid Chuachua, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Chagula na Mheshimiwa Mwalimu Margaret Sitta.

Hao ndio tutaanza nao, nitajua baada ya hapo mzunguko wa pili nitaanza kubeba wa dakika tano upande wa CUF na upande wa CHADEMA halafu na dakika kumi, tunaenda vizuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Niliwataja Waheshimiwa Wabunge watatu wa kwanza jioni hii, nirudie tena. Mheshimiwa Rashid Chuachua, Josephine Chagula na Mwalimu Magreth Sitta. Tunaanza na Mheshimiwa Rashid Chuachua.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye eneo letu hili la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa juhudu kubwa inazofanya kwenye sekta hii, pia kwa namna ya kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Ndalichako kwa kazi kubwa anayoifanya katika elimu pamoja na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nilipokuwa ninasimama kwa ajili ya kutoa mchango kwenye wizara hii muhimu

nimekuwa nikizungumza kuhusu *non formal* na *adult education*, yaani elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi. Nina hamu sana ya kuiona Wizara ya Elimu, kisera ikiwa inatambua kwamba ina jukumu la kuwaelimisha Watanzania wote bila ya kuzingatia wale tu ambao wako madarasani kwa sababu Watanzania wote wanategemea wizara hii ili kupata elimu kwa namna moja ama nyagine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza hili ninaiona kabisa Serikali yetu ilishaamua kuiunda taasisi maalum ambayo itafanya kazi ya kusimamia elimu nje ya mfumo rasmi pamoja na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hapa ninaitaja Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na ninaitaja hii kwa makusudi kwa sababu mionganini mwa majukumu yake ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanajua kusoma na kuandika hata kama wako nje ya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha kutojua kusoma na kuandika kinaongezeka sana kwa wananchi wa Tanzania. Katika kipindi kilichopita katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alilisimamia sana hili la kuhakikisha kwamba ni lazima kumuelimisha kwanza mtu mzima halafu mtoto baadaye kwa sababu mtu mzima tunamtumia sasa hivi wakati mtoto tuna muda wa kusubiri kumtumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, ukiangalia Ripoti ya *Adult Literacy Survey* ya mwaka 2014 inaonesha kwamba kutoka mwaka 1986 Watanzania asilimia 9.6 walikuwa hawajui kusoma, lakini sasa katika mwaka 2012 wameongezeka mpaka asilimia 31, sasa leo ni mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inao mkakati ambao inapanga kuutekeleza, mkakati huu unaitwa *National Literacy and Mass Education Strategy*. Huu ni mkakati madhubuti waliouandaa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma pamoja na kutoa elimu na

hamasa maalum kwa wale watu ambao hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuishauri na kuimba sana Serikali kwanza iangalie Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, lakini pia ihakikishe inatoa mchango mkubwa katika kuhakikisha utekelezaji wa mkakati huu unakwenda mbele ili Watanzania waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ambalo ni lugha, nimekuwa nikisema kila siku. Kama kuna jambo ambalo linatatatiza mfumo wetu wa elimu ni lugha tunazozitumia. Hili lazima niliseme wazi. Ukiwasikiliza baadhi ya wataalamu wanaozungumza kuhusu elimu wanazungumza kuhusu tatizo kubwa la ufaulu katika sekta yetu ya elimu, lakini wanapozungumza jambo hilo hawazungumzi kama tuna mkanganyiko mkubwa sana katika matumizi ya lugha, hawasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza ripoti za TWaweza, ukiwasikiliza Haki Elimu pamoja na mashirika mengine wanaofatilia michakato ya kujifunza katika mfumo wetu wa elimu hawasemi wazi kama tuna tatizo kubwa la matumizi ya lugha. Hakuna nchi yoyote duniani iliyօendelea na kupata mafanikio makubwa katika sekta ya elimu kwa kutumia lugha za watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi nalisema wazi. Ninaweza nisieleweke kwa sababu hata pengine wasimamizi wa mfumo huu tumepeita katika mfumo ambao bado kwetu ni kikwazo. Kwa hiyo, ukiambiwa leo tujifunze kemia au fizikia kwa kutumia kiswahili utaona shida lakini kujifunza kemia au fizikia kwa kutumia kireno, kifaransa, kichina, kijerumani tunaona inawezekana. Kwangu mimi hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hakuna lugha iliyօ bora kuliko lugha nyingine, na hii ni kwa mujibu wa Profesa Noam Chomsky ambaye ni mtaalamu wa isimu ya lugha, anasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ndiyo inayotufundisha namna ya kutazama na kuutafsiri ulimwengu wetu. Hakika tuna mkanganyiko mkubwa. Leo hii katika zile shule ambazo wanatumia lugha ya kiingereza kujifunza kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la tatu hautakiwi kugusa kiswahili. Katika shule wanazotumia kiswahili kama lugha ya kufanya mawasiliano ya kujifunza hawatakiwi kugusa kiingereza mpaka wanafika darasa la tatu. Lakini wakifika darasa la nne wanafanya mtihani mmoja hawa wanafanya kwa kiingereza, hawa wanafanya kwa kiswahili, lengo letu ni nini? Lengo letu ni kuwashindanisha wanafunzi kwenye umahiri wa lugha au kuwashindanisha wanafunzi kwenye umahiri wa maudhui ya masomo yetu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana katika jambo hili na ni lazima Serikali ifike wakati wa kufanya maamuzi magumu. Mimi nataka nikwambie kama Serikali inaamua leo, kwa mfano wanafunzi wajifunze kwa kutumia lugha yetu inawezekana kabisa wakajitokeza watu wakasema tunataka tusingaidie mfumo wa elimu ya Tanzania kwa sababu tunaondokana na kujifunza kwa lugha ya wakoloni, hili ni jambo gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba ni vyema sasa hivi tukafikiria namna bora ya kujifunza, kwa sababu watoto wetu wana kikwazo kikubwa sana katika kujifunza wanajifunza kwanza kukielewa kiingereza halafu wanajifunza kuelewa maudhui ya somo. Lakini hivi ni kitu gani kinawenza ...

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa kwa kifupi sana.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Wabunge wote, Mawaziri wote na viongozi wote wa nchi hii watoto

wao wote wanasoma shule za kiingereza, hakuna anayesoma shule za kiswahili.

**MWENYEKITI:** Una uhakika?

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowea kukataa ni kwamba ni Wabunge wote na Mawaziri wote, lakini wapo ambao watoto wao wanasoma katika mfumo huo wa kukwepa kiswahili na kwenda kwenye kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ni sememe jambo moja, kwamba umefika wakati wa Watanzania kufanya maamuzi. Tunawaweza watoto wetu katika mfumo wa lugha ya kiswahili mpaka wanafika darasa la saba, tukitoka darasa la saba tunakwenda *form one* mpaka *form four* tunabadilisha ghafla wanasoma kwa kiingereza, halafu baadaye wanakwenda tena chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nchi gani duniani inafanya mambo haya? Tumebakwa ni nchi za kiafrika ambazo tunalazimika kutumia aidha kifaransa au kiingereza kwa sababu ni lugha ambazo tulialihiwa. Tufanye maamuzi, nchi nyingi ambazo zimeendelea wanatumia lugha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuwe na chombo maalum kitakachoangalia na kusimamia mfumo wetu wa ubora wa elimu, hili ni tatizo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli kabisa ni kwamba zipo shule binafsi ambazo zinaanzishwa na zinasimamiwa vilivyo na Serikali ili kukidhi mahitaji, lakini pia tunazo shule za Serikali ambazo nazo pengine zingeweza kusimamiwa na chombo kinachojitegemea ili kuziongezea ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima tufike wakati wa kuona tuwe na chombo maalum ambacho kinaangalia pia shule zetu za Serikali, kwa sababu shule za *private* kukiwa kuna walimu watatu kuna uwezekano wa kusema tunafunga shule, lakini katika shule za Serikali ili *ku-maintain* ubora wa elimu mimi naishauri Serikali ione umuhimu wa kuwa na *independent board* ambayo inaweza pia kuzisimamia shule hizo. Lengo ni kuondoa pia matabaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matabaka makubwa wapo watoto ambao wanaonekana wanasoma shule bora sana wanatumia lugha bora sana lakini wapo watoto ambao wanaonekana wanasoma shule za chini sana. Ili kuondoa haya matabaka pia kingekuwepo chombo kinachowenza kuiangalia Serikali na kuisimamia ili tuweze kwenda vizuri na shule zetu pia nazo ziwe shule bora kama ilivyo katika shule zingine za *private*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya nashukuru sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Josephine Chagula na Mheshimiwa Margret Sitta ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa leo, pia kwa kutulinda sisi sote Wabunge na kuwa hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana anazofanya. Ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumuongoza, amlinde, amtunze na ampe maisha marefu. Nimpongeze Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Baraza lote la Mawaziri kwa kazi nzuri sana wanazozifanya. Nimpongeze sana Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Ndlichako kwa hotuba nzuri.

Pia nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara kwa kazi nzuri sana wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba nichangie sasa kuhusu elimu katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati shule kongwe hapa nchini. Kazi iliyofanyika na inayoendelea kufanyika katika kukarabati shule kongwe hapa nchini ni nzuri mno na inafaa kupongezwa na kila Mtanzania anayependa maendeleo. Hongera sana Serikali, hongera sana TAMISEMI na hongera sana Wizara ya Elimu kwa kuweza kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee upungufu wa walimu katika Mkoa wangu wa Geita. Katika Mkoa wa Geita shule nyingi za msingi hazina walimu wa kutosha hivyo kupelekea walimu wachache sana na sera yetu ya elimu inasema mwalimu anatakiwa afundishe wanafunzi 45, lakini kwa mapungufu yaliyopo katika Mkoa wa Geita mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 100 mpaka 150. Kwa hiyo, kwa kweli ni changamoto, niombe sana Serikali iweze kutupatia walimu wa kutosha kulingana na mahitaji yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika shule zetu za sekondari za kata kuna mapungufu makubwa sana ya walimu na hasa walimu wa sayansi. Hatuwezi kufikia uchumi wa kati bila kuwa na walimu wa kutosha wa sayansi. Hivyo niombe sana Serikali iweze kuliona hilo watupatие walimu wa kutosha katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa nyumba za walimu na mabweni, changamoto hii ni kubwa sana. Mwalimu anapokuwa mbali na kituo chake cha kazi hukupelekea kuchelewa kufika kazini, matokeo yake shule huwa chini ya kiwango. Niombe sana Serikali, mimi nishauri kwa nini tusitumie Shirika letu la Nyumba kuweza kujenga

nyumba za walimu pamoja na mabweni ili kuondoa kabisa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine la walimu kutopanda madaraja. Kuna walimu *morale* ya kufundisha inashuka kutokana na kutopanda madaraja kwa wakati. Mwalimu anapokaa kwenye daraja moja mwaka mmoja mpaka miaka mitano bila kubadilishwa kwa kweli inakatisha tamaa, matokeo yake walimu wanashindwa kufundisha vizuri. Mimi niombe Serikali iweze kuona inafanyaje ili walimu hawa waweze kupandishwa madaraja kwa wakati unaofaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakushukuru sana, Mheshimiwa Mwalimu Margaret Sitta atafatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi lakini vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama humu Bungeni siku ya leo na wakati huo nawashukuru wapiga kura wa Urambo ambao wanaendelea kunipa ushirikiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuponjeza Rais Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa kwa hii elimu bure. Kwa kweli hata kwenye Wilaya yangu Urambo imesaidia sana kuongeza wanafunzi madarasani, namwombea kwa Mungu aendelee kufanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo nachukua nafasi kumpongeza Profesa Ndalichako, Naibu Waziri wake, Makatibu Wakuu na wasaidizi wake na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayofanya. Jamani Wizara ya Elimu si mchezo mimi nimekaa pale kwa miaka miwili na

nusu ni kazi kubwa, hongera Profesa Ndalichako, kazi ni kubwa na unaiweza, Mungu akusaidie usikilize tu yale tunayopendekeza ya kusaidia kuboresha yale unayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono Waheshimiwa Wabunge wote walioongea hapo awali waliopendekeza kuwe na *Independent Education Regulatory Board*. Kwa jinsi hali ya elimu inavyokwenda lazima tuwe na chombo ambacho kitaangalia na kuchambua Sera ya Elimu ikoje, itaangaia elimu ya msingi maana yake nini, kwa sababu mpaka sasa hivi watu wengi hawajui maana ya elimu ya msingi inatoka wapi inakwenda wapi. Kwa hiyo, *Regulatory Board* itatusaidia kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itazungumzia suala la lugha za kufundishia, tuendeje wakati huu wa karne hii ya 21 wakati huo huo itaangalia mitihani inayotungwa lendelee kama ilivyo au iangalie aina ya shule, mazingira ya shule na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono kwamba kuwe na *Independent Education Regulatory Board*. Kwenye Sheria ya Elimu ilivyo sasa hivi kuna chombo kinaitwa *Education Advisory Board* hakifanyi kazi, kwa hiyo, mimi naomba kabisa Serikali itusikie wengi ambao tumeongea kwamba kuwe nan *Independent Education Regulatory Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani huwa tunaongea sana, tunapiga sana vita ndoa za utotoni, lakini niambie kwenye Jimbo langu kama Urambo, mtoto amemaliza darasa la saba hakuchaguliwa, wazazi wake hawana uwezo kumpeleka *private*, anafanya nini? Mimi huwa najiuliza sana, ili huyu mtoto afikie umri wa kuolewa anafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napendekeza kwa Serikali itilie mkazo sana vyuo vya maendeleo ya wananchi, *FDCs*, lakini pia *VETA*. *VETA* zikitoa mafunzo ya aina mbalimbali ambayo wasichana hata na

wavulana pia watakwenda yatawasaidia kukua kidogo, lakini niambie mahali ambako hakuna *VETA* kama Wilaya ya Urambo, *FDC* haina hela, huyu mtoto wa kike ili nimtunze mimi mpaka afikie umri wa kuolewa anafanya nini pale nyumbani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi natoa wito kwa Serikali itusaidie kuwa na *Vocational Training Centres* nyingi ili angalao ziwafanye wototo wapate ujuzi ambao utawasaidia kwenye hii sera ya viwanda, lakini pia na wenyewe kujajiri, ili angalao kuwafanya wakue kidogo kuliko kuwaacha kama ilivyo.

Kwa hiyo, wakati huu naomba nitoe ombi kwa Mheshimiwa Waziri Urambo haina *VETA*, karibuni nitaleta barua ili watoto wangu wa kike wakuekue kidogo, wajifunze sayansi klimu, wajifunze ushonaji na mambo mengine, mapishi wawe ma-caterers na kadhalika, kwa hiyo, nitaleta ombo maalum Mheshimiwa Waziri kwenye ofisi yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hili jambo ambalo naliongelea sasa hivi ni suala la *TSC*. Nimeshasema jambo hili mpaka wakati mwagine natamani sijui nilie hivi au nifanyeje? Maana ya *TSC* ni nini na *functions* zake ni nini? Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, najua iko TAMISEMI, ilishtukia tu ikahamia TAMISEMI, lakini mimi kwa maoni yangu ungeniuliza ingekuwa kwako Mheshimiwa, kwa sababu wewe ndiye unayetaka Sera ya Elimu ifanye kazi, hawa watu wanavyohudumiwa ni sawa? Wanatekeleza sera yako kama ilivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeomba msaidiane na Mheshimiwa Jafo, Waziri wa TAMISEMI, mupime hiki chombo *TSC* kinafanya kazi iliyokusudiwa au ni li jitu tu limekaa au unaweza kuita *a white elephant?* *TSC* inafanya nini? Imerahisisha vipi kutoa huduma kwa walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaamini kabisa ukimtaka mwalimu afanye kazi vizuri, wanasema wajibu na haki. Je, hii *TSC* inafanya kazi iliyokusudiwa? Ukiangalia

majukumu yake mengi tu kuajiri, kuhamisha, sijui kufanya nini, inafanya kazi hiyo? Ili kurahisisha kweli wanaotekeleza Sera ya Elimu wafanye kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningeomba kuishauri Serikali kuhusu mtoto wa kike. Kuna wakati mimi nilifanya kazi Wizara ya Elimu kwenye miaka ya themanini na kitu palikuwa na kitengo kilichokuwa kinaangalia elimu ya mtoto wa kike. Mimi ningeshauri kwa hali ilivyo ya watoto wa kike na mambo tunayoyaona, napendekeza kwa Serikali kwamba iwe na kitengo kinachoangalia mtoto wa kike na elimu. Kwa sababu ukichukua pale wanapoanza elimu ya msingi wote wako karibu idadi sawa tu, inaweza kuwa 50/50, lakini ukiangalia inaenda kwa msonge mpaka unafika chuo kikuu wote wameshaisha hapa njiani. Sasa kulikuwa na haja ya kuwa na chombo ambacho kitamshughulikia mtoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwaambie Serikali kwamba, haijafikia hatua ambayo tukaridhika, kwamba watoto wa kike na wa kiume wanaenda sawa kwa upande wa elimu. Kwa hiyo, natoa wito kwa Serikali kuwa na kakitengo kadogo ambako zamani kalikuwepo, sijui Serikali iliridhika ikakaondoa. Mimi nilikuwa naomba bado Kitengo cha kumuangalia mtoto wa kike na elimu kirudishwe, ili watoto wa kikenao wafike kama wenzao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni *in-service training*. Naishauri Serikali *in-service training*, yaani mafunzo kazini yanavyotolewa mpaka sasa kwangu mimi naona bado. Nimesoma kitabu nimeona idadi ya walimu waliopata mafunzo ni wachache sana. Naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu bado ibebe jukumu la mafunzo kazini kwa ajili ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanapotoka chuoni wengine wameshafundisha miaka 30 wanahitaji kupigwa msasa ili waende na wakati. Kwa hiyo, mimi naomba kabisa kwamba, *in-service training* bado inahitaji kufanyiwa kazi na kusimamiwa na Wizara ya Elimu yenywewe, lakini ukiwapa TAMISEMI kwa jinsi ambavyo Wilaya zilivyo, Wilaya nyingine

zitakwenda juu nyingine zitabaki chini. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiria kwa upande wa mafunzo kazini Mheshimiwa Waziri tusaidie ili *in service training* iendelee kutolewa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nilitaka niipongeze Serikali kwa hii *performance based (P4R)*. Mimi nimeipenda sana kwa sababu, utaratibu ulioko sasa hivi unakwenda kwenye shule, shule yenye we inaangalia utaratibu gani wa kutafuta fedha, kwa hiyo, inapunguza gharama kuliko ile ambayo fedha inachukuliwa anapewa mtu *contractor* na nini. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri hii *P4R* ni nzuri, naomba tu iendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nadhani la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la ukaguzi. Bado mimi kwa mtazamo wangu na *understanding* yangu, tunahitaji chombo cha ukaguzi kinachojitegemea. Wakaguzi walivyo bado wako chini ya idara, hawapewi fedha za kutosha, lakini kule Wilayani kwenye Halmashauri wanapokosa mafuta kwenda kukagua wanamuomba Mkurugenzi. Huyu uliyekwenda kumpigia magoti asubuhi, ukamuomba mafuta ya dizeli au petroli, huyo huyo akakusimanga ukaenda ukamkagulia shule zake halafu jioni unamleteea taarifa, ataisoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kukiwa na *independent kabisa* chombo ambacho kinaangalia *quality assurance* na jinsi idadi ya taasisi zinazotoa elimu zilivyoongezeka kwa kweli, nakusihii kabisa Mheshimiwa Waziri anayehusika muangalie umuhimu wa kuwa na chombo cha ukaguzi kinachojitegemea ili kikague shule za Serikali na shule za binafsi bila kujali kwamba haya mafuta yametolewa. Kwa sababu, watakuwa wanajitegemea wanapata mafuta yao wao wenye we kuliko kwa hali ilivyo bado ni idara tu ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Ndalichako na wote wanaofanya kazi katika Wizara ya Elimu nikiamini kwamba

wametusikiliza mengi na hasa hili la *Independent Education Regulatory Board*. Kwa kweli, Mungu awasaidie abariki kazi yenu ni ngumu, lakini mnajitahidi kadiri muwezavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, tunaendelea, Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuata Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Silafu Maufi ajiandae.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi pia nimpongeze Profesa Waziri wetu, Naibu wake, Katibu Mkuu, watendaji wote na Wakurugenzi walioko Wizarani pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na sehemu moja Serikali yangu wakati inakuja inipe majibu. Nianze kwenye muundo huu ambao ni sera ya shule za msingi na sekondari ambapo wanafunzi wanatakiwa hawa walioanzia mwaka 2015 tangu sera imetungwa wataenda mpaka darasa la sita. Lakini hapo nyuma mwaka 2014 kuna wanafunzi nao ambao wanamaliza mwaka mmoja huo huo. Kwa hiyo, tuna watu wawili mara mbili, wengine wa darasa la sita wengine wa darasa la saba kutokana na muundo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ninalolipata Serikali yangu imeshajiandaa kuwapokea hawa wanafunzi watakaomiliza la saba na la sita wote kwenda sekondari kwa mara moja? Kwa sababu hawa wanafunzi watakuwa wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mtindo huu kwa hawa walioanza kwa maana ya mwaka 2015 wanaoishia la sita na hawa wa mwaka 2014 wanaoishia la saba, sijui mtafanyaje? Tunawapokeaje? Shule tunazo, maandalizi mmenza rasilimali watu na walimu wa kufundisha? Kwa sababu ni *double*, kwa sababu wamemaliza hawa na hawa wamemaliza, mtihani ni huo huo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo napata tabu kidogo kwa maana sijui, maana mwaka 2020 tuna mambo mengi, kuna uchaguzi, tuna mambo gani, kuna wanafunzi wengi wanamaliza wenye mitihani miwili la sita na la saba kwa wakati mmoja. Naomba Serikali ijipange kidogo na ikija hapa inipe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kuhusu suala la elimu. Ndugu zangu Awamu ya Tano kwenye elimu bure ni suala linaloenda kumuangalia mtoto wa maskini, si la bahati mbaya na elimu hii sio wale ambaao mmezaliwa ninyi kwenu mnasoma tu, wale watoto wa wavuvi, watoto wa wakulima wasisome, hapana. Awamu ya Tano inaposema elimu bure ina maana huyu mama mpika kitumbua hawezি kulipa mtoto wake asome. Ndiyo dhamira ya Serikali iliyopo, kwamba kila mtoto anayetakiwa kwenda shule na aende na iko wazi, walivyosema elimu bure wameetoka millioni moja wameenda milioni mbili, hiyo ni picha halisi inayoonesha kwamba tunao wengi waliokuwa wanabaki nyumbani bila kwenda shule kwa sababu ya mambo ya kulipa, naipongeza Serikali yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna watu wanasema elimu imeshuka, elimu sijui kufanya nini, mimi nakataa. Nakataa kwa sababu zifuatazo, nitakataa wewe una miaka 20 mimi nina 57, lazima nikatae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakataa kwa sababu, zifuatazo; sisi miaka yetu ilikuwa unafanya darasani mtihani vipindi vitano, kila kipindi *marks* 50. Ukipata *marks* 244 huendi sekondari, kwa sababu shule hazipo, lakini wale wazazi ambaao walikuwa na uwezo akikupeleka *private* na huyu aliyeshinda kwenye kijiji mtu mmoja mkienda *form four* wote mnakutana kwenda *high school*; miaka hiyo ambayo watu hawataki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kila mwaka ukienda watoto wanaendelea kuzaliwa na changamoto ya elimu inaendelea, idadi inaongezeka, haiwezi kufanana. Unalinganisha na nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kila kitu ni historia, historia inakataa kwamba mwalimu fulani aliposoma kwa sababu madarasa yalikuwepo na shule zilikuwa chache wanaenda wachache. Leo hii ukienda elimu ya juu watoto ni kama 150,000 wanaendo kwenye vyuo wanadahiliwa na wanalipiwa na Serikali, lakini miaka ile walikuwa labda 20,000, sasa tutalinganishaje? Ndio maana nawapa Serikali yangu tahadhari kwamba kuna kitu kinaongezeka hapa. Mnapodahili watoto wa la saba wakawa wengi, je, miundombinu tumeongeza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naipongeza Wizara ya Elimu kwamba mnachokifanya ni sahihi na elimu iko vizuri. Marekebisho lazima yawepo, hatuwezi kutoka mbinguni, lakini kuna rafiki yangu mmoja amesema pale kwamba lakini watoto wa Wabunge wanasoma nje, *okay*, wako watu wanasomesha watoto nje, lakini mtoto wa dada yake je? Wa mjomba wake je? Kwa hiyo, tunapoongelea elimu tunaongelea kwamba elimu ya watu wote sio ya watu baadhi ambao wamechaguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na watu ambao wamelisemea suala la lugha. Mimi nafikiri tufikie mahali Serikali ifanye maamuzi na maamuzi yenye yawe magumu tu. Kama tunaanza chekechea mpaka *form five* mpaka *form six* ni kiswahili, iwe kiswahili basi. Kwa sababu mtoto ili aweze kujifunza ni lugha gani anatokanayo nyumbani kwao. Hakuna mzazi ambaye ana mtoto akishajifungua ameanza kutambaa akaanza kizungu, ninyi wa mjini ndio mnafanya hivyo, lakini wa vijijini wote ni kiswahili, sasa tunakikwepaje kiswahili kwenda kujifunza lugha za watu wengine? Ndiyo lugha yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na leo kiswahili kina nafasi kubwa ulimwenguni, watu wanaotaka kujuu kiswahili ni wengi, wanaokuja kujifunza kwetu ni wengi, tunakiogopa kwa nini? Serikali mimi nasema biashara ya kizungu mtakutananayo huko Ulaya, hebu tuamue kwamba tunataka Kiswahili kutoka chekechea mpaka chuo kikuu, dhambi ni ipi? Kwa nini tunakwepa chetu? Fanyeni maamuzi tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuna watu wana sema kweli kiswahili ni kigumu, lakini ni kwa sababu hatufundishwi tunakiongea tu. Wakija wenzetu wanakuja kujifunza kiswahili wanajua fasihi, wanajua fasaha, wanajua nini. Kwa hiyo, Serikali yangu iamue kwamba lugha iwe ni fulani kufundisha kuanzia chekechea mpaka chuo kikuu, sio aibu. Mbona tukienda mikutano ya kimataifa kila mtu anawekewa lugha yake mnaelewana? Kwa nini sisi tunaogopa kiswahili kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende Mkoa wa Kagera; Mheshimiwa Waziri Kagera pale tumeona mnadalili za kujenga Chuo cha *VETA*, pesa mnazo, watu kila siku wanazunguka. Naomba wakati kwa majibu yenu, mnaanza lini na mabilioni mmeshapewa yako benki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wamesema pale watoto wanamaliza la saba hawana mahali pakwenda. *VETA* ingekuwepo, Mkoa mkubwa kama Kagera ingesaidia sana hawa wazazi. Tunawaomba sana, suala hili la elimu jamani tuhurumieni wengine, Mkoa kama Kagera kwenye karne hii *VETA* haipo, pesa mnazo mmekaa nazo Wizarani. Pamoja na tunawapongeza, lakini mnatuumiza, haiwezekani. Kama pesa zipo si watu waanze, tatizo ni nini? Naomba wakati Waziri unarudi hapa kuja kuleta majibu uje vizuri maana sisi wengine! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, michango..., Dakika tano au kumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango shulenii. Kuna shule nataka kushauri tu; kuna shule ambako kule michango tumeiondoa, lakini watoto wengine walishazoea kunywa uji, wengine kula mchana, kule kumeporomoka sana, watoto hawarudi shulenii. Hamuwezi kuja na mawazo mapya kwamba pamoja na kwamba michango bure kwenda shule na na nini, lakini ile ambayo wazazi wanafanya kwa hiyari mkaipa nafasi ili angalao watoto wao wasishinde njaa wakapata hata uji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu shule za kwetu kule vijijini kuna hamasa nyingi ambazo watoto wanaenda shule. Akishika kikombe asubuhi anawahi shulenii anaenda, lakini akishajua na uji haupo na mchana hamna chochote hali inakuwa mbaya. Tumeamua tusichangishane, lakini je, ile michango ya hiyari nayo ni migumu? Mtufafanulie kidogo tujue maana tukienda huko nje tunaulizwa maswai mengi na maelezo mengi yanakuwa hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, juzi hapa niliuliza maswali hapa kuhusu Vyuo vya Michezo, nikajibiwa haraka haraka na wapenzi wenzangu wale wa michezo. Hebu Wizara ya Elimu mtuambie, zilikuwepo shule kama Butimba ambazo ni *special*/kwa sababu ya elimu ya michezo tu. Ziko nyingi, zilikuwepo shule kama Korogwe, vilikuwepo vyuo kama flani, kwa nini mmezuwia michezo isiendelee shulenii? Kwa nini? Kwa nini hilli suala mnaliondoa? Hawa watu watafundishwa wapi? Naomba mniipe majibu mazuri kwenye suala la michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vyuo vilienda Wizara ya Habari ambavyo navyo vinachechemea, lakini ninyi kwa sababu ni fani yenu, turudishieni vyuo vyetu. Kama mlikuwa na *crush programme* imeisha, lakini suala la wanamichezo kupata mahali pa kusoma ni la muhimu sana.

Sasa msije mkatuambia kuna UMITASHUMTA, kuna UMISETA, lakini vyuo havipo, mmevifunga havifundishi, masomo haya darasani hayafundishwi michezo mmeondoa, kwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaombeni sana suala la michezo msilifanyie mchezo. Suala la michezo ni ajira.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

## T A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa kwa kifupi sana.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mzungumzaji ambaye anaendelea kuzungumza mda huu ametoa hoja moja kwamba ni vizuri tukatumia lugha ya kiswahili kufundishia kuanzia chekechea hadi chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwalimu, nina wasiwaso kidogo kwa sababu wakati mwingine tunaweza tukatengeneza viongozi ambaa baadae watashindwa kusafiri kwenda nje ya nchi na kuwasiliana na wengine.

**MWENYEKITI:** Toa Taarifa basi, toa Taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ndio hilo tu, nilitaka nimpe taarifa kidogo anapochangia achukue tahadhari kidogo kuhusu hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa siipokei sana kwa sababu inawezekana mwenzangu hata tangu mwaka umeanza hajagonga *passport*, kwa hiyo, sio tatizo sana. Lugha ziko nydingi, watu hana anayesafiri na lugha moja ya kizungu kuna nchi zinaongea kiarabu peke yake, kuna nchi zinaongea kireno, kiitaliano, hawajui kiingereza chenu hiki, kiingereza kiko kwenu huku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa namalizia kwa kusema kwamba mimi kwenye michezo, bado naendeleo huko huko, Wizara ya Elimu mrudi mijipange, muangalie vyuo vyetu vilivyokuwa vinafundisha michezo mturudishie ili taaluma hii isipotee, lakini tukiwa na walimu ambaa wanajua kucheza, akipiga mpira ndio mtaalam, haitusaidii katika nchi. Tutaacha kizazi ambacho hakiwezi kucheza na utamaduni ule ukipotea Taifa linapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishia hapo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea, Mheshimiwa Silafu Maufi atafuatiwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf ajlajdae

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuzungumza mbele ya Bunge lako tukufu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kunipatia afya na nguvu na kuweza kusimama leo hii mbele ya Bunge lako na kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia suala zima la bajeti ya elimu. Bajeti ya elimu imeweza kufanyiwa kazi kwa mwaka 2017/2018 na kuweza kupatikana kwa asilimia 65 ndani ya matumizi ya kawaida na asilimia 68 katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini elimu ni kila kitu, bila kuwa na elimu huwezi kupata maendeleo yoyote katika maisha ya mwananchi, ni lazima apate elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi ninaiomba Hazina ijipange kwa ukamilifu angalau kwa Wizara ya Elimu iweze kupata bajeti yake kwa asilimia 85 ili waweze kutekeleza mambo yao kwani wana changamoto nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Mkoa wetu wa Rukwa tuna mapungufu ya madarasa, tuna mapungufu ya matundu ya vyoo, tuna mapungufu ya nyumba za walimu na vilevile tuna mapungufu ya maabara pamoja na vifaa vyta maabara. Ukiachia mbali suala zima la upandishaji wa vyeo vyta walimu na hata kuhakikisha kwamba wanapata stahiki zao zilizo sahihi katika Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanakosa hata ule motisha na kufanya kazi yao katika uweledi na kufanya kazi yao katika hali iliyio nzuri zaidi. Kwa hiyo, ninaiomba Hazina kuweza kutoa fedha za kutosha kutokana kufuatana na jinsi

bajeti tutakavyoipitisha hapa leo ili kuhakikisha kwamba elimu waweze kutimiza malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa naomba Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba inajikita sana katika elimu ya awali. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuseme kwa kweli kabisa kwamba lugha yetu ya Tanzania ni kiswahili, lakini lugha ya kiingereza ni muhimu kwa watoto wetu. Kwa hiyo tunawaomba Wizara ya Elimu tujikite kuhakikisha kwamba haya masomo ya awali (chekechea) waanze na lugha ya kiswahili na lugha ya kiingereza mpaka kuendelea huko mbele. Kufikia hapo ndiyo kusema ya kwamba walimu wanafundisha shule za chekechea naomba wafanyiwe maandalizi mazuri ili waweze kwenda kuwaandaa watoto wetu katika elimu ya awali ambao ndiyo msingi wa kuibua elimu bora ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima lililozungumzwa katika ukurasa 143, kuhusu nyumba za walimu. Suala la nyumba za walimu ni tatizo la nchi nzima. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Mama Ndalichako na timu yako mnafanyakazi pamoja na changamoto zilizopo hamyumbi na wala hamtikisiki ilhali kwamba mnafanyakazi kwa pamoja. Ninawaomba hizi nyumba 40 zimetajwa katika shule kadhaa na Rukwa tumetajiwa shule moja ya Kasanga. Lakini nilikuwa naomba, kwa kuwa bajeti hii tumechelewa kuwekewa zaidi ya shule mbili/tatu kwa Mkoa wa Rukwa ninaomba awamu ijayo Mkoa wa Rukwa uweze kuangaliwa katika kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesema mnajenga nyumba za walimu katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi, hata sisi kwetu Mkoa wa Rukwa ziko sehemu hizo; Milepa, Kaoze, Kipeta, Ninde, Wanpembe, Kala, Senga, Molo ni maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi. Ningeomba kwamba tuweze kupatiwa nasi vilevile ujenzi wa nyumba za walimu

ili walimu wawepo wa kutosha ili watoto wetu waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, napenda kuzungumzia suala la usafi wa mazingira. Usafi wa mazingira shule zetu za msingi na sekondari katika upande wa vyoo kwa kweli hauridhishi, unasikisitisha sana na kwa kuwa Wizara imeamua kujenga madarasa 2,000 na matundu ya vyoo 2,000, hata wakijenga 10,000 lakini hayatakuwa bora zaidi ikiwa kwamba hatuna huduma za maji katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Hazina (Wizara ya Fedha) wahakikishe kwamba zile shilingi bilioni 17.033 ambazo wizara imeweka kama bajeti yao 2018/2019 fedha hii itoke kwa sababu imeshawekwa hapa, lakini ingeongezeka ikawa ni kubwa zaidi kwa sababu zoezi wallionalo kuhusu vyoo vya shule kwa kweli eneo ni kubwa zaidi na vyoo kwa sababu vinahitaji maji na maji hayapo shulenii wanahitaji kuweka miundombinu ya maji, aidha, ya kukinga maji ya mvua au kuhakikisha kwamba wanaweka mifereji na kufikisha maji katika shule zetu zote za nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni zoezi kubwa, kwa hizi shilingi bilioni 17 kwa kweli ni ndogo zingeweza zikaongezeka ili wakaweza kufanisha hili zoezi ambalo ni gumu na tete kwa watoto wetu; na hasa watoto wetu wa kike hawawezi kuzihifadhi kwa sababu zile siku zao tatu au siku zao tano wanakosa maji katika maeneo yao ya shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda vilevile kuzungumzia suala la ujenzi wa shule za mikoa. Imetajwa mikoa saba inayojengewa shule, ninawaomba kwamba hata Mkoo wa Rukwa nao unahitaji kuwa na shule. Tuna shule chache na hata shule za sekondari za wasichana hatuna. Tunayo sekondari ya wasichana moja ambayo ni ya dhehebu ya wenzetu wa kikristo iko pale Kizwite, lakini tunahitaji kupata shule za sekondari za wasichana hata mbili, tatu kwa Mkoo wetu wa Rukwa na mjue wazi kabisa kwamba Mkoo wa Rukwa ulikuwa uko pembezoni na imechelewa na mambo mengi. Kwa hiyo suala la elimu ni mojawapo.

Kwa hiyo, tunawaomba kipindi kijacho, naomba katika ujenzi wa sekondari hizo za mikoa na Mkoa wa Rukwa uwemo katika mipangilio hiyo ya kikao kinachokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya ukurasa wa 126 wa hotuba wamezungumzia suala la ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi. Ninashukuru kuona Mkoa wa Rukwa nao umo mionganoni mwa hiyo mikoa, tunashukuru sana Wizara. Lakini je, hii shule ya ustadi inakwisha lini? Ni ndani ya mwaka huu wa 2018/2019 ama zaidi ya mwaka mmoja? Kwa hiyo, tunapenda kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naifahamu wazi kwamba ndugu zangu wa Wizara ya Elimu tulishazungumza mara nyingi sana ndani ya Bunge hili kwamba Mkoa wa Rukwa hatuna Chuo cha VETA. Tunaomba Chuo cha VETA nayo inaanza lini kujengwa pale katika Mkoa wetu wa Rukwa ili vijana wetu wa darasa la saba na darasa la kumi na mbili waweze kupata mahali pa kuweza kupata stadi na kuweza kujajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililokuwa napenda kulizungumzia ni kuhusiana suala ya walimu. Walimu wanahitajika kupata motisha. Lakini pamoja na hivyo Wizara imeelekeza katika ukurasa wa 123 kwamba kuna fedha zimetengwa, takribani trilioni moja ambazo watazitumia kwa kuhusu na kutoa na motisha kwa Halmashauri na kwa shule mbalimbali ili waweze kuonesha nguvu ya kuongeza elimu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, lakini tatizo linakuja ubora wa hizi Halmashauri na kupata motisha hizo na ubora wa hizi shule kupata motisha hizo kwa walimu wale kutaendelea na kuwezekana kuwepo kuwa na bora zaidi ikiwa Idara ya Ukaguzi ikiwezesewa. Hawana magari, hawana mafungu ya kujijendesha wao wenyewe katika suala zima la ukaguzi. Ukaguzi si maafisa wanaokaa ofisini, ukaguzi ni watu ambao wanakwenda *field* si kwa ratiba maalum hata wakati mwingine kuvamia zile shule na kuona zinaendelea namna gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba hiyo motisha iliyokuwa imetengwa ninaomba Hazina itoke ili kwamba wale watakaoshinda na wale watakaoshindwa waweze kuhamasika ili na wao pia kipindi kichokuja waweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusiana na ubora wa elimu. Ubora wa elimu ni mambo mawili; wale wanaoandaliwa na wale wanaowaandaa hao wanaoandaliwa. Kwa hiyo tunaomba elimu waweze kuangalia kitu hicho wale wanaowaandalia hawa wanaoandaliwa wawe katika ubora zaidi na katika ukamilifu zaidi. Na hawa watu wapo tunao walimu walimaliza kusoma vyuoni wako mitaani hawajapata bado ajira, tunaomba hao walimu wato...

*(Hapa kengele lillia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nashukuru kwa kunipa nafasi hivyo, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jadi Kadika, Mheshimiwa Dkt. Suleiman Yussuf, Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Susan Kiwanga waanze kujandaa.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema kuweza kusimama hapa kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu. Pia natoa pole kwa Watanzania wote waliopata mafuriko wakafiwa na wapendwa wao pamoja na kupoteza mali zao. Baada ya kuzungumza hayo sasa naanza kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuulize ni jambo gani linalotupa kuteremka kiwango cha elimu katika nchi yetu?

Tuna changamoto kubwa sana ndiyo inayoleta kuperomoka kwa elimu.

Changamoto ya kwanza ni upungufu wa walimu. Tuna upungufu mkubwa wa walimu, ukosefu wa vitabu vyatya kusomea na vitabu vyatya kujifunzia, maslahi ya walimu ni madogo na wanafundisha kwa muda mrefu bila ya kupandishwa daraja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wapandishwe madaraja na waongezwe maslahi yao kwa sababu mama ikiwa hashibi hawezi kutoa maziwa ya kumlisha mtoto wake. Kwa hivyo ni lazima tuwaangalie kwa jicho kubwa ili wawze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna ukosefu wa matundu ya vyoo pamoja maji. Hilo ni tatizo kwa sababu maji ndiyo uhai wa binadamu. Leo watoto wengi wa kike wanafeli kutokana na kwamba wakiwa katika siku zao za hedhi kuwa hawawezi kuhudhuria masomoni muda wa wiki moja mpaka wiki mbili. Hiyo inachangia watoto wa kike kufeli, kwa hivyo ni lazima Serikali liitatue kwa haraka tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu na hasa walimu wa sayansi. Tuna upungufu wa walimu wanaofika 15,968; huo ni upungufu kubwa sana. Tunataka nchi ya viwanda tutakwendaje kwenye viwanda ikiwa hatuna wasomi wa sayansi na ukiangalia upungufu mkubwa nao uko katika shule za msingi; kwa hiyo, ni lazima Serikali iajiri walimu mara moja kuziba mapengo ya wale wa vyeti *fake* walitolewa na tupate walimu wa kuendeleza elimu ili elimu yetu iweze kupanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za Serikali zinasomesha lugha ya kiswahili wenzangu wengi wamezungumza. Lugha ya kiswahili kuanzia chekechea mpaka darasa la tatu. Wakati ni tofauti shule za *private* zinasomesha lugha ya kiingereza kuanzia chekechea mpaka darasa la tatu. Ukiangalia mtihani wao uko sawa sawa, je, watakuwa sawa

hao kwenye matokeo wakati wale wameshaiva, wale ndiyo kwanza wanaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo natoa ushauri kwamba Serikali ikae na wadau wa shule za *private* ili kushirikiana na kutoa elimu iliyo bora ili wote wafaidike kwa sababu wote ni watoto wa Tanzania na wote ni watoto wetu, tusibague wale wakawa bora kwetu sisi wakawa si bora. Leo inafika hadi shule za Serikali darasa la saba mtoto hajui kusoma wala kuandika, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu mitaala. Kila baada ya kipindi mitaala inabadilika. Inapobadilika tunawapa mzigo wazazi kwa sababu itabidi wanunue vitabu vipyta. Wanaponunua vitabu vipyta wengine wahana uwezo utawakutia watoto watano wanasomea kitabu kimoja, hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunawapa mzigo mkubwa walimu, kwa sababu mwalimu lazima kwanza ajifunze mtaala ule ndipo aweze kufundisha. Kwa hiyo, nashauri angalau miaka 10 ndipo baadae mtaala uangaliwe na kufanya tathimini kwamba je, mtaala huu utaendelea au mtaala huu bado haufai ili ubadilishwe ili kuwaondoshea mzigo walimu na wazee? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu watoto wenyе hali ngumu. Tukiangalia hapa Dodoma ukienda pale... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* kwa kunipa afya

njema na kuwepo hapa leo, na namswalia Mtume Mohamad *Swalallahu Alayhi Wassallam.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, mimi nina mambo machache sana tu ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kila matokeo ya *form four* na *form six* yanapokuja kwa upande wa Zanzibar inakuwa ni vilio tu, hakuna vicheko kabisa kabisa. Tukiziangalia katika shule ambazo zinashika mkia zile shule 10 bora zinazoshika mkia basi kati ya sita mpaka saba zinatoka Zanzibar.

Mheshimia Mwenyekiti, tunataka kujiliza Wazanzibar kwa nini kila siku tunafanywa kuwa watu wa daraja la pili? Ni kwa nini inakuwa hivyo? Na ikiwa masuala ya elimu ya juu ni masuala ya Muungano, nauliza Wizara ni jitihada gani ambayo inachukua kuweza kuisiaidia Zanzibar kuepukana na udhaifu ulio mkubwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia njue hivi katika Bodi ya Mitihani, katika Bodi ya Wakurugenzi ile Bodi ya Mitihani kweli tuna wawakilishi kutoka Zanzibar pale? Mara nyingine inawezekana sababu ya udhaifu huu ni kwamba hakuna watu ambao wanawenza wakaishauri bodi vizuri katika masuala ya Zanzibar. Nataka Waziri aje anieleze kweli tunao watu pale? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka nilijue kwa kifupi tu ni suala la mikopo. Bodi ya Mikopo imekuwa siku zote ikitoa mikopo kwa upande wa wanafunzi wa Zanzibar. Lakini mpaka hivi sasa hatujui haki ya Zanzibar katika mikopo ile ni kiasi gani. Wazanzibari ni asilimia ngapi tunapata? Kwa sababu tukijua hili itasaidia kuondoa yale malalamiko ambayo yako kwa wanavyuo wa Zanzibar kwamba Wazanzibari hatupendwi, Wazanzibari tunadhulumiwa. Hebu tuambieni Mheshimiwa Waziri, ni asilimia ngapi, tunataka kujua asilimia yetu katika Bodi ya Mikopo ni kiasi gani ili kuondosha haya malalamiko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Mheshimiwa Waziri atakapokuja atufahamishe kati ya wanafunzi 122,623, Wazanzibari wangapi ambao wanapata mikopo mionganoni mwao? Kati ya hao Wazanzibar ni wangapi? Kadhalika kuna wanafunzi 350 ambao wanasomesha nje kwa kupewa mikopo, nataka njue kati ya hawa 351 Wazanzibar ni wangapi ili tujue haki yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala dogo pia nataka nilijue, ni kwa nini Wazanzibari hawapati *grade A* katika hii mikopo, wote ni *B, C* na kwenda chini. Ni kwa nini Wazanzibar hawapati nafasi hiyo ya kuwa *full sponsored* badala yake ni wa upande mmoja tu ndio ambao wanapata? Nataka uje unijibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda haraka haraka tukija upande wa *TCU*. Upande wa *TCU* umeandika kwamba katika kazi zake ni kuhakiki ubora wa elimu na kuidhinisha programu zifundishwazo. Nataka kujua ni kwa nini *TCU* au *TCU* imeona nini katika elimu za dini? Elimu za dini hapa nijuavyo zinasomesha katika Chuo cha *Muslimu University (MUM)* na pia kinasomesha katika Chuo cha Abdulrahman Sumait kule Zanzibar. Lakini hawajaidhinisha chochote ni udhaifu gani walioniona au ni kitu gani kibaya... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Utayapata tu ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Susan Kiwanga na Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko hapa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliosema kwamba kwa kweli elimu yetu inaendelea kushuka sana na elimu hii imeshuka

kwa sababu kadhaa; na pia tumeshuhudia walimu wakuu wakifukuzwa kazi, walimu wakuu wakishushwa vyeo kwa sababu shule zao zimefanya vibaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tunaita kwenye taaluma ya *management services* tunaita *blame culture*. *Blame culture* ni utamaduni ambao unatafuta mchawi. Jambo limeharibika unamatafuta mchawi wa kumbebesha huo mzigo kwamba yeye ndiyo amesababisha bila kuangalia ni sababu zipi zimefanya hizi shule zisiweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ziko nyingi, sababu moja ya kwanza ambayo naiona mimi kubwa sana ni mfumo ambao kila Waziri anayekuja anakuja na ajenda yake. Tulianza kuona shule zile za mchepuo *agriculture* na biashara zikaondolewa, akaja mwingine kaondoa michezo, kaja mwingine ka-*introduce GPA*, amekuja wa sasa amerudisha *division, curricular* zinabadilishwa kabla walimu hawajazifahamu vizuri, zimebadilishwa. Kwa hiyo kuna mambo mengi ambayo yanababisha shule zetu zisiweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza kwamba sasa tuiombe Serikali iweke mfumo ambao utazuia Mawaziri wa Elimu kubadilisha mitaala, kubadilisha mifumo ya elimu bila ya kupata majadiliano na tukakubaliana elimu yetu iwe vipi na isiwe rahisi kwa Waziri tu anaamka asubuhi, anabadilisha mitaala au anabadilisha mfumo wa elimu, hilo ndiyo pendeleko langu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuungana na marais wale wawili Mheshimiwa Mkapa na Mheshimiwa Kikwete waliosema tunahitaji mjadala mpana kuhusu elimu yetu kwa sababu kwa kweli elimu yetu haiko vizuri. Kwa hiyo, nashauri Serikali huo mjadala uweze kufanyika ili tuweze kuamua elimu yetu tunayoitaka ipi ambayo itatupeleka kwenye Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri pia Serikali juu ya mazingira ya kufundishia kwamba si mazuri, tukianzia na

walimu. Walimu wote tunajua malimbikizo yao hawalipwi, hawapandishwi vyeo na hata mazingira ya kufundisha hayapo mazuri, msongamano wa wanafunzi madarasani, hizo ni changamoto kubwa ambazo zinaathiri elimu yetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha ya walimu; tukiangalia *statistics* za *BEST* zinasema walimu 35 tu ndio ambao wana motisha, wakati walimu 63 hawana motisha ya kufanya kazi. Kwa hiyo, ili tuweze kupata elimu bora kwa kweli rasilimali watu ya walimu ingekuwa ndicho kitu cha kwanza kabisa kwa ajili ya kuwapa motisha waweze kupata moyo, waweze kufundisha, waweze kuwekwa kwenye mazingira mazuri na elimu yetu itaweza kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia mnyororo wa elimu kwa ajili ya Tanzania ya Viwanda. Nimeangalia taarifa ya Mheshimiwa Waziri na bado sijaona kwa mfano katika *admission* au usajili wa wanafunzi hasa katika sayansi sijaona ni *pool* gani kubwa ambayo tumesema tutawasajili au tutaweka kwenye vyuo waweze kukidhi yale matakwa ya Tanzania ya Viwanda. Nimeona kwenye *VETA* tunaongeza wanafunzi 200,000 mpaka 250,000 na nikawa najiuliza, je, hawa 200,000 mpaka 250,000 ndio ambao tumewa-target kwa ajili ya Tanzania yetu ya viwanda? Maana ni muhimu kuinyambua na kujua ni *skills* zipi ambazo tutazihitaji kwa ajili ya shughuli zote za viwanda kwa Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia katika taarifa ya Mheshimiwa Mpango ambaye alitaja baadhi ya madaktari sijui ma-*engineer* na nini, lakini tunahitaji kunyambua na kujua. Kwa mfano tungeweza kuona katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri ni *pool* gani kubwa ambayo tutakwenda kuisomesha kwa ajili ya Tanzania ya viwanda. Bado sijaona na ninapendekeza sana Mheshimiwa Waziri ajipange kusudi hata ile *pool* ya sayansi na teknolojia ikidhi yale mahitaji ya Tanzania yetu ya viwanda, kwa sababu bila hivyo tutajikuta tumekuwa na viwanda, tumekuwa sijui na *Stieglers*, tumekuwa na reli lakini hatuna *pool* kubwa ya wataalam...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. SUSAN L. KWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niende moja kwa moja kwenye *point* zangu; kwamba kidato cha tano na cha sita Wilaya ya Kilombero mwaka huu wametupa shule moja ndani ya Jimbo la Kilombero pale Sanji. Sasa mimi siwezi kusema sana, lakini Jimbo la Mlimba linaeleweka yaani ni kubwa, pana, miundombinu mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulikuwa tumeomba na sisi tupate kidato cha sita, kwa hiyo kwa sababu bajeti ya mwaka huu inapita na mmeshapanga hicho kwa hiyo naomba mkumbuke kunako majaliwa kipindi kijacho cha mwaka ujao wa fedha mtuwekee na sisi ndani ya Jimbo la Mlimba na tumeshapendekeza hizo shule za kuweka kidato cha sita, hiyo itasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya walimu. Ukipungumzia kuhusu madeni ya walimu nchi nzima ni shida. Walimu wameshahakikiwa na katika kazi zao kule katika ofisi zao wameshaweka vizuri, sasa kwa nini Serikali hailipii hawa walimu madeni yao, kigugumizi cha nini jamani? Hamuoni kama mnawavunja moyo hawa walimu? Afadhali huku mjini watu wanapiga biashara labda *ice cream* nini wanauza shulenii, kule kijijini hamna wenzenu, walimu wanategemea mshahara tu na wakisema waende wakalime mara mvua imekuja imebeba mazao yote. Sasa hawa walimu wanaishi viyi katika mazingira hayo? Naomba tafadhalii lipeni na mtupe majibu katika bajeti hii ni lini mnalipa madeni ya walimu nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu walimu wa sanaa mnasema wametosha. Tangu walivyoajiriwa mwaka 2014 ajira hamna tena, lakini cha kushangaza Serikali hii hii inadahili

walimu hao hao wa sanaa, wazazi maskini wanemosha hawa watoto wao na Serikali inatoa pesa kwa ajili ya kuwapa mikopo baadhi yao lakini mnasema wametosha. Sasa kama ndiyo hivyo basi msitishe hawa walimu wa sanaa, la sivyo kwa sababu nchi hii sasa inaenda kwenye viwanda basi badilisheni mtaala, badala ya kuwapeleka kwenye ualimu muwapeleke katika masuala ya ufundi hawa wanaosoma *degree*, waanzishe viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji watu wa kuanzisha viwanda vidogo na viwanda vyatiki. Kwa hiyo badilisheni acheni mambo ya sanaa lakini hata mkisema walimu wanatosha, hawatoshi. Kule kijijini *ratio*; kwa kawaida *ratio* yenu ni 1:40; 1:45; 1:25. Leo nina chekechea mimi tena *satellite area* hakuna mwalimu lakini wanafunzi 100 chekechea, hivi kuna elimu pale? Kwa hiyo, si kwamba walimu wanatosha, lakini Serikali bado haljajipanga ni namna gani wathibitishe hiyo *ratio* mliyoipanga ili walimu waende wakafundishe hizo shule, hali ni mbaya kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukariri, jamani eee, hivi kukariri hamna, sasa kukariri hamna watoto wasichana Mama Ndalichako na wewe mwenyewe ni mwanamke watoto wasichana wasipokariri waende wakaolewe wakiwa bado wadogo? Mimi naona hiyo kukariri acheni, watoto waendelee kusoma ili wapate elimu wakue shulen baadae hata wakitupwa huko mbali kama ataolewa yeye, atakuwa mkulima yeye, lakini hiyo kukariri achanane nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa maabara. Somo la Baiolojia ni asilimia 51.5, Fizikia asilimia 43.5, huko vijijini huu upungufu huko vijijini kwetu hakuna walimu hao jamani. Sasa matokeo yake eti mtoto anayefundishwa *private*, anayefundishwa mjini, mwenye walimu, mwenye maabara anafanya mtihani mmoja na mtoto wa Mlimba. Huo ni uonevu ama si uonevu huo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri akija anijibu, huo si uonevu? Kwanini mnampa mtoto wa Masagati, mtoto wa Utengule,

mtoto wa Mlimba anafanya mtihani mmoja na mtoto wa Dar es Salaam au wa mijini ambaye ana maabara, ana walimu ana kila kitu, huo ni uonevu, ni ubaguzi haukulbaliki ndani ya nchi yetu, haikubaliki kabisa, kwa hiyo hilo naomba mliangalie, tunaoteseka ni sisi wa vijijini siyo wa mijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nauliza hivi *remote area* zile shule za *satellite* yaani kwenye jimbo langu kutoka shule ya msingi mpaka kwenye kitongoji ni kilometa 20, hapa katikati kuna mito ya ajabu. Mimi leo mpaka mfuko wa jimbo nahangaika nao nawaambia wananchi jengeni madarasa mawili halafu mimi naleta bati na nimeshapeleka bati Mpande kule Kata ya Mchombe, Ijia na sehemu nyiningine nyingi. Kule Tanganyika, Masagati, Lwamate mpakani na Njombe lakini walimu hamna. Vigezo mnavyoweka mijini hebu legezeni masharti na vigezo vya vijijini jamanii. Haki ya Mungu unaenda unalia, watoto 200 hakuna mwalimu, mwalimu wa kujitolea, hebu nendeni mkaangalie halafu mjue mpange mipango yenu. Hamuwezi mkalinganisha... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, endelea kupambana na hali yako. Tunaendelea, Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae na Mheshimiwa Susanne Maselle. (*Kicheko*)

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nataka kusema kwamba elimu ni uwezo si idadi tu ya watu ambao wanaingia shuleni. Tunatarajia watoto wanaoingia wafundishike, wawe na uwezo wa kutatua changamoto zilizopo katika mazingira yao; hapo tutapata maendeleo katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akija atujibu kwa ufasaha kuhusu hivyo vitabu vya darasa la nne ambavyo mpaka sasa hivi bado havijafika shuleni, watoto wetu wanajifunza kwa kutumia kitu gani? Ukifungua

katika hotuba yako ukurasa wa 69 yaani tunaanza mbele kabla ya nyuma. Ukurasa wa 69.

**MWENYEKITI:** Hicho kiswahili cha wapi bwana.  
(*Kicheko*)

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 69 pale namba 62 *roman (ii)* inasema; "Mradi wa kuendeleza elimu ya ualimu imeandaa mapitio ya mitaala wa elimu ya ualimu ili kuwa na mtaala unaokidhi mahitaji ya sasa na unaoendana na mtaala wa elimu msingi ulioboreshw."

Mheshimiwa Mwenyekiti, muone mambo ya ajabu ya Serikali ya CCM, kumbe mpaka wanapeleke mtaala shule za msingi, huku kwenye ualimu hawajawafundisha. Tunategemea wallimu wale wakawafundishe wale watoto ambao mtaala ule hawaujui sasa wanaenda kufundisha kitu gani. Mheshimiwa Waziri naomba unapokuja hapa uje na majibu, haya ni maneno yako siyo ya kwangu nimekwambia ukurasa wa 69 *roman (ii)*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia vyuo vya ualimu; hawa watu wamesahaulika sana. Wakufunzi wa vyuo vya ualimu wamesahaulika, mimi nimetoka kule, takriban wazungumzaji wote waliozungumza hapa hawajataja vyuo vya ualimu. Wakufunzi wanadai, *morale* imeshuka, wana matatizo mengi katika kazi yao ya ualimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri una vyuo 35 tu vya ualimu nchi hii, mwenzako Mheshimiwa Jafo ana shule za msingi ngapi, ana shule za sekondari ngapi lakini wewe una vyuo vya ualimu 35, naomba uende ukawasikilize, utatue matatizo yao. Shida ya ualimu inatokea huko kwa sababu watu wamechoka, mpaka leo unamwambia amfundishe mwalimu, mtaala wenywewe maskini haujui anamfundisha kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye fedha za ruzuku. Hizi fedha zimekadiriwa tangu mwaka 2001; mwaka

2001, shilingi 10,000 kwa mtoto wa shule ya msingi, shilingi 25,000 kwa mtoto wa sekondari. Katika hiyo shilingi 10,000 shilingi 4,000 inabakia Serikali haiendi shulenii kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Sasa nakuuliza Mheshimiwa Waziri shilingi 6,000 inayoenda shule kumgharamia mwanafunzi kwa karne hii inatosha? Na kama haitoshi utuambie mkakati wa makusudi ambao umeuweka wa kuhakikisha kwamba hiyo fedha inaongezwa. Pendekezo langu ifike shilingi 20,000 kwa mtoto wa shule ya msingi na ifike shilingi 50,000 kwa mtoto wa shule ya sekondari. Pia uniambie katika hiyo 4,000 inayobakia Serikali Kuu imenunua vitabu kiasi gani na kwa takwimu zippi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo; katika Wizara ya Elimu fedha zinazotengwa ni chache karibu zote asilimia 100 ya fedha za maendeleo mnategemea wahisani, ninyi mapato yenu ya ndani hayatengi fedha za maendeleo. Sasa nataka kukuuliza Mheshimiwa Waziri tunajua kuna miradi mingi, kwa mfano mradi wa KKK, ni mradi mzuri ambao *implementation* yake ingekuwa nzuri tunaamini ingesaidia, lakini mnategemea wahisani. Mtuambie nyinyi kwenye mradi huu mmewe kiasi gani na mmefuatilia kwa kiasi gani mradi huu unaweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la walimu wa sayansi tumekuwa tukiliongea na tutaendelea kulio... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Susanne Maselle na Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa niweze kutoa pole kwa Mheshimiwa Heche kupotelewa na ndugu yake, Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naenda moja kwa moja katika kuchangia na naomba nianze na maneno yafuatayo ya aliyejewa Rais wa Marekani Abraham Lincoln ambaye alishawahi kusema naomba ninukuu; “*The philosophy of the school room in one generation will be the philosophy of the government in the next.*” Ana maana kwamba falsafa ya elimu inayotolewa darasani kwenye kizazi cha leo ndiyo itakayokuwa hatma ya Serikali ya kesho. Tunaona jinsi ambavyo elimu yetu inakwenda /CU. Elimu yetu haiko katika muafaka kabisa, watoto wengi wanamaliza wakiwa hawana ujuzi, maarifa na ubunifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika ripoti ya Kamati jinsi ambavyo shule binafsi zinaongoza kuanzia mwaka 2016. Mwaka 2016/2017 shule 10 bora zote za kitaifa ziliikuwa za *private* na watoto bora wote wa kitaifa walikuwa wanatoka shule za *private* na ukiangalia kidato cha pili hivyo hivyo. Hii maana yake nini, maana yake kwamba kama kungekuwa hakuna shule zisizo za kiserikali *division one, two* na *three* zingekuwa hazipo kabisa. Sasa tufanye nini? Mimi naumia sana ninavyosikia kwamba mnazuia kukaririsha katika shule za *private*. Shule za *private* wanakaririsha kwa sababu wanataka wapate vijana wenye ujuzi, wenye maarifa, wasiende kama taburara, waende wakiwa wanaelewa nini wanachokifanya kwa kila kidato, kuanzia darasa la nne, saba, *form one, two* mpaka *form four*, sisi tunataka walingane, ama mnataka kutekeleza ule usemi wa Mheshimiwa Rais aliyejewa kwamba matajiri wanataka waishi kama maskini. Kwa sababu wanapeleka watoto kule ili waweze kujikwamua katika elimu ninyi mnataka walingane wote tupate ma-zero, hili halikubaliki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la Bodi ya Walimu ambayo itakuwa ni *independent board*. Naomba hili lifanyike, Mheshimiwa Waziri unapokuja utuambie ni lini Bodi hii itaanza, kwa sababu itawianisha na kupima shule za *private* zinakaguliwa na kupewa masharti lukuki, lakini shule za Serikali hakuna masharti yoyote yanayotolewa. Iwe haina choo, iwe ina choo ni kuendelea, hili haikubaliki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda sasa katika suala la walimu. Walimu wamekata tamaa, asilimia 37.8 ya walimu ndio wenye hamasa ya kufundisha, lakini asilimia 60 ndio hawana hamasa kabisa ya kufundisha. Ina maana hawa walimu kama mlivyosema kauli zile zinazotolewa mara kwa mara kwamba asiyetaka kazi aache.

Sasa walimu wameacha kazi wamebaki na utumishi. Mheshimiwa Waziri walimu wameacha kazi, wako na utumishi. Wamekata tamaa kwa sababu hawana motisha kama ambavyo wanapewa shule za *private*, walimu hawa unakuta anafanya bora liende, shule hakuna *discipline*, mwalimu anaendaanasoma anaweza akawa anafundisha au asifundishe, haya yanatokea Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tukuombe Mheshimiwa uliangalie kwa jicho la ndani kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la lugha ya kufundishia; kiingereza na kiswahili. Wamezungumza wenzangu hapa lugha za kufundishia ni jambo muhimu sana katika elimu. Usipokuwa na lugha ambayo umeamua ifundishiwe tunakuwa na mchanganyiko. Tumeona katika shule za *private* wanafundisha kwa Kingereza. Wanaanza darasa la tatu kiingereza wanakwenda nacho na shule za *government* ni Kiswahili lakini darasa la nne wanakutana na mtihani wa pamoja, sijui kusudi na maudhui yake mnataka wapate nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakienda kufika darasa la saba wanamaliza, wakienda sekondari hawa waliotoka shule za *government* wamesoma Kiswahili, wanaenda kukutana na lugha ya Kiingereza wanapata taabu, matokeo yake unakuta wanaanza kuibia. Kwa hiyo, kunakuwa na kazi kubwa sana watoto wanaibia wanasema wanapiga chabo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa toka *form one* mpaka *form four*, anakwenda *form five* mpaka *form six* anapiga chabo; unatarajia huyu mwanafunzi akija kupata kazi atapiga chabo wapi sasa wakati anafanya kazi? Kwa hiyo, hii ni changamoto Mheshimiwa Waziri uangalie kama

hakuna lugha maalum ya kufundishia muone jinsi mtakavyofanya. Mimi ni mwalimu *by profession*, lugha ya kiingereza unakuta zile *phonetics* watoto wadogo wanasoma kwa sauti, unajua sauti ndiyo inaingia na inakaa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Susanne Maselle, Mheshimiwa Dkt. Semesi na Mheshimiwa Zainab Mndolwa wajiandae.

**MHE. SUSANNE P. MASALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hii Wizara ya Elimu. Nitaenda moja kwa moja kwenye hoja zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu mikopo ya elimu ya juu. Kumekuwa na malalamiko mengi sana ya vijana wetu kutopata mikopo na hata kama wakipata mikopo hiyo kwa mwaka wa kwanza, mwaka unaofuata wanakosa sifa kutokana na kwamba masharti yamekuwa yakibadili kila wakati. Kila mwaka Serikali imekuwa ikija na masharti mapya. Hali hii inamfanya kijana anashindwa kusoma na ku-concentrate katika masomo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali, naomba masharti haya kabla hawajayatoa wayalete hapa Bungeni ili tuweze kuyajadili maana yamekuwa yakibagua wanafunzi wetu. Mwanafunzi anakuwa na uhakika wa kusoma mwaka mmoja, mwaka wa pili anajikuta anakosa sifa kutokana na masharti ambayo yanabadili kila wakati na yanamfanya anashindwa kuendelea, anabaki kutangatanga. Matokeo yake sisi Wabunge ndiyo tunakuwa kama msaada wa hao wanafunzi maana wanashindwa kuendelea na masomo kwa sababu sifa zimemwondoa moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu asilimia 20 ya bajeti ya Serikali. Iliamuliwa kwamba asilimia 20 ya bajeti ya Serikali iwe inaenda Wizara ya Elimu, lakini mpaka leo hakuna pesa ambayo inatolewa kwenye hiyo bajeti. Bajeti ya mwisho kabisa ambayo ilitoa hiyo asilimia 20 ilikuwa ni bajeti ya mwaka 2008/2009 kipindi cha JK. Sasa sasa hivi mnajigamba kwamba mnakusanya pesa nyingi, lakini hatuoni hizo pesa zikienda huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri akija hapa atuambie hizo pesa zitakwenda lini kwa sababu pesa hizi kwa mfano zingeenda kila mwaka zingesaidia sana changamoto hizi ambazo zinawapata walimu, kununua vitabu, kujenga maabara na kutengeneza mazingira mazuri ya wanafunzi. Lakini tumekuwa tukipiga tu *mark time* tunakwepa hili jukumu letu. Waziri anapokuja hapa naomba atuambie hiyo hela itaanza kwenda lini kwa sababu tunaenda kuitisha bajeti ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu madai ya walimu. Wengi wameongea hapa, mwaka jana tulipitisha bajeti lakini bado walimu hawajaanza kulipwa na wana malalamiko mengi sana. Sasa hivi tunaenda kuitisha bajeti, naomba Waziri akashughulikie madai haya kwa sababu walimu wetu wamekuwa wakihangaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alishakuwa mwalimu anajua kabisa changamoto zinazowakuta walimu. Sidhani kama na yeye alipata matatizo haya. Inawezekana labda alipata matatizo haya ndio maana analipiza kisasi labda niseme hivyo kwa sababu ni kwa nini sasa tunapitisha bajeti na hashughulikii matatizo yao? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie wanafunzi wetu. Wanafunzi wengi hawana madawati kwa maana kwamba shule nyingi hazina madawati. Tunaomba hiki kilio kiishe maana malalamiko yamekuwa mengi sana, naomba hiki kilio kiishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu *capitation grants*. Mheshimiwa Tunza amezungumzia, lakini mimi ningeenda moja kwa moja kwenye Mkoa wangu. Nataka hii shilingi 4,000 ambayo ilikuwa inabaki kwenye Halmashauri kwa ajili ya kununua vitabu waniambie wameifanyia nini kwa sababu vitabu vyenyewe hawajanunua, sasa wameipeleka wapi. Nataka wananchi wangu wa Mkoa wa Mwanza hasa shule zangu za Mkoa wa Mwanza waambiwe kwa nini hiyo pesa haikununua vitabu na imeenda wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nakushukuru kwa kututunzia muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Katika Wizara hii maoni yangu yatajikita katika elimu ya msingi na sekondari. Nimeamua ku-concentrate hapa kwa leo kwa sababu hawa ndio *foundation*. Tunasema elimu ni ufunguo wa maisha na hawa ndio *foundation* yetu, ni msingi wa kile tunachokizalisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa mwaka huu uliopita ni asilimia 60 ya wanafunzi wetu wa elimu ya msingi na sekondari wamefeli. Nita-specify katika kidato cha pili na cha nne kwa mwaka 2017, wanafunzi hawa wamepata *division four* na *division zero*. Ni janga wala siyo dogo, lakini Serikali inatakiwa iliangalie sana na kati ya hawa waliobaki asilimia 40 ya waliofaulu 90% wametoka katika shule binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kadhaa za wamiliki wa hizi shule binafsi wanakuwa wanakandamizwa na Serikali. Mifano miwili kutoka kwa wanafunzi wale wanafunzi wanaosoma katika hizi shule binafsi hawana ruhusa au hawawezi kwenda kusoma shule za *government* kama kukatokea tatizo lolote. Pia hawa

wanafunzi wanaosoma shule binafsi hawapati mikopo kwa ajili ya kupata *access* ya elimu ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika shule binafsi ambazo sasa zinatuokoa katika elimu zetu za msingi na sekondari, wana maeneo ambayo yanawakandamiza. Moja kati ya hayo wanasema kwamba wanalipishwa *service levy* na Halmashauri husika. Wanalipishwaje *service levy* wakati hawa tayari wanatoa *service* ya elimu? Naomba muwaangalie kwa jicho la kitofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo shule binafsi wanakandamizwa sana ni kwenye malipo ya *property tax*, wanalipa viwango sawa kama vile ni kumbi au ni hoteli wakati hawa ni watoa huduma wa elimu. Kwa hiyo, kama kuna umuhimu wa kulipia *property tax* basi wawe kwenye *certain criteria/category* ya kuangalia hawa ni watoa huduma lakini siyo wafanyabiashara wa moja kwa moja kulipisha madarasa au kumbi za shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo mengi mbadala yametolewa na Kamati husika imetoa maoni mazuri sana naomba yazingatiwe. Moja kati ya hayo ni kujifunza kwa nini shule binafsi zinafanya vizuri ukilinganisha na shule hizi za Serikali. Majibu yapo pale, walimu na wanafunzi wanakuwa *treated* vipi na miundombinu inakuwa *treated* vipi. Huitaji *rocket science* kusema kwamba kwa nini tunafeli kwa sababu mazingira ni hafifu katika shule zetu za Serikali. Naomba tujifunze kutoka *private sector* na tusiwa-*treat* kama *competitors* bali tuwa-*treat* kama ni *partners*, ni wadau ambaao wanaliokoa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea maendeleo pia yanakuwa *reflected* kwenye bajeti ambazo tunazi-set aside kwa ajili ya maendeleo. Umuhimu wa elimu wala hauhitaji mjadala, kwa mfano ukienda kwenye *subvote 2001*, kwenye *Basic Education Office*, itemya 4321, *Primary Education Development Programme LANES*, mwaka 2016/2017 mliwatengea shilingi bilioni 65, mwaka 2017/2018 mliwatengea shilingi bilioni 39 na 2018/2019 mmewatengea

shilingi bilioni nne tu. Sasa tujulize lengo hapa la Serikali ni nini? Tayari tunafanya vibaya sana, hamuoni kama hii ni *alert* inabidi tujbadilishe. Tayari kuna tatizo, lakini hatuweki nguvu ambayo inakuwa *reflected* kwenye bajeti husika ili kuinua kiwango cha elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo imeimbwa sana ni *issue* ya walimu, kwenye elimu ya hawa wanaoelimisha ambao ni walimu pamoja na idadi yao. *Ratio* yetu ya sasa hivi mnasema ni uwiano wa 1:50 wakati inayotakiwa *ki-standard* ni uwiano wa 1:25. Hapo hapo tunasema kwamba baadhi ya walimu wa sekondari wanaenda kufundisha sasa *primary school*, inakuwaje wakati tayari kuna upungufu wa walimu na bado mnataka tena kuwatoa kwenye *level* nyingine kuwapeleka kwenye *level* nyingine ambapo hawa walimu hawajasomea kwa sababu ule ualimu ni taaluma ambayo ina *level* mbalimbali, aidha, ni wa sekondari, chuo kikuu au *nursery*. Naomba tuliangalie kwa uangalifu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine ambalo nataka niligusie ni kuhusu *continuous assessment*. Tunajikita kuwa *grade* hawa wanafunzi wetu kwa mitihani mikuu labda ni darasa la nne, *form two*, *form four* au *form six* lakini kati ya hawa wanafunzi ambao tunawa-*grade* ambao tunawapa siku moja au mbili kuwa-assess na kubadilisha maisha yao, tunakuwa hatuwatendei haki na baadhi ya hawa wanafunzi katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Mndolwa atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim na Mheshimiwa Bobali ajiandae.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia machache katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Pili napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia na tatu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake pamoja na Naibu wake na pongezi nyingi ziende kwa Kamati ambayo imetoa maoni, naomba Serikali izingatie maoni hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na mpango wa elimu bure, lakini haikuwa na maandalizi ya kutosha. Wazazi na Taifa likahamasika kupeleka wanafunzi mashulenii, lakini katika shule zile madarasa na madawati ni machache. Serikali ikajitahidi kufanya harambee kwa taasisi mbalimbali pamoja na wadau kuleta madawati, lakini ilikuwa haifikirii kwamba yale madawati yanaenda kuwekwa wapi. Matokeo yake wanafunzi wakawa wengi kuliko madarasa yaliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta darasa moja kuna wanafunzi 100 mpaka 120 na natolea mfano hivi karibuni nilienda katika shule ya msingi Ungindoni iliyopo Kata ya Mjmwema, Wilaya ya Kigamboni, wanafunzi wanakaa zaidi ya 120 kiasi kwamba mwalimu anashindwa kumsaidia yule ambaye ni *slow learner* ili aweze kufaulu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa ijpange, isilaumu walimu kwamba hawafundishi ndiyo maana watoto wanafeli. Kuwaadhibu walimu kwa kufeli kwa watoto wetu kwa kweli wanawaonea. Kama Serikali ingekuwa ina-*provide incentives* zote kwa walimu, mishahara mizuri, mazingira mazuri ya kufundishia, nyumba bora na mishahara ya walimu inatakiwa iongezwe kwa kiwango cha juu ili walimu waweze kuvutiwa na fani hii. Tunaona tuna ukosefu mkubwa wa walimu kutokana na wengi hawapendi kujifunza fani hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke sote sisi tumepita kwa walimu, madaktari wamepita kwa walimu, wanasheria wamepita kwa walimu lakini walimu wamefanywa kuwa madaraja kwa taaluma nyingine, hatuwajali. Mheshimiwa Ndalichako mama yangu nakuomba sana, wewe umepitia kwa walimu mpaka

umekuwa Profesa, wasaidie walimu hawa katika kuboresha maslahi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai yao sasa hivi imekuwa kama ni wimbo wa Taifa maana yanaandikwa kwenye vitabu hayatekelezwi. Mimi naona sasa imekuwa mgomo baridi kwa wao kutojitunga ili kuleta ufaulu wa hali ya juu. Shule za *private* zinafaulisha kwa sababu utakuta mwalimu anatoka Serikalini anakwenda kufundisha *private* kwa sababu ya *incentive* anazopata, mshahara na mazingira mazuri, kwa nini Serikali haioni haja basi na sisi kuboresha mazingira ya walimu wetu katika shule hizi za Serikali? Kwa nini sisi ambao tumepitia kwa walimu tunadharau walimu wetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, nakuomba mama yangu umepitia kwa mwalimu mpaka umefikia hatua hii na angalia yule mwalimu uliyemuacha kule kijijini ulikosoma hali yake ilivyo. Nakuomba tuwaboreshi maslahi yao ili walimu hawa waweze kufanya kazi zao sawasawa ili kusaidia wanafunzi wetu kuweza kufaulu kwa kiwango cha juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea shule ya msingi Yombo Dovya iliyopo Kata ya Makangarawe, Wilaya ya Temeke, shule ile kwa kweli ni mtihani. Ina wanafunzi walemavu na wa kawaida, madarasa hayatoshi. Nimejitelea pale tani moja ya mifuko ya saruji na mabati 20 lakini pia hayakidhi mahitaji. Vyoo ni vichache, walimu wanangojea wanafunzi wakajiasaidie na wao waingie katika vyoo vilevile, ofisi za walimu hawana meza za kutosha, wanatumia madawati kama meza zao, huwezi kujua kama hili ni darasa au ni ofisi ya walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwajali walimu wetu, hii ndio *source* ya kushuka kwa elimu yetu. Tusiwaadhibu walimu wala shule zile kuzifungia, sisi Serikali ndio wenye matatizo. Serikali inatakiwa *ku-provide* kila kitu ili walimu waweze kufanya kazi kwa bidii na kujituma.

Nadhani tukifanya kila kitu wanafunzi wetu watafaulu kwa kiwango cha juu na hatuwezi kumtafuta mchawi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwafukuza walimu kwamba hawajafaulisha tunawaonea. Kuwasimamisha au kufungia shule kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe mimi siafiki, kwa sababu mwalimu hawezi kujenga darasa wala maabara, kwa nini unamuadhibu kwamba kasababisha wanafunzi wafeli. Inayotakiwa iadhibiwe ni Serikali ambayo haijaweka mazingira rafiki ya kufundishia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana pindi tutakapopitisha bajeti yako Mheshimiwa Waziri uwajali sana walimu ndio kila kitu, bila walimu sisi tusingefika hapa, bila walimu wewe Mheshimiwa Waziri usingekuwa Profesa.

Kwa hiyo, haya ya kujenga maabara, ukununue vitabu bila kumwezesha mwalimu huwezi kumlazimisha ng'ombe kunywa maji kama hataki kunywa maji. Utamwekea mazingira, lakini kama mshahara yake hujamboreshea, hujamwekea nyumba bora zenye umeme, anafanya andalio la somo na azimio la kazi kwenye giza hawezi kufanya kazi vizuri. Ndiyo maana wengi hawataki kukaa vijijini wanakimbilia mjini angalau kufanya biashara huku wanafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa tueleze una msimamo gani kwa walimu wetu wa Tanzania kuwaboreshea maslahi yao ambayo yataleta ufaulu wa juu kwa shule zetu. Kwa sababu ukisema uwafukuze walimu unawaonea, ufungie shule zile pia unazionea kwa sababu hawana uwezo. Hata wewe mshahara wako huwezi ukasema ukajenge maabara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ishauri Serikali na Rais walimu ndiyo kila kitu katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsanteni sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala*, kwa kunijalia uwezo huu wa kusimama hapa kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Baada ya shukrani hiyo, pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja kwenye vyuo vikuu. Kwenye nchi yetu kuna vyuo vikuu mbalimbali na kwenye vyuo vikuu hivi kuna wanafunzi ambao wanalipiwa na Bodi ya Mikopo, lakini pia kuna wanafunzi ambao hawakupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo wanagharamiwa na familia zao, familia za kimaskini na kinyonge. Leo kuna baadhi ya vyuo vikuu baada ya kumalizika mwaka wanabadilisha malipo yaani malipo yanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoilewa kwa ambavyo nilisoma mimi katika vyuo vikuu, mkataba ule unapobadilika kwa yule ambaye anaendelea mwaka mwingine unakuwa haumuathiri lakini kilichotokezea kwa baadhi ya vyuo vikuu ni kwamba wanapobadilisha mkataba mwanafunzi aliyeo mwaka wa pili na wa tatu pia mkataba ule unamuathiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, juzi nilikutana na wanafunzi wa *Zanzibar University*, kuna wanafunzi wanafanya *degree ya nursing* na walikuwa wanalipia kwa mwaka shilingi 2,197,000 kwa wale walioanza mwaka jana lakini mabadiliko yalipotokea mwaka huu uliopita wamepandishiwa kutoka shilingi 2,197,000 mpaka shilingi 2,486,000. Tumuangalie mwanafunzi huyu ambaye analipiwa na familia ya kinyonge, ataelekea wapi mzazi keshajipangia kwamba hana uwezo wa kuongeza shilingi 400,000 kwa mwaka za kumsaidia mtoto wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi wa diploma ambaye alikuwa analipa shilingi 1,500,000 sasa anatakiwa ali pe shilingi 1,900,000, athari hii ilitakiwa imu angalie yule ambaye anaanza sasa. Naomba Waziri atakapokuja kujumuisha atupe maelezo, vyuo kama hivi ambavyo vinapandisha *tuition fee* katika hali ambayo si ya kiutaratibu wanavichukulia hatua gani? Kwa sababu wanafunzi hawa tayari walishaanza na mkopo ambao unakubalika lakini wanapandishiwa mkopo ule katikati ya masomo, hilo ni la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala zima la upungufu wa walimu. Tunasema kwamba hakuna elimu bila ya walimu, kama hatuna walimu na elimu inakuwa haipo. Upungufu wa elimu uliopo katika nchi yetu ni mkubwa sana. Tukichukua *data* ya mwaka 2016/2017 na suala hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni illisema katika bajeti ya mwaka 2016 na ya 2017 na mara hii tunalizungumza tena kwamba upungufu wa walimu ni mkubwa sana. Kwa mfano, katika bajeti ya 2016/2017 kwa shule za msingi kulikuwa na upungufu kutoka walimu 191,772 mpaka kufikia walimu 179,291 ambapo hii ni sawa na asilimia 6.5. Ushukaji huu mkubwa wa idadi ya walimu umesababisha uwiano wa mwalimu mmoja kuweza kufundisha wanafunzi zaidi ya 50 mpaka kufikia 70. Tuangalie, hapa tutapata elimu bora au tutapata bora elimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waziri atakapokuja atueleze ni mkakati gani wameuandaa kwa sababu toka 2016 mpaka leo hakuna ajira ya walimu iliyofanywa. Hali kadhalika kuna walimu ambao wanastaafu katika kipindi chote hicho, kwa hiyo, ina maana kwamba bado idadi hii niliyoisema hapa inawezekana ikawa ni kubwa zaidi kufikia leo kwa sababu hii ni idadi ambayo ilikuwa imeoneshwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika shule za awali hali kadhalika upungufu nao ni mkubwa. Katika shule za awali alitakiwa *ratio* iwe ni 1:25 lakini *ratio* hiyo inakuwa ni 1:150. Hebu tuangalie, wanafunzi hawa wanaoanza sasa

tunawasomeshaje wanafunzi 150 kwa mwali muoja, matokeo yake yatakuwa ni yapi? Mtoto anatoka shule ya awali anarudi nyumbani, ukimuuiliza umefundishwa nini anakwambia kwamba nimefundishwa kukata (kuvuka) barabara. Hivi kweli ufanisi utakuwepo jamani? Mkakati unahitajika, Waziri atueleze ni mkakati gani pia wameuanda katika kutatua suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la maslahi ya walimu, madeni pamoja na kupandishwa madaraja. Jamani ni kitu cha aibu, tulisema kwamba tunafanya uhakiki ukikamilika tutapandisha walimu madaraja na tutalipa madeni. Kuna walimu tokea siku waliyopewa barua za kulipwa madeni yao ni mwaka mzima sasa hivi Halmashauri zimeshindwa kuwalipa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, watalipwa tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watanzania wote wana haki ya kushtaki ama kushtakiwa isipokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo linaloshangaza, mwanafunzi yupo kwenye kiwango cha elimu ya juu anafanya masomo yake ya *degree* ya *kwanza university* anashtakiwa, *prospectus* ya chuo yaani kanuni ya uongozaji wa chuo inazuia mwanafunzi yule asiendelee na masomo, ni jambo la kushangaza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya chuo kikuu ni *tertiary education* na tafsiri yake ni *third level education*, ni elimu ya ngazi ya tatu. Amepita elimu ya msingi, elimu ya sekondari, *university education level* ni elimu ya watu wazima.

Wanaosoma pale sio lazima wawe vijana, wengine ni watu wazima; wengine wanashakti na wengine wanashaktiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, jambo la mwanafunzi Abdul Nondo kuwa ameshtakiwa na chuo kikamsimamisha masomo, *it is contrary to human rights, very contrary*. Kama *prospectus* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inasema hivyo, *prospectus* ya namna hiyo haifai na sheria hiyo inapaswa ifutwe. Ni sheria isiyokwenda na wakati lakini pia inanyima na inazuia haki za binadamu lakini pia inakwenda kinyume na Katiba yetu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaoa fursa ya mtu kushtaki na kushtakiwa. Sasa hivi ni kweli wanafunzi wote waliopo vyuo vikuu aliyekuwa na kesi mahakamani ni Abdul Nondo peke yake? Hivi ni kweli? Kwa hiyo, kama sheria za chuo zinasema hivyo, sheria hii hebu ifuteni, inawatia aibu, vinginevyo mtuamble kwamba jambo hilli mmelichukulla kisasa.

## TAARIFA

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Bobali, kama alivyosema ni haki kushtaki au kushtakiwa na bila ya kupoteza nafasi yake, kwa sababu tunao Waheshimiwa Wabunge ambao wameshtakiwa mahakamani na wengine wamefungwa, lakini hawakupoteza nafasi zao. Inakuwaje mwanafunzi huyu ambaye kashtakiwa tena kwa makosa ya kubambikiziwa na kesi hajathibitishwa... (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unachangia, hutoi taarifa. Waheshimiwa Wabunge, toa taarifa tu, usichangie. (*Makof!*)

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na taarifa yake nimeipokea kwa msisitizo kabisa.

Jambo hili linakichafua Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tuseme ukweli, *to be sincerely*, hadhi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inashuka kwa sababu mnataka kuwaingiza kwenye siasa. Hata hapo *UDSM*tukifanya leo sensa ya wanafunzi wangapi wenyе kesi mahakamani hawatapungua hata wanafunzi 20, 30 lakini aliyeonekana mwenye makosa ni mmoja tu, *this is quite unfair. (Makof!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kama ingekuwa vyuo vikuu vinafanya mtihani wa pamoja kama ilivyokuwa elimu ya sekondari, vyuo vikuu vya Serikali vingekuwa vinashindwa kama ambavyo shule za sekondari za Serikali zinashindwa dhidi ya shule binafsi. Pamoja na mambo mengine yanayochangia ni hizi kanuni na sheria zilizopo kwenye vyuo, hizi *prospectus* za chuo Mheshimiwa Waziri jaribuni kuzipitia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambapo mimi nimesoma pale. Hivi unakwendaje kwenye chuo unakuta kuna mchepuo au fani wanafunzi wanasoma, chuo cha Serikali miaka mitatu wanahitim, wakienda Serikalini wanaambiwa hii haitambuliki, yaani chuo cha Serikali lakini mtu amehitim anaambiwa haitambuliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere watu wamesoma *faculties* zaidi ya tatu, lakini mwisho wa siku wanaambiwa hizi hazitambuliki. Sasa chuo cha Serikali inakuwaje wanasomesha kitu ambacho hakitambuliki? Jambo hili na lenyewe ni la aibu sana. Mheshimiwa Waziri nitakuja kukupa orodha ya hizo *faculties* ambazo wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wamezisoma, leo mtaani huko wakiomba ajira wanaambiwa kwamba hizi hazipo kwenye *system* ya *Lawson* na huwezi kuajiriwa, ni jambo la aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Mchinga lina shule nydingi za sekondari. Shule ya Sekondari ya Mchinga sasa ni kongwe inafanya vizuri sana, ni mionganoni mwa shule zinazofanya vizuri, tumeomba muipandishe hadhi iwe shule

ya *A-Level*. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri mwaka huu uje unithibitishie kwamba ile shule mtaitengea fedha. Shida yetu sisi ni mabweni tu, mkitupatia mabweni shule itapanda hadhi, ina walimu wa kutosha, ina walimu wengi wenye *degree*, ina wanafunzi wengi, lakini pia *catchment area* yake ina shule nyingi ambazo wanaweza wakai-feed shule ya sekondari Mchinga ikaweza kuwa shule ya *A-Level*/na ikaweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni jambo la kuhamisha walimu kuwatoa shule za sekondari kuwapeleka shule za msingi. Jambo hili sio bay a kwamba kama dhamira ni hiyo sio mbaya, tatizo ni namna linavyotekelawa. Leo mwalimu aliyesomea kufundisha wanafunzi wa sekondari anakwenda kupelekwa akafundishe wanafunzi wa darasa la kwanza, darasa la pili bila kumfanyia *orientation*, jambo hili haliwezi kuwa na tija. Walimu wenyewe wana *frustrations* za kutosha, *information* yenyewe hajatolewa vizuri, namna ilivyochukuliwa na Wakurugenzi kule chini Mkurugenzi huyu analitekeleza kivyake, Mkurugenzi mwingine anatekeleza kivyake, wengine wamepewa fedha ya uhamisho...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mheshimiwa Maftaha Nachuma atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Abdallah.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kunijalia afya njema. Pia nikushukuru wewe kuweza kunipa nafasi niweze kuchangia kwa dakika hizi tano kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaalam mmoja anaitwa Kunzi alisema mwaka 1988/1989 alipomaliza kuandika kitabu chake akasema kwamba *failure to plan is planning to fail*

(ukishindwa kupanga maana yake umepanga kufeli). Nilikuwa nasikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa, maneno yake mengi amezungumza, lakini sijaona hata mstari mmoja kwenye kitabu chake hiki ameeleza ana mkakati gani juu ya elimu ya watu wazima Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima taarifa ya Kamati imeeleza hapa kwamba wako vijana wengi, wapo Watanzania wengi sana hawajui kusoma na kuandika. Hawa wawekewe mkakati maalum, wapewe masomo maalum na watengewe bajeti kwenye Wizara hii. Elimu ya watu wazima imekufa, tunaomba sana Wizara mwaka huu iweze kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kugharamia elimu ya watu wazima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne ilinikuta mimi nikiwa mwalimu na nilikuwa *Headmaster* wa Mchinga Sekondari, shule ambayo Mheshimiwa Bobali kazungumza hapa, nimekaa pale kwa miaka mitano kama Mkuu wa Shule. Tulikuwa na mpango huu kwa muda mrefu sana wa kuipandisha hadhi ile shule iweze kuwa ni kidato cha tano na sita, miundombinu yote tulikamilisha, mimi naungana mkono na Mheshimiwa Bobali hii shule iweze kupanda kuwa ya kidato cha tano na sita. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilikuwa ni zuri sana ni suala la *BRN*, mpango ambao Serikali waliuiga kutoka Malaysia na kule Malaysia walikuwa wanaita *The Big Fast Result*. Serikali ya Awamu ya Nne ikasema tuige mpango huu wa kuinua kiwango cha elimu na sekta nyingine tano ili tuweze kuwa na matokeo makubwa. Mimi nashangaa sana kwamba hivi sasa huu mpango wa *BRN* (*Big Results Now*) wameuacha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ulikuwa una tija sana katika shule zetu za msingi na sekondari. Walimu walikuwa wanafanya kazi kwa bidii sana kwa sababu walikuwa wanaahidiwa kwamba somo lako wakifaulu wanafunzi kwa kiasi hiki utakuwa *motivated* kwa kiasi hiki cha pesa, kwa kiasi hiki cha *tourlakini* na mambo mengine.

Kuuondoa Mpango wa *Big Results Now* kwenye Wizara hii ya Elimu maana yake tunarudisha nyuma elimu yetu. Tunaomba sana Serikali irudi kwenye *BRN*, ilikuwa inafanya vizuri sana, ilikuwa inachochea sana elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwaka 2014, shule yangu ya Mchinga sekondari pale ilikuwa ni shule ya kwanza katika shule za Serikali, Kanda ya Kusini kuititia mpango huu wa *BRN*. Tuliweza kusimamia vizuri sana, tulipeleka vijana wengi, takribani 21 kwenda *form five* na *six*. Naomba sana mpango huu tuweze kuuresheja ili kuweza kurudisha morali katika shule zetu za sekondari na za msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili suala la uhaba wa madarasa. Ni kweli kabisa kwamba shule zetu zina *enrollment* kubwa sana, kutokana na Mpango wa Elimu Bure wanafunzi wengi wanaingia darasa la kwanza madarasa hayatoshi. Shule ya Msingi Mbae, Mtwara Mjini hii ni mara yangu ya tatu nazungumza hapa, ina wanafunzi zaidi ya 600, madarasa yaliyopo ni mawili pekee. Wanafunzi 600 madarasa mawili, ni jambo la ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ipeleke pesa Shule ya Msingi Mbae iliyopo Mtwara Mjini tuweze kujenga madarasa na vyoo, hata vyoo pale hakuna, naomba sana Wizara iangalie suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la upungufu wa walimu wa sayansi pia ni jambo muhimu sana. Nashauri kwamba vyuo vyetu ambavyo vilikuwa vinafundisha walimu wa masomo ya sayansi viwekewe msisitizo, vitengewe bajeti ya kutosha na walimu wafundishwe masomo ya sayansi sawasawa. Hivi sasa imekuwa walimu wengi wanakimbia kwa sababu hakuna *motivation*. Walimu wengi wa sayansi waliofundishwa na Serikali wanakwenda katika shule za *private* kwa sababu kule kuna malipo ya kutosha, *incentives* za kutosha, *motivation* ya kutosha, shule zetu za sekondari za Serikali zinakosa walimu wa sayansi kwa sababu hatuna vivutio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati fulani ilielezwa sana hii sera kwamba tunahitaji walimu wa sayansi waweze kubaki katika hizi shule za Serikali, tutawapa *motivation* maalum, lakini mpaka leo hakuna wanachopata cha ziada walimu wa sayansi katika shule zetu za Serikali. Tunaomba yale yanayozungumzwa yaweze kutekelezwa ili elimu yetu iweze kuwa kama maeneo mengine.

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, hebu subiri kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa, naomba nimpe taarifa mzungumzaji wa sasa, kwanza, nimeona anazungumza kwa busara sana, lakini nimeona kwa sababu jambo hili linajirudia sana la ulinganifu kati ya shule za binafsi na shule za Serikali. Ninachotaka kutoa taarifa ni kwamba kuititia Dira yetu ya Maendeleo ya 2025, sisi wenyewe kwa hiari yetu tuliamua kwamba sekta binafsi ndiyo itakuwa *engine* ya ukuaji wa uchumi wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, sekta binafsi kufanya vizuri siyo vibaya na Serikali inaendelea kufanya hivyo kwa sababu haiwezi kuiachia peke yake sekta binafsi kwa misingi kwamba elimu ni huduma, elimu ni jambo muhimu na ndiyo maana inaendelea kutoa elimu. Kwa misingi hiyo, tuone kwamba elimu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unachangia sasa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nikuongezee hilo tu Mheshimiwa kwa sababu unachangia vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha, endelea.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa yake naichua lakini ni kwa sababu *PPPtunayozungumza* Tanzania siyo kwenye elimu tu, tunazungumza kwenye sekta nyingi kuwe na ushirikiano huu sekta binafsi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze suala lingine kwamba elimu yetu wanafunzi wanaishia katika elimu ya juu. Tulitembelea baadhi ya Vyuo Vikuu Tanzania katika Kamati yetu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tumefika pale *MUCE* (*Mkwawa University College of Education*) kuna ujisadi mkubwa unaofanywa na watendaji ambao Serikali ama sisi Watanzania tumewapa dhamana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna jengo la maabara linajengwa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha.

Tunaendelea na kundi hili ni la dakika kumi, Mheshimiwa Hamida Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa George Lubeleje ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kusimamia masuala mbalimbali ya maendeleo yenye kuleta tija na kuboresha suala zima la elimu. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha taarifa yake ya mapato na matumizi katika kipindi hiki cha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa

kuwasilisha taarifa yao nzuri, taarifa ambayo imetoa maelezo mbalimbali ya kuishauri Serikali lakini wameona changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi hiki ambacho tunamaliza cha 2017/2018. Kwa hiyo, imeturahisishia sana kwa sababu kila Mbunge aliyesimama amezungumzia mambo ambayo tayari Kamati wameshayaona, imekuwa ni rahisi kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpetia taarifa hii ya Waziri, nimeona namna ambavyo Serikali imepiga hatua kwa namna mbalimbali kwa lengo la kutaka kuleta tija katika suala zima la kuleta mabadiliko makubwa sana upande huu wa elimu, lakini kuwafanya vijana wetu waingie katika mfumo huu wa sekta ya viwanda. Katika kipindi hiki cha bajeti tunayoimaliza, Wizara ilijitahidi sana katika kuboresha vyuo vikongwe na mimi kama Mbunge wa Mkoa wa Lindi nillzungumzia sana Chuo cha Ualimu Nachingwea (*TTC Nachingwea*) kwa sababu chuo kile ni kikongwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu alisikia kilio chetu na napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, dada yangu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, kwa kweli amesikiliza kilio chetu na kwa bahati njema aliweza kututengea fedha, ametupatia shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Ualimu Nachingwea.

Kwa hiyo, hizo ni jitihada kubwa sana ambazo Serikali yetu inazifanya za kutaka kukiimarisha Chuo cha Ualimu cha Nachingwea ili kiendelee kuleta tija na kuzalisha walimu kwa sababu bado changamoto kubwa ya walimu tunayo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiki, lakini nimeona ambavyo Serikali inaweza kuboresha elimu kwa upande sekondari. Labda nizungumzie katika Mkoa wangu wa Lindi ambapo tuna Shule ya Lindi Sekondari, shule hii ni kongwe, ilijengwa na wakoloni toka mwaka 1959 lakini ilikabidhiwa Serikalini mwaka 1963.

## TAARIFA

**MHE.CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu nina-*manage* muda hapa.

**MHE.CECIL D. MWAMBE:** Ndiyo, kuna taarifa sasa.

**MWENYEKITI:** Hizi taarifa zinasumbua sana, kwa kifupi tu Mheshimiwa.

**MHE.CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiki, ndiyo, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Hamida kwamba tatizo la ufaulu mdogo na utoro wa wanafunzi shulenii Mkoa wa Lindi inasababishwa pia na watoto wetu kule kupata mimba za mapema, lakini kuna Wabunge wenzetu wanaotokea Mkoa wa Lindi wanasema watoto hawa wakishapata mimba wasirudi shulenii. Sasa sijui yeeye msimamo wake ni nini kwenye jambo hill? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ndiyo haya mimi sipendi kabisa, hiyo siyo taarifa unataka akupe maoni yake, Mheshimiwa endelea.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiki, namwomba Mheshimiwa Mwambe asinipotezee muda wangu na hiyo taarifa yake ni ya kwake mwenyewe, sina *time nayo* kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Shule ya Lindi Sekondari ni kongwe na naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ili shule hii iingizwe katika mpango wa ukarabati wa shule kongwe kwa sababu ni shule ya muda mrefu, tumeirithi kutoka mikononi mwa wakoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka 2016 shule hi imepata ajali ya moto kutokana na hitalifu ya umeme na imeathirika vibaya mno. Katika madarasa 28, 18 yameathirika

vibaya sana lakini bado kuna matundu ya vyoo 24 nayo yameathika na shule hii ina wanafunzi zaidi ya 900. Kwa hiyo, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameungana na wananchi wa Mkoa wa Lindi katika kufanya *harambee* na kuhakikisha shule hii inajengwa. Pamoja na jitihada hizo kubwa tulizozifanya bado tuko nyuma kabisa katika kufanikisha ujenzi wa shule hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa sababu shule hii ina *four one, form four, form five* na *form six* na watoto wanaosoma *form five* na *form six* ni watoto wa Tanzania nzima na si watoto wa Lindi peke yake na hii shule ni ya Serikali. Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali kutia mkono wake kuhakisha wanatuunga mkono ili shule hii iweze kujengwa na watoto warudi katika mazingira safi na salama ili waweze kupata elimu bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mawaziri ambao wametembelea mkoani kwetu Lindi na kila Waziri aliyejita alikuja kutoa pole katika eneo la shule ile. Lakini cha kusikitisha, wageni hao wote waliokuja wametoa pole ya mdomo tu na kutuahidi kwamba tutasimamia suala hili na shule itajengwa. Kwa kweli mimi nasikitika sana imekuwa kama ni sehemu ya utalii wageni kuja kutembelea pale, lakini bado katika ujenzi wameendelea kutuachia wananchi wa Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iweze kusimamia na kuweza kutuunga mkono katika kuhakikisha shule hii inajengwa kwa sababu ilikuwa ni shule tu ya kawaida lakini sasa hivi baada ya kuungua moto viongozi walishauri kwamba tujenge shule ya jengo la ghorofa. Mahitaji ya ghorofa ni shilingi 2,200,000,000; lakini pamoja na kuwa tumefanya *harambee* tumepata shilingi 700,000,000 tu. Sasa shilingi 700,000,000 kujenga jengo la shilingi 2,200,000,000 kwa kutumia *harambee* tutafika miaka 15 jengo lile halijakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba kwa dhati kabisa Serikali yangu itutazame kwa jicho la huruma, itusaidie kutuunga mkono kuhakikisha Shule ya Lindi Sekondari inajengwa ili watoto wapate mahali pazuri pa kukaa na kupata masomo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali na natumaini kabisa Mheshimiwa Profesa Ndalichako atasikiliza kilio chetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu katika Mkoa wetu wa Lindi tunafanya vibaya sana. Katika shule ambayo inakuwa ya mwisho Mkoa wa Lindi tunaongoza, tunaweza kuwa wa pili mwishoni, wa kwanza mwishoni lakini kuna mambo mbalimbali yanachangia elimu kushuka katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Lindi tuna shule za sekondari za Serikali 113 lakini asilimia 60 ya shule hizi hazina walimu wa hesabu wala masomo ya sayansi. Sasa ukitilinganisha sisi na shule zingine ambazo zimekamilika, zina maabara za kutosha na vifaa vya kutosha, zina walimu wa hesabu na sayansi, hivi kweli sisi tutakuwa wa kwanza au wa pili au hata kumi bora tutaingia, hata 20 hatuwezi, hata tukaishi kwa miaka 100 kwa *style* hii hatuwezi kufika.

Kwa hiyo, bado tunaendelea kuleta kilio chetu kwa Serikali kuhakikisha mnatupatia walimu wa hesabu na sayansi ili watoto wetu wa Mikoa hii ya Kusini ya Lindi na Mtwara waweze kupata masomo haya ya hesabu na sayansi ili tuweze kulingana na wanafunzi wa maeneo mengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Mkoa wa Lindi ni mkoa ambao umesahaulika, tunaitwa mikoa ambayo imesahaulika, ni mikoa maskini, mikoa ambayo iko pembezoni. Kwa hiyo, Mkoa wa Lindi ni mojawapo ya mikoa hiyo lakini Serikali ilituambia kwamba bajeti hizi zitazingatia mikoa ile ambayo iko pembezoni mwa mji. Tunaiomba Serikali iutazame Mkoa wa Lindi ukizingatia kwamba ni mkoa ambao umesahaulika. Kwa hiyo, tuna matumaini makubwa sana kuona kwamba Serikali inatubeba kwa nguvu zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia ukurasa wa 26, umeelezea masuala mazima ya elimu na ufundi stadi. Mimi naipongeza sana Serikali kwa sababu sasa imeonesha kwamba inataka kuendeleza ujenzi wa Vyuo hivi vya Ufundu Stadi katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu pamoja na maeneo mengine Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkao wa Lindi tumebahati kupa Chuo cha VETA na kipindi kilichopita nilizungumzia chuo hiki kwamba kina changamoto mbalimbali ikiwemo miundombinu ya majitaka, lakini bado mpaka leo tatizo hili lipo linaendelea. Pia Chuo kile cha VETA hakina mabweni na tunategemea wanafunzi kutoka Wilaya za Mkao wa Lindi wapate mafunzo pale wale ambao hawakubahati kuendelea na masomo, lakini wazazi wanashindwa kwa sababu mazingira ya kuishi mzazi anapanga nyumba. Leo mzazi ampangie nyumba mtoto wa kike, hivi kweli tunamtakia kheri mtoto huyu wa kike akae kwenye nyumba ya kupanga peke yake, hana mtu wa kumtazama na gharama za chakula mzazi agharamie? Kwa hiyo, inakuwa ni mzigo mzito na kusababisha baadhi ya Wilaya za Mkao wa Lindi wanashindwa kumudu kuwaleta watoto wao pale...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na momi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa kweli wanajitahidi, tunawaona wanakimbiakimbia, mara wako Njombe, Bukoba, Arusha kuangalia miundombinu mbalimbali ya shule na kuhakikisha kwamba watoto wa Kitanzania wanapata elimu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni fundi na fundi niliyesoma kutoka shule ya sekondari ya ufundi na nikaenda chuo cha ufundi. Sasa hivi tunazungumza Tanzania ya viwanda lakini Tanzania hii ya viwanda tunayoizungumza kama vijana wetu wasipopata elimu ya ufundi ina maana kwamba vijana hawa wa Kitanzania watakuwa watumwa ndani ya nchi yao kwa sababu hawatakuwa na ujuzi wowote wa kufanya kazi katika viwanda hivyo ambapo wote tunasema tunaiendea Tanzania ya viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ndiyo yenye jukumu la kutoa elimu na maarifa kwa Watanzania iache kufikiria kwamba ili kutoa elimu ya ufundi ni lazima tuwe na karakana kubwa sana, mashine kubwa sana, mitambo inayoendana na mitambo ya viwanda, hapana. Sisi wakati ule tunasoma ufundi tulisoma ufundi katika nyenzo ambazo zilituwezeshe kuwa mafundi mpaka leo tunafanya kazi hizo za ufundi na tunajivunia ufundi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako nikuambie humu ndani kuna mafundi sita ambao tumesoma na tunaujua ufundi vizuri na tunafanya kazi ya ufunzi vizuri kabisa. Uwekezaji kwenye ufundi kwa *level* ya sekondari ni kiasi kidogo sana, unaweza ukawa na shilingi 500,000 ukaanzisha fani ya ufundi sekondari. Kwa mfano, ufundi wa kujenga unahitaji kuwa na pimamaji, ndiyo kifaa cha ghamrama kuliko vifaa vyote, pimamaji moja ni shilingi ngapi? Chukulia shule ya sekondari inahitaji pimamaji kumi, unahitaji kamba ya kunyooshea ukuta, ubao, mwiko na konobao, hapo tayari fani ya ufundi kwa maana ya *practical/imekamilika*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unahitaji kitabu cha ufundi kwa maana ya *theory* na kitabu cha ufundi kwa maana ya

michoro. Kwenye *theory* unahitaji ubadilishe masomo mawili tu, ubadilishe somo la *physics* liwe *engineering science*, lakini uondoe somo la *biology* uingize somo la somo la urasimu ama ufundi wenyewe. Kwa hiyo, ni rahisi sana kuweka ufundi sekondari kuliko kujenga Vyuo vya *VETA*. Leo hii kila mtu hapa analia ajengewe Chuo cha *VETA*, tutajenga Vyuo vya *VETA* mpaka lini ili tuweze kuendana na kasi ya ufundi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu tuanzishe shule za sekondari za ufundi na si lazima kwenye shule ya sekondari ya ufundi tuanzishe fani sita au saba, tuanzishe shule moja, fani moja. Tunachukua shule moja tunaanzisha fani ya ujenzi, tunakwenda shule nyingine tunaanzisha fani ya umeme, shule nyingine tunaanzisha fani ya useremala, tunakwenda shule nyingine ya sekondari hivyo hivyo. Kwa hiyo, utakuja kuona jimbo zima ama nchi nzima sasa tunakuwa na shule nyingi za ufundi ambazo vijana wanapata maarifa na wakitoka pale wanakuwa tayari wanaanza kujitegemea. Tukisema tusubiri tuenze kujenga *VETA*, hela zenyewe sijui tunaomba wapi, wanaotupatia hela wana masharti, mpige magoti, mfumbe na macho, muombe na kuomba ndiyo hela zije, lini, tunachelewa, tufundishe ufundi vijana tujikomboe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wakisoma ufundi itawasaidia sana. Nataka niwaambieni wanaosoma ufundi sekondari wanakuwa ni mafundi wazuri kuliko mfano wake. Ufundi wa umeme unahitaji chini ya shilingi 500,000 kuanzisha umeme shulenii. Unahitaji bisibisi, koleo, kipande cha waya na kipande cha ubao, biashara imekwisha, huyo ni fundi. Hata akienda *university* atatumia vifaa hivyo hivyo kujifunza umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimwa Profesa Ndlichako hebu toa maamuzi angalau kila Halmashauri ianzishe shule moja ya ufundi kwa fani moja kama jaribio ili tuone tunakwendaje. Baada ya hapo tutafanya maamuzi kila Halmashauri iwe na shule ngapi za ufundi kadri watakavyoona mazingira, lakini kwenye maeneo yale ya wafugaji anzisheni mafunzo ya mifugo huko

sekondari, watu wajifunze ufundi lakini kuititia fani za mifugo, sehemu za wavuvi wajifunze uvuvi sekondari kitaalum ili kusudi vijana hawa wakitoka hapo sekondari wawe tayari wana elimu ya kutosha kuliko kusubiri hizo *VETA* ambazo tunajua kwamba ni ngumu sana kuzijenga. Karakana zinazojengwa ni gharama sana, tunahangaika kujenga mabweni na kachalika, shule za kata zipo tuanzishe ufundi kwenye shule za kata angalau kila halmashauri au kila jimbo shule moja ya ufundi kadri watakavyoona mazingira yanaruhusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulishauri Serikali uko mkanganyiko ambao nauona katika ya *NECTA* na *NACTE*. *NACTE* wanasi mamia mitihani ya ufundi katika vyuo vya kati, lakini *NECTA* wanasi mamia mitihani ya shule ya msingi, sekondari na mitihani ya ualimu. *NACTE* imeanzishwa kwa sheria ambayo imeipa nguvu ya kusimamia vyuo vyote vya kati; vyuo vya majeshi, vya afya, vya mifugo, vya madini, lakini jambo la kushangaza kozi ya ualimu wa elimu ya msingi imekwenda *NECTA*, lakini imerudishwa *NACTE* kwa hoja kwamba ule mfumo ambao *NECTA* wanautumia kudahili na kutoa mitihani si mfumo ambao unawenza ukamjenga mwalimu kuja kuwa mwalimu bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema huu ni mkanganyiko, kama Wizara ya Elimu ndiyo iliyosimamia kuanzisha kwa *NECTA* na ikaagiza kwamba sheria ile iliyotungwa vyuo vyote vya kati viwe chini ya *NECTA* halafu yenye Wizara ya Elimu imeamua kujipendelea kuchomoa kozi moja tu ya ualimu wa *primary* na kubaki nayo kule kusema kwamba hii tunabaki nayo sisi. Wakati huo huo inaongezea masharti mengine kwamba chuo chochote kinachofundisha ualimu kisiwe na kozi nyngine hapo mahali yaani hawa watu wanaojifunza ualimu wakae wao tu kama walimu wasiwe na mtu mwengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani hii dunia ni pana, tunapowaweka wale walimu wakae hivyo tunamaanisha nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kozi ile ya walimu irudishwe *NACTE* na waisimamie na walishaweka mifumo mizuri ya kuhakikisha kwamba hata mwalimu wa *primary* ambaye yupo kazini arudi apate elimu zaidi na aweze kuendelea kielimu. Kwa sababu kozi ile ya *grade A* ilikuwa ni kozi ambayo mwalimu akisoma si sifa ya kuendelea na masomo yoyote anabaki pale miaka yote, lakini ukiangalia kwenye Sera mpya ya Elimu inataka walimu waliojiendeleza na waweze kuendelea zaidi.

Kwa hiyo, naomba sana Wizara muangalie muwape nafasi hiyo *NACTE* waendelee na mafunzo ya ualimu. Najua mlisema kwamba mniamashaka na ile mitaala na kadhalika lakini naomba basi hayo mashaka muwe mnayaondoa haraka, kama mnaona mashaka hayaondoki haraka basi tuwatafute na waombezi wawaombee ili kusudi mashaka yenu haya yaondoke haraka ili kazi iende. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nalionia nalo ni muhimu sana nilichangie hapa ni kuanzishwa kwa chombo huru cha kusimamia elimu. Tunasema kwamba chombo hiki kitasaidia sana kupata elimu vizuri katika nchi yetu, kitasimamia kwa haki na kitahakikisha kwamba kila mmoja anayehusika na elimu anaafuata utarabu. Unaona kabisa kwamba kwenye taasisi au Wizara nydingine kuna vyombo kama *OSHA, EWURA*, hizi ni *regulatory bodies*. Kwa hiyo, sisi elimu tuwe nayo basi kusudi elimu yetu sasa isiguswe na mtu, asitoke mtu alikotoka akasema hiki kiwe hivi, hiki kiwe hivi, ikae hivyo na isimamiwe hivyo naomba sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala Sera ya Elimu ya mwaka 2014, suala hili leo hii ndiyo linaleta mkanganyiko. Sera mpya ya Elimu imeanza kutumika na watoto walioanza kutumia sera hii mpya leo wako darasa la nne. Niungane na Mheshimiwa Bulembo aliyesema kwamba hivi itakuwaje, tunaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utuambie kwamba watoto hawa waliopo darasa la nne leo watafika darasa la sita ama wataishia darasa la saba ili kusudi hata wazazi huko mitaani tuwajenge kisaikolojia wawe wanajua

nini kitafanyika. Sera hii ya Elimu pamoja na kuizindua wakati ilipozinduliwa maandalizi yalikuwa bado, ndio maana leo unaweza ukakuta sera ipo haina sheria, sera ipo haina kanuni, matokeo yake linaweza likatokea kundi lisilojulikana likaja likaipeleka Serikali Mahakamani kupinga sera hii na mkashindwa hata kujitetea kwa nini mnatoa elimu kwa kutumia sera hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana tufuate utaratibu wa sera, leteni sheria Bungeni, sheria ipitishwe wekeni na kanuni zake kusudi sera hii ikae vizuri. Vilevile andaeni vitabu na mviweke katika msingi kwamba zinafuata sera hiyo kuliko sasa tunaambia vitabu vya darasa la nne havipona wakati mwingine mnaambiwa mtaala upo lakini vitabu hakuna, mafunzo kwa walimu hakuna kwa sababu sera hii tumeiendea haraka mno. Kama tumeiendea haraka tujitahidi kwa sababu watoto sasa wako darasa la nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ufaulu. Ni kweli ufaulu unasikitisha, *ni-declare interest* kwamba mimi ni mmiliki wa shule, lakini ufaulu katika shule za umma unasikitisha. Kinachosikitisha si kingine si kwamba hakuna walimu, bali mazingira siyo mazuri Serikali iijtahidi kuweka mazingira mazuri. Hata kama unapata majibu rahisi, ukikutana na watendaji wa Serikali wanakwambia nyie *private* si mnachuja, huwezi kuchuja darasa zima lakini Serikali una uwezo wa kuchuja, una shule za vipaji Ilboro, Mzumbe, zipo zile shule na mmekuwa mkipeleka hao mnaowachuja vilevile. Kwa hiyo, mimi nafikiri Serikali iandae mazingira mazuri ili kusudi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja na

nawatachia kila la kheri Wizara ya Elimu wafanye kazi vizuri.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Lubeleje atafuatiwa kama nilivyosema na Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Fatma ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Wizara hii ya Elimu.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii pamoja na walimu wote wa shule za msingi pamoja na shule za sekondari, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, lakini hawana nyumba.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata mradi wa MMEM tumejenga madarasa, tukasahau nyumba za walimu, tumepata mradi wa MMES tumejenga madarasa, tunesahau nyumba za walimu. Kwa hiyo, walimu wanaishi katika mazingira magumu sana na ndiyo maana elimu inashuka. Tusilaumu walimu kwamba kwa nini elimu inashuka ni kwa sababu ya mazingira wanayoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni ukarabati wa vyuo na shule za sekondari kongwe. Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana, Chuo cha Ualimu Mpwapwa kimekarabatiwa vizuri sana pamoja na Shule ya Sekondari ya Mpwapwa ambayo ilianzishwa mwaka 1926. Hata hivyo, kwa nini mnakarabati vyuo na shule za sekondari, nyumba za walimu hamkarabati? Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri umefika Mpwapwa mara nyingi sana wakati wa ukarabati wa chuo cha ualimu. Ukipika Kijiji cha Mwanakianga angalia kushoto nyumba za walimu zina hali mbaya sana, nyingine zimejengwa mwaka 1926. Kwa nini hatuna huruma na hawa walimu wetu jamanii? Nyumba imechakaa mtu anaishi katika mazingira magumu sana. Pangeni fungu mkarabati nyumba za walimu wa sekondari pamoja na walimu wa Chuo cha Ualimu Mpwapwa. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu elimu bure. Kwa kweli wananchi wanashukuru sana likiwemo Jimbo langu la Mpwapwa na Wilaya ya Mpwapwa kwa ujumla. Hata hiyo, elimu bure ni kutoka darasa la kwanza mpaka kidato cha nne lakini kidato cha tano na cha sita wameachwa. Mheshimiwa Waziri hawa wote ni wako, hiyo shule ina *form one* mpaka *form six*, wengine wamesamehewa wengine hawakusamehewa, wanajisikiaje wale wanafunzi? Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hawa nao muwasamehe, ni watoto wa Serikali moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa shule huko huko kuhusu chakula wanachopata wanafunzi wa bweni cha shilingi 1,500 kwa siku. Hivi kweli Mheshimiwa Waziri upewe shilingi 1,500 unywe chai asubuhi, chakula cha mchana na chakula cha jioni itatosha? Kwa nini tunawaweka katika mazingira magumu sana wanafunzi wetu? Mimi nashauri tuongeze hii posho ya chakula angalau wapate shilingi 2000 inaweza kusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni maslahi ya walimu. Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini kila Wilaya walimu wanadai maslahi yao ya likizo, mishahara na wengine wamepandishwa vyeo. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri shughulikia maslahi ya walimu wetu. Walimu wakidai posho zao muwalipe mapema. Mtu anatoka kijijini anakuja mjini kwa *DEO*, anakaa pale wiki nzima anaafuatilia maslahi yake. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, hawa walimu lazima tuwaheshimu, hakuna mtu ambaye hakupitia darasani hapa, lazima tuwape heshima yao walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini nimuombe sana Mheshimiwa Waziri pangeni bajeti maalum kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu. Wananchi wamejenga shule za msingi, shule za sekondari na sasa Serikali imeanzisha kidato cha tano na cha sita katika baadhi ya shule, mfano, katika Wilaya ya Mpwapwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mazae na Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Berege, lakini hakuna

nyumba za walimu wala *hostel*, wanafunzi hawa wa *form five* na *six* wanalala madarasani. Naomba sana Mheshimiwa Waziri tuwaonee huruma wananchi wamefanya kazi kubwa sana. Shule zote za msingi na sekondari madarasa yote wamejenga wenyewe, tuwaonee huruma na Serikali nayo iweke mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nikushukuru na naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na pongezi. Pongezi hizi nazipeleka kwa Mheshimiwa Raís kwa kauli yake ya kuhakikisha kwamba elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Tumeona mafanikio makubwa ya watoto ambao walikuwa wamekaa majumbani wanashindwa kwenda kuandikishwa kwa sababu ya fedha ambazo zilikuwa zinatakiwa shulenii. Baada ya tangazo la elimu bure sote tumeshuhudia mafuriko ya watoto waliokwenda kujilandikisha. Wapo wanaobeza kaulimbiu hii ya elimu bure wakifananisha na kwamba Serikali haikujiandaa, lakini nataka kupongeza kwa sababu Mheshimiwa wewe ulikuwepo tulipoanzisha shule za sekondari za kata, angalia sasa hivi ukienda kwenye vyuo vikuu vyetu watoto wa shule za sekondari za kata ndiyo waliojaza vyuo vikuu vyetu hapa nchini, hayo ni mafanikio makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kufanikiwa ni lazima uamue na uthubutu ili uanze. Changamoto zinazojitokeza ndiyo mafanikio yenyewe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba nikupe moyo, kazi ni nzuri, tuendelee, tuwachukue

watoto wote, asiachwe mtu nyuma eti kwa kisingizo kwamba elimu bure inawajaza watoto bila huduma kwa sababu Serikali haikujiandaa. Serikali mmejilandaa na wananchi wamejilandaa, nimeshuhudia kwenye Mkoa wangu wa Singida, nipende kuwapongeza Wabunge wote wa Majimbo ya Mkoa wa Singida wamejitahidi sana na Madiwani wote wa Mkoa wa Singida wameweza kusimamia ujenzi wa kuongeza madarasa ya wanafunzi hawa walioongezeka na watoto wako madarasani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi upande wa shule za kata nimeshapongeza na watoto sasa hivi wako vyuoni wanaendelea na masomo isipokuwa naomba niishauri Serikali kuanzishwa kwa shule maalum kwa ajili ya masomo ya sayansi. Hatuwezi tukazifanya shule zote zikawa na masomo ya sayansi kutokana na upungufu wa walimu tullionao. Kwa hiyo, cha msingi ni kuanzisha shule maalum ili walimu wale wapelekwe kwenye hizo shule ambazo tutakuwa tumezianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie suala la mikopo ya elimu ya juu. Mheshimiwa Waziri amezungumzia ni namna gani wanafunzi ambao wamebainika ni wadaiwa sugu takribani 147,000 na ukasema 42,000 ndiyo wameonesha nia ya kutaka kuchangia, sasa mimi naomba niulize, hawa wengine 103,000 au 100,000 wako wapi? Je, wana ajira ya kuweza kulipa? Kama hawana Serikali inaweka mkakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwamba wanafunzi wetu hawa tunaowakopesha wanapomaliza elimu ya juu tujitahidi wapate ajira, tuwasaidie ili waweze kurudisha mikopo yetu kwa sababu wakibaki mitaani watashindwa kurudisha mikopo yetu. Pamoja na kwamba watatakiwa wakidhi vigezo, lakini bado wanafunzi hawa watambulike hata kwenye Halmashauri zetu kwa sababu kuna mikakati ya ule Mfuko wa Vijana, Wanawake na Walemavu wanaweza wakawezeshwa kwa sababu tunasema uchumi wa viwanda, wawezeshwe waweze kujajiri wenyewe, Serikali iwafuatilie, isiwaache hivi

hivi, iwasaidie ama waajiriwe ama waweze kujajiri wenyewe.  
*(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo nilisimama siku moja hapa nikaomba mwongozo kwamba wanafunzi wanapo-*qualify* kupata mkopo iwe ni nusu au asilimia 100 cha kushangaza wanapofika vyuoni wanaumbuliwa sana. Inatakiwa walipe wanasema *advance payment* ambayo inawasumbua sana watoto wetu. Kumbuka watoto wengi wanaotaka mikopo ni watoto wa wakulima wetu, waliosoma shule hizi za kata, baba auze nyanya, mahindi au asubiri auze alizeti kwa mfano kule Singida au vitunguu, unakuta zile fedha hazitoshi, anapofika kule anateseka.

Mimi nina watoto ambao walifika mpaka vyuoni leo hii wamerudi kwa sababu walishindwa kulipa ile *advance payment* ya shillingi 600,000. Naomba jambo hilli Mheshimiwa Waziri utakaposimama hapo utufafanulie umelichukuliaje na Serikali inasemaje ili tuwanusuru watoto wetu hawa ambao wanakwenda kuteseka, itawakatisha tamaa wengine.  
*(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba nimpongeze sana Profesa Kikula, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, wakati tunakwenda kukagua maeneo ya kaunzishwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, tulipofika kule kwanza magari yetu yalikuwa hayawezi hata kupita wakati tunaukagua ule mlima, tukasema hivi ni nani atakayekabidhiwa kuja kusimamia chuo hiki ili kitambulike na kiwe chuo bora? Tunamshukuru Rais wa Awamu ya Nne alimteua Profesa Kikula, wakatafuta pesa, Serikali ikakijenga kile chuo ambacho sasa hivi tunajivunia kwamba ni chuo kikuu ambacho kinachukua wanafunzi wengi sana.

Mheshimiwa Waziri mimi sifahamu wewe kwenye Wizara yako, huyu Profesa angepata *award* kwa sababu aliweza kusimamia vizuri sana pamoja na changamoto zote ambazo zilikuwa zinajitokeza pale, amesimamia vizuri sana. Hakuna ubadhirifu wa pesa, kwa hiyo, mimi kwa kweli nimeona leo nimpongeze Profesa Kikula. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye upande wa shule za kata bado kuna changamoto kubwa sana kwa watoto wetu wa kike. Watoto wetu wa kike wanakaa mbali, wanapopangiwa kwenye zile shule wanakwenda kupanga kwenye nyumba za watu wanapata changamoto kubwa sana ya masomo. Wengine wanashindwa kuendelea na masomo kwa sababu wanakatishwa tamaa, miluzi ni mingi sana kwa watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali hii ianze kumjali mtoto wa kike, zijengwe *hostel* kwa ajili ya kumhifadhi mtoto wa kike. Sikatai kwamba na mtoto wa kiume anapaswa alindwe, lakini bado kwa mtoto wa kike hali ni ngumu sana, anasoma kwenye mazingira magumu sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana uangalie suala la *hostel* za watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuna suala la vyoo mashulen. Tumeendumia watoto wa kike wamekuwa wakiadhirika sana kwa sababu shule nyingi bado hazina vyoo vya kutosha na fedha ziko kwako siyo TAMISEMI. Kwa hiyo, naomba sana fedha zitolewe kwenye shule kwa wingi kwa ajili ya kujenga hivi vyoo lakini ramani ile ya vyoo lazima iwe na choo kinachoweza kumsitiri mtoto wa kike anapokuwa kwenye siku za maumbile ya mtoto wa kike ili aweze kusitirika kwa sababu walio wengi wanakata tamaa hata kwenda shuleni. Akishapitwa ile wiki moja anapokuja wiki ya pili kwa kweli anakuwa amenyong'onyea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, *aluta continua*, tuko pamoja Mheshimiwa Rais, kaza buti, tafuta pesa, tunajua unatafuta pesa ili shule zetu ziweze kuwa za *standard*, tupate walimu wa kutosha lakini zile shule pia hebu zipekelewe visima vya maji ili kuwe na maji ya kutosha kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mlata kwa mchango wako. Tunaendelea na mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hii hoja iliyo mbele yetu ambayo ni hotuba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze zaidi kwenye udhibiti wa ubora wa elimu. Nikianzia ukurasa wa 63 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amebainisha kwamba Wizara imeandaa michoro kwa ajili ya kujenga ofisi 50 za Wadhibiti wa Ubora wa elimu. Naomba tu niishauri Serikali kwamba iharakishe ujenzi wa Ofisi hizi za Wadhibiti Ubora wa Elimu na ikiwezekana basi kwa kuwa Dodoma ni makao makuu na kwenye kitabu chake hiki hakubainisha kwamba ni Wilaya zipi ambazo zitajengewa, basi angetupa kipaumbele sisi Mkoa wa Dodoma kujengewa ofisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili elimu iwe bora zaidi naamini kabisa masuala ya utendaji wa kazi kwa ajili ya hawa wenzetu wa udhibiti ubora wa elimu yanatakiwa yawe mazuri sana. Katika maeneo mengi ya nchi hii, Wadhibiti wa Ubora wa Elimu hawana kabisa ofisi za kutosha na kama zipo, zipo chache, lakini nyangi ya ofisi hizi ziko katika majengo ambayo ni au yamekodishwa au vipi, kwa hiyo, inawaletea kadhia sana wenzetu hawa. Nikichukulia kwa mfano katika Mkoa wa Dodoma kuna zile Wilaya mpya ambazo zimeanzishwa, katika Wilaya hizi zote hakuna ofisi za Wadhibiti wa Ubora wa Elimu. Kwa hiyo, naomba tu nisisitize juu ya umuhimu wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, hawa wenzetu wa Wadhibiti wa Ubora wa Elimu pia nyumba hawana. Sambamba na nyumba lakini pia suala la vitendea kazi, wanahitaji vitendea kazi ili kusudi waweze kutoa taarifa muhimu wanapokuwa wanakwenda kukagua hizi shule. Kwa hiyo, niitie shime Serikali kwamba lazima vitendea kazi

vipatikane ili hawa Wadhibiti wa Ubora wa Elimu waweze kuleta mrejesho wanapokuwa wamekwenda kukagua katika hizi shule basi zile shule ambazo zinakaguliwa ziweze kujua wapi zinatakiwa zijirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye suala la usafiri katika hizi Ofisi za Udhibiti wa Ubora wa Elimu. Naipongeza Serikali wametoa magari katika baadhi ya hizi Ofisi za Udhibiti wa Ubora wa Elimu lakini tatizo liko kwenye madereva. Bado madereva hawajaajiriwa kwa wingi, utakuta kwamba kuna baadhi ya ofisi inabidi waazime madereva kutoka idara nyingine. Inapotokea kwamba madereva hawa wakaazimwa na yule anajua kabisa kwamba ameazimwa, haoni ni muhimu kuitunza gari ile.

Kwa hiyo, kama imeshindikana basi kuwaajiri hawa madereva, Wizara ione utaratibu itawezaje kufanya itoe kibali maalum ili kusudi kuweza kuwapatia wale Maafisa Udhibiti wa Ubora wa Elimu waweze kuyaendesha wao wenyewe yale magari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kuhusu suala la *OC*. *OC* kwenye Ofisi za Udhibiti wa Ubora wa Elimu kwa kweli imekuwa ni tatizo na hivi ninavyozungumza hata *OCya* kuanzia mwezi Januari mpaka hii leo bado hazijapatikana. Tumekuwa tukisema kwamba tunataka elimu iboreshwe, itaboreshwaje ikiwa hawa ndugu zetu ambao wanafanya udhibiti wa ubora wa elimu inakuwa ni mtihani kwao kupata *OC*? Kwa kweli naomba Wizara ilione hili jambo ili kusudi hawa Wadhibiti wa Elimu waweze kufanya kazi kwa kusimamia suala zima la elimu kwa weledi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 76 wa hotuba hii imezungumzia kuhusu kuendeleza ujuzi kwa kuboresha vyuo vya ufundi. Naipongeza sana Serikali kwa sababu tutakapopata mafundi mbalimbali kama walivoyzungumza wenzangu walitangulia itasaidia nchi yetu inavyokwenda kwenye uchumi wa viwanda wa kat. Kwa hiyo, suala la ufundi stadi ni la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri kwamba katika baadhi ya shule za msingi kuna vituo vya ufundu stadi, hebu Serikali ione jinsi ya kuvi boresha vile vituo vya ufundu stadi ambavyo viko katika zile shule za msingi kwa sababu baadhi ya wazazi hawawezi kuwapeleka watoto wao *VETA* na utakuta vyuo vingi vya *VETA* viko mijini. Kwa hiyo, Serikali ione itashirikiana vipi na *VETA* kuweza kuhakikisha kwamba vile vituo ambavyo viko katika shule za msingi vinapatiwa walimu wenyewe ujuzi pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niyapongeze sana taasisi na mashirika mbalimbali ya elimu katika kutekeleza majukumu yake. Niipongeze Serikali kwa kui-*task TET* iweze kuandaa masuala mbalimbali yanayohusiana na elimu kwa sababu tuliona kabisa kwamba siku za nyuma kumekuwa kuki tokea malalamiko kwamba vitabu vya kiada, mihtasari na vinginevyo vimkuwa havilandaliwi kwa maudhui yaliyo sahihi. Kwa hiyo, naomba niipongeze sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudini kubwa sana za Serikali katika kuboresha elimu bado tumeona kwamba suala la miundombinu ni changamoto hasa katika shule za Serikali. Mfano, makataba, maabara, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu pamoja na samani havitoshelezi. Kwa kuwa Serikali inajitahidi sana kukabiliana na upungufu huu na bado Watanzania wengi wanajitahidi kuzaa kwa kupata watoto wengi, naomba nitoe ushauri kwa Serikali ione umuhimu wa kuhamasisha Halmashauri zote za Miji, Manispaa, Majiji na Wilaya waanzishe mifuko ya kuendeleza elimu katika maeneo yao. Kwa kuanzisha mifuko hii ina maana kwamba itasaidia sasa ku-*supplement* zile shughuli za Serikali ambazo inawezekana upungufu ni mkubwa ikasaidia kujenga baadhi ya miundombinu na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kuhusu shule binafsi. Wenzangu wengi wamelizungumzia, lakini shule binafsi zinafanya kazi kwa kushirikiana na Serikali siyo *competitor*, lakini kuna kodi nyingi sana kwa hizi shule za

binafsi. Hebu Serikali ione kwamba hawa ni wadau ambao wanakwenda pamoja badala ya kuwawekea hizi kodi nyingi wazipunguze ili kusudi hizi shule za binafsi ziweze kutoa elimu inayotakiwa na tunajua kwamba zinatoa elimu ili wasije wakakwama, wakaona kwamba Serikali inatafuta mbinu ya kuwakwamisha ili wasifikie malengo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kuhusu wahitimu wa Chuo cha Ukutubi Bagamoyo. Serikali imekuwa ikiingia gharama sana kwa kuwafundisha hawa wakutubi lakini wengi wao hawana kazi na tunasema kwamba vyuo vianzishe maktaba sasa kwa nini hawa wahitimu wasipate fursa hiyo kwa kuajiriwa ili kusudi sasa hizi maktaba ziendeshwe kitaalam? Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali ione hilo hitaji kubwa kwamba hawa Wakutubi wanahitajika katika shule ili kusudi waweze kufanya kazi yao kwa jinsi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nitoe ushauri kwamba kwenye Ofisi za Udhhibitii wa Ubora wa Elimu nako kuwe kuna maktaba maalum na nashauri katika maktaba hizo vitabu vyote vyaa marejeo, vitabu vyaa kiada na vitabu vyaa ziada viwepo ili kusudi viweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la vifaa vyaa kujifunzia na kufundishia bado ni changamoto kwenye mtaala mpya kuanzia darasa la tatu na kuendelea kwa ufundishaji ambao ulikuwa uanze tangu mwaka 2015. Wenzangu wengi wamelizungumzia, lakini kuna baadhi ya walimu wanatumia vitabu vyaa zamani. Mfano, hisabati darasa la nne havijafika mashulenii na walimu wanatumia vile vitabu vyaa zamani. Hebu Serikali itafute ufumbuzi wa kuhakikisha kwamba vitabu hivi vyaa mtaala mpya vinafika shulenii kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, suala la mgawanyo wa fedha bado hauzingatii mahitaji maalum ya shule ambazo zina matokeo mabaya. Tumeona kabisa kwamba kuna baadhi ya shule zina matokeo mabaya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makof)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tunafikia tamati ya uchangiaji wa leo kwenye hoja hii, tutaendelea siku ya Jumatano, lakini lazima niseme nimefurahishwa sana na michango yenu kwenye sekta hii muhimu kwa Taifa letu na naamini mtaendelea kufanya hivyo keshokutwa. Nimetenda haki kwa makundi yote na naamini viongozi wa Kambi kama watajipanga kwa namna hii uchangiaji utakuwa ndani ya muda. Niwashukuru sana leo hapakuwa na ile amsha amsha, imesaldia kuwa ndani ya muda. Kwa hiyo, nawashukuru sana na pia niwashukuru kwa support mliyonipa katika kuongoza kikao cha leo. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, tangazo la kwanza, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mnakaribishwa kutembelea Maonesho ya Wajasiriamali walioshiriki Tamasha la Utamaduni na Sanaa Afrika Mashariki. Wajasiriamali hawa wanaonesha bidhaa zao katika viwanja vya Bunge, nyuma ya jengo la utawala. Watakuwepo na sisi mpaka tarehe 6 Mei, 2018. Kwa hiyo, mnaombwa sana Waheshimiwa Wabunge mkipata nafasi mtembelee eneo hilo mjonee hayo yanayofanywa na hawa ndugu zetu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili ni kutoka kwa Katibu wa Bunge, amenitaka niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo nje ya Mkoa wa Dodoma kikazi. Kwa kipindi hicho ambacho hatakuwepo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makof)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo mawili niliyokuwa nayo, sina lingine la ziada, kwa maana hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatano, tarehe 2 Mei, 2018 saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 2 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*